

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Sita – Tarehe 4 Februari, 2019

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Nne, Kikao cha Sita. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. AGNESS M. MARWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOBINU):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018.

MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 53

Ombi la Halmashauri ya *Geita DC* Kugawanywa

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA aliuliza:-

Halmashari ya *Geita DC* ina Majimbo mawili ya Geita Vijijini na Busanda ambayo kiutawala husababisha usumbufu na hali tete kwa wananchi kijiografia na mkoa ulishapitisha kuomba Serikali iigawe kuwa na Halmashauri ya Busanda:-

Je, ni lini Serikali itaridhia ombi hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura Na. 287 (Mamlaka za Wilaya) na Sura Na. 288 (Mamlaka za Miji) pamoja na Mwongozo wa Serikali kuhusu Uanzishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2014, mapendekezo ya kuigawa Halmashauri yanapaswa kujadiliwa kwanza kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imeshajadili suala hili katika Kikao cha Baraza la Madiwani

ingawa bado halijapelekwa kwenye Vikao vya Ushauri vya Wilaya (DCC) na Mkoa (RCC). Mara mchakato utakapokamilika na maombi kuletwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tathmini itafanywa na kuona kama kuna haja ya kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Spika, aidha, kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Tano ni kuimarisha maeneo yaliyokuwa yameanzishwa ili yaweze kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa badala ya kuendelea kuanzisha maeneo mapya ambayo hayaondoi kero ya kusogeza huduma kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, ameridhika.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, sijaridhika.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwana naomba niweke kumbukumbu sawa. Mimi ni Mbunge wa Geita, siyo Geita Vijijini. Hakuna Jimbo la Geita Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya *Geita DC* ina *population* ya takribani watu 1,200,000 kwa sensa ya mwaka 2012/2013. Sasa kwa majibu ya Serikali, inavyoonekana, bado tutakwenda hata uchaguzi ujao tukiwa bado tunakaa Halmashauri moja. Je, Serikali inatoa kauli gani ya uharaka kwa ajili ya kuharakisha hizo taasisi zilizobaki ili tuweze kupata mgawanyo wa Halmashauri mbili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba Mheshimiwa Waziri atamke kitu kwamba kulingana na ukubwa na wingi wa watu wa Halmashauri ya *Geita DC*, Serikali inaona umuhimu gani wa kutuongezea *ceiling* ya bajeti kwa wingi wa watu tulionao?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba suala la kugawa Mamlaka za Serikali za Mitaa linatakiwa lianzishwe na mamlaka yenyewe kwenye eneo hilo. Nimesema tayari jambo hili limejadiliwa kwenye Halmashauri yao ya Wilaya ya Geita. Sasa ni wajibu wao kupeleka mjadala huo kwenye ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa, nasi tupo tayari kupokea mapendekezo yao na tuangalie uharaka na ulazima wa kufanya maamuzi ya kugawa Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Spika, jibu la swali la pili ni kwamba bajeti ya Serikali inategemea na uwezo uliopo. Nia ya Serikali ni njema kabisa kwamba bajeti iongezeke na kila mtu angeweza kupata mgao ambao angehitaji. Hili nalo linategemea pia uwezo wa Serikali, kadri itakavyoruhusu basi bajeti itaongezeka ili huduma iweze kupelekwa kwa wananchi wa Geita na maeneo mengine ya nchi. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Swali hili linagusa Busanda na mwenye Jimbo lake yupo. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, jirani wa Mheshimiwa Musukuma.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katoro ambao una *population* kubwa sana: Je, Serikali inaonaje sasa hii mamlaka ya mji mdogo iwe mamlaka kamili ya mji? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI. Tena mnaweza mkachanganya Katoro na Buseresere ikawa mamlaka moja mkaihamisha hii huku. Majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kama nilivyosema, mchakato huu wauanzishe wenyewe watu wa Geita na hususan Busanda; nasi Ofisi ya Rais TAMISEMI tutapokea mapendekezo yao na tutawahisha jambo hili kadri itakavyohitajika kulingana na ukubwa wa bajeti na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Bado tuko Wizara hiyo hiyo ya TAMISEMI, swali linaulizwa na Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota. Kwa niaba yake, ndiyo.

Na. 54

Kumaliza Ujenzi wa Maboma ya Zahanati

MHE. STANLAUS S. MABULA (K.n.y. MHE. KEMILEMBE J. LWOTA) aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza ujenzi wa maboma ya Zahanati yaliyoanzishwa kwa juhudi za wananchi pamoja na kuyawekea vifaa tiba?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 Serikali ilifanya tathmini kubaini idadi ya maboma nchi nzima ambayo ni Vituo vya Afya, Zahanati na nyumba za watumishi na kubaini kuwa kuna maboma 1,845 ambayo yanahitaji jumla ya shilingi bilioni 934 ili kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliona ni vigumu kukamilisha maboma hayo kwa pamoja kutokana na upatikanaji wa fedha. Hivyo, ikabuni mkakati wa kujenga na kukarabati Vituo

vya Afya 350 nchini vilivyochaguliwa kwa kutumia vigezo ambavyo ni uhitaji mkubwa wa huduma za dharura na upasuaji wa akina mama wajaawazito, sababu za kijiografia na umbali mrefu ambao wananchi wanatembea kupata huduma za dharura.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019, jumla ya maboma 207, Vituo vya Afya sita, Zahanati 191 na nyumba kumi yalifikamilishwa kwa fedha kutoka Mradi wa Mfuko wa Pamoja wa Afya na Mapato ya Ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuzielekeza Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwenye makusanyo yake ya ndani na kuendelea kushirikisha wananchi na wadau wengine wa maendeleo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha za ujenzi na ukarabati wa maboma hayo.

SPIKA: Mheshimiwa Mabula Stanslaus, tafadhali.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wizara wanakiri kwamba kumekuwa na changamoto kutokana na maboma mengi ambavyo yamekuwa katika Halmashauri zetu, lakini pamoja na mkakati wao, walipofanya utafiti waligundua kwamba Halmashauri hazina uwezo wa kukamilisha maboma yote yanayojengwa kule kwenye Majimbo yetu; na ni ukweli usiopingika kwamba Mfuko wa Pamoja bado hauwezi kutosheleza:-

Sasa ni nini mkakati thabiti hasa wa Serikali kuhakikisha aidha kuwe na mkakati wa kusema kiasi cha maboma kinachopaswa kujengwa kwenye kila Halmashauri ili wao waweze kumaliza au tuendeleo na kusubiri ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati kutoka Mfuko wa Pamoja?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu. Hata Kongwa tuna zaidi ya maboma kadhaa ambayo yana zaidi ya miaka 10 hayajamalizika. Majibu tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoa majibu kwenye majibu yangu ya msingi; na Mheshimiwa Mbunge naye atakubaliana name kuhusu azma njema ya Serikali ambayo anaiona jinsi ambavyo tunapambana kuhakikisha kwamba tunapeleka huduma kwa maana ya kujenga Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Zahanati. Ndiyo maana katika majibu yangu ya msingi nimejibu kwamba ni vizuri tukafungua *avenue* pale ambapo Halmashauri zile ambazo ambazo zina uwezo, lakini pia kwa kushirikisha wananchi na wadau wengine tuendeleo kujenga kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma za matibabu karibu kabisa na wananchi, lakini pia vipaumbele ni vingi. Kwa hiyo, ni vizuri tukashirikiana pale bajeti inaporuhusu, Serikali inapeleka lakini pia na Halmashauri na wadau wengine ni vizuri wakashiriki katika suala hili muhimu sana kwa wananchi wetu.

SPIKA: Tunahamia Wizara ya Madini. Swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini.

Na. 55

Ujenzi wa Mtambo wa Kuchenjua Shaba

MHE. DAIMU I. MPAKATE aliuliza:-

Serikali imeweka zuio la kusafirisha shaba ghafi kabla ya kuchakatwa, jambo ambalo limesababisha uchimbaji mdogo wa Mbesa wa Shaba usimame na wachimbaji wadogo kukosa kazi za kufanya:-

Je, ni lini Serikali itajenga mtambo wa kuchenjua shaba katika Kijiji cha Mbesa?

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa tarehe 3 Machi, 2017, Serikali iliweka zuiu la kusafirisha nje ya nchi madini ghafi na kuelekeza madini yote yanayoongezewa thamani yaongezewe thamani hapa nchini. Zuiu hilo lilikuwa na nia njema ya kutaka shughuli zote za uongezaji thamani madini zifanyike hapa nchini ili kuongeza manufaa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla kutokana na rasilimali ya madini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na zuiu hilo, kuna *GN* Na. 60 ya mwaka huu, yaani tarehe 25, Januari, 2019, Serikali imetoa mwongozo wa kuhakiki uongezaji thamani madini au miamba nchini kabla ya madini hayo kupata kibali cha kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, madini ya shaba yanapatikana katika maeneo mbalimbali nchini. Hivyo, kwa kuzingatia hilo, Serikali imepokea maombi ya kampuni 11 zenye nia ya kujenga vinu vya kuyeyusha madini hayo (*smelters*) baada ya kutangaza uwepo wa fursa hiyo. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuteua kampuni zitakazojenga *smelters* hizo ili kuwaondolea adha ya soko la madini hayo wachimbaji wadogo na wakubwa.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, ila nina maswali mawili ya nyongeza. moja ya Kampuni zilizoomba kujenga mtambo wa kuchenjua shaba pale Mbesa ni *Metalicca Commodities Corporation* ya Marekani ikishirikiana na *Minerals Access System Tanzania (MAST)* lakini ni muda mrefu toka wameomba na majibu hayatolewi kutokana na kuchelewa kwa mwongozo. Je, Serikali mpaka sasa imefikia wapi kutengeneza mwongozo mzuri ukizingatia shaba ina tabia tofauti na madini mengine ili kuwezesha wawekezaji hao walioomba kupata kibali cha kuweza kujenga mitambo yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kumekuwa na leseni nyingi sana za utafiti zilizotolewa na Serikali kwa kampuni tofauti mbalimbali kwa muda mrefu na wamekuwa wanakaa kwa muda mrefu bila kuweza kuendeleza maeneo hayo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanyang'anya au kufuta leseni zile za utafiti kwa yale makampuni ambayo yamekaa muda mrefu na badala yake maeneo yale kupewa wachimbaji wadogo ili waweze kujikimu na kujitafutia riziki kwa njia ya kuchimba madini katika maeneo hayo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali imetoa mwongozo na mwongozo wenyewe umetoka tarehe 25, Januari, unaoonesha aina zote za madini yanaweza yakachenjuliwa katika kiwango gani na baada ya kuchenjuliwa yanapewa sasa ruhusa (*permit*) kwa ajili ya kusafirisha kupeleka nje ya nchi. Kwa hiyo, kwa kila aina ya madini tumetoa mwongozo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge afuatilie tu na aone kwamba sasa wale wawekezaji wanaokuja ambapo sisi tumejipanga kutafuta mwekezaji ambaye kweli yuko *serious* na kampuni zimekuja zaidi 11 wameonesha nia ya kuwekeza kwenye *smelter*, tunataka tuwawekee kampuni ambazo tuna uhakika nazo kwamba zinaweza kuwekeza kwenye kuchenjua au kuyeyusha zile shaba kwa maana ya *smelter*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu hizi leseni za utafiti za makampuni mbalimbali, ni kwamba mpaka sasa hivi, katika meza zetu tunapitia leseni zote ambazo zinaonesha ni leseni zilizotolewa mwaka gani. Tunataka kuangalia *status* zake zikoje? Tunapitia leseni ambazo zinafanyiwa kazi; lakini zile leseni ambazo ni za *PL* walipewa makampuni mbalimbali, wengi tumeona wameshikilia maeneo na hawafanyi kazi yoyote. Sasa hivi Wizara yetu tunapitia leseni zote. Kwa kampuni ambayo haifanyi chochote katika leseni ambazo tumewapatia, tunakwenda kuzifuta.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa leseni ambazo tumewapa watu kwa ajili ya uchimbaji kwa maana ya *Primary Mining License, Mining License, Special Mining License* na zenyewe tunaangalia kwa mujibu wa sheria na taratibu. Kama umekuwa na leseni huwezi kuifanyia kazi, sisi Wizara ya Madini muda siyo mrefu tutawapa *default notice* na tunakwenda kuzifuta leseni zote.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali la Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini.

Na. 56

Kuwapatia Masoko Wakulima wa Mkoa – Mtwara

MHE. AJALI R. AKBAR aliuliza:-

Wananchi wa Mtwara ni wakulima wakubwa wa zao la muhogo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia masoko ya uhakika wakulima hao?

(b) Je, kwa nini Serikali isiwapatie wajasiriamali, hasa akina mama, viwanda vya kuchakata muhogo?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao la muhogo ni miongoni mwa mazao ambayo Wizara yangu imepanga kuyapa msukumo wa kuyaongezea thamani ili yaweze kuchangia katika ukuzaji wa uchumi na kuongeza pato ya Taifa. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imekuwa na mkakati mbalimbali

wa kulingezea thamani na kupanua wigo wa soko la zao la muhogo. Itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 28 Juni, mwaka 2018 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aliagiza Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuunda Kamati Maalum ya Wataalam na kupitia changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima na kushindwa kuuliza zao hili katika soko la China. Kamati imeshakamilisha kazi yake na imeshatoa mapendekezo yake Serikalini kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanda cha *Cassava Starch of Tanzania Corporation* kilichopo Mbalala Mkoa wa Lindi chenye uwezo wa kuchakata tani 60 za muhogo kwa siku umekamilika kwa asilimia 90. Kiwanda hiki kimeanza uzalishaji wa unga wa muhogo kwa majaribio mwezi Januari, 2019. Kukamilika kuanza uzalishaji rasmi katika kiwanda hiki kutatoa fursa ya soko kwa wakulima wa muhogo wa Mikoa ya Kusini. Vilevile kutokana na kukua kwa soko la unga wa muhogo duniani nawahimiza wajasiriamali kupata ushauri kutoka kwa wataalam wakiwemo *SIDO* na *TIRDO* kwa lengo la kuelimishwa namna bora kuchakata zao hili ili kuuza katika masoko hayo hususan China ambako mahitaji ya muhogo ni makubwa.

SPIKA: Mheshimiwa Akbar, nimekuona swali tafadhali.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna taarifa kwamba kiwanda hiki anataka kutarajia kuchakata yeye mwenyewe, mchakato wa muhogo pale Lindi. Je sisi ambao tunalima muhogo sana katika Wilaya ya Newala na Mtwara kwa ujumla, huu muhogo wetu tutauza wapi na jitihada gani Serikali imefanya kututafutia soko lingine nje kwa kuwa hili yeye mwenyewe anasema kwamba *already* hilo soko linamtosha kwa ajili ya kiwanda tu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Stella Manyanya, Naibu Waziri, Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa kuanzia kiwanda hiki kimepata mashamba katika maeneo ya Nankauka (a) na (b) na maeneo mengine ili kuweza kuzalisha muhogo kwa kiwango ambacho kinatakiwa. Pia kwa kufuata taratibu zinazotakiwa, lakini katika majadiliano tuliyofanya ni pamoja na kuwawezesha wakulima wanaozunguka maeneo hayo, nao waweze kuuza muhogo wao katika eneo hilo na vilevile waweze kufaidika kwa sababu kiwanda hiki kitauza, unga lakini vilevile kitauza wanga.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Hawa pia utamalizia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama ilivyo kwa wananchi wa Newala, Wilaya ya Kyela ina zao la kokoa. Je, ni lini Serikali itatusaidia kupata wafanyabiashara wengi zaidi kuweza kusaidia kununua zao la kokoa kwa wananchi wa Wilaya ya Kyela? Ahsante.

SIPKA: Mheshimiwa swali linahusu muhogo, umeshahama mara hii, sijui kama Waziri wa Kilimo au wewe mwenyewe. Karibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, naomba kama ilivyo kwa mazao mengine, Wizara yetu inalo jukumu kupia *TANTRADE*, kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Wizara ya Kilimo kutafuta masoko ya uhakika na wawekezaji ili kuweza kuendeleza mazao yote. Kwa hiyo zao la kokoa ni mojawapo ya mazao ya kimkakati na linapendwa duniani na hivyo nalo ni sehemu mojawapo ambayo linashughulikiwa.

SPIKA: Nilikutaja Mheshimiwa Hawa Ghasia, swali la mwisho.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami naomba kuuliza swali la nyongeza. Ni kwa kiasi gani Serikali imefikisha taarifa ya uwepo wa soko la muhogo huko China katika mikoa yetu, kwa sababu katika *RCC* iliyopo

Mkoa wetu wa Mtwara ajenda ambayo ilikosa majibu ya uhakika ni ajenda hii. Je hizo taarifa walizonazo za uhakika wa masoko wamezifikisha mikoani?

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, tunatarajia tupate na majibu ya nyongeza kutoka kwa Waziri wa Kilimo, muhogo, muhogo, muhogo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIAFHARA: Mheshimiwa Spika, kimsingi kama nilivyosema kwamba kwanza kuliundwa Kamati ya Wataalam kwa ajili ya kutathmini changamoto mbalimbali juu ya zao hilo. Vilevile *TANTRADE* iliwaita wadau ambao nilikaa nao katika mkutano na kuwaelimisha juu ya upatikanaji wa masoko hayo. Kwa misingi hiyo kwa sababu Mheshimiwa Hawa Ghasia amezungumzia katika eneo maalum la Mtwara; nimwahidi tu kwamba, watumia fursa hiyo kwenda kuelimishwa ili waweze kushiriki kikamilifu.

SPIKA: Majibu ya nyongeza kutoka Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri wa Viwanda kwa majibu mazuri aliyoyotoa kwa niaba ya Serikali. Katika nyongeza ya swali hilo kwamba, ni kweli kama Serikali tarehe 1 mwezi huu tumekaa na mnunuzi mkubwa wa mhogo kampuni ya *Epoch Tanzania Limited* ambaye tumeshampa kibali kama uthibitisho ili kwenda kukionesha kwenye Serikali ya China. Tumefanya hivyo, kwa sababu mnunuzi yoyote anatakiwa kwanza athibitishwe na Serikali wazalishaji wa zao hilo na tumempa jana na hiyo taarifa imeshafika Ubalozi wa China maana Serikali ya China kuthibitisha hilo. Kwa hiyo, baada ya mkataba huo sasa tunakuja maana yake tumepata soko la uhakika na linalotambulika kisheria. Kwa hiyo mwaka huu 2019 tutakuja kuwatangazia rasmi ni lini sasa tutaanza usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kampuni hiyo ya *Epoch Limited*, kuna kampuni zingine tatu tumeshawapa

vibali, zote zimeshapata idhini ya kuuza mhogo katika soko la China, kwamba siyo kazi rahisi kwa utaratibu waliojiwekea wenzetu China, kwamba mtu yeyote tu ukiwa na mhogo sehemu unauingiza, hapana ni lazima upate uthibitisho kwenye Serikali ya uzalishaji ili kupata uhalali kama mzigo huo ni salama kwa matumizi ya nchi yao.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, sasa swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Kawe, kwa niaba yake.

Na. 57

Zoezi la Ununuaji wa Korosho Nchini

MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)
aliuliza:-

Mwezi Novemba, 2018, Rais aliutangaza ulimwengu kwamba Serikali yake itanunua korosho zote kwa bei isiyoungua shilingi 3,000/= kwa kilo.

(a) Je, mpaka sasa ni kiasi gani kimetumika na kimetoa chanzo kipi na je, tani ngapi zimenunuliwa?

(b) Je, Wakulima/Vyama vya Msingi vingapi vimelipwa na vingapi bado havijalipwa?

(c) Je, zoezi hilo linatarajiwa kukamilika lini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Jimbo la Kawe lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, makadirio ya uzalishaji wa korosho msimu wa 2018/2019 ni zaidi ya tani 240,000 za korosho

ghafi. Hadi kufikia tarehe tarehe 30 Januari, 2019, Serikali imekusanya jumla ya tani 214,269.684 za korosho ghafi zenye thamani ya Sh.707,089,957,200 sawa na asilimia 89.3 ya lengo la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa korosho unafanywa na Taasisi ya Serikali ya Bodi ya Nafaka na mazao mchanganyiko ambapo malipo yaliyolipwa na kuingizwa kwenye akaunti za wakulima hadi tarehe 30 Januari, 2019 ni kiasi cha Sh.424,849,405,110 zilizotokana na korosho za wakulima kiasi cha tani 134,535,904. Aidha Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko ni Taasisi ya kibiashara yenye lengo la kupata faida na mtaji wake unatokana na ruzuku kutoka Serikali na mikopo kutoka Taasisi kama Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*), *NMB*, *CRDB* na Benki zinginezo.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya wakulima laki 390,466 wamekwishalipwa hadi kufikia tarehe 30 Januari 2019. Aidha Vyama vya Msingi 603 vimelipwa kati ya Vyama vya Msingi 605 vilivyohakikiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, zoezi la operesheni korosho linaendelea vizuri na linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 15 Februari, 2019.

SPIKA: Muuliza swali, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza wakati Mheshimiwa Rais anasema kwamba Serikali itanunua korosho yote kutoka kwa wakulima na aliwatangizia wakulima wote wa Watanzania kwamba korosho kilo moja itanunuliwa Sh.3,300 kwa maana ya kutaka kuwasaidia wakulima wanyonge. Pia hivi karibuni tumeshuhudia Serikali hiyo inawalipa wakulima chini ya bei ya Sh.3,300 maeneo mengine Sh.2,600 na maeneo mengine chini hapo ikiwemo Mikoa ya Pwani, Mtwara pamoja na Lindi. Sasa nataka kufahamu kauli ya Serikali, Mheshimiwa Waziri hapa atuambie, je, ni kwa nini wanakiuka

maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuwalipa wakulima hao korosho zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwenye majibu ya msingi ya swali (a) anaongelea suala la Bodi ya Mazao Mchanganyiko na kwamba ni ya wao kukusanya korosho ni pamoja na kuzuia biashara ya kangomba, lakini hapa kwenye majibu yake na tumeona karibuni kampuni ya *INDO*, kutoka Nairobi imepewa kazi ya kuuza korosho kwa niaba ya Serikali. Sasa nataka anitofautishie kangomba hii inayofanywa na Serikali kupitia *INDO* pamoja na Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa sababu wamesema wanaziuza korosho zile kwa faida, kuna tofauti gani na wale kangomba wadogo wadogo waliokuwa wanakusanya korosho kwa wakulima na kuzipelekwa kwenye Vyama vya Msingi? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba tafadhali.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cesilia Mwambe Mbunge wa Ndanda, samahani...*(Makofi)*

SPIKA: Jamani majina yanafanana, Cesilia na Cecil ndiyo huyo huyo.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Endelea, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumwomba radhi Mheshimiwa Mbunge kwa kutamka vibaya jina lake. Nachukua nafasi hii sasa kujibu maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli, Serikali kupitia Mheshimiwa Rais aliutangazia umma wa Tanzania na ulimwengu kwamba korosho mwaka huu 2019 tutanunua kwa Sh.3,300 na ni kweli sasa tunanunua na tunalipa hivyo kwa korosho daraja la kwanza.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuongeza jibu hilo Mheshimiwa Mwambe anafahamu, tunapozungumza korosho ina madaraja mawili makubwa; daraja la kwanza yaani *standard grade* na daraja la pili maana yake *under grade*, Mheshimiwa Rais alipokuwa anazungumza tunakwenda kununua korosho kwa Sh.3,300 maana yake ni kuhamasisha ubora katika nchi hii, kwamba hiyo ni bei ya daraja la kwanza. Kwa hiyo inafahamika kisheria na kikanuni mahali popote pale.

Mheshimiwa Spika, korosho daraja ya pili bei yake ni asimilia 80 ya bei ya daraja la kwanza. Ndiyo maana nilikwishawatangazia wakulima na wanafahamu wenyewe, daraja la pili litanunuliwa kwa asilimia 80 ya bei ya daraja la kwanza, maana yake inakwenda kununuliwa kwa Sh.2,640 na korosho hapo hapo ikizidi chini ya daraja la pili, haitanunuliwa, atarudishiwa mkulima akaichague ili ailete ama iwe daraja la pili au daraja la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipomaanisha tunanunua korosho hatumaanishi tunanunua mpaka vigawe au mawe, mnafahamu mwaka jana 2019 nchi hii iliharibika duniani kwa kupata sifa potofu na mbovu, tumepeleka matofali badala ya korosho kwenye soko la kimataifa. Kama Serikali hatuwezi kurudia hilo na mtu yeyote hawezi kuchafua jina la nchi yetu na kuharibu ubora wa korosho yetu ikakosa soko katika soko la kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili anataka kufahamu kati ya kampuni iliyonunua korosho kutoka Bodi ya Nafaka ya Mazao mchanganyiko na kangomba. Kwanza Mheshimiwa kuna mambo ya msingi tuyaweke kwenye mambo ya msingi kama nchi, siyo kila jambo linahitaji siasa, korosho ni uchumi, nilitarajia Waheshimiwa Wabunge tuwe pamoja katika hili

kwa nia nzuri ya Serikali kupitia Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alipoamua kununua korosho hizi kwa bei ya Sh.3,300 badala ya ile wakulima walikuwa wanakwenda kulipwa Sh.2,700 ambayo wameikataa wakulima wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tusingeweza kukaa kuona wakulima wanagoma, bei ni ndogo hailipi gharama zao, Serikali ndiyo imechukua jukumu hilo kuhakikisha kwamba tunanunua kwa Sh.3,300. Leo tunapopata wanunuzi ambao wananunua zaidi hilo, siyo kubeza, mlipaswa kupongeza la sivyo sasa hivi wakulima wote wangelipwa Sh.2,700. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anasema tofauti ni nini, katika biashara ya korosho kuna watu kwenye mnyororo wa thamani kuanzia mzalishaji, kuna mawakala, kuna madalali, kuna wafanyabiashara wadogo na kuna wanunuzi wakubwa, tofauti kati ya kangomba na yule, yule ni mnunuzi, hizi korosho tumezinunua au kuzikusanya kwa mkulima siyo kuzila ila kuziua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yule ni mnunuzi kwenye soko la kimataifa, tofauti ya yule na kangomba, yule ananunua kwenye mfumo rasmi unaotambulika kisheria. Kangomba ni watu ambao wananunua korosho kinyume cha sharia. Kama tunavyofahamu korosho ni moja ya zao la kimkakati ambalo tumeliweka ununuzi wake kwenye mfumo rasmi tunanunua na tunakusanya kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani na kwa maana hiyo haruhusiwi mtu yoyote kwenda kununua ila ni Vyama vya Msingi na Ushirika..

SPIKA: Mheshimiwa...

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):
...vilivyopewa jukumu hilo....

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ameelewa, yanatosha usiongeze, Mheshimiwa Naibu Waziri inatosha...*(Makofi)*

NAIBU WAZIRI KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba niongezee kidogo...

SPIKA: Inatosha kabisa.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Pamoja na kwamba Mheshimiwa Mwambe ni mgumu wa kuelewa lakini kwa hili leo kasomeshwa shule. Ahsante sana Mheshimiwa Omary Mheshimiwa Mwambe ameelewa leo shule hiyo, maana alikuwa hajui tofauti ya kangomba na mnunuzi wa kimataifa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel tafadhali uliza swali lako, bado tuko Wizara ya Kilimo.

Na. 58

Ubadhirifu Katika Ushirika na Mashamba ya Kilimo Wilaya ya Siha

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL aliuliza:-

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Olenasha alitembelea Wilaya ya Siha kufuatilia ubadhirifu kwenye Shamba la Ganrangua na *SACCOS* ya Sanya Juu wa shilingi milioni 337 na Siha Kiyeyu shilingi milioni 840 ambapo aliigiza TAKUKURU kuchunguza ubadhirifu huo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kufanya upembuzi na kutambua mashamba ya umma, yasiyotumika vizuri na kurejesha kwa wananchi kwa kutumia vijiji na ushirika wao kama wazo la kwanza la Baba wa Taifa J. K. Nyerere, mfano wa baadhi ya mashamba hayo ni *Kafoi Farm* (Mifugo), Leoni(Ushirika-Mfilisi), Msingi (Ushirika-Mfilisi), Pirita (Ushirika-Mfilisi), Pongo (Ushirika-Mfilisi) na mengine mengi?

(b) Pamoja na juhudi nzuri zilizofanywa na Waziri Mkuu kuhusu ubadhirifu *KNCU*, je, Serikali ina taarifa kuwa ubadhirifu

kwenye mali za *KNCU* na Vyama vya Ushirika ni mkubwa na unaendelea kulindwa na wahusika hawagusiki na bei ya zao la kahawa linaendelea kuathirika?

(c) Je, Serikali inaweza kuwaeleza nini wananchi wa Siha kuhusu Shamba la Gararagua lililouzwa na *KNCU* mwaka 2014 na makabidhiano kufanyika mwaka 2016, likitoka mkononi mwa *Ocean Link* lakini Kampuni hii mpya imepata *EPZ Exemption* mwaka 2012 na je, Serikali haioni kuna harufu ya ufisadi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha, lenye sehemu (a),(b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upembuzi na utambuzi wa mashamba umekuwa ukifanywa na Serikali kila inapohitajika ili kufanya maamuzi sahihi ya matumizi ya mashamba. Mashamba ya Leoni, Msingi, Pirita na Pongo yanamilikiwa na Vyama vya Ushirika isipokuwa Shamba la Kafoi ambalo linamilikiwa na mtu binafsi. Mashamba haya yalikuwa na migogoro kwa muda mrefu kati ya vyama na wawekezaji ambao kwa sasa migogoro hiyo imekwishatuliwa. Aidha, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika inasimamia kwa karibu vyama husika ili kupata wawekezaji wapya kwa maendeleo ya wanachama wa Vyama vya Ushirika na wananchi wa Vijiji vya Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imechukua hatua kwa viongozi na watendaji waliobainika kujihusisha na ubadhirifu wa mali za *KNCU* kwa kuwafikisha Mahakamani kwa kesi ya uhujumu uchumi. Aidha, Serikali kwa kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kutekeleza jukumu lake la ukaguzi wa mara kwa mara kwa Vyama vya Ushirika, itaendelea kufanya ukaguzi kwa Vyama vya Ushirika, ikiwemo *KNCU* na pale itakapobainika kuwa kuna ubadhirifu wa mali

za vyama, Serikali haitasita kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika bila kujali nyadhifa au uwezo wa aina yoyote walionao.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Gararagua limeuzwa na *KNCU* mwaka 2014 kwa kuzingatia taratibu za manunuzi. Aidha, msamaha wa kodi yaani *exemption* uliotolewa kwa mwekezaji huyo mwaka 2012 unahusiana na uwekezaji wa Shamba la Kifufu na siyo Gararagua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tuhuma za ufisadi, Wizara itafuatilia suala hilo na itakapobainika kuna viashiria hivyo, Serikali itachukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Mollel, tafadhali swali la nyongeza.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, vilevile Waziri Mkuu na Mawaziri kwa kazi kubwa ambayo inafanywa kwenye eno hili la ardhi. Najua nia njema ya Waziri aliyejibu swali langu, namfahamu vizuri lakini nimpe taarifa kwamba katika majibu aliyonipa bado umeendelea ule utaratibu wa baadhi ya watendaji wa Serikali wasio waaminifu kupotosha kwenye vitu ambavyo ni vya msingi. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na baadhi ya majibu yaliyotolewa hapa, mojawapo ya jibu lililotolewa ni jibu ambalo Waziri Mwanjelwa aliwahi kulikataa na kutoa maelekezo tofauti lakini bado jibu hilo limeendelea hapa. Kuhusu *exemption* tuna barua ya Wizara ya Viwanda ikionesha kwamba mojawapo ya mashamba yaliyopewa *exemption*, mwaka 2014 Shamba la Gararagua limeuzwa lakini mwaka 2012 tayari mwekezaji aliyenunua mwaka 2014 tuna barua ya Wizara ya Viwanda inayoonyesha kwamba alipewa *exemption* mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, leo tukiwa hapa hatujui tuna wananchi wetu wa Kata ya Levishi, Kijiji cha Mese mashamba yao ya kahawa yamechukuliwa na *TANAPA*, Donumoru

wananchi sasa hivi wa Kilolepori wanaishi nje, wamebomolewa nyumba zao. Leo hatujui mpaka wa Siha na Wilaya ya Arusha lakini bado huko chini tuna watu ambao wanafanyakazi hiyo. Vilevile kwenye Wizara ya Kilimo tutaona kwamba...

SPIKA: Mheshimiwa Mollel swali sasa.

MHE.DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye swali langu sasa.

SPIKA: Swali moja kwa moja.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Mawaziri wa Wizara husika watakuwa wako tayari kufuatana nami sasa ili twende kwenye maeneo husika kwa sababu tuna Wazungu wanaouza mashamba ya Siha ili wapate mtaji wa kuendeleza maeneo mengine na kuchapa watoto ndani ya Wilaya ya Siha na nitawapa ushahidi hapa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Ardhi zitakuwa tayari sasa kukaa chini baada ya Tamko la Rais ili tuone ni namna gani tunaweza tukawapatia wananchi wa Ngarenandume makazi zaidi ya 38,000 wanaoishi kwenye heka 500?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Innocent Bashunga kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Dkt. Mollel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa namna anavyofuatilia migogoro ya mashamba ya ushirika katika Jimbo lake la Siha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mollel angependa kusikia *commitment* ya Serikali kama tuko tayari kuambatana naye kwenda Jimbo la Siha ili kutatua migogoro hii. Jibu ni kwamba tuko tayari na mara tu baada ya Bunge tutaeelekea katika Jimbo la Siha ili kuangalia migogoro hii katika mashamba ya ushirika. Pia kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, azma ya Serikali ni kuhakikisha tunakarabati ushirika kwa manufaa ya wananchi wetu.

SPIKA: Ahsante sana. Tunahamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua.

Na. 59

Mkandarasi Anayejenga Barabara ya Urambo-Kaliua

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA aliuliza:-

Mkandarasi aliyepewa tenda ya kujenga barabara ya lami kutoka Urambo kwenda Kaliua kilometa 28 ameonyesha udhaifu mkubwa katika kutekeleza kazi hiyo tangu awali:-

Je, kwa nini Serikali isisitishie mkataba wa mkandarasi huyo haraka kwa kumpata mkandarasi mwenye uwezo na uzoefu ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo muhimu kwa wakati na ubora?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa Ujenzi wa kwa kiwango cha lami wa barabara ya Urambo-Kaliua kilomita 28 ni moja kati ya miradi iliyotengwa mahsusi na Serikali kwa ajili ya wakandarasi wa ndani ili kuwajengea uwezo na kupata miradi mikubwa ya barabara. Mchakato wa kumpata mzabuni ulifanyika kwa malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, muungano wa Wakandarasi watatu wazalendo, *Salum Motor Transport Limited, Annam Road Works Company Limited* na *Jossam Company Limited* walikidhi vigezo na hivyo kushinda zabuni hiyo. Utekelezaji wa mradi huu ambao unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 ulianza rasmi tarehe 30 Agosti, 2017 na muda wa utekelezaji ni miezi 26. Hadi sasa wakandarasi hawa wameendelea na kazi japo kwa kasi ndogo lakini kwa kiwango cha kuridhisha ambapo utekelezaji umefikia asilimia 35.

Mheshimiwa Spika, kasi ndogo ya utekelezaji ilichangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa ambapo mvua nyingi ziliathiri utekelezaji ambapo mkandarasi ameomba kuongezewa muda. Hatua nyingine zinazochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mhandishi Mshauri wa mradi anaendelea kuwafundisha wakandarasi hawa kuhusu usimamizi wa miradi ili lengo lililopangwa liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kutokana na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, mradi huu utakamilika kwa ubora na viwango vilivyopangwa kimkataba. Hivyo, kusitisha mkataba kwa hatua iliyofikiwa haitakuwa na tija kwa Serikali kwani tuna imani kuwa kutokana na mafunzo wanayoyapata wakandarasi hawa wazawa watakamilisha mradi huu kwa viwango vinavyotakiwa.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Kaliua, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mradi wa barabara hii ya Kaliua-Urambo wa kilomita

28 ambao unatekelezwa na fedha ya Tanzania shilingi bilioni 37 ulitakiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2019 ambapo ni sasa hivi lakini mpaka leo wakati mradi unatakiwa ukabidhiwe una asilimia 37 tu kwa hiyo huu ni udhaifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, wakati wakandarasi hawa watatu wanaomba zabuni mpaka wanapewa walikuwa watatu na ndiyo maana walikidhi vigezo lakini wengine walikuwa ni kama mwavuli sasa hivi ni mkandarasi mmoja tu ambaye ni Jossam ndiyo anatekeleza mradi huo na hana uwezo wa kutosha ndiyo maana anakwenda *speed* ndogo sana na barabara hii ni muhimu kwa uchumi na haiwezi kukamilika kwa wakati. Kwa kuwa wakati wanapewa kazi walikuwa makampuni matatu na sasa hivi amebaki mmoja ambaye ni Jossam na udhaifu unaonekana, kwa nini Serikali isielekeze wale wote watatu ambao waliomba tenda waungane pamoja na kwa kuwa wameomba kuongezewa muda waweze kukamilisha barabara hii kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kigezo kwamba mvua ilikuwa nyingi ndiyo maana barabara haiendi kwa wakati nakikataa kwa sababu majira ya kanda mbalimbali Tanzania za mvua na jua yanajulikana lakini hata wakati wa jua barabara hii bado haitengenezwi. Unaona wakati wa jua kabisa wamelala usingizi na mvua ikija wanasema ni mvua. Toka mwezi wa Julai na Agosti tuko kwenye jua karibu miezi tisa hapa imekwenda lakini bado *speed* ni ndogo. Kwa hiyo, tunaomba kisingizio kwamba majira hayajulikani kiondoke lakini pamoja na muda walioongezewa Serikali inatambie barabara hii itakamilika lini kwa viwango vinavyotakiwa? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kutoka kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Katibu wa Mkuu wa CUF, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

MBUNGE FULANI: Naibu.

SPIKA: Naibu Katibu Mkuu wa CUF. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mbunge wa Jimbo la Kaliua, Mheshimiwa Magdalena Sakaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, barabara ya kutoka Tabora – Urambo - Kaliua - Uvinza - Kigoma yote sasa hivi itakamilika kwa sababu vipande vitatu vilivyobaki, kimojawapo hicho anachokizungumzia Mheshimiwa Magdalena Sakaya cha kutoka Urambo - Kaliua ambacho kina mkandarasi lakini pia Kazilambwa - Chagu tumetangaza tenda na wakati wowote tutatangaza tenda ya Malagarasi – Uvinza. Kwa hiyo, barabara nzima itakamilika na fedha tunayo kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimetembelea kule na nimewakuta wale wakandarasi wote watatu na msingi wa wakandarasi watatu ulianzishwa na Mheshimiwa Rais akiwa Waziri. Unakumbuka kule Mbutu aliwaunganisha wakandarasi 10 wakafundishwa na hao sasa hivi ndiyo wanakuwa wakandarasi wazuri. Kwa Urambo - Kaliua nimetembelea yule mkandarasi nikaona changamoto zilizokuwepo, tumekaa, tumezungumza na tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya mwenyewe ni shahidi, wamenunua mtambo mkubwa sana kwa ajili ya kusaga kokoto, kwa hiyo, barabara itakamilika kwa muda uliowekwa. Hakuna haja ya kuwasimamisha, tayari nimeshakwenda kule nikaongea na Mhandisi Mshauri na wale wakandarasi watatu wote wamerudi sasa wanaendelea na kazi, kwa hiyo, mradi huo utakamilika kwa muda walioongezewa. Nimhakikishie Mheshimiwa Sakaya na wananchi wa Urambo kwamba hapana shaka mradi huo unakamilika pamoja na barabara yote kuelekea Kigoma.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali la Mheshimiwa Mbunge wa Manonga, Mheshimiwa Seif Gulamali tafadhali.

Na. 60

Vibali kwa Ajili ya Kuweka Minara ya Mawasiliano

MHE. SEIF K. S. GULAMALI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa vibali kwa Kampuni za *Halotel* na *Vodacom* ili kuweza kuweka minara yao katika Kata ya Igoweko, Uswaya, Tambarale, Mwashiku, Ngulu, Ntobo na Mwamala?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Atashasta Nditiye, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kulipatia vizuri kabisa jina langu la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina kizuizi kwa kampuni yoyote inayotoa huduma za mawasiliano kama itazingatia utaratibu wa kuomba vibali vya ujenzi wa minara yao kwa mujibu wa sheria pamoja na kupata cheti cha tathmini ya mazingira kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira (*NEMC*).

Mheshimiwa Spika, Kata ya Igoweko, Ngulu na Sungwizi zimeainishwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kuingizwa katika orodha ya miradi itakayotekelezwa na

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) ambapo TTCL wako katika hatua za mwisho za taratibu za manunuzi ili kuanza kutekeleza miradi hiyo. Miradi hiyo yote inategemewa kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kata za Uswa, Tambarale, Mwashiku, Ntobo na Mwamala zitaingizwa katika orodha ya miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kutekelezwa kutokana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, tunatoa wito kwa makampuni mbalimbali kuendelea kuwekeza minara ya mawasiliano katika Jimbo la Manonga na maeneo mengine nchini yale hasa yenye uhitaji kwa kuzingatia taratibu.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Manonga.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo imeweza kutekeleza upatikanaji wa mawasiliano katika maeneo tajwa kwa wakati kwa sababu hatua mbalimbali zinaonekana zinaendelea kufanyika. Kwa hiyo, niiombe tu Serikali iongeze *speed* katika yale maeneo ambayo mradi huu unatekelezwa katika kata hizo.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali katika hizo Kata ambazo tumezitaja kwa maana ya Uswaya, Tambarale, Mwamala ni maeneo ambayo yana watu wengi sana, kwa sababu Serikali ilikuwa imeweka mpango huu katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 na bajeti hii sasa inaelekea mwishoni, je, haioni sasa umuhimu wa kuweka katika mpango wa bajeti wa mwaka 2019/2020?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwa rufusa yako, kwanza nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika lakini pia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Zungu na wengine wote wadau kwa yale ambayo yametokea kule Misri. Sisi tunawaomba muendeleo vizuri yasitokee tena kama yalitokea kule Misri. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu lakini hilo la pili nimelifuta siyo swali. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata mawasiliano ya uhakika kwa asilimia 100. Hadi sasa hivi tunapongea Watanzania kwa *record* za Serikali wanawasiliana kwa asilimia 94.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba mwezi Aprili, kuna orodha ya vijiji na kata nyingine itakayotolewa na Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ambazo zitakuwa zimependekezewa kwa ajili ya miradi ya mawasiliano. Asiwe na wasiwasi, tumejipanga kutekeleza kuhakikisha kwamba Watanzania wanawasiliana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Bado tuko Wizara hiyo, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa visiwani Mafia, nimekuona Mheshimiwa Vulu.

Na. 61

Kuongeza Njia ya Kurukia Ndege - Kiwanja cha Ndege Mafia

MHE. ZAYNABU M. VULU (K.n.y. MHE. MBARAKA K. DAU) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza urefu wa njia ya kurukia (*run way*) katika Uwanja wa Ndege wa Mafia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Usafiri wa Anga inataka kila mkoa kuwa na Kiwanja cha Ndege cha Daraja la 3C chenye uwezo wa kuhudumia ndege za kubeba abiria kati ya 50 na 100. Aidha, kwa mikoa inayowakilisha kanda, Viwanja vya Ndege vinavyopendekezwa ni kuanzia Daraja la 4C kwa ajili ya kuhudumia ndege za kubeba abiria kati ya 100 na 200 zinazoweza kufanya safari za kikanda na kimataifa. Kiwanja cha Ndege cha Mafia ni miongoni mwa viwanja vya Daraja la 3C.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha Viwanja vya Ndege nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilikamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa viwanja saba ikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Mafia mnamo mwaka 2009. Kazi hii ilifuatiwa na ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege kwa kiwango cha lami katika ya mwaka 2011 na 2013. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege kufikia urefu wa mita 1,620 na upana wa mita 30, ukarabati wa kiungio na maegesho ya ndege kwa ikiwango cha lami, ujenzi wa mfumo wa maji ya mvua kiwanjani na ujenzi wa uzio wa usalama.

Mheshimiwa Spika, kazi hizi zilifanyika kwa ufadhili wa Shirika la Changamoto za Milenia (MCC) la Serikali ya Marekani. Baada ya maboresho haya, kiwanja kipo kwenye kiwango cha Daraja la 2C ambapo kina uwezo wa kupokea

na kuhudimia ndege zenye ukubwa wa aina ya *ATR42, DASH 8* na *Fokker 50* ambazo zina uwezo wa kubeba abiria kati ya 30 na 50.

Mheshimiwa Spika, katika mipango yake ya muda wa kati na mrefu, Serikali itaendelea kukamilisha kazi zilizobaki ambazo ni pamoja na ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake yaani barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, barabara ya kiungo na maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Pamoja na kuwa kwa sasa kiwanja hiki kipo Daraja la 2C, eneo la ziada limeshatengwa ili kukidhi mahitaji ya upanuzi wa kiwanja kwa siku za baadaye na kukamilishwa kwa kiwanja kuwa Daraja ya 3C.

SPIKA: Mheshimiwa Zaynabu Vulu nilikuona atafuatia Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu yaliyotolewa na Serikali, nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali sasa hivi ina ndege zaidi ya sita; na kwa kuwa ndege hizo zina uwezo wa kubeba abiria wengi; na kwa kuwa Mafia ni kisiwa ambacho kiko katika ramani ya Tanzania kutokana na shughuli zake za utalii, utalii wa samaki aina ya potwe ambapo kila mwaka watalii wengi wanakwenda, je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kuongeza ukubwa wa kiwanja na kuhakikisha Shirika la Ndege la Tanzania linapeleka ndege zake kwa ajili ya abiria wanaosafiri na wanaokwenda kuangalia utalii huko wanakokwenda?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa bado hakuna utaratibu wa Serikali kupeleka ndege kubwa; na kwa kuwa wananchi wa Mafia wana adha kubwa ya usafiri wa baharini na ndege. Je, huoni sasa kuna haja ya kuongeza *speed* ya kupata meli au boti ambayo itasaidia na kurahisisha usafiri kwa wananchi wa Mafia? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa tafadhali.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ni kweli Mafia ni eneo muhimu na kuna vivutio vingi sana vya utalii katika eneo hili, lakini nimuhakikishie tu Mheshimiwa Vulu, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba hatua madhubuti Serikali inazichukua ili kuhakikisha kwamba tunaboresha usafiri wa Mafia ikiwemo usafiri huu wa ndege na usafiri wa vyombo vya majini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Vullu usiwe na wasiwasi kwa sababu kama nilivyosema tunakwenda kuufanya uwanja huu uwe katika kiwango cha daraja C. Lakini kikubwa ambacho kama Serikali tutafanya kwa sababu tumeendelea kuongeza kununua ndege pia tutaongeza idadi ya miruko katika kisiwa hiki. Tukiongeza idadi ya miruko katika kisiwa hiki tutaweza sasa kuweka uwiano wa abiria na huduma ambayo inahitajika Mafia kwa hiyo sisi kama Serikali tuko makini kuhakikisha kwamba tutakwenda kuhuduamia kisiwa cha Mafia kulingana na mahitaji ya wakati ili tuweze kusaidia pia kuchangia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuwa na usafiri wa majini kama Mheshimiwa Vullu alivyosema Serikali inayo Mpango wa kutengeneza boti maalum ambayo itakuwa inatoka Nyamisati kwenda Kilindoni Mafia. Kwa hiyo, utaratibu wa manunuzi Mheshimiwa Vulu zinaendelea , kwa hiyo baada ya muda ambao siyo mrefu wananchi wa Mafia wataweza kuunganika vizuri na upande huu wa bara. Kwa maana hiyo kwamba Mheshimiwa Vulu na wananchi wa Mafia wasiwe na wasiwasi tunatambua umuhimu wa kuhudumia kisiwa cha Mafia kwa umaridadi wa hali ya juu. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini uliza swali.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru niko kwenye *runway*, ningependa kujua kwa Mheshimiwa Waziri ni lini ujenzi wa jengo la abiria pamoja na taa kwenye njia za kurukia yaani *runway* zitakamilika kwenye uwanja wa ndege wa Songwe Mbeya ili uwanja ule uweze kuufikia *full capacity*? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi hata kukiwa na ukungu tu kidogo kwa sababu hakuna taa na unajua ndege nyingi *pilot* hawezi kutua kama haoni umbali wa futi 700 kutoka juu kwenda uwanja wa ndege kama haoni hawezi kutua. Sasa kukiwa na ukungu kidogo ndege haitui, mwenyewe nimesharudi Dar es Salaam mara mbili na ndege kwa kushindwa kutua mchana kabisa kwa sababu ya ukungu na tatizo kubwa likiwa ni taa za kwenye *runway*.

Sasa ningependa kujua lini vitu hivi vitakamilika jengo la abiria pamoja na taa ili *Songwe International Airport* iwe *full capacity*? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na kukamilisha mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Songwe ni kwamba tunatangaza *tender* mwezi huu, mwezi wa tatu tutakuwa tumeshampata mkandarasi na kukamilisha *runway* kutachukua miezi miwili. Baada ya hapo sasa tutaenda kwa ajili ya *tender* ya kukamilisha jengo. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi kiwanja cha Songwe ni katika viwanja vikubwa kikiwepo cha Julius Nyerere kiwanja cha Mwanza na KIA. Kwa hiyo, malengo ya Serikali ni kuhakikisha viwanja vyote hivyo vinaboreshwa na kufanya *dreamliner* iweze kuruka viwanja vyote. (Makofi)

SPIKA: Swali la mwisho Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, *runway* ya uwanja wa ndege au uwanja wa ndege wa Kigoma ni uwanja wa kimkakati kiuchumi

ukizingatia mali iliyopo katika Jamhuri ya Demokrasia ya Congo na majirani zetu. Sasa mgogoro uliokuwepo wafidia kwa wananchi umekwisha, sasa ni lini Serikali na *European Investment Bank* ambao ndiyo *finance* wa mradi ule sasa watakaa pamoja ili uwanja wa ndege ule uweze kupanuliwa na kutujengea jumba la wageni na maegesho ya ndege? (Makofi)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge Nsanzugwanko na jibu lake ni fupi, mazungumzo kati ya Serikali na *European Investment Bank* yamekamilika tunachosubiri watulettee *no objection* ili tusaini mkataba mkandarasi aendelee na kazi. (Makofi)

SPIKA: Tunaendelea sasa na Maji na Umwagiliaji swali linauliza na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli.

Na. 62

Tatizo la Maji – Jimbo la Monduli

MHE. JULIUS K. LAIZER aliuliza:-

Tatizo la maji Jimbo la Monduli limeongeze kwa sasa baada ya Mabwawa zaidi ya 43 kati ya 51 kujaa tope na mengine kupasuka:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuwapatia maji wananchi wa Esilalei, Makuyuni, Mswakini na Ohukai kabla ya mwaka 2020?

(b) Mradi wa maji ya kisima cha Ngaramtoni umefika katika Kata ya Monduli Mjini na Engutoto; je, ni lini Serikali itasambaza maji kwa wananchi wa Vijiji vya Lashaine, Ar Katan na Meserani chini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Maji Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuwapatia maji wananchi wa Esilalei Makuyuni, Mswakini na Otukai kabla ya mwaka 2020 Serikali imekuwa ikijenga mabwawa ya kuhifadhi maji katika Wilaya ya Monduli kutokana na Wilaya hiyo kukosa vyanzo vya uhakika vya maji kama vile chemchem na vyanzo vya maji chini ya ardhi. Kwa upande wa Vijiji vya Makuyuni na Mswakini vinapata maji kupitia visima virefu vilivyochimbwa kwenye vijiji hivyo na vijiji vya Esilalei na Otukai vinapata maji kupitia vyanzo vya Bwawa ya Otukai, Esilalei na JKT Makuyuni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 Serikali ilitekeleza mradi wa maji wa Ngaramtoni ambapo awamu ya kwanza ilihusisha huduma ya usambazaji katika kijiji cha Meserani Juu. Awamu ya pili itahusisha usambazaji wa maji katika Kijiji cha cha Meserani Chini na kazi hiyo inategemea kuanza mwezi Julai, 2019. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Monduli imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Serikali itaendelea kutenga fedha na kutoa fedha ili kuhakikisha hadi kufikia mwaka 2020 vijiji vyote vya Arktana, Nanja, Esilalei, Makuyuni, Mswakini, Otukai na Mti Mmoja vimepatiwa huduma ya maji.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Monduli, nimekuona swali tafadhali.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushuku, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu yao katika swali hilo la

msingi, lakini nasikitika kwamba maeneo mengi ya Serikali katika majibu haya hayakidhi swali ambalo nimeuliza.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo amesema kwenye jibu la msingi eneo la Mswakini na Makuyuni wanapata maji, lakini tumekuwa tumeleta malalamiko Serikali ya muda mrefu kwamba visima hivyo havitoi maji kwa sababu hakuna nishati ya umeme na Serikali imekuwa ikiahidi kila siku kwamba wanatuletea nishati ya umeme katika visima hivyo. Je, ni lini Serikali itatuwekea umeme katika visima vya Makuyuni na Mswakini ili wananchi wetu waweze kupata maji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nataka *commitment* ya Serikali kwa kuwa wamesema watatupa fedha kwa ajili ya miradi hii ya maji katika vijiji alivyotaja nini *commitment* ya Serikali kwamba kwa mwaka wa fedha 2019/2020 tutapata fedha ya kutosha kwenye Bajeti kwa ajili ya miradi hii ambayo usanifu wake umekamilika? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Kalanga kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Jimbo lake la Monduli na nimeshakwishafika Monduli tumeona kazi kubwa anayoifanya na sisi kama Wizara ya Maji tutahakikisha tunamuungisha mkono katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Lakini kuhusu suala zima la nishati ya umeme nataka nimuhakikishie tutafanya mawasiliano ya haraka na watu wa Wizara ya Nishati katika kuhakikisha eneo la Makuyuni wanapatiwa umeme ili uendeshaji wake uwe wa nafuu na wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, lakini suala zima la bajeti la mwaka 2019/2020 tunakumbuka Mheshimiwa Kalanga mbele ya Mheshimiwa Rais katika wakati anaweka jive la msingi katika mradi wa maji Arusha ulitoa malalamiko yako na ukaomba

atakapotembea na kudhulu wengine asikupite. Sisi kama Wizara ya Maji hatutokupita wala hatutokuacha wala hatutokutosa katika kuhakikisha tunakuongezea bajeti na wananchi wako waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana bado tuko Wizara ya Maji swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Nsimbo, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, tafadhali.

Na. 63

Hitaji la Bajeti ya Kuboresha Miradi ya Maji – Nsimbo

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

Upatikanaji wa maji safi na salama katika Jimbo la Nsimbo ni asilimia 40 chini ya wastani wa kitaifa vijijini wa asilimia 61.1 ili kufikia wastani huo inahitajika fedha kiasi cha bilioni 15:-

Je, Serikali ipo tayari kuitengea Halmashauri ya Nsimbo angalau bilioni tatu kila mwaka wa fedha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri Maji. Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 imeitengea Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kisi cha shilingi bilioni 1.413 ikiwa ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji inayoendelea kutelezwa katika vijiji vya Sitalike, Igongwe, Itenka, Nduwi pamoja na ufungaji wa pampu za mkono katika vijiji vya Kashelami, Kapanda, Wenyeji,

Imilamate, Kambuzi Halt, Ofisi ya DED - Nsimbo, Katambike, Kabuga, Kituo cha Afya Katumba, Buremo, Ikondamoyo na Ndurumo A.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wote wananufaika na huduma ya maji wakiwemo wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Serikali imejiwekea lengo la kuhakikisha huduma ya maji inafikia asilimia 85 upande wa maji vijijini na asilimia 95 miji ya mkoa ifikapo 2020. Hivyo, Serikali itaendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi maji nchi kote ili kuweza kufikia malengo hayo.

SPIKA: Mheshimiwa Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, swali la nyongeza.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi pamoja na majibu ambayo yametolewa na Serikali niishukuru kwamba Serikali imekuwa ikiongeza bajeti tulikuwa shilingi milioni 500, shilingi milioni 800 na mmefika shilingi bilioni 1.4. Lakini swali la msingi lilikuwa ni kwamba tunapandisha vipi kiwango ha upatikanaji maji safi na salama kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na tupate angalau bilioni tatu.

Sasa je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwa na mjadala na Mbunge pamoja na watendaji wake wa Wizara ili kuona namna gani kiwango kinaongezeka kutoka shilingi bulioni 1.4 angalau tuwe na *reasonable amount* ambayo itaweza kutatua changamoto hii?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mafupi Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya. Lakini kikubwa tunatambua kabisa maji ni uhai na jukumu la Wizara yetu ya Maji ni kuhakikisha watanzania na wana Nsimbo wanapata maji safi, salama na yenye kutosheleza. Sasa katika

kuhakikisha tunalinda uhai wa wana Nsimbo sisi kama Wizara ya Maji tupo tayari kufanya mjadala na Mheshimiwa Mbunge nadhani baada ya Bunge hili tukutane tuweze kukutana na watendaji wetu ili tuweze kujadiliana ni namna gani tunaweza tukatatua tatizo la mji Nsimbo kwa haraka. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto swali linaulizwa na Mheshimiwa Julius Masele Mbunge wa Shinyanga Mjini kwa niaba yake upo endelea tafadhali.

Na. 64

**Wananchi Wanaotumia Bima ya Afya
Kunyimwa Dawa**

MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y. STEPHEN J. MASELE)
aliuliza:-

Kumekuwepo na kero kubwa ya wananchi wanaotumia Bima ya Afya kunyimwa dawa katika zahanati na maduka ya dawa nchini kwa kisingizio cha malipo kutoka *NHIF* kuchelewa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kimkakati wa kuhakikisha malipo yanafanyika kwa ufanisi ili kuboresha mfumo mzuri wa matumizi ya kadi za Bima hususani kwa wazee nchini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Stephen Julius Masele leo ni Siku ya Saratani Duniani na naomba kuwakumbusha Watanzania kwamba saratani ni

tatizo kubwa ndani ya nchi yetu takribani watu 55,000 kwa mwaka wanapata ugonjwa huo wa saratani na ni 13,000 tu ambao wanafika katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya ikiwa ni takribani ni asilimia 25 na asilimia 70 wanafika wakiwa na hatua ya mwisho kabisa ya ugonjwa. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kutumia fursa hii kuwaomba Watanzania kujitokeza kwa wingi kupata huduma na upimaji na matibabu ya saratani ni bure. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya huingia mkataba na vituo vya kutolea huduma , mkataba ambao huanisha makubaliano juu ya utaratibu wa kutoa huduma bora kwa wanufaika wake na uwasilishaji wa madai ya gharama ya huduma za afya zinazotolewa kwa wanachama wake. Utaratibu huo huwataka watoa huduma kuwasilisha madai yao kwa wakati ndani ya siku 30 baada ya mwezi husika wa madai ili kuwezesha kuanza kwa mchakato wa madai hayo kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sheria inautaka mfuko kukamilisha malipo ya madai ya watoa huduma ndani ya siku 60 toka siku ambayo madai husika yamewasilishwa katika Ofisi za Mfuko zilizopo katika mikoa yote nchini. Kwa sasa mfuko unalipa madai kwa wastani wa siku 45. Hata hivyo baadhi ya madai yamekuwa yakichelewa kulipwa kutokana na ucheleweshaji wa kuwasilisha madai kwa baadhi ya watoa huduma. Watoa huduma kutozingatia miongozi ya tiba kama ilivyoainishwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa maana ya *Standard Treatment Guidelines*. Vitendo vya udanganyifu na baadhi ya watoa huduma kutozingatia makubaliano yaliyoainishwa katika mkataba wa huduma baina yao na mfuko.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mfuko kwa sasa unaendelea kufanya maboresho ya huduma zake ikiwa ni pamoja na kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kutumia zaidi TEHAMA katika utayarishaji wa madai na kuwezesha watoa huduma kutayarisha madai kwa wakati;

(ii) Kuimarisha ofisi za mikoa na kugatua zaidi shughuli za mifuko hasa malipo kwa watoa huduma, viwango vya malipo mikoani vimeongezwa ili kuzipa ofisi za mikoa uwezo wa kulipa madai makubwa;

(iii) Kuendelea kutoa elimu kwa watoa huduma wote waliosajiliwa na mfuko ili kuwasilisha madai kwa wakati na kujiepusha na vitendo vya udanganyifu;

(iv) Mfuko unaendelea kuwakumbusha watoa huduma kuzingatia miongozo ya tiba na maelekezo mengine yanayotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa lengo kuhakikisha watazania wanapata huduma bora za afya.

SPIKA: Mheshimiwa Maige nilikuona swali la nyongeza hapo.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri naomba tu kuuliza tu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kumekuwepo malalamiko sehemu nyingi za Shinyanga na hata Kahama kwa baadhi ya wazee kutokukamilishiwa utaratibu wa kupata vitambulisho ili wapate huduma za tiba bure kama Serikali ilivyowaelekeza. Je, Serikali inachukua hatua gani kuweka maelekezo maalum kwa Watendaji wa Serikali wa Kata na hata Vijiji ili kukamilisha zoezi hili wazee wapate tiba baila usumbufu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili wananchi pamoja na Serikali hasa katika maeneo ya Msalala wamefanya kazi kubwa ya kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya na hivi sasa kwa mfano Msalala tuna vituo vya afya vipya viwili, kituo cha Bugalama na Chela. Lakini vituo hivi havina vifaa tiba wala madawa ya kutosha pamoja na watumishi. Je, Serikali inachukua hatua gani kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba, dawa na watumishi kwenye kituo cha afya cha Chela pamoja na Bugalama ambavyo ni vituo vya afya vipya nashukuru? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Dkt. Ndugulile tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kwa lengo la kutoa vitambulisho ambavyo vitawatambua wazee zaidi ya miaka 60 ili waweze kupata matibabu kwa mujibu wa sera tunatambua kwamba baadhi ya Halmashauri hazijatekeleza hilo na nitumie fursa hii kuzikumbusha hizo halmashauri kuzingatia hili agizo la Serikali kuhakikisha kwamba wazee wote ambao wako zaidi ya miaka 60 wanapata vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri alifanya uzinduzi wa mpango mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wazee na Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo kwamba Wizara iharakishe zoezi la kufanya mapitio ya sera ya wazee ya mwaka 2003. Lakini vilevile kuanzisha na sheria ya wazee ili sasa haya mahitaji ya wazee yawe kwa mujibu wa sheria na sisi kama Wizara tumeshaanza utekelezaji wa hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili kuhusiana na vituo vya afya ambavyo vimeboreshwa nimthibitishie tu kwamba Mheshimiwa Mbunge kwamba baada kazi ya kukamilika ya ujenzi wa maboma ya vituo vya afya. Serikali inaendelea na utaratibu wa kupata vifaa kwa ajili ya vituo vyote vya afya ambavyo vimeboreshwa, baadhi ya vifaa vimeshafika na vingine viko njiani vinakuja.

Nimthibitishie tu kwamba Mheshimiwa Mbunge vifaa hivyo vinakuja na tutaendelea kupatia watumishi wa kutosha kadri ya uwezo na Serikali itakapokuwa inaajiri. Lakini nimuhakikishie kwamba dawa tunazo za kutosha zaidi ya silimia 90 kwa hiyo, mgao wa dawa tutauongeza kulingana na mahitaji. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tunaendelea mniwie radhi sana. Swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma ambalo bado liko Wizara ya Afya na swali linafanana na la mwanzo.

Na.65

Wananchi Kujiunga na Mifuko ya Bima ya Afya kwa Mujibu wa Sheria

MHE. KITETO Z. KOSHUMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta sheria ya kuwataka wananchi wote kujiunga Mifuko ya Taifa ya Bima ya Afya?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya Dkt. Ndogulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea na maandalizi ya utaratibu wa kuhakikisha Watanzania wote wanakuwa katika mfumo wa bima na hivyo kuwa na uhakika wa kupata huduma wakati wote wanapohitaji bila ya kuwa na kikwazo cha kifedha. Katika kulitekeleza jambo hili Wizara imeandaa mapendekezo ya kuanzisha bima ya afya moja, kwa maana ya *Single National Health Insurance* na kuwasilisha katika

ngazi mbalimbali za maamuzi Serikalini. Pindi Serikali itakaporidhia mapendekezo haya suala hili litawasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, endapo Bunge lako litaridhia muswada huo kutakuwa na ulazima wananchi wote kujiunga na bima ya afya. Matarajio ni kuanza kutekeleza mwaka huu 2019. Kwa sasa Wizara inaendelea kutekeleza mikakati ya kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya na CHF iliyoboreshwa. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwahimiza wananchi kujiunga na bima ya afya na CHF zilizoboreshwa wakati tunasubiri muswada huo kupitishwa.

SPIKA: Mheshimiwa Kiteto!

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwa sababu ni miongoni mwa Mawaziri ambao wana ushirikiano mkubwa sana katika Wizara hii ya Afya. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri amekiri kwamba Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya utaletwa Bungeni na kwa kuwa wananchi wengi waishio vijijini na mijini hawana uelewa mkubwa kuhusiana na huduma hii ya bima ya afya. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa kutosha, ili waweze kujiunga na bima ya afya na kuweza kupata huduma nzuri?

SPIKA: Majibu ya swal hilo, Mheshimiwa Naibu waziri, tafadali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli, sasa hivi tuna takribani asilimia 34 ya Watanzania ambao wapo katika mfumo wa bima na tunatambua kwamba Serikali imeendelea kuboresha sekta ya afya na huduma zimezidi kuboreshwa, lakini uwezo wa wananchi kugharamia

matibabu umekuwa ni moja ya changamoto. Sisi kama Wizara tumeendelea kujikita kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa umma na tumeendelea kufanya uhamasishaji na tunajaribu kuja na vifurushi vipya ambavyo vinaweza vikajibu baadhi ya hizi changamoto za uwezo wa wananchi kuweza kugharamia matibabu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alikuwa katika mikoa ya Kusini katika kuhamasisha fao jipya la washirika ili hawa wakulima ambao wako katika mazao ya mkakati basi na wao waweze kupata *cover* ya bima hii ya afya. Sisi kama Wizara tutaendelea kufanya hivyo kuhakikisha kwamba jamii nzima ya Watanzania wanakuwa katika mfumo wa bima ya afya.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mlinga, nilikuona.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wananchi wengi hasa wa Ulanga wamekuwa na muamko mkubwa wa kujiunga na *CHF*liyoboreshwa, lakini wamekuwa wakilipa hela wanapoenda hospitali huduma zimekuwa haziridhishi, na hii inatokana na usimamizi mbovu wa *CHF* iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali mwezi Aprili, 2018 imetoa mwongozo kuwa mtumishi atakayepangiwa kuwa *CHF Manager* asiwe na majukumu mengine yoyote, lakini huu mwongozo umekuwa haifuatwi. Je, kauli ya Serikali ni ipi kwa watumishi hawa wanaopangiwa kuwa Mameneja wa *CHF*, lakini wanapangiwa na majukumu mengine?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri. *CHF* iliyoboreshwa ina matatizo mahali pengi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba, mfumo huu wa *CHF* umekuwa na changamoto na sisi kama

Serikali tumeiboresha, kuongeza mafao, zamani CHF ilikuwa unapata huduma katika kituo kilekile ambacho ulikatia, lakini sasa hivi unaweza kwenda mpaka katika ngazi ya mkoa. Hili tunalipokea, hii changamoto ambayo Mheshimiwa Goodluck Mlinga ameitoa kwenda kuboresha mfumo wa usimamizi wa CHF iliyoboreshwa ili iwe na matarajio na makusudio ambayo yamelenga.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo sasa hivi mwelekeo wa Serikali ni kwenda katika *One National Health Insurance Scheme* kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunakuwa na bima moja ya afya kwa wananchi wote. mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tutakapoleta muswada huo Bungeni, basi mtusaidie kuunga mkono.

SPIKA: Labda niseme neno moja katika hatua hii, ni kwamba wenzetu Serikalini kama kuna jambo moja tunalisubiri kwa hamu Watanzania kabla ya uchaguzi wa mwakani ni uwezekano wa kupatikana kwa huduma ya afya kwa wote. Mimi nawaomba mfanye kazi usiku na mchana tufike mahali tupate kitu kinachoitwa huduma ya afya kwa wote, ili iwe ndio zawadi kubwa ya Mheshimiwa Rais wetu Magufuli kwa Wananchi katika kumalizia miaka mitano. *(Makofi)*

Kama Wabunge tumeshapeleka *group* Ghana kuangalia wenzetu wanafanyaje, tumeshapeleka *group* la Wabunge Rwanda kuangalia wanafanyaje, kwa hiyo tuko katika kusikilizana kwa maana ya Bunge na Serikali. Tunawaombeni sana jambo hili lipate msukumo wa kipeke yake ili Watanzania wapate huduma ya afya kwa wote. *(Makofi)*

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani kwa niaba yake Mheshimiwa Selasini.

Na. 66

Serikali Kutowalipa Wananchi kwa Wakati

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. AIDA J. KHENANI)
aliuliza:-

Kumekuwa na utaratibu wa Serikali kuchukua maeneo kwa wananchi na kuahidi kuwalipa, lakini huchukua muda mrefu kuwalipa.

Je, Serikali haioni kuwa kufanya hivyo ni kuwanyima wananchi haki yao ya msingi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa fidia hufanyika kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria Namba 5 ya mwaka 1999. Sheria hizi zinaelekeza kwamba pindi Serikali au mamlaka nyingine inapotwaa maeneo ya wananchi, wanatakiwa kulipa fidia stahiki, kamili na kwa wakati. Pamoja na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 Serikali ilitunga Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Namba 7 ya mwaka 2016 ambayo imeelekeza kuwa pindi uthamini unapofanyika waliothaminiwa mali zao wanapswa kulipwa ndani ya miezi sita. Baada ya miezi sita tozo yaani *prevailing interest rate in commercial banks* inapaswa kuongezwa kwenye malipo ya madai ya fidia husika. Aidha, baada ya kupita kwa kipindi cha miaka miwili toka uthamini wa awali ufanyike, sheria inaelekeza pia, uthamini wa eneo hilo utafanyika upya.

Mheshimiwa Spika, licha ya taratibu za ulipaji wa fidia kuwekwa wazi katika sheria, kumekuwepo na malalamiko

kutoka kwa wananchi katika maeneo mbalimbali kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya fidia. Katika kutatua changamoto hizo Wizara imeandaa mwongozo unaozitaka taasisi zote zinazotaka kuchukua mali za wananchi kuwasilisha uthibitisho wa uwezo wa kulipa fidia kabla ya kuidhinishiwa kwa taarifa za uthamini wa mali unaotarajiwa kuchukuliwa. Aidha, mwaka 2016 Wizara ilizindua Mfuko wa Fidia ya Ardhi utakaosaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza katika ulipaji wa fidia. Mfuko huo umepewa jukumu la kuratibu malalmiko ya ulipaji fidia na kusimamia malipo yote ya fidia yanayofanywa na watu au taasisi binafsi, ili kuhakikisha kuwa viwango vinavyotumika ni vile vilivyokubaliwa kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa changamoto ya ucheleweshaji wa malipo ya fidia imepatiwa ufumbuzi kwa kiasi kikubwa. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa changamoto hii inafikia mwisho ili kuondoa usumbufu usio wa lazima kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Naibu Waziri pamoja na Waziri kwa jinsi ambavyo wanasimamia masuala mbalimbali ya Wizara hii vizuri, lakini pia nishukuru kwa haya majibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya swali hili bado changamoto zipo, bado kuna watu wanaokiuka huu mwongozo wa Wizara. Sasa ningependa kujua, Wizara iko tayari kufanya utafiti ili kujua ni maeneo gani katika nchi hii, Mikoa gani, Wilaya zipi ambazo bado taasisi za Serikali, watu binafsi wanakiuka mwongozo huu wa Wizara na kuchukua hatua stahiki ili kuondoa hii kero kwa Wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ziko taasisi, ziko Halmashauri ambazo pia hazifuati utaratibu wa namna ya kuchukua maeneo ya wananchi. Kwa mfano katika jimbo langu, Kata ya Kirongo, Samanga, Kijiji cha Kiwanda, eneo la Mteri, Mkurugenzi alikwenda kuchukua ardhi ya wananchi

ili kupata eneo la kujenga Ofisi ya Wilaya, lakini amewaacha wananchi katika malalmiko makubwa sana kwa sababu, hakuwahusisha kijiji, kata wala Halmashauri.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari ukipata nafasi uje Rombo ili twende pale tusaidie kutatua hili tatizo ili kuondoa hayo malalamiko kwa wananchi?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angeline Sylvester Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameongelea habari ya taasisi ambazo zinakiuka utaratibu, kwanza nipokee shukrani ya pongezi zake kwa niaba ya Waziri kwa Wizara, lakini pia nijibu swali lake ambalo ameongelea taasisi ambazo zinakiuka utaratibu kwa kukiuka.

Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba pale ambapo inatokea taasisi yoyote au watu binafsi wanapotwaa maeneo kwa kukiuka utaratibu au mwongozo tulioweka tunaomba tupate taarifa mapema ili tuweze kuichukulia hatua kwa sababu si rahisi kuweza kujua kwamba wapi na wapi wamekiuka kama hatukuletewa taarifa. Kwa hiyo, mimi naomba hilo liweze kufikishwa ili tuweze kulifanyia kazi. Nitoe rai tu kwa taasisi zote kuzingatia taratibu na miongozo iliyowekwa katika utwaaji wa maeneo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amesema baadhi ya Halmashauri kutozingatia utaratibu wa kutwaa maeneo na akatolea mfano eneo la Kironga Somanga kule kwake.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Halmashauri zote na tumeishatoa utaratibu, ni marufuku kutwaa ardhi ya mwananchi yoyote kwa sasa kama hakuna fidia ya kulipa. Kwa hiyo ni lazima kwanza fidia ipatikane ndipo uweze kutwaa ardhi, kwa sababu tumekuwa na changamoto nyingi kuna watu wengi wanadai fidia kutokana tu na taratibu ziliikiukwa katika kuchukua maeneo. Kwa hiyo sasa hivi

tumesema hatutaki kuongeza migogoro, unapotaka kutwaa ardhi ya eneo lolote lazima taratibu zizingatiwe na lazima kuwa na mazungumzo na wahusika wenye ardhi.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Flatei Massay.

Na. 67

Hitaji la Baraza la Ardhi Wilaya ya Mbulu

MHE. FLATEI G. MASSAY aliuliza:-

Serikali iliahidi kuanzisha Baraza la Ardhi la Wilaya ya Mbulu. Aidha, wataalam wa Serikali walifika Mbulu na kukabidhiwa majengo kwa ajili ya Baraza hilo katika Mji wa Dongobesh na Mheshimiwa Mbunge akachangia shilingi milioni tatu za kuongeza miundombinu.

Je, ni lini Baraza la Ardhi la Wilaya ya Mbulu litaanzishwa?

SPIKA: Bado tupo Wizara ya Ardhi, Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Mabula majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tuna jumla ya Mabaraza 97 ambayo yameundwa, ambapo kati ya hayo Mabaraza 53 yanatoa huduma na Mabaraza 44 likiwemo Baraza la Mbulu hayajaanza kutoa huduma kutokana na changamoto za uhaba wa rasilimali watu. Ili Baraza liweze kuanza kufanya kazi linahitaji kuwa na angalao Mwenyekiti mmoja, Katibu Muhtasi, Msaidizi wa Kumbukumbu, Msaidizi wa Ofisi, Dereva na Mlinzi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali imeipatia Wizara Wenyeviti 20 ambao ni wajiriwa wapya. Wenyeviti tisa kati ya hao ni kwa ajili ya kuongeza nguvu katika maeneo hayo yaliyoelemewa kwa wingi wa mashauri katika Wilaya za Mbulu, Sumbawanga, Kibondo, Kigoma, Temeke, Bukoba, Mwanza, Musoma na Ulanga. Wenyeviti 11 kwa ajili ya mabaraza 11 ambayo hayana Wenyeviti katika wilaya za Ukerewe, Maswa, Kilosa, Same, Kyela, Shinyanga, Lindi, Iramba, Nzega, Lushoto na Tunduru. Taratibu za mafunzo ya awali zinafanywa ili Wenyeviti hawa waweze kupangiwa vituo na kuanza kazi katika Mabaraza hayo ambayo yana uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba Baraza la Mbulu linaanza kufanya kazi mapema iwezekanavyo, Wizara imeshatuma barua kwenda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara kupata mapendekezo ya wananchi wenye sifa, ili Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi aweze kufanya uteuzi wa Wazee wa Baraza la Ardhi na Nyumba kwa Wilaya ya Mbulu.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zitakazopata Wenyeviti wapya wa Mabaraza kutuma mapendekezo ya Wajumbe wa Mabaraza kwa wakati, kila wanapotakiwa kufanya hivyo, ili wananchi wasikose huduma kwa kukosekana Wajumbe wa Baraza. Aidha, Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanashauriwa kuangalia uwezekano wa kutoa maeneo ya ofisi kwenye majengo yaliyo katika hali nzuri ili kurahisisha uanzishwaji wa Mabaraza katika Wilaya ambazo Mabaraza hayajaanza kazi.

SPIKA: Mheshimiwa Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisiposhukuru kwa kweli kwa utayari wa Serikali kuanzisha Baraza la Ardhi la Wilaya ya Mbulu.

Mheshimiwa Spika, lakini bado, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameonesha katika majibu yake ya msingi

kwamba kuna changamoto hizi za watumishi na kwa kuwa wananchi wa Mbulu bado watakuwa wanakwenda Babati ambaki ni mbali kwa kutafuta hiyo huduma. Je, ni lini sasa ataanzisha Baraza hili ili wananchi hao wasisafiri umbali mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wataalam walishakuja kuangalia maeneo ya kuanzisha Baraza hilo na tumeshawapa na jengo na kwa kuwa Wilaya ya Mbulu ni kubwa. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuja kuangalia na kuona eneo gani sahihi la kuanzisha barabara hilo?

SPIKA: Ahsante sana kwa maswali hayo, Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameuliza ni lini Baraza hili litaanzishwa. Katika majibu yangu ya msingi nimesema tayari Serikali imeshatupa Wizara Wenyeviti 20 ambao watapunguza kero katika baadhi ya Mabaraza ambayo hayakuwa na Wenyeviti wa kutosha, lakini pia kuna wale ambao hawakuwa na Wenyeviti kabisa watapelekwa. Kwa hiyo, mimi nimesema kwamba tayari Wenyeviti wapo, wanachosubiri kufanya sasa ni kupata tu maelekezo ya awali (*induction course*) kidogo ili waweze kwenda kufanya kazi zao, wakati wowote Baraza litaanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza kwamba Baraza hilo litawekwa wapi. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda katika eneo husika kwanza kujiridhisha na jengo lililoandaliwa, lakini pia na eneo lililopo. Kwa hiyo nitafika Mbulu ili kuweza kuona eneo sahihi ni lipi ambalo tutaweka baraza na wananchi hawatapata usumbufu.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Devotha Minja.

Na. 68

Migogoro ya Wakulima na Wafugaji Morogoro

MHE. DEVOTHA M. MINJA aliuliza:-

Migogoro ya wakulima na wafugaji katika Wilaya za Mvomero na Kilosa Mkoani Morogoro inaendelea kugharimu maisha ya watu, mifugo pamoja na uharibifu wa mazao.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kutafuta suluhu ya kudumu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo bado tupo Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na migogoro ya matumizi ya ardhi katika Wilaya za Mvomero na Kilosa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri husika imekuwa ikichukua jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya vijiji na Wilaya kwa ajili ya kuainisha matumizi mbalimbali ikiwemo suala la kilimo na ufugaji; kupima mipaka ya vijiji na kuiwekea alama za kudumu; kupima vipande vya ardhi za wananchi na kuwapatia hati za hakimiliki za kimila, lakini pia kubatilisha miliki za mashamba yasiyoendelezwa na kuyapangia matumizi mengine na kufanya ziara za mara kwa mara katika maeneo yenye migogoro ili kuyapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo Wizara inaelekeza mradi wa majaribio ya kuwezesha umilikishaji wa

ardhi ya vijiji (*Land Tenure Support Program*) katika Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi. Mradi huu unatarajiwa kusambaa (ku-*scale up*), katika Wilaya zingine za Mkoa wa Morogoro zikiwemo Wilaya za Mvomero na Kilosa. Lengo la kukamilika kwa kazi hii ya uandaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, upimaji wa mipaka na vijiji na upimaji wa vipande vya ardhi na kukamilisha kumilikisha wananchi na hivyo kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wananchi katika Wilaya ya Kilosa na Kilombero kuendelea kuheshimu Sheria za Ardhi, hususan kufuata mipango ya matumizi ya ardhi iliyoainishwa na hivyo kuondoa uwezekano wa kuibuka kwa migogoro isiyokuwa ya lazima.

SPIKA: Mheshimiwa Devotha Minja ameridhika.

MHE. DEVOTA MINJA: Hapana Mheshimiwa Spika bado.

SPIKA: Una swali la nyongeza? Endelea.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji katika Mkoa wa Morogoro umetokana hasa na kutokuwepo na mipango mizuri ya matumizi ya ardhi. Maeneo yanayofaa kwa kilimo wamepewa wafugaji na maeneo yanayofaa kwa wafugaji wamepewa wakulima. Je, Serikali inampango gani kuainisha upya maeneo hayo ili kuwapa wananchi na kuondoa hii migogoro? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa migogoro hii ya wakulima na wafugaji mingi imechangiwa na Watendaji wa Ardhi katika Vijiji na Kata: Serikali haioni sasa kuna haja ya kuwalipa fidia wananchi ambao wamebaki na makovu kutokana na migogo hii? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameongelea habari ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo na amesema kwamba maeneo ya ufugaji wamepewa wakulima na maeneo ya wakulima wamepewa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimdhibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba upangaji wa matumizi ya ardhi haufanywi na Wizara. Upangaji wa matumizi wa ardhi, mdau wa kwanza ni mwananchi wa eneo husika. Tunapokuja *ku-facilitate* lile zoezi la upangaji, wananchi wenyewe wanakuwa wameshaainisha maeneo yao kwa ajili ya ufugaji na maeneo kwa ajili kilimo. Kwa hiyo, kinachofanyika pale ni kuweka mipaka kwa maana ya kwamba maeneo ya ufugaji yafahamike na maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pale inapotokea vurugu, ni kati ya watumiaji wa ardhi wanapokiuka makubaliano ya awali, kwamba mfugaji anatoka kwenye eneo lake la ufugaji anakwenda kwenye maeneo ya kilimo; au mtu wa kilimo anakwenda kulima kwenye maeneo ya wafugaji. Kwa hiyo, mgogoro mkubwa ulioko hapa ni kwa watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai tu katika maeneo yote yenye migogoro kati ya wakulima na wafugaji na ambapo mpango wa matumizi bora ardhi umepangwa, waheshimu maamuzi ambayo wameyafikia wao wenyewe na yanakuwa yameingia katika mpango wa matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, hili ni jambo la watumiaji ardhi ambapo tunasisitiza waheshimu pale ambapo haijafanyika. Kwa wale ambao hawajapanga matumizi bora ya ardhi, basi nitoe rai tu kwamba mpango huo ufanyike na Wizara ipo tayari kwa ajili ya kuratibisha zoezi hilo ili angalau wananchi wote waweze kuwa na maeneo yao yaliyopangiwa matumizi kuepuka hii migogoro na inapotokea wanakiuka utaratibu, basi sheria ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, swali lingine amesema Watendaji ambao wanachangia pengine kupata migogoro na licha

ya hivyo kunakuwa na fidia za watu, niseme kwamba Watendaji hao kama wapo, ndiyo maana Wizara kuna baadhi ya Watendaji imewasimamisha kazi na wengine wameondolewa kwa kukiuka maadili ya utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, suala la kusema kwamba kunakuwa na suala la kulipa fidia, hilo ziwezi kulitolea maamuzi sasa kwa sababu hatujawa na changamoto nalo kama Wizara na kuangalia hasa changamoto hii imetokana na nini? Kwa Watendaji waliokiuka taratibu zao, hatua zinachukuliwa. Sasa hivi tunamshukuru Mungu kwamba angalau wameanza kuwa na maadili kiutendaji tofauti na siku za nyuma.

SPIKA: Ahsante Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha. Nashukuru tuishie hapo. Kuhusu wageni, nina wageni 30 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni marafiki zake anaoshirikiana nao kwenye shughuli za kimaendeleo Wilayani Rungwe Mkoani Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Enzi Seme. Wageni wa Naibu Spika, simameni. Karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wabunge wengine wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi, ambaye ni mwanafunzi wa *Ph.D* katika Sheria za Kodi za Kimataifa Beijing – China, Ndugu Joseph Laizer. Karibu Laizer popote pale ulipo. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Keissy ambao ni watoto wake, Ndugu Samira Keissy na Ndugu Mohamed Humud, kutoka Jimboni kwake Nkasi. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni wajasiriamali kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Balozi Eliza Kola. Karibu sana. Wapo pale. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Phillip Mulugo ambao ni wadogo zake kutoka Songwe, Ndugu Fabian Mulugo na Ndugu John Zawiba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanane wa Mheshimiwa Hamida Abdallah, ambao ni Madiwani watatu wakiongozwa na Wavuvi wa Mkoa wa Lindi. Ooh, karibuni sana Madiwani kutoka Lindi. Naambiwa Madiwani hawa kabla walikuwa ni Madiwani wa CUF na sasa ni wa Chama cha Mapinduzi. Wamekuja kufuatilia suala la nyavu ndogo ndogo zile za uvuvi wa wale dagaa wadogo wadogo wale. Mheshimiwa Waziri Mifugo na Uvuvi uwasikilize vizuri, warudi na majibu mazuri hawa. Wanasema wao sasa wameanza kazi na watarudi na majibu huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Ndugu Lutusyo Mbeleka ambaye ni ndugu yake kutoka Tukuyu Mkoani Mbeya. Karibu, yule pale. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo; Wawakilishi wanne kutoka Chama cha Wazazi wa Watoto wenye Ulemavu wa Mtindio wa Ubongo, Akili na Viungo Tanzania CHAWAUMAVITA. Karibuni sana pale mlipo. *(Makofi)*

Wanafunzi 120 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi Nzuguni ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Ndugu Suleiman Bakobile. Aaah, wale pale. Karibu sana watoto wetu, mnapendeza kweli kweli. Karibuni watoto wa Nzuguni. *(Makofi)*

Wanafunzi 42 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara, ni majirani zetu kutoka hapa Dodoma CBE. Wale pale CBE, karibuni sana, kasanieni sana masomo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo ndugu yetu mmoja, Dkt. Jacob Lubuva ameandika kijitabu kizuri sana kinachohusu Utawala wa Awamu ya Tano, lakini pia kipekee kazi ambazo zimefanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika uwanja wa rushwa; *"Corruption in Agony."* Rushwa ikiwa mahututi, *contemporary Nyerere of our time*. Kitabu hiki kinapatikana pale panapouzwa magazeti, ni kitabu kizuri sana. Kimeandikwa kwa ufundi mkubwa, nawashauri Waheshimiwa Wabunge

tukipita pale tuweze kukinunua kitabu hiki kwa ajili ya rejea zetu. Ni pale kwenye magazeti, tunaponunua magazeti siku kwa siku.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata habari kwamba Mheshimiwa Kunti amejunga nasi kwamba yupo hapa leo, naomba usimame Mheshimiwa. Aaah! Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunakupa pole sana kwa yote yaliyokupata, mwachie Mwenyezi Mungu, tutakukumbuka na sisi katika maombi, ni mitihani mikubwa umepata. Karibu tena Bungeni, tunafurahi kuwa pamoja nawe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Jana nilikuwa naangalia vyombo vya habari nikamwona Mkuu wa Mkoa wa Mara akiwa Tarime Vijijini akihangaika na kushangaa sana jinsi ambavyo kwa miaka mitatu iliyopita Halmshauri ya Tarime Vijijini wamepewa na mgodi ule wa *North Mara* zaidi kidogo ya shilingi bilioni tisa na hazijulikani zimefanya kazi gani.

Nikasema niwaambieni Wabunge wangu, hivi inakuwaje? Kwa sababu sisi Wabunge ni Madiwani pia. Inawezekanaje hela nyingi kiasi hicho kwenye Halmshauri zinachezewa ovyo ovyo na Halmshauri yenyewe ni ya Chama chake Mheshimiwa Heche? Tukija hapa sisi ni mafundi wa kuwaonyeshea vidole Mawaziri, kumbe sisi wenyewe huko mambo yetu yaani ni taabani. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Heche, hebu aende akashughulikie hiyo boriti kwanza. Hiyo boriti ni kubwa sana kwenye jicho lake. Vinginevyo, kampeni ya mwakani ni nyepesi tu. Shilingi bilioni tisa ipo wapi, bilion tisa iko wapi; utajibu nini? Tumeona haya huko huko, kama siyo kweli atatueleza siku moja. Hela nyingi sana hii kwa Halmshauri yoyote. Nyie Madiwani mpate shilingi bilion tisa; Kongwa kule nipate hizo, mimi aah, wala Serikali sihitaji chochote cha kwenye bajeti yao, namaliza mengine yote bila tatizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi wakati nakuja huku nilikutana na Mheshimiwa Mkuchika, Waziri; sasa siku zote tukikutana tunasalimiana, lakini leo hataki kunisogelea, ananisalimia kwa mbali, anafanya hivi, ananipungia. *(Kicheko/Makofi)*

Kila nikimsogelea anarudi nyuma anafanya hivi, sasa nikasema sijui hii maana yake nini! Nikaona nijjulize kwenu, huyu Mheshimiwa leo kulikoni?

MBUNGE FULANI: Tano bila!

SPIKA: Baada yake nikakutana na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, yeye ananifanyia namna hii (alionesha kama mtu anayeendesha pikipiki). Sasa wewe Mheshimiwa Nchemba unaendesha bodaboda? Kwa kweli juzi tumepigwa! *(Kicheko/Makofi)*

Leo asubuhi namuuliza mwenzangu Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi juzi, ilikuwaje? Ananiambia acha kabisa, sikulala kabisa! Mimi baada ya dakika arobaini, zile goli tano, nikafunga na tv nikaenda kulala. Maana haiwezekani hata kuangalia tena. Ila tumegundua vijana wetu kule baridi bwana. Hali ya kule ni baridi sana! *(Kicheko/Makofi)*

Sasa na wenzetu kwa vile hawawezi joto, tumepanga mechi ya Dar es Salaam ichezwe kuanzia saa nane kamili. Kwa joto lile la Dar es Salaam, Waarabu wataipata. *(Kicheko/Makofi)*

Mwisho, jamani si tulikubaliana uzalendo! Sasa Yanga mbona uzalendo hamna! Wameshangilia kweli kweli!

MBUNGE FULANI: Ndiyo maana tumetoa pole. *(Kicheko)*

SPIKA: Kwa hiyo, nawaasa ndugu zangu wa Yanga, uzalendo jamani. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, basi tuendelee na mengine. Mheshimiwa Hongoli nimekuona.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nasimama kwa Kanuni ya 69(1) nikiomba hoja iliyopo Mezani iweze kuahirishwa kwa muda tuweze kujadili jambo linaloendelea Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Njombe kuanzia mwanzoni mwa mwaka huu Januari, Halmashauri wa Mji wa Njombe watoto watatu wameshauawa na baada ya hapo wamehamia kwenye Halmashauri yangu, *Njombe DC* kwa maana Jimbo la Lupembe. Mpaka ninapooonga hivi, watoto wanne wameshauawa, watoto watatu kutoka kwenye familia moja na mtoto mmoja katika Kijiji cha Matembwe aliuawa siku ya Ijumaa na kuzikwa Jumamosi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mauaji hayo, lakini pia kuna taharuki kubwa sana na watu wamekuwa na hasira kubwa sana kwa sababu shughuli zote za kiuchumi katika Mkoa wa Njombe hazifanyiki, akina mama kila siku asubuhi wakiamka wanatakiwa kwenda kuwasindikiza watoto shuleni na mchana kwenda kuwachukuwa na wengine kwenda kuchukuliwa jioni. Kwa hiyo, mambo yote yamesimama.

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, kutokana na hiyo hasira, tayari kuna mauaji yameshajitokeza kwenye baadhi ya Halmashauri kwa mfano juzi wiki iliyopita Ludewa wameua mtu mmoja ambaye alikuwa anadhaniwa pengine ni kati ya watu ambao wanatafuta hao watoto wadogo wa chini ya miaka kumi, lakini kumbe alikuwa ni mtu ambaye hakuwa anashughulika na shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile wameshaua Wagingo'mbe kwa dhana tu kwamba inawezekana watu wanajihusisha na hayo mauaji. Pia kuna watu kadhaa wamejeruhiwa kwenye maeneo yetu; kwenye Jimbo langu wiki iliyopita kuna mtu mmoja alinusurika kuuawa na juzi

imetokea kwenye Kijiji cha Matembwe, mtu mmoja amenusurika kuuawa. Kwa hiyo, hali ni mbaya sana katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, kuna watu sasa wamejitokeza ambao ni kama wanaongeza hasira, wanahamasisha, wanatuma picha kwenye mitandao ikionyesha watoto wameuawa. Kwa mfano, Ijumaa walituma kwenye mitandao picha inayoonyesha miili ya watoto takribani zaidi ya 20 hivi wameludikwa kwenye chumba kimoja na wanasema kwamba mauaji haya yametokea Njombe.

Mheshimiwa Spika, vile vile juzi na jana wametuma kwenye mtandao wakionyesha watoto watano wameuawa na wametupwa kwenye shimo limechimbwa na wako tayari kufukiwa, wanasema kwamba ni Mkoa wa Njombe. Nasi Wabunge wa Mkoa wa Njombe tumepeleleza kama kuna mauaji yametokea hivi karibuni ya idadi ya watu hiyo, taarifa zinaonyesha kwamba hakuna idadi iliyotokea zaidi ya wale watoto watatu waliouwawa Njombe Mjini na hawa wanne waliouawa kwenye Jimbo langu na mmoja aliyejeruhiwa Njombe Mjini na hawa waliouawa kutokana kudhaniwa.

Mheshimiwa Spika, naomba angalau kwa dakika 20 kwa idhini ya kiti chako, Bunge lako liweze kujadili juu ya hali inayoendelea katika Mkoa wa Njombe, maana leo ipo Njombe, kesho inaweza kuendelea na Mikoa mingine na nchi nzima ikawa iko kwenye taharuki na hasira kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitoe hoja angalau kwa dakika 20 tuweze kuijadili hoja hii na Serikali pengine iweze kuchukua jukumu la kuhakikisha kwamba mauaji haya hayatokei.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Eh! Hoja imetolewa na sijawahi kuona hoja imeungwa mkono kama hii. Imeungwa mkono sana. *(Makofi)*

Kabla hatujaamua, nimpe dakika mbili Mbunge mmojawapo wa Njombe, nimekuona Mheshimiwa Deo Sanga na leo umepiga suti, ebu tupe kidogo, nini kinaendelea huko pia? Karibu Mheshimiwa.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia nini kinaendelea Njombe. Kama alivyosema Mheshimiwa Hongoli, hali ya Njombe ni tete na imeleta taharuki kubwa sana na baadhi ya wageni wakifika katika maeneo mbalimbali, inaonekana hao wamekuja kuteka watoto na kuwaua.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunavyozungumza, baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wamekamatwa katika Mji wa Makambako katika Wilaya ya Njombe. Wafanyabiashara wakubwa wana siku nne ndani hivi sasa na hatujui nini kinachoendelea. Wapo wafanyabiashara wengine ambao walikuwa ni wakazi wa Makambako, walihama wakawa wapo Dar es Salaam, ni wawekezaji wakubwa, wamerudi kuwekeza katika Mji wa Makambako, hivi sasa wamekamatwa.

Mheshimiwa Spika, watu waliokamatwa mpaka sasa wako takribani 10, wafanyabiashara wale wakubwa ambao kuna baadhi yao wana viwanda na watumishi zaidi ya 200. Kwa hiyo, shughuli sasa zimesimama na baadhi ya watu wengine wamewekeza hapa Dodoma pia, wafanyabiashara hao wakubwa. Taharuki hii imechochewa sana na baadhi ya watu ilipoonekana kwamba baadhi ya wafanyabiashara wamo.

Mheshimiwa Spika, sasa wafanyabiashara hawa, dola nadhani wanaendelea na shughuli zao, lakini ombi ambalo nataka kulizungumzia hali ya Mji wa Makambako na Njombe kwa kweli siyo nzuri. Mpaka sasa shughuli mbalimbali za watu

zimesimama, hazifanyiki; ukienda kule Lupembe kama ambavyo amesema Mheshimiwa Hongoli, Mji wa Lupembe katika Wilaya Njombe ndiyo unaozalisha kwa wingi zao la mbao. Kwa hiyo, watu wanapokwenda kununua mbao kule kama alivyosema, juzi kuna watu wamekwenda na bodaboda, walipofika mahali wamesimama, watu wakasema hao hao! Watu wakakimbia wako nao. Bahati nzuri watu wakampigia simu Mheshimiwa Mbunge, Mbunge akasema, hapana msiwaue.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hali ni tete, nadhani kuwe na tamko la Serikali ni namna gani hali ya Njombe iweze kutulia kutokana na hali hiyo. Hata Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani alipokwenda kuongea na watu wa Njombe akiwepo yeye mwenyewe, akiwa kwenye ukumbi anafanya mazungumzo na waganga mbalimbali na wadau wa Njombe, nje kukawa na watu wanapita wawili wakavamiwa na ndio mkasikia yalipigwa mabomu na walikuwa ni wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa mwanafunzi amekwenda kwa mwanafunzi mwenzake kumsalimia, alipofika pale nyumba ile kuna watoto, mwanafunzi mwenzake hakumkuta, alipotoka watu wakasema ametoka kufanya nini? Wakampigia simu yule mama mwenye nyumba, mama yule alikuwa shambani, wakamuuliza kuna mtu ameingia hapa ni mtoto wako? Akasema hapana, basi amekuja kuiba watoto, wakamkamata wakataka kumuua na ndio maana ukasikia yalipigwa mabomu ili kumnusuru.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hali ya Njombe ni tete shughuli hazifanyiki.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Kabla Spika hajasema sasa tufanyaje, nadhani kuna umuhimu wa kuisikiliza Serikali. Nadhani kama tutakubaliana kwamba mngepanga muda, tutawasiliana lini mje mtoe taarifa fulani maalum ya Serikali

kuhusu jambo hili, hatutaki kuwakurupusha kwa haraka haraka, sijui lakini mnavyoona. Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali, jambo hili kama ulivyolisikia na lilivyoeelezwa ni jambo zito na linachukua taswira nzito ndani ya Taifa na tunadhani kwamba sisi kama Serikali ili tuweze kutoa maelezo ya kina ni bora kiti chako kitupe nafasi tutayarishie Kauli ya Serikali na tuilete ndani ya Bunge lako haraka, Bunge lako liveze kujua hatua kubwa ambayo pia Serikali imeshachukua katika jambo hili, lakini na kuwapa *comfort* Watanzania na hasa wenzetu wananchi wa Mkoa wa Njombe ili waweze kuwa na amani na kuona kuwa Serikali pia iko kazini.

Mheshimiwa Spika, ukiridhia basi sisi kama Serikali tuko tayari na tutatekeleza jambo hilo.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge ni kweli jambo hili ni kubwa, linahuzunisha na linasikitisha sana, nakubaliana na ushauri uliotolewa na Serikali kabla hatujamaliza Bunge hili, mwisho wa wiki hii tupate maelezo kutoka Serikalini ya nini kinachoendelea huko Njombe, Tukishapata maelezo hayo, ndio kama kuna neno lingine tutaona namna gani ya kufanya.

Kwa hiyo, Serikali ijiandae kabla hatujamaliza shughuli zetu hapa wiki hii mwishoni tupate taarifa hiyo, lakini kwa kutangulia Bunge hili linawapa pole sana wazazi wote walioguswa na vifo vya watoto. Tunaendelea kuihimiza Serikali kwa kweli ipo haja vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuhamia huko Njombe ili kuhakikisha jambo hili linakomeshwa kabisa. Maana kama kuna jambo halikubaliki ni huu ukatili kwa watoto. Ni jambo la kusikitisha sana, mtoto ambaye ni malaika wa Mungu anauawa hivi hivi bila sababu za msingi. Kwanza linaipaka matope nchi yetu kimataifa, kwamba kuna watu nchi fulani wanaua watoto, hili jambo halipendezi hata kidogo.

Basi ahsante sana. Kwa hatua hii, naomba nimwite Mheshimiwa Zungu aje aendelee na shughuli za hapa mezani. *(Makofi)*

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu
Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018 na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda,
Biashara na Mazingira Kuhusu Shughuli za
Kamati kwa 2018**

MWENYEKITI: Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA MIUNDOMBINU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Miundombinu juu ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari, 2018 hadi Januari, 2019. Taarifa imegawanyika katika maeneo makuu matatu; eneo la kwanza ni utangulizi, la pili ni sehemu ya uchambuzi na sehemu ya tatu inahusu maoni ya Wajumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taarifa imegawiwa kwa Wabunge wote naomba nijielekezi moja kwa moja kwa moja katika Sehemu ya Tatu ambapo inahusu maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu yaliyotolewa wakati wa shughuli za Kamati kuanzia mwezi Januari, 2018 hadi Januari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; katika kipindi cha miaka mitatu ya Fedha, yaani Mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019, Serikali imeonesha kuzingatia ushauri wa Kamati kwa kuongeza fedha kwa ajili

ya kuendeleza na kuimarisha miundombinu nchini. Mwaka wa fedha 2016/2017, ilitenga shilingi trilioni 4.3, mwaka 2017/2018, ilitenga shilingi trilioni 4.5 na mwaka 2018/2019 Serikali ilitenga shilingi trilioni 4.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele na kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa miundombinu nchini. Hata hivyo, pamoja na shabaha nzuri ya Serikali katika masuala ya miundombinu, Kamati inasisitiza fedha kutolewa kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka malimbikizo la madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Bandari Tanzania; katika Sekta ya Uchukuzi, Mamlaka ya Bandari Tanzania ndiyo Mamlaka iliyokasimiwa jukumu la kusimamia bandari nchini, mamlaka hii inayo miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa bandari ambapo kwa sasa Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua ya kuboresha kwa kufanya ukarabati wa bandari kama vile Bandari ya Dar es Salaam na Mtwara. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kubakisha angalau asilimia 40 ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake, kama vile, miradi ya ujenzi wa Bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara, ambayo inagharimu takribani shilingi bilioni 20 wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni takribani shilingi bilioni 270;

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuharakisha mchakato wa ununuzi wa *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Kutokuwepo kwa mtambo wa kupima kiasi cha mafuta kunasababisha kutokujua uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia Bandari ya Dar es Salaam;

(iii) Vile vile Kamati inashauri kufanyike juhudi za makusudi ili kuweza kuhamisha Gati la Mafuta lililopo kurasini (KOJ) na kujenga Gati Namba 13 na 14;

(iv) Serikali iharakishe kufanya ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile Bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Bandari za Ziwa Nyasa. Vilevile, bandari zingine zilizopewa vipaumbele ni kama vile Bandari ya Mbegani- Bagamoyo na Bandari ya Mwambani- Tanga ili ziweze kutekelezwa;

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kutoa ushauri Serikali kuharakisha ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa Dodoma, Katosho-Kigoma na Misungwi bado hayajatekelezwa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iweze kuharakisha ujenzi huo; na

(vi) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuharakisha majadiliano na wabia ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwani kukamilika kwa bandari hii kutatoa fursa nyingi za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali kulipa fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya ujenzi wa reli nchini; Serikali imeonesha nia ya dhati ya kujenga upya reli ya kati katika kiwango cha kisasa (*standard gauge*); ambapo mradi umeanza mwezi Aprili, 2017 na unatekelezwa kwa awamu tano. Katika uhalisia Tawi la kutoka Tabora- Kigoma-Uvinza-Msongati na Kaliua-Mpanda-Kalema ndilo lenye mizigo mkubwa inayotoka na kwenda nchi za jirani kama vile DR Congo, Burundi na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa ujenzi wa reli hii uzingatie kwanza maeneo yenye faida za kichumi na kipaumbele cha kwanza kiwekwe katika tawi lenye mizigo mkubwa ambalo ni Tawi la Tabora – Kigoma -Uvinza- Msongati, Kaliua – Mpanda –Kalema. Hata hivyo, bado Serikali inaambiwa izingatie kuwashirikisha wa wataalam wa ndani yaani wazawa katika ujenzi wa reli ya

kati ili kuwa na mradi endelevu pale wataalam wa nje watakapoondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Reli ya Tanzania na Zambia (*TAZARA*), *TAZARA* inamilikiwa na nchi mbili Tanzania na Zambia kwa asilimia 50 kwa 50, kwa muda sasa utendaji wa *TAZARA* umekuwa si wa kuridhisha. Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mkakati wa dhati kuinusuru *TAZARA* ili iweze kujiendesha. Moja ya mkakati uwe ni kufanya mazungumzo na Serikali ya Zambia na kufikia muafaka wa namna bora ya uendeshaji wa reli hii, ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya kurekebisha Sheria iliyoianzisha *TAZARA* Na.23 ya Mwaka 1975;

(ii) Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi pamoja na kuendelea kusaidia kulipa wafanyakazi wa *TAZARA* mishahara mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha; na

(iii) Serikali kujenga kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa, hivyo unaweza kupatia *TAZARA* mapato ya kutosha kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ndio iliyokasimiwa jukumu la kusimamia na kuendesha viwanja vya ndege nchini. Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazokabili viwanja vya ndege nchini ikiwemo migogoro ya mipaka. Hivyo Basi, Kamati inaishauri yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha inapata hati za Viwanja vya Ndege kwani Kamati imejulishwa kuwa viwanja vya ndege nane (8) vimeshapatiwa hati miliki kati ya viwanja hamsini na nane (58) vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege; na

(ii) Vile vile, kuhakikisha viwanja vingine vilivyobakia vinapimwa na kupatiwa hati miliki pamoja na uzio ili kujiepusha na uvamizi wa maeneo jambo ambalo huleta migogoro kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Ndege ya Tanzania (*ATCL*), Serikali imechukua hatua ya kufufua Shirika la Ndege la Tanzania kwa kununua ndege mpya. Ndege hizo zitakuwa kichocheo cha uchumi wa Tanzania katika kuwawezesha kupata usafiri wa ndani na nje ya nchi, hivyo kutimiza malengo na kukuza Pato la Taifa. Kamati inashauri yafuatayo:-

Moja, kuwa na mikakati mikubwa ya kitaifa ya kuhakikisha kuwa *ATCL* inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida; Pili iangaliwe kama Kampuni ya kibiashara na sio yakutoa huduma. *ATCL* ijitangaze kwenye vyombo vya Kimataifa ambavyo huonesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali. Shirika liendeleo kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ndio umekabidhiwa jukumu la ujenzi na ukarabati wa barabara kuu nchini. Pamoja na jitihada za Serikali za kujenga barabara bado kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali kama vile barabara kuharibika, matuta yasiyo na viwango, uzito uliozidi wa mizigo unaoharibu barabara na wizi wa alama za barabarani. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kukarabati baadhi ya barabara za mikoa zilizo katika hali isiyoridhisha na kutopitika hasa wakati wa mvua na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii;

(ii) Kuhakikisha inaunganisha Miji yote Mikuu na Mikoa iliyosalia kama vile Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera na Njombe-Makete- Morogoro –

Ruvuma kwa barabara za lami ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo hayo;

(iii) Kuendelea na ujenzi wa barabara za lami hasa maeneo yanayochochea uchumi wa Taifa letu kama vile maeneo yenye vivutio vya utalii, kilimo, viwanda na madini;

(iv) Vilevile kamati inashauri Halmashauri zishirikiane na *TANROADS* na *TARURA* kutenga maeneo ya kuegesha magari (*parking*) ili kuzuia magari yanayoegeshwa muda mrefu kandokando ya barabara na kusababisha uharibifu;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Viwanja vya Ndege, Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) umepewa jukumu la ujenzi wa Viwanja vya Ndege nchini. Bado kuna changamoto kubwa ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali kuhakikisha inatoa kwa wakati malipo ya fedha yaliyoidhinishwa kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, Songwe na Mtwara;

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, Serikali ijikite zaidi katika kujenga na kuendeleza viwanja vya ndege vya kimkakati ambavyo vitasaidia kukuza pato la Taifa kwani Kamati imebainika kuwa kati ya viwanja vya ndege 58 viwanja vitano ndivyo vinavyochangia pato la Taifa Serikalini;

(iii) Wakati ujenzi wa jengo la tatu la abiria (*Terminal III*) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere unaendelea, ni vema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi; na

(iv) Kuharakisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa viwanja ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara Jijini la Dar es Salaam; Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na changamoto kubwa ya msongamano wa magari barabarani. Msongamano huu wa magari umekuwa ukisababisha adha kubwa kwa jamii kwani magari yamekuwa yakitumia muda mrefu, mafuta mengi na hata kuchelewa kufika ofisini, shuleni, kwenye biashara na huduma zingine muhimu kwa wakati. Hivyo, Kamati inaendelea kushauri barabara za juu (*flyovers*) zijengwe hasa katika makutano ya barabara kuu zenye msongamano mkubwa kama vile, Magomeni, Morocco, Mwenge. Wadau kama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweza kushirikishwa kwa kujenga barabara ambazo zitatozwa tozo kwa ajili ya kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kamati inashauri kuendelea na ujenzi wa barabara zinazosaidia wananchi kufika maeneo yao bila kupita katikati ya Jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja kukamilisha barabara kutoka Goba-Madale-Wazo Hill, Goba -Kimara, Ardhi-Makongo-Goba na kadhalika. Pia barabara za mitaani (*ring roads*) nazo zifunguliwe kwa kuwekwa lami kwani zitapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano ni sekta ambayo hutegengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo Fungu 68. Katika utendaji kazi Kamati imebaini kuwa sekta hii haipewi kipaumbele katika utolewaji kwa ajili ya maendeleo ambapo fedha miradi zimekuwa ama hazitolewi kwa wakati au hazitolewa kabisa, mfano, hadi mwezi Machi, 2018 hakuna fedha yoyote ambayo ilikuwa imetolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Serikali ione umuhimu wa sekta ya mawasiliano na kutoa fedha zote zilizoidhishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Mamlaka ya Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kusimamia mawasiliano nchini, kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazotokana na ukuaji wa

teknolojia katika mawasiliano. Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

(i) TCRA iendelee kuutunza na kuusimamia Mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa mawasiliano ya simu (TTMS);

(ii) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao; na

(iii) Kuendelea kukabiliana na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake kama vile uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostahili, hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania TCRA iendelee kulisaidia Jeshi la Polisi katika kutekeleza Sheria ya *Cyber Crime* na kuwabana wahalifu na wakati wa utoaji wa leseni za Makampuni ya Simu ni vizuri pia kuweka masharti ya kulazimisha makampuni ya Simu kujishughulisha na shughuli za kijamii (*Corporate Social Responsibility*) katika maeneo yake ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) Kamati ilifanya ziara ya kutembelea minara ya mawasiliano inayojengwa kwa ruzuku ya Serikali katika mikoa kumi na mbili ya Tanzania Bara. Katika ziara hiyo Kamati ilibaini masuala mbalimbali yanayohitaji kutafutiwa ufumbuzi ili Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uweze kuimarika na kufanya kazi zake vizuri. Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

(a) Serikali kupitia na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhi hasa maeneo yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za Vijiji husika. Hii itasaidia sana kwani fedha zitakazopatikana kutokana na kukodi ama kununua eneo la mnara zitatumika

kwa ajili ya maendeleo ya wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache na baadhi ya Serikali za Vijiji kutokuambulia kitu chochote.

(b) Serikali kuhakikisha wanaweka mabango yanayoonesha ushiriki wake katika ujenzi wa minara ambayo imetoa ruzuku. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Serikali za mikoa, wilaya hadi ngazi za chini pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kwamba miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana iliyopo maeneo mengi ni kuwa minara imejengwa na makampuni binafsi yenyewe na si ruzuku iliyotolewa na Serikali.

(c) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuweka masharti na kutoa leseni kwa makampuni ya simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii wa *Corporate Social Responsibility*.

(d) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu wa uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi wote washirikiane na kulinda vifaa vyote vya minara.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta. Kutekelezwa kwa mradi huu kuna manufaa makubwa kwani kutaweza kuwepo na utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimaye kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa mradi huu kwani umekuwa ukisuasua. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi.

(b) Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kama zilivyoidhinishwa na kwa wakati ili mradi huu muhimu ukamilike.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania. Shirika hili linahitaji mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na kukabiliwa na ushindani wa soko katika sekta ya posta. Pamoja na changamoto ya mtaji pia linakabiliwa na changamoto ya madeni ya pembeni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na deni ambalo Posta inadaiwa na Mamlaka ya Mapato TRA. Takribani shilingi bilioni 26 umekuwa ni mzigo unaolielelea Shirika hili la Posta. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali ichukue jukumu la kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa wastani wa shilingi milioni 74 kwa kila mwezi fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa Shirika ili nalo liweze kujiendesha lenyewe.

(b) Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ya kufuta deni la shilingi bilioni 26 ambalo Shirika la Posta inadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

(c) Serikali iliondoe Shirika la Posta katika orodha ya mashirika yanayosubiri kurekebishwa ili liweze kutumia rasilimali zilizopo kufanya uwekezaji kwa lengo la kujiendesha kwa tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*). Shirika la Mawasiliano Tanzania linaendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya madeni ambayo yameripotwa kufika takriban shilingi bilioni 9.8. Madeni haya yanaathiri utendaji wa kazi wa Shirika hilo. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali pamoja na vyombo vyake ambavyo kwa kiasi kikubwa ndiyo wadaiwa kulipa madeni hayo kwa kuwa fedha hizo na gharama za simu hutengwa kila mwaka katika bajeti ya Wizara, Taasisi na Mashirika yao.

(b) Shirika liweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni.

(c) Serikali iweke mazingira wezeshi kwa *TTCL Corporation* kuweza kupata mkopo wa gharama nafuu kwa kuwa Shirika hili ni mali ya Serikali lazima kuwe na mpango thabiti wa kuliwezesha ili liweze kufanyakazi vizuri.

(d) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuendeleza Mkongo wa Taifa. Hili lifanyike kwa kuangalia upya utaratibu ambao umeruhusu makampuni ya simu mengine kumiliki mikongo yao sambamba na Mkongo wa Serikali kwani mikongo hii binafsi itaffisha maendeleo ya Mkongo wa Serikali na hata kuhatarisha usalama wa wananchi na usalama wa nchi kwa ujumla na kuikoshesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Miundombinu. Vilevile napenda kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya kipekee, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Engineer Isaack Kamwelwe akishirikiana na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Elias Kwandikwa. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Arch. Elius A. Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonazi. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalum wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson M. Bisile pamoja na Katibu wa Kamati Ndugu Hosiana John. Pia, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, maoni na ushauri, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019 pamoja na Maoni na Ushauri uliopo katika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imeungwa mkono.

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI
KWA KIPINDI CHA JANUARI 2018 HADI JANUARI 2019
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 117 (15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge, Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii megawanyika katika maeneo manne yaani, Sehemu ya Kwanza ambayo ni utangulizi wenye maelezo ya jumla; Sehemu ya Pili inahusu Majukumu yaliyotekelezwa; Sehemu ya Tatu inahusu Ushauri wa Kamati na Sehemu ya Mwisho ambayo ni Hitimisho.

Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii ni hawa wafuatao:-

- (1) Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb
- (2) Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb
- (3) Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mb
- (4) Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb
- (5) Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb
- (6) Mhe. Joyce John Mukya, Mb
- (7) Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb
- (8) Mhe. Susan Chogisasi Mgonukulima, Mb
- (9) Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb
- (10) Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili, Mb
- (11) Mhe. James Francis Mbatia, Mb
- (12) Mhe. Saul Henry Amon, Mb
- (13) Mhe. Ahmed Makbhuty Shabiby, Mb
- (14) Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb
- (15) Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb
- (16) Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb
- (17) Mhe. Dua William Nkurua, Mb
- (18) Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb
- (19) Mhe. Agness Mathew Michael, Mb
- (20) Mhe. Charles Kitwanga, Mb
- (21) Mhe. Rukia Kassim, Mb
- (22) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb
- (23) Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb
- (24) Mhe. Munde Abdalah Tambwe, Mb
- (25) Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati hii inamajukumu yafuatayo:-

- (a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inayoismamia;
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara;
- (c) Kufuatilia Utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inayoismamia;
- (d) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara husika; na
- (e) Kufuatilia Utekelezaji unaofanywa na Wizara kwa Mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

1.2 ***Shughuli zilizotekelezwa katika Kipindi cha Mwaka 2018/2019***

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2018 hadi mwezi Januari, 2019 , Kamati ilitekeleza majukumu yake njia ya vikao mbalimbali pamoja na ziara kama ifuatavyo:-

a) Vikao

i) Vikao vya kushughulikia taarifa za utendaji wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ambayo Kamati inaisimamia; Vikao hivyo vilihusisha taasisi na Mashirika yafuatayo; -

Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA, Shirika la Reli Tanzania-TRC, Shirika la Reli la Tanzania na Zambia-TAZARA, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA, Kampuni ya Meli Tanzania- MSCL, Mamlaka ya Usafiri wa Anga- TCAA, Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na majini-SUMATRA, Kampuni ya Ndege ya Tanzania- ATCL, Chuo cha Usafarishaji Tanzania- NIT, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Ujenzi wa Reli ya Kisasa (*Standard Gauge*) sehemu ya Dar es Salaam- Morogoro, Wakala wa Barabara Tanzania- TANROADS, *Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency-TEMESA*, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, Shirika la Mawasilino Tanzania-TTC, Tume ya TEHAMA, Shirika la Posta Tanzania-TPC;

(ii) Vikao vya kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2018/2019; Sekta ya Ujenzi Fungu 98, Sekta ya Uchukuzi Fungu 62, Sekta ya Mawasiliano Fungu 68;

(iii) Vikao vya kuchambua Miswada ya Sheria. Katika kipindi cha mwaka kuanzia Januari 2018 hadi Januari 2019, Kamati ilichambua Miswada ifuatayo; -

- Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 (*The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018*); na
- Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka, 2018 (*The Land Transport Regulatory Authority, Bill 2018*).

b) Ziara

(i) Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo (Kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kanuni ya 98(1), miradi iliyotembelewa na kukaguliwa ni pamoja na;

- Ujenzi wa barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora;
- Ujenzi wa barabara ya Tabora-Kaliua-Uvinza;
- Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza; na
- Uboreshaji wa bandari ya Mwanza.

(ii) Ziara za kufuatilia utendaji wa shughuli za Serikali ni kama zifuatazo: -

Kamati ilitembelea Mikoa minne ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Dar es Salaam. Katika mikoa hiyo Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kiwanja cha ndege cha Kimataifa-KIA, reli ya *meter gauge* kutoka Tanga (Korogwe)-Kilimanjaro mpaka Arusha, Kiwanja cha Ndege cha Moshi, Shirika la Simu la Tanzania-TTC, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Shirika la Posta

Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF.

Vile vile kwa Sekta ya Uchukuzi; Kamati ilitembelea Bandari ya Dar es Salaam, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania.

Aidha, kupitia Mfuko wa Mawasiliano Tanzania- UCSAF Kamati ilifanya ziara katika mikoa kumi na mbili kujionea hali ya mawasiliano nchini. Mikoa iliyotembelewa ni Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara, Simiyu, Shinyanga, Iringa, Njombe, Ruvuma na Lindi.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

2.1 *Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; pamoja na Mapendekezo na Makadirio YA Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliidhinishiwa **Shilingi trilioni 4.2 (4,270,879,381,344)**. Mgawanyo wa fedha hizi katika kila Sekta ni **Shilingi 1,864,991,280,066** Ujenzi, **Shilingi 2,387,031,678,278** Uchukuzi na **Shilingi 18,856,423,000** Mawasiliano.

Sekta hizi zinahitaji fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, ujenzi na ukarabati wa reli, ujenzi na ukarabati wa bandari, ujenzi na ukarabati wa meli na vivuko. Mwenendo wa Bajeti

inayotengwa kwa ajili ya Sekta hii ni wakuridhisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake.

2.2 Sekta ya Uchukuzi

2.2.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na Bagamoyo. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki bandari kadhaa za maziwa makuu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Majukumu ya Mamlaka hii ni kuendeleza, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari nchini. Vilevile, Mamlaka ya Bandari licha ya kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi; pia inahudumia nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbabwe. Hata hivyo, Mamlaka ya Bandari inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- a) Uwezo mdogo wa kuhudumia meli kubwa na kina kifupi katika bandari ya Dar es Salaam pamoja na Tanga;
- b) Uchakavu wa miundombinu ya bandari nchini;
- c) Uwepo wa bandari bubu na ushindani wa Bandari zingine kama vile Beira-Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini; na
- d) Uchakavu wa Miundombinu ya bandari na reli inayounganisha bandari na maeneo mengine

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea

kuboresha huduma za bandari nchini kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati. Kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa.

Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na kurekebisha mgongano wa tozo zilizokuwa kikwazo kwa wafanyabiashara, kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma zitolewazo na mawakala kwenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani (VAT on transit goods), Himaya ya Forodha kwa pamoja (Single Customs Territory) kwa mzigo wa Congo ambayo iliwafanya wafanyabiashara ya Congo kutokutaka kutumia bandari ya Dar es Salaam.

Vile vile, kuimarisha utendaji wa bandari kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya bandari ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2018 baadhi ya shughuli zilizokuwa zimefanyika ni pamoja na: -
Kukamilisha ujenzi wa Jengo la kuweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam, kuanza mchakato wa kununua na kufunga mita mpya za kupima mafuta wakati wa kupakuwa kutoka kwenye meli (*flow meters*), ujenzi wa gati la Ndumbi katika Ziwa Nyasa, ujenzi wa gati la Nyamirembe na Magarine katika Ziwa Victoria pamoja na ukarabati wa bandari zingine nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam, Kamati imejulishwa kuwa hatua mbalimbali za utekelezaji zimefikiwa kama ifuatavyo:-

Tafiti na usanifu wa mradi Gati Na. 1-7, tafiti na usanifu kwa Gati Na. 1-3 umekamilika;

- (a) Tafiti na usanifu wa gati la kuhudumia magari (*RoRo berth*) zimekamilika na ujenzi wa gati la kuhudumia meli za magari katika eneo la Gerezani Creek umeanza kwa kujaza kifusi;

- (b) Gati Namba 13&14, Kamati imejulishwa kuwa mradi huu utatekelezwa katika awamu ya pili ya mradi wa kuboresha bandari ya Dar es Salaam; na
- (c) Upanuzi wa lango la kuingia bandarini, Mkarandasi anategemewa ifikapo mwezi, Septemba 2019 kuanza kazi za uchimbaji wa kina na upanuzi wa lango la bandari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa *Flow Meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia bandari ya Dar es Salaam. Kamati ilipotembelea Bandari ya Dar es Salaam mwezi Julai, 2018 ilijionea kuendelea kwa tatizo la kutokuwepo kwa *flow meter* jambo linalosababisha kutokuwa na uhakika wa kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa bandari kavu eneo la Ruvu (Vigwaza), Kamati ilijulishwa kuwa baadhi ya kazi zilianza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kufanya *levelling* ambapo kazi hiyo imekamilika, kazi zinazoendelea ni kuweka changarawe na ujenzi wa uzio. Awamu ya pili ya mradi wa Bandari Kavu ya Ruvu utahusisha kujenga reli kuunganisha na ile Shirika la Reli la Tanzania-TRC ambapo Mkataba umesainiwa na kazi inatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2019. Inatarajiwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2018/2019 mradi huu utakuwa umekamilika katika awamu zote tatu.

2.2.2 **Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)**

Mheshimiwa Spika, *Kampuni ya Huduma za Meli inatoa huduma za usafiri wa majini kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Hata hivyo utoaji wa huduma umeshuka kutokana na changamoto ya uchakavu wa Meli na Meli zingine kusimama kutoa huduma. Meli zilizosimama kutoa huduma ni*

MV. Serengeti, MV. Liemba, MV. Umoja na MV. Songea.

*Wakati Kamati ilipokuwa ikifuatilia utatuzi wa changamoto hii ilijulishwa kuwa, katika mwaka wa Fedha 2017/2018 Serikali ilitoa fedha zote **shilingi bilioni 24.496 (24,496,000,000)** ilizokuwa imetenga kwa ajili ya kununua meli mpya mbili (2). Hivyo, kazi zilizokusudiwa za ujenzi wa Meli mpya mbili za ziwa Victoria na ukarabati wa meli ya MV. Victoria na MV. Butiama zinaendelea kufanyika.*

Mheshimiwa Spika, mwaka wa Fedha 2018/2019 zimetengwa **Shilingi 20,000,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Kamati inaamini fedha hizi zitatolewa zote na kwa wakati ili kuharakisha maendeleo katika huduma za usafiri katika maziwa makuu.

2.2.3 Reli

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ili kufufua na kuimarisha mtandao wa reli nchini. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge*) ambapo Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/19 imetenga kiasi cha **shilingi Trilioni 1.5** kwa ajili ya ujenzi wa reli hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaha wa kutembelea mradi mkubwa wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *Standard Gauge* Soga-Kibaha mnamo mwezi Julai, 2018 ambapo shughuli mbalimbali za ujenzi zilikuwa zikiendelea.

Aidha, katika kikao chake na Sekta ya Uchukuzi kilichofanyika Mwezi Oktoba, 2018; Kamati ilipokea taarifa ya maendeleo ya Ujenzi wa reli hii ambapo ilijushwa kuwa ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 32 kwa

sehemu ya kwanza ya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300) na asilimia 3.31 kwa sehemu ya pili ya kutoka Morogoro-Makutupora (Km 422). Kazi zilizokuwa zinaendelea ni pamoja na utwaaji wa ardhi, ulipaji wa fidia, ajira mpya na mafunzo kwa watumishi, maandalizi ya uendeshaji, mchakato wa manunuzi wa mabehewa na vichwa vya treni za umeme za abiria, upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umeme, kutengeneza mataruma na utandikaji wa reli ambapo jumla ya Kilometa 10 zimetandikwa.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa reli hii umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza itahusisha kutandika reli kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kupitia Tabora na Isaka (Km 1219); na awamu ya pili itahusisha kutandika reli kutoka Tabora kwenda Kigoma (Km 411).

Mheshimiwa Spika, Kuhusu mradi wa ukarabati wa reli ya kutoka Tanga- Arusha-Musoma (km 1,108), Kamati ilitembelea kipande cha mradi huu cha kutoka Tanga hadi Arusha mnamo mwezi Julai, 2018 ambapo ilikuta shughuli za usafishaji wa njia ya treni zikiendelea. Katika ziara hiyo, kamati ilibaini changamoto kubwa ya uvamizi wa maeneo ya reli hasa kwa Mkoa wa Kilimanjaro ambapo baadhi ya wananchi wanazo hati za kumiliki maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza miundombinu ya reli katika maeneo mengine, mwaka wa Fedha 2018/2019 imetengwa **Shilingi 6,500,000,000** kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia za reli kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge*) kati ya Mtwara hadi Mbaba Bay na matawi Mchuchuma na Liganga (km 1, 092); Tanga- Arusha-Musoma, na matawi yake kwenda Engaruka na Minjingu; pamoja na njia mpya za reli katika Jiji la Dar es Salaam.

2.2.4 Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia-TAZARA

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya TAZARA Namba 23 ya Mwaka 1995 iliyorekebisha kwa Sheria ya TAZARA Namba 4 ya Mwaka 1995. Reli hii inamilikiwa na nchi mbili kwa uwiano sawa wa hisa (50:50). Majukumu ya TAZARA ni kusafirisha abiria na mizigo kwa njia ya reli kati ya Dar es Salaam-Tanzania na New Kapiri Mposhi-Zambia pamoja na kulinda na kuimarisha miundombinu ya reli yenye urefu wa Km 1,860.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Oktoba,2018; Kamati ilipokea taarifa ya Utendaji wa TAZARA. Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka 2017/2018, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 220,818 za mizigo ambazo ni ongezeko la asilimia 28.8% ikilinganishwa na utendaji wa mwaka 2016/2017 ambapo ilisafirisha tani 171, 405. Hata hivyo, ufanisi huu ulikuwa chini ya kiwango kwani lengo lilikuwa kusafirisha tani 250,000. Baadhi ya sababu za kutofikiwa kwa malengo ni pamoja na uchakavu wa vitendea kazi, kutokuwa na vitendea kazi vya kutosha, maeneo korofi ya njia yaliyowekewa ukomo wa mwendokasi na kutokuwa na mitambo madhubuti ya kuimarisha njia. Aidha, kuhusu usafirishaji wa abiria, Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka 2017/2018 jumla ya abiria 543,194 wa safari za mbali walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 482,856 waliosafirishwa 2016/2017 sawa na ongezeko la asilimia 12.2 ambapo lengo lilikuwa kusafirisha abiria 500,000. Hata hivyo, hadi Septemba 2018 jumla ya abiria 149,850 wa safari ndefu walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 166,315 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu malipo ya mishahara ya watumishi wa TAZARA, Serikali ya Tanzania imeendelea kutenga Fedha ambapo katika bajeti

ya mwaka 2018/2019 imetenga jumla ya **Shilingi 14,983,218,000.00** ambapo kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka yaani (mwezi Julai-Septemba, 2018) zimetolewa **Shilingi 3,745,804,500.00**.

Mheshimiwa Spika, Ili TAZARA iweze kuwa na ufanisi inahitaji kuwa na Injini 30 ambapo injini zilizopo ni 12. Aidha, Kamati imejulishwa kuwa mradi wa ukarabati wa mabehewa unaendelea ambapo kati ya mabehewa 400, mabehewa 315 yameshafanyiwa ukarabati na kuingizwa kwenye mzunguko wa kazi. Aidha, ipo haja kubwa kwa nchi hizi mbili kukaa na kuangalia changamoto zilizopo za uendesaji wa reli hii ili kuweza kuboresha kwa kuimarisha reli hii.

2.2.5 **Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za dhati na makusudi za kufufua Kampuni hii ya Ndege ya Tanzania kwa kununua ndege mpya sita.

Kuongezeka kwa ndege kumeiwezesha Kampuni kuongeza idadi ya miruko ili kukidhi mahitaji ya usafiri wa anga katika baadhi ya vituo kikiwepo kituo cha Dodoma ambapo ndege ilikuwa inafanya safari mara tatu kwa wiki na sasa inafanya safari mara nne kwa wiki. Ongezeko la idadi ya miruko limeongeza idadi ya abiria waliosafirishwa hadi kufikia abiria 242,668 ikilinganishwa na abiria 206,788 waliopangwa kusafirishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Katika mwaka 2018 ATCL imeongeza safari za kikanda kuelekea Entebe-Uganda na Bujumbura-Burundi. Aidha, ATCL inamipango ya kuongeza safari za Johannesburg-Afrika Kusini, Harare-Zimbabwe na Lusaka-Zambia. Vilevile, kuanza safari za Kimataifa katika vituo vya Guangzhou-China, Bangkok-Thailand na Bombay-India.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zinazoikabili ATCL ni pamoja na uchache wa wataalam hususan marubani, uchache wa nyenzo za kiutendaji hususan magar na madeni ambayo yameendelea kulipwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

2.2.6 Chuo cha Taifa cha Usafirishaji Tanzania

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- a) Upungufu wa watumishi 180 (wanataaluma 106 na Watekelezaji 74). Hali hii imesababisha Chuo kutumia watumishi wa muda kutoka nje hasa wanataaluma utaratibu ambao una gharama kubwa;
- b) Kutokamilika kwa wakati ujenzi wa jengo la Rasilimali Mafunzo (Maktaba) kutokana na ufinyu wa Bajeti;
- c) Uhaba wa Hosteli za wanafunzi, Chuo kina jumla ya wanafunzi 6,553, ambapo mabweni yaliyopo ni mawili yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 324.
- d) Upungufu wa vifaa vya kufundishia ikizingatiwa kuwa Chuo kinatoa mafunzo ya ufanisi (*Competence Based Education*) ambayo yanaendeshwa kwa vitendo; na
- e) Upungufu wa miundombinu ya Chuo ikiwemo madarasa, ofisi za wahadhiri, ofisi za watumishi na mabweni.

2.3 Sekta ya Ujenzi

2.3.1 Wakala wa Barabara Tanzania- TANROADS

Mheshimiwa Spika, *Jukumu kubwa la wakala huu ni kuhudumia mtandao wa barabara, ambao unakadiriwa kuwa na urefu wa jumla ya kilometa 35,000; ambapo kati ya hizo, kilomita 12,786 ni barabara kuu, na kilometa 22,214 ni barabara za*

Mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye, kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi, kama ilivyofafanuliwa katika Mpango na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, Hali ya barabara kwa ujumla hadi mwezi Juni, 2018 ilionesha kuwa jumla ya barabara zenye urefu wa km 12,427 sawa na asilimia 37 zilikuwa na hali nzuri. Barabara zenye urefu wa km 15,864 sawa na asilimia 48 zilikuwa na hali ya wastani na barabara zenye urefu wa km 4,919 sawa na asilimia 15 zilikuwa na hali mbaya. Icha ya mafanikio hayo, Wakala wa Barabara unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: -

- a) Kutokutolewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hali inayosababisha kazi zilizopangwa kwa baadhi ya miradi kutotekelezwa ama kutekelezwa kwa kiasi kidogo;
- b) Uharibifu wa Miundombinu unaofanywa na watumiaji wa barabara hususan uzidishaji wa mizigo, uharibifu/wizi wa alama za barabarani;
- c) Utaratibu wa kupata misamaha ya kodi kuchukuwa muda mrefu na hivyo kusababisha miradi kuchelewa kuanza kutekelezwa;
- d) Uvamizi wa baadhi ya maeneo ya barabara unaofanywa na baadhi ya wananchi kwa kujenga ama kufanya shughuli za kiuchumi; na
- e) Matumizi mabaya ya barabara kama vile mwendokasi (*over speeding*) na uendeshaji usiofaa wa magari vinachangia ajali za barabarani na uharibu wa barabara; na
- f) Msongamano wa magari barabarani hasa jiji la Dar es Salaam, na miji mingine inayokuwa kwa kasi, kama Mbeya, Mwanza na Arusha;

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine katika ujenzi wa barabara kwa sasa imekuwa uvamizi wa barabara, uliofanyika miaka iliyopita ambapo wananchi walikuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi za barabara bila kujali Sheria ya barabara Namba 13 ya Mwaka 2007.

Vilevile, kumekuwa na migogoro na mvutano kutoka kwa wananchi mbalimbali unaotokana na wasiwasi wa kutolipwa fidia au kulipwa fidia kidogo isiyoendana na hali ya uchumi wa sasa; jambo hili linasababisha wananchi kugoma kuondoka katika maeneo ya miradi; na kusababisha kuchelewa kuanza kwa miradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matuta barabarani, licha ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kuahidi kuendelea kurekebisha matuta makubwa, ili kuyaweka katika viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa Wizara kuhusu usanifu wa barabara wa mwaka 2011, bado kumeendelea kuwapo matuta makubwa hasa katika barabara kuu ambayo yamekuwa chanzo cha uharibifu wa barabara, kwani magari yenye mizigo hulazimika kwenda mwendo mdogo; hivyo uzito kuwa mkubwa na kusababisha barabara kutitia, mizigo kuhama na kuelemea upande mmoja; jambo ambalo wakati mwingine limekuwa chanzo cha ajali kwa magari ya mizigo. Pia, matuta husababisha myumbo wa matairi hivyo kuchochea ubovu na kuongeza uwezekano wa magari kuharibika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali zinazofanywa kuhakikisha jiji la Dar es Salaam linakuwa halina msongamano mkubwa wa magari. Juhudi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo kasi (BRT), kujenga barabara za juu (*flyovers*) katika eneo la TAZARA, barabara za juu (*Interchange*) katika eneo la Ubungo, mradi wa ujenzi wa daraja jipya la Selander

litakalopita baharini kuanzia katikati ya Hospitali ya Aga Khan mpaka Coco Beach, kusaini mkataba wa mradi wa ujenzi wa Daraja la Gerezani na barabara nyingine za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam. Ni lazima sasa kuweka mipango kabambe ya kuongeza barabara za michepuko katika majiji mengine kama vile Mwanza, Mbeya na Arusha, na sasa Makao Makuu Dodoma. Hii itasaidia kupunguza msongamano kwani unaathari nyingi za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa uzito wa magari; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kudhibiti wa uzito wa magari na sasa kuna mizani 38 ya kudumu, mizani 22 zinazohamishika na mizani moja (1) inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo. Hizi ni jitihada za kuzuia uharibifu wa barabara unaosababishwa na magari kubeba mizigo yenye uzito mkubwa ambapo huchimba barabara na kusababisha mabonde na hata wakati mwingine kusababisha ajali.

2.3.2 Ujenzi wa Viwanja vya Ndege

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanja vya ndege nchini umeendelea kutekelezwa chini ya Sekta ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Aidha, Kamati imejulishwa kuwa, ushauri wa Kamati kuhakikisha kuwa viwanja vyote vinakuwa na Hati Miliki unaendelea kutekelezwa. Hata hivyo, kati ya viwanja hamsini na nane (58) vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- TAA, viwanja vyenye Hati Miliki ni vinane (8) tu. Kamati imejulishwa kuwa viwanja vingine kumi (10) viko kwenye mpango wa kupata Hati Miliki mwaka huu.

a) **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere**

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, mkataba ulisainiwa 18 Aprili, 2013. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Mwezi Julai, 2018 utekelezaji wa kazi ulifikia asilimia 78.32. Mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- i) Kucheleweshwa kwa malipo ya *Treasury Voucher Cheque* kuanzia mwishoni mwa mwezi Juni 2018, ambapo kumesababisha kutotoka kwa baadhi ya mitambo bandarini ambayo inahitajika kwa ajili yamajaribio ya awali; na
- ii) Mabadiliko ya sheria ya kodi zilizokuja baada ya mkataba kusainiwa ambapo kumesababisha ongezeko la gharama za mradi.

b) **Kiwanja Cha Ndege cha Songwe**

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe Mkoani Mbeya ulianza mwaka 2000. Kiwanja hiki ni fursa muhimu kwa wakazi wa mkoa wa Mbeya na mikoa ya jirani katika kukuza uchumi kutokana na shughuli mbali mbali za zitakazofanyika kutokana uwepo wa kiwanja hiki. Tangu Kiwanja hiki kilipofunguliwa rasmi mwaka 2012 kumekuwepo na ongezeko kubwa la abiria na ndege. Pamoja na mafanikio hayo, tangu mwaka 2016, Kamati imekuwa ikihimiza umuhimu wa kuwekwa kwa taa za kuongozea ndege ambazo zitasaidia ndege kutua nyakati za usiku na hata mchana wakati wa ukungu mkubwa. Hali kadhalika, kuwekwa kwa uzio kuzunguka mipaka yote ya Kiwanja ili kuongeza usalama wa kiwanja na kuepuka uvamizi na wananchi

wa maeneo jirani kukatiza katika maeneo ya Kiwanja. Hata hivyo, Kamati imejulishwa kuwa zoezi la usimikaji taa litafanyika pamoja na mradi wa ukarabati wa barabara ya kutua na kurukia ndege na unaotarajiwa kukamilika kabla ya Desemba, 2019.

c) Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ndicho Kiwanja kikubwa cha Ndege kwa Kanda ya Ziwa. Kutokana na umuhimu wake; Serikali imekuwa ikikiendeleza Kiwanja hiki kwa kukipanua ili kiweze kukidhi mahitaji mengi ya sasa ya wakazi wa Kanda ya Ziwa na hatimae ndege kubwa za Kimataifa kutua.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyotolewa mwezi Agosti, 2018, Kamati ilifahamishwa shughuli za ukarabati wa barabara ya kutua na kurukia ndege, barabara ya kiungio na upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, jengo la mizigo na kituo cha umeme zimeefika asilimia 75.

d) Kiwanja cha Ndege cha Kigoma

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha kuwa miundombinu ya Kiwanja hiki inaboreshwa na kuweza kutoa huduma za kuridhisha.

Kwa sasa, ujenzi wa Kiwanja hiki unahusisha ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami, ujenzi wa jengo la abiria, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia uwanjani, na maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongezea ndege. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2018 mchakato wa kumpata mkandarasi ulikuwa ukiendelea na

utekelezaji wa mradi unategemea kuanza katika mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, ujenzi wa viwanja vya ndege ni muhimu sana hasa ukuzingatia wakati huu ambapo tunajivunia kuwa na ndege zetu wenyewe. Hivyo ni vema changamoto ya kutokutolewa fedha za ujenzi wa viwanja vya ndege kwa wakati ikafanyiwa kazi ili kutoathiri utekelezaji wa miradi hii muhimu.

2.4 *Sekta ya Mawasiliano*

2.4.1 **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

Mheshimiwa spika, Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA ni kusimamia Makampuni ya Mawasiliano nchini yakiwemo Makampuni yanayotoa huduma za Simu, Utangazaji, Intaneti, Posta na Usafirishaji wa Vifurushi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TCRA imeweka mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu (*Tele-Traffic Management System – TTMS*), ambao umechangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni zilizopo katika udhibiti wa mawasiliano. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha muda wa mkataba wa miaka mitano ambao uliingiwa wa kujenga, kuendesha na kuhamisha umiliki (*Build, Operate and Transfer*). Mkataba huu ulianza kufanya kazi rasmi tarehe 1 Oktoba 2013 na umemaliza muda wake tarehe 30 Septemba, 2018.

Mheshimiwa Spika, Mfumo huu umewezesha kubaini takwimu mbalimbali za mawasiliano yanayopita katika mitandao ya mawasiliano kama vile:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- a) Kupata takwimu za mawasiliano ya simu yanayofanyika ndani na nje ya nchi (*local and international traffic*);
- b) Kuhakiki mapato yote ya watoa huduma za Mawasiliano nchini;
- c) Kupata takwimu zinazohusiana na matumizi ya huduma za wamasiliano (simu za sauti, matumizi ya data, na jumbe fupi).
- d) Kugundua mawasiliano ya simu za ulaghai (fraudulent traffic);
- e) Kutambua takwimu za ada za miamala ya fedha mtandaoni (mobile money transaction);
- f) Kusimamia kwa ufanisi ubora wa huduma za mawasiliano (*Quality of Service*) na hivyo kuboresha viwango vya huduma hizo;
- g) Kutambua taarifa za laini ya simu (*SIM Card profile*) na namba tambulishi za kifaa cha mawasiliano;
- h) Kubaini na kufungia simu zenye namba tambulishi zilizopakiliwa (*Duplicate IMEIs*); na
- i) Kuwasilisha kwa Serikali mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazolingia na kuishia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kuanzia Oktoba 2013 mfumo ulipoanza kufanya kazi mpaka Septemba 2018, Serikali imeweza kupata chanzo kipya cha mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazolingia nchini, ambapo kiasi cha Shilingi **93,665,645,344.55** ziliwasilishwa Serikalini. Kwa ujumla, Mfumo huu umeongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Mawasiliano ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi yanayotokea katika Sekta ya Mawasiliano duniani.

2.4.2 Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta

Mheshimiwa spika, mradi wa anuani za makazi ni muhimu sana kwani mradi ambao utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kuweza kufanyika kwa urahisi na kuokoa muda. Miongoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na; huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto ,magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

Mheshimiwa spika, Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa. Vile vile fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu zimekuwa hazitolewi kwa wakati.

2.4.3 Shirika la Posta Tanzania –TPC

Mheshimiwa Spika, Imebainika kwamba, Shirika hili linakabiliwa na changamoto ya mzigo wa kulipa pensheni wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika mashariki ambapo hadi mwezi Julai, 2018 Shirika limelipa **shilingi bilioni 4.9** pasipo kurejeshewa na Serikali.

Aidha, TPC inadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) deni la shilingi bilioni 26 na kila mwezi inalipa shilingi milioni 50 na hivyo itachukua miaka 40 kumaliza deni hilo.

Vilevile, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ya kurekebisha Shirika la Posta tangu lilipowekwa kwenye orodha ya mashirika yaliyotakiwa kurekebisha na Serikali mwaka 1997. Hatua hii inalifanya Shirika kutoelewa hatima yake na hivyo kuathiri utendaji wake.

2.4.4 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Service Access Fund-UCSAF*) ulianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 11 ya Mwaka 2006 ukiwa na lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Mfuko huu unafanyakazi kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan Makampuni ya simu kama vile TIGO, VODACOM, HALOTEL.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa awali katika sehemu ya kwanza ya taarifa inayoelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati; Mnamo mwezi Julai, 2018, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua minara ya mawasiliano ya simu iliyojengwa kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF na kwa ushirikiano na Makampuni binafsi. Lengo la ziara hii ni kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa mawasiliano hasa katika maeneo ya pembezoni ambayo Serikali imetoa fedha zake (ruzuku).

Mheshimiwa Spika, ziara hii ya Kamati ilijumuisha Mikoa kumi na mbili (12) ya Tanzania Bara ambayo ni Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara, Simiyu, Shinyanga, Iringa, Njombe, Ruvuma na Lindi. Katika Mikoa hiyo Kamati ilitembelea minara ifuatayo;

-
Mkulazi- Morogoro (Vodacom); Hembeti-Mvomero Morogoro (Halotel); Nongwe -Gairo Morogoro (MIC); Doma –Mikumi Morogoro (MIC); Mikumi –Kilosa Morogoro (Halotel); Misozwa- Muheza (Halotel); Mazinde Juu- Korogwe (TTCL); Mshewa- Same (MIC); Naberera- Simanjiro (VODACOM); Nainokanoka-Ngorongoro (MIC); Machodume- Serengeti (VODACOM); Nyamakendo- Serengeti (VODACOM); Sanga Itinje-Simiyu (TTCL); Mwawalaza- Shinyanga; Malenga Makali-Iringa Vijijini (MIC); Wang’ing’ombe-Njombe (Vodacom); Nampungu-Tunduru Ruvuma (TTCL); Namichiga- Ruangwa Lindi (Vodacom);

Mandawa-Ruangwa Lindi (TTCL); na Sali-Ulanga Morogoro (MIC).

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mambo yaliyobainika katika ziara hiyo: -

- a) Ushiriki wa Serikali katika kuwezesha mawasiliano

Pamoja na Serikali kutoa ruzuku za ujenzi wa minara ili kuhakikisha mawasiliano yanawafikia watu wote, hakuna alama yoyote iliyowekwa katika minara kutambulisha wananchi na jamii mchango wa Serikali. Hili linafanya mchango wa Serikali katika kuwezesha mawasiliano kutojulikana kabisa na badala yake Makampuni husika ndio yanayoonekana na kufahamika kutoa huduma hiyo muhimu.

- b) Umiliki wa Maeneo yaliyojengwa Minara

Taratibu za upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa minara kutokuwa wazi jambo linalosababisha Serikali za Vijiji husika kutokunufaika kwa namna yoyote na malipo ya pango la eneo lililojengwa mnara. Kamati imebaini kuwa watu binafsi ambao si wakazi wa vijiji husika ndio walionunua maeneo hayo na kupangisha Makampuni ya simu. Mfano, katika mnara uliopo Doma –Mikumi Morogoro unaomilikiwa na Kampuni ya MIC. Kamati ilijulishwa mmiliki wa eneo lililojengwa mnara ni Mwalim asiye mkazi wa kijiji hicho ambaye alinunua eneo hilo kwa shilingi laki mbili tu (200,000/=) toka kwa mzawa wa kijiji hicho muda mfupi kabla ya kujengwa mnara. Mwalim huyu amekuwa akipokea kodi kila mwisho wa mwezi toka kwa Kampuni (MIC) huku Serikali ya kijiji ikiwa hainufaiki kwa malipo ya pango la eneo lililojengwa mnara.

c) Ushiriki katika Kazi za Maendeleo

Makampuni ya Simu hayashiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo (*Corporate Social Responsibility*) katika maeneo yanayofanya shughuli zake za kibiashara mathalani maeneo ambayo wamejenga minara.

d) Kutokuwepo Mawasiliano wakati Wote

Kamati imebaini pamoja na kuwepo kwa minara, upatikanaji wa huduma ya simu kwa wananchi wa baadhi ya vijiji vilivyotembelewa imekuwa si wakati wote kama ambavyo Serikali imekusudia. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; minara kuwepo mbali na watoa huduma, minara kujengwa katika vilima ambapo hakuna miundombinu ya barabara za magari kufikisha huduma jambo linalosababisha ucheleweshwaji wa huduma ya matengenezo au mafuta ya *generator* na kusababisha kukosa mawasiliano na uelekeo wa mnara na uwepo wa milima inayozuia za mawasiliano kufika katika vijiji vilivyokusudiwa.

e) Utunzaji wa Mzingira

Kamati imebaini kuwa maeneo yaliyojengwa minara inayomilikiwa na Kampuni ya Tigo (MIC-), Vodacom na Halotel hakuna huduma za msingi kama vile chumba cha kulala na choo cha mlinzi. Jambo hili si sahihi na huchangia uchafuzi wa mazingira kwani walinzi hujisaidia vichakani na ikiwa mnara upo jirani na makazi ya watu, hulazimika kuomba huduma katika makazi ya wananchi.

Aidha, kutokuwepo kwa nyumba ya mlinzi kumekuwa ni changamoto kubwa kwani maeneo mengine yapo katika hifadhi au mbuga

za wanyama na hivyo kuhatarisha maisha ya walinzi wa minara.

f) Ujenzi wa Minara katika eneo moja

Ni ukweli usiopingika kuwa wananchi wanahitaji huduma za mawasiliano toka kwa watoa huduma mbalimbali kulingana na uchaguzi wa huduma bora. Hata hivyo, kwa matumizi bora ya ardhi, Kamati inaona si sahihi kwa kila Kampuni kujenga mnara wake kwani baada ya muda nchi yetu itakuwa imetapakaa minara ukiachilia mbali miundombinu mingine muhimu.

g) Uhitaji wa Huduma za "*Internet*"

Katika maeneo yote ya minara ambayo Kamati imetembelea, kumbainika uhitaji mkubwa wa huduma ya *internet*. Hii ni kutokana na minara mingi iliyojengwa kupitia mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuwa ya kiwango cha 2G ambayo hutoa huduma ya sauti na ujumbe pekee.

h) Minara Maeneo ya Mipakani

Kumekupo na changamoto ya wananchi wanaishi maeneo ya mipakani kukosa huduma ya mawasiliano au wakati mwingine kupata huduma ya mawasiliano toka nchi jirani jambo ambalo si sawa na ni hatari kwa usalama wanchi.

i) Rasilimali watu katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote

Kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali wa kujenga minara, imebainika kuwepo kwa wafanyakazi wachache katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote jambo ambalo limekuwa

changamoto hasa katika kufuatilia miradi hiyo wakati wa ujenzi na hata kufuatilia na kuona ikiwa minara inafanya kazi kama ilivyokusudiwa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

3.1 *Bajeti*

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha miaka mitatu ya Fedha, yaani Mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019, Serikali imeonesha kuzingatia ushauri wa Kamati kwa kuongeza fedha kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha Miundombinu nchini. Mwaka wa fedha 2016/2017 ilitenga **shilingi trilioni 4.3**, mwaka 2017/2018 **shilingi trilioni 4.5**, na mwaka 2018/2019 **shilingi trilioni 4.2**.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele na kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa Miundombinu nchini. Hata hivyo, pamoja na shabaha nzuri ya Serikali katika masuala ya miundombinu, Kamati inasisitiza fedha kutolewa kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka limbikizo la madeni.

3.2 *Sekta ya Uchukuzi*

3.2.1 **Mamlaka ya Bandari Tanzania**

Kwa Kuwa, Mamlaka ya Bandari Tanzania ndiyo Mamlaka iliyokasimiwa jukumu la kusimamia bandari nchini;

Na kwa Kuwa, Mamlaka hii inayo miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa bandari ambapo kwa sasa Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua ya kuboresha kwa kufanya ukarabati wa bandari kama vile bandari ya Dar es Salaam na Mtwara;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri yafuatayo; -

- a) Kubakisha angalau **asilimia 40** ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake, kama vile, miradi ya ujenzi wa bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara, ambayo inagharimu takribani **shilingi bilioni 20** wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni takribani **shilingi bilioni 270**;
- b) Kuharakisha mchakato wa ununuzi wa *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Kutokuwepo kwa mtambo wa kupima kiasi cha mafuta (*flow meter*) kunasababisha kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam;
- c) Kufanyike juhudi za makusudi ili kuweza kuhamisha Gati la Mafuta lililopo kurasini (KOJ) na kujenga Gati Namba 13 na 14
- d) Serikali kufanya ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na bandari ya ziwa Nyasa. Vilevile, bandari zilizo katika vipaumbele vya Serikali kama vile Bandari ya Mbegani-Bagamoyo na Bandari ya Mwambani- Tanga kuanza kutekelezwa;
- e) Wadau wote wa bandari waunganishwe kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia mkuu, Shirika la Viwango Tanzania-(TBS), Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo;

- f) Mchakato wa kuwa na eneo Kurasini-Shimo la Udongo ambalo litatumika kuegesha magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyabishara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika;
- g) Serikali kuharakisha ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar es salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Katosho-Kigoma na Misungwi –Mwanza;
- h) Serikali kuharakisha majadiliano na wabia ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwani kukamilika kwa bandari hii kutatoa fursa nyingi za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali kulipa fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza
- i) Watumishi wa bandari nchini wapewe nafasi ya kwenda kujifunza katika Bandari nyingine zinazofanya vizuri ili kuweza kufahamu wenzao wanachokifanya; na hatimaye kuweza kubaini mbinu za ushindani katika biashara;
- j) Uhifadhi wa mizigo inayoshikiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA katika bandari kavu mathalani Ubungo; Iwapo utapita muda wa kisheria wa kuhifadhi mizigo hiyo, taratibu za kutaifisha zitumike kuiwezesha Serikali kutumia katika maendeleo ya nchi kama ujenzi wa shule na vituo vya afya kwani kumekuwapo

na mlundikano wa mizigo inayoshikiliwa kwa muda mrefu kutokana na kutozingatiwa kwa taratibu za forodha jambo linalosababisha kuharibika, hatari ya sumu kwa mizigo ambayo ni kemikali, pamoja na ufinyu wa nafasi;

- k) Bandari Bubu zirasimishwe haraka ili zifanye kazi kulingana na kanuni na taratibu za kisheria na kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi na udhibiti wa biashara haramu.

3.2.2 Ujenzi wa reli nchini

Kwa Kuwa, Serikali imeonesha nia ya dhati ya kujenga upya Reli ya Kati katika kiwango cha kisasa (*standard gauge*); ambapo mradi umeanza mwezi April, 2017 na unatekelezwa kwa awamu tano;

Na kwa Kuwa, katika uhalisia Tawi la kutoka Tabora-Kigoma-Uvinza- Msongati na Kaliua-Mpanda-Kalema ndilo lenye mizigo mingi inayotoka na kwenda nchi za jirani kama vile DR Congo, Burundi na Rwanda;

Kwa hiyo basi, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa; -

- a) Ujenzi wa reli hii uzingatie kwanza maeneo yenye faida za kichumi na kipaumbele cha kwanza kiwekwe katika tawi lenye mzigo mkubwa ambalo ni tawi la Tabora – kigoma - Uvinza- Msongati; Kaliua – Mpanda –Kalema;
- b) Serikali izingatie kuwashirikisha wataalam wa ndani (wazawa) katika ujenzi wa reli ya kati ili kuwa na mradi endelevu pale wataalam wa nje watakapoondoka;
- c) Ujenzi wa reli hii ufanyike kwa tahadhari kubwa ili kuepusha uharibifu wa miundombinu ya reli hasa maeneo kama Gulwe na Godegode,

Morogoro ambako hukumbwa na mafuriko ya mara kwa mara; na

- d) Serikali iangalie uwezekano wa kupata mkopo wa gharama nafuu ambao utatumika kununua vichwa na mabehewa ya treni ili Shirika la Reli Tanzania- TRC liweze kuondokana na changamoto ya upungufu wa vichwa vya treni arobaini na tano (45) pamoja na mabehewa ili TRC iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuanza kupata faida;

3.2.3 Utendaji wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

Kwa Kuwa, TAZARA inamilikiwa na nchi mbili (Tanzania na Zambia) kwa asilimia 50:50;

Na kwa Kuwa, kwa muda sasa utendaji wa TAZARA umekuwa si wakuridhisha;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali iweke mkakati wa dhati kuinusuru TAZARA ili iweze kujiendesha. Moja ya mkakati uwe ni kufanya mazungumzo na Serikali ya Zambia na kufikia muafaka wa namna bora ya uendeshaji wa reli hii, ikiwa ni pamoja na, kufanya mapitio ya kurekebisha Sheria iliyoanzisha TAZARA, Namba 23 ya Mwaka 1975;
- b) *Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi; pamoja na, kuendelea kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha;*
- c) *Serikali kujenga kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kupatia TAZARA mapato ya kutosha kujiendesha;*

3.2.4 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA

Kwa Kuwa, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ndio iliyokasimiwa jukumu la kusimamia na kuendesha viwanja vya ndege nchini;

Na kwa kuwa, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazokabili viwanja vya ndege nchini ikiwemo migogoro ya mipaka;

Kwa Hiyo Basi, Kamati inaishauri yafuatayo; -

- a) Kuhakikisha inapata hati za Viwanja vya Ndege kwani Kamati imejulishwa kuwa viwanja vya ndege vinane (8) vimeshapatiwa hati miliki kati ya viwanja hamsini na nane (58) vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Vile vile, kuhakikisha viwanja vingine vilivyobakia vinapimwa na kupatiwa hati miliki pamoja na uzio ili kujiepusha na uvamizi wa maeneo jambo ambalo huleta migogoro na wananchi na kusababisha Serikali kuingia gharama kubwa kwa ajili ya fidia; na
- b) Kuongeza udhhibiti na ulinzi katika Viwanja vya Ndege vilivyopo Mikoani hasa vilivyopo mpakani kama vile Mtwara, Kigoma na Kagera ili kuepuka viwanja hivi kupitishwa biashara haramu;

3.2.5 Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL

Kwa Kuwa, Serikali imechukuwa hatua ya kufufua Shirika la ndege la Tanzania kwa kununua ndege mpya;

Na kwa Kuwa, ndege hizo zitakuwa kichocheo cha Uchumi wa Tanzania katika kuwawezesha kupata usafiri wa ndani na nje ya nchi, hivyo kutimiza malengo na kukuza Pato la Taifa;

Kwa hiyo Basi, Kamati inaishauri yafuatayo; -

- a) Kuwa na mikakati mikubwa ya kitaifa ya kuhakikisha kuwa ATCL inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida;
- b) ATCL iangaliwe kama Kampuni ya kibiashara na sio yakutoa huduma;
- c) ATCL ijitangaze kwenye vyombo vya Kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali;
- d) Shirika liendelee kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake;
- e) ATCL ichukue hatua madhubuti ili kuimarisha utalii wa ndani ya nchi;
- f) Ni vema Shirika likajipanga kumudu ushindani wa kibiashara pindi litakapoanza kufanya safari za Kimataifa kama kwenda Gwangzuu, Bankoc na Bombay;
- g) Kuwa na mkakati wa kuongeza marubani ili kuwa katika nafasi nzuri kibiashara;
- h) ATCL, itekeleze mpango wa kuwa na vazi rasmi la Shirika ambalo, pamoja na, kuwa nadhifu litaitangaza Tanzania na vivutio vya utalii vilivyopo nchini;
- i) Shirika lisimamie ipasavyo nidhamu ya watumishi wake kwani yamekuwapo malalamiko kutoka kwa wateja kuhusu vitendo vya ukosefu wa nidhamu kwa baadhi ya watumishi. Vilevile,

watumishi waajiriwe kwa kuzingatia vigezo vya sifa na uwezo.

3.2.6 Chuo cha Taifa cha Usafirishaji

Kwa Kuwa, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kimekuwa Chuo bora katika utoaji wa elimu katika fani mbalimbali za usafirishaji kama vile udereva na urubani;

Na kwa Kuwa, sasa nchi yetu imejielekeza katika kuimarisha sekta ya usafiri na uchukuzi;

Kwa Hiyo Basi, Kamati inaishauri yafuatayo.

- a) Wakati Serikali inaendelea kuimarisha sekta ya uchukuzi kwa ujenzi na ukarabati wa reli pamoja na ununuzi wa ndege, uimarishaji huu uende sambamba na kuboresha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji pamoja na mitaala yake ili kupata wataalam wa ndani wa kutosha;
- b) Serikali iangalie namna ya kuendelea kukipanua Chuo hiki na kuhakikisha kinajengwa katika maeneo mengine nchini hasa kwa kuzingatia Kanda kwani eneo la Mabibo kwa sasa ni dogo na halikidhi tena idadi ya wanafunzi;
- c) Endapo Chuo hiki kitakuwa Chuo Kikuu ni muhimu sana kikaendelea kutoa kozi za kati ambazo ni za msingi; na
- d) Serikali izingatie kutoa fedha ambazo inatenga kwa ajili ya Chuo hiki kwa wakati kwani hii imekuwa ni changamoto katika uendelezaji wa miradi ya Chuo.

3.3 Sekta ya Ujenzi

3.3.1 Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS

Kwa Kuwa, Wakala wa Barabara nchini- TANROADS ndio umekabidhiwa jukumu la ujenzi na ukarabati wa barabara kuu nchini;

Na kwa Kuwa, pamoja na jitihada za Serikali kujenga barabara; bado kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali kama vile barabara kuharibika, matuta yasiyo na viwango, uzito uliozidi wa mizigo unaoharibu barabara na wizi wa alama za barabarani;

Kwa hiyo Basi, Kamati inaishauri yafuatayo; -

- a) *Kukarabati baadhi ya barabara za Mikoa zilizo katika hali isiyoridhisha na kutopitika hasa wakati wa mvua na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii;*
- b) Kuhakikisha inaunganisha Miji yote Mikuu na Mikoa iliyosalia kama vile Mikoa ya Katavi-Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera na Njombe-Makete-Mbeya kwa barabara za lami ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo hayo;
- c) Kuendelea na ujenzi wa barabara za lami hasa maeneo yanaochochea Uchumi wa Taifa letu kama vile maeneo yenye vivutio vya utalii, kilimo, viwanda na madini;
- d) *Wizara ya Ujenzi isimamie Sheria za barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama runinga, magazeti na redio. Pia kufanya mikutano na kuweka alama zitakazoonesha mwisho wa eneo la barabara;*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- e) Matuta madogo madogo ya barabarani maarufu kwa jina la rasta na matuta makubwa yasiyo na kiwango yaondolewe kwa kuwa yanasababisha ajali na uharibifu wa magari. Aidha matuta yabaki sehemu zenye umuhimu tu na yawe na kiwango maalumu;*
- f) Kutungwa kwa Sheria ya kudhibiti uuzaji wa vyuma chakavu ili kunusuru miundombinu yetu iliyogharimu fedha nyingi na kwa usalama wa watumiaji wa barabara zetu; na*
- g) Kuendelea kununua mizani ya kisasa ambazo zinauwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (Weight in Motion) na kuzifunga katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa kupima magari;*
- h) Halmashauri zishirikiane na TANROADS na TARURA kutenga maeneo ya kuegesha magari (parking) ili kuzuia magari yanayoegeshwa muda mrefu kandokando mwa barabara na kusababisha uharibifu;*
- i) Barabara zinazounganisha Mikoa hususan barabara ya Lindi- Morogoro ijengwe ili kurahisisha usafiri na kupunguza umbali kwa wananchi wanaotoka Mikoa ya Lindi, Mtwara; Pia barabara ya Arusha-Ngorongoro-Serengeti na barabara ya Simiyu-Arusha, barabara ya Kibondo-Kasulu-Boarder na barabara ya Kazilambwa-Ilunde.*
- j) Fidia itolewe kwa wananchi ambao wamepisha ujenzi miundombinu mbalimbali nchini hususan barabara; na*
- k) Ujenzi wa barabara uzingatie pia ahadi mbalimbali zilizotolewa na viongozi;*

3.3.2 Ujenzi wa Viwanja vya Ndege

Kwa kuwa, Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS umepewa jukumu la ujenzi wa Viwanja vya Ndege nchini;

Na kwa kuwa, bado kuna changamoto kubwa ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali kuhakikisha inatoa kwa wakati malipo ya fedha yaliyoidhinishwa kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha ndege cha Mwanza, Songwe na Mtwara;
- b) Katika ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege, Serikali ijikite zaidi katika kujenga na kuendeleza viwanja vya ndege vya kimkakati ambavyo vitasaidia kukuza pato la taifa kwani Kamati imebainika kuwa kati ya Viwanja vya ndege 58, Viwanja vitano tu (5) tu sawa na 8% ndivyo vinavyochangia mapato ya Serikali;
- c) Wakati ujenzi wa jengo la tatu la abiria (*Terminal III*) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere unaendelea, ni vema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi; na
- d) Kuharakisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa viwanja ndege;

3.3.3 Barabara Jijini la Dar es Salaam

Kwa Kuwa, jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na changamoto kubwa ya msongamano wa magari barabarani;

Na Kwa Kuwa, msongamano huu wa magari umekuwa ukisababisha adha kubwa kwa jamii kwani magari yamekuwa yakitumia muda mrefu, mafuta mengi, na hata kuchelewa kufika Ofisini, shuleni, kwenye biashara na huduma zingine muhimu kwa wakati;

Kwa hiyo basi, Kamati inaendelea kushauri yafuatayo: -

- a) Barabara za juu (*flyovers*) zijengwe hasa katika makutano ya barabara kuu zenye msongamano mkubwa kama vile, Magomeni, Morocco, Mwenge. Wadau kama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweza kushirikishwa kwa kujenga barabara za kulipia.
- b) Kuendelea na ujenzi wa barabara zinazosaidia wananchi kufika maeneo yao bila kupita katikati ya Jiji la Dar es salaam, ikiwa ni pamoja kukamilisha barabara kutoka Goba-Madale-WazoHill, Goba –Kimara, Ardhi-Makongo-Goba n.k. Pia barabara za mitaani (*ring roads*) nazo zifunguliwe kwa kuwekwa lami kwani zitapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa;
- c) Kufanyike upya mapitio ya viwango vya tozo la daraja kwa magari ya abiria yanayopita katika daraja la Mwl. Nyerere Dar es salaam ili ziwe tozo ambazo zitawezesha magari madogo ya abiria kumudu kupita katika daraja hili kuliko ilivyo sasa magari madogo ya abiria hushusha abiria upande mmoja kukwepa tozo na kusababisha abiria kutembea kwenda upande wa pili;

Aidha, ili kwenda na wakati na kuokoa muda, ni vema kuwekwa kadi maalum zitakazokuwa zimetoza malipo ya kabla (*prepaid*) kwa

wanaotumia daraja hili mara kwa mara ili kuepusha usumbufu wa kukata tiketi kila siku kwa wananchi wanaotumia daraja hili;

3.3.4 Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi Mbeya

Kwa Kuwa, vyo hivi vimekuwa vikitoa mafunzo ya teknolojia stahiki ya nguvukazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara kwa wasimamizi, wakaguzi wa barabara, wahandisi na mafundi;

Na Kwa Kuwa, vyo hivi vimekuwepo kwa muda mrefu, lakini bado havijasajiliwa jambo ambalo halitoi hamasa kwa wengi kujifunza katika Vyo hivi;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) *Serikali iviunganishe vyo hivi na kuvisajili ili mafunzo yanayotolewa katika vyo hivi yaweze kutambulika;*
- b) *Serikali ivitengee bajeti ya kutosha vyo hivi ili viweze kuwa na mvuto kwa watu wengi kujiunga na kupata elimu kwani bado kuna uhitaji mkubwa wa wataalam hasa wa barabara katika Halamashauri nchini ambapo wataalam hao wanategemewa kutoka katika vyo hivi; na*
- c) *Serikali inunue mitambo angalau mitatu (3) mipya kwa ajli ya kufundisha kwa vitendo kwani taaluma inayotolewa katika Chuo cha Ujenzi Morogoro inahitaji elimu ya vitendo zaidi kuliko nadharia.*

3.3.5 Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania-TEMESA

Kwa kuwa, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania unakabiliwa na changamoto zikiwemo za ukosefu wa rasilimali watu wenye ueledi wa kwenda samabamba na mabadiliko ya teknolojia, vifaa vya kisasa

vinavyoweza kuendana na magari, na ukosefu wa mitambo ya kisasa;

Na kwa Kuwa, changamoto hizi zinaisababisha TEMESA kufanya kazi kwa kubahatisha ambako kunatumia muda mwingi na gharama kubwa;

Kwa hiyo Basi, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali kuajiri wataalaum waliobobea kwenye fani ya ufundi wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nyingi magari ya Serikali yamekuwa yakitengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;
- b) Wakala wa Ufundi na Umeme kuharakisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo kwani kuna Wilaya zingine ziko umbali mrefu kwenda Makao Makuu ya Mkoa;
- c) Wakala kuchukuwa hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo kwa kiasi kikubwa inazidai taasisi za Serikal ili Wakala huu uweze kijiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini;
- d) Udhibiti wa Mapato katika vivuko, ni vema Serikali ione umuhimu wa kuwa na mashine za kukata tiketi za kieletroniki na kutenga eneo kwa abiria ambao tayari wameshakata tiketi kama inavyofanyika katika kivuko cha Magogoni Dar es Salaam kwani bado watu wengi wanapita na kusafiri kutumia vivuko pasipo kulipa nauli. Haya yafanyike katika vivuko vyote nchini ili kuepusha upotevu wa mapato kwa Serikali;

- e) Serikali kupitia TEMESA kuhakikisha inakaguwa vivuko mara kwa mara ili kuepuka ajali zisizo za lazima na hatimaye kulinda usalama wa abiria na mali zao. Ukaguzi huu ni muhimu kufanyika hata kwa vyombo binafsi;

3.4 Sekta ya Mawasiliano

3.4.1. Fedha za Miradi ya Maendeleo

Kwa Kuwa, Sekta ya Mawasiliano ni miongoni mwa sekta ambazo hutengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika fungu 68;

Na kwa Kuwa, katika utendaji kazi; Kamati imebaini kuwa, Sekta hii haipewi kipaumbele katika utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za miradi zimekuwa ama hazitolewi kwa wakati au hazitolewi kabisa; Mfano, hadi mwezi Machi 2018 hakuna fedha yoyote iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo;

Kwa Hiyo Basi, Serikali ione umuhimu wa Sekta ya Mawasiliano na kutoa fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

3.4.2 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA

Kwa kuwa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kusimamia mawasiliano nchini;

Na kwa Kuwa, kumekuwepo changamoto mbalimbali zinazotokana na ukuaji wa teknolojia katika mawasiliano;

Kwa Hiyo Basi, Kamati inashauri Serikali yafuatayo: -

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- a) TCRA, iendelee kuutunza na kuusimamia Mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa mawasiliano ya simu (TTMS);
- b) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao; na
- c) *Kuendelea kukabiliana na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake kama vile uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zizozostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kuisaidia Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya Cyber Crime na kuwabana wahalifu; na*
- d) Wakati wa utoaji wa leseni za Makampuni ya Simu, ni vizuri pia kuweka masharti ya kulazimisha Makampuni ya Simu kujishughulisha na shughuli za kijamii (*Corporate Social Responsibility*) katika maeneo yake ya kazi.

3.4.3 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF

***Kwa Kuwa**, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea minara ya mawasiliano inayojengwa kwa ruzuku ya Serikali katika Mikoa kumi na mbili ya Tanzania Bara;*

***Na kwa Kuwa**, katika ziara hiyo Kamati ilibaini masuala mbalimbali yanayohitaji kutafutiwa ufumbuzi ili Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uweze kuimarika na kufanya kazi zake vizuri;*

***Kwa Hiyo Basi**, Kamati inashauri Serikali yafuatayo: -*

- a) *Serikali kupitia na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhi hasa maeneo yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo*

yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji husika. Hii itasaidia sana kwani fedha zitakazopatikana kutokana na kukodi ama kununua eneo la mnara zitatumika kwa maendeleo ya wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache na baadhi ya Serikali za vijiji kutokuambulia chochote;

- b) Serikali kuhakikisha kunawekwa mabango yanayoonesha ushiriki wake katika ujenzi wa minara ambayo imetoa ruzuku. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Serikali za Mikoa, Wilaya hadi ngazi ya chini pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote UCSAF; na kwamba, miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana iliyoko maeneo mengi ni kuwa minara inajengwa na Makampuni ya simu yenyewe; hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki kabisa; Aidha, wakati wa uzinduzi wa kuwasha minara iliyojengwa kwa ruzuku za Serikali, licha ya kuweka bango la kuonesha mchango wa Serikali; ni muhimu pia kufanya uzinduzi kwa kualika vyombo mbalimbali vya habari ili kujulisha wananchi kazi na maendeleo ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF;
- c) *Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA kuweka masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (Corporate Social Responsibility);*
- d) Serikali kuweka mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki ya kupata taarifa za nchi yao;

- e) Serikali kuhakikisha inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (*Infrastructure Sharing*) na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa mlundikano wa minara katika eneo moja;
- f) Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano;
- g) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi watoe ushirikiano wa ulinzi ili vifaa vya minara viwe salama;
- h) Kuongeza rasilimali watu kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili Mfuko uweze kusimamia ipasavyo kwa kukagua na kutembelea maeneo ambayo Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa minara na kuhakikisha kazi hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama ilivyokusudiwa;
- i) Serikali kujenga miundombinu ya barabara katika maeneo yaliyojengwa minara ili kurahisisha utoaji wa huduma za minara na wananchi kwa ujumla. Vilevile kurahisisha

shughuli zingine za maendeleo kama vile utalii, kilimo na hata uwekezaji; na

- j) Kwa kuwa teknolojia imeendelea na wananchi wengi wamekuwa na mwamko katika huduma za TEHAMA na hivyo kuhitaji huduma ya *data (internet)*. Ni muhimu sana, minara yote iliyojengwa na inayoendelea kujengwa iwe kwenye uwezo wa 3G na 4G tofauti na ilivyo sasa katika viwango vya 2G ambayo inanyima wananchi wengi fursa ya huduma ya data ambayo ingeweza kurahisisha huduma za afya (afya mtandao), elimu mtandao n.k.

3.4.4 Mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta

***kwa Kuwa**, kutekelezwa kwa mradi huu kunamanufaa makubwa kwani utawezesha kuwepo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimae kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa;*

***Na kwa Kuwa**, Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa mradi huu kwani umekuwa ukisuasua;*

***Kwa Hiyo Basi**, Kamati inashauri yafuatayo; -*

- a) *Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi ; na*
- b) *Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kama zilivyoidhinishwa na kwa wakati ili mradi huu muhimu ukamilike.*

3.4.5 Shirika la Posta Tanzania

Kwa Kuwa, Shirika la Posta linahitaji mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na kukabiliwa na ushindani wa soko katika sekta ya posta;

Na Kwa Kuwa, pamoja na changamoto ya mtaji pia linakabiliwa na changamoto ya Madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na deni ambalo Posta inadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA takribani **shilingi bilioni 26** yamekuwa mzigo unaolielemea Shirika la Posta;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri yafuatayo: -

- (a) Serikali ichukuwe jukumu la kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa wastani wa **shilingi milioni 74** kila mwezi, fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa shirika;
- (b) Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ya kufuta deni la **shilingi bilioni 26** ambalo Shirika la Posta inadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA; na
- (c) Serikali iliondoe Shirika la Posta katika orodha ya mashirika yanayosubiri kurekebisha ili liweze kutumia rasilimali zilizopo kufanya uwekezaji kwa lengo la kujiendesha kwa tija;

3.4.6 Shirika la Simu Tanzania-(TTCL Corporation)

Kwa Kuwa, Shirikala Mawasiliano Tanzania linaendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya madeni ambayo yameripotiwa kufikia takribani **shilingi bilioni 9.8**;

Na kwa Kuwa, madeni haya yanaathiri utendaji kazi wa Shirika;

Kwa Hiyo Basi, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali pamoja na vyombo vyake ambavyo kwa kiasi kikubwa ndio wadaiwa; kulipa madeni hayo, kwa kuwa fedha hizo za gharama za simu hutengwa kila mwaka katika bajeti za Wizara/ Taasisi na Mashirika yao;
- b) Shirika liweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni;
- c) Serikali iweke mazingira wezeshi kwa TTCL *Corporation* kuweza kupata mkopo wa gharama nafuu kwa kuwa Shirika hili ni mali ya Serikali lazima kuwe na mpango thabiti wa kuliwezesha ili liweze kufanya vizuri zaidi; na
- d) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa. Hili lifanyike kwa kuangalia upya utaratibu ambao umeruhusu Makampuni ya Simu mengine kumiliki Mikongo yao sambamba na Mkongo wa Serikali kwani Mikongo hii binafsi itafifiisha maendeleo ya Mkongo wa Serikali na hata kuhatarisha usalama wananchi pamoja na kuikoshesha Serikali Mapato;

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya

pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Eng. Isack Kamwelwe (Mb) akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Eng. Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias Kwandikwa, (Mb).

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Arch. Elius A. Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonazi. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalum wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndugu. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Dickson M. Bisile pamoja na Katibu wa Kamati Ndugu Hosiana John. Vilevile, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

4.1 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, Maoni na Ushauri, sasa naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari 2019 pamoja na Maoni na Ushauri uliopo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Moshi Seleman Kakoso, Mb
Mwenyekiti
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu
04 Februari, 2019

MWENYEKITI: Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo. Naomba kuwasilisha taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kipindi cha kuanzia Machi 2018 hadi Januari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* pamoja na majina ya wajumbe wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, naomba kuwasilisha taarifa inayoeleza shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2018 hadi Januari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambapo, Sehemu ya Kwanza inaelezea Utangulizi; Sehemu ya Pili inaelezea namna Kamati imetekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha kuanzia Machi 2018 hadi Januari, 2019 na matokeo yaliyobainishwa; Sehemu ya Tatu inaelezea Maoni na Mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Fasili ya 6(1) ya Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inajukumu la kusimamia shughuli za Sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira. Kwa muktadha huo na kwa kuzingatia matakwa ya Fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Kamati hii inatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji, na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake kwa lengo la kuisimamia na kuishauri Serikali, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kupokea na kujadili na kukaa na Watendaji wa taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati; Taarifa hizi zilijumuisha taarifa za kawaida za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara ambapo Kamati ilizipokea, kuzichambua na kuzijadili na hatimaye kuishauri Serikali kadiri Kamati ilivyoona inafaa;

(ii) Ziara katika miradi mbalimbali kwa lengo la kubaini ufanisi uliopo katika kutekeleza miradi hiyo;

(iii) Vikao na wadau wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa lengo la kufahamu mafanikio na changamoto zao kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha;

(iv) Kamati ilihudhuria semina mbalimbali zilizoendeshwa na wadau wa sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira wa lengo la kuwajengea wajumbe uelewa juu ya sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Katika kipindi cha kuanzia Machi, 2018 na Januari, 2019, Kamati iliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni katika kuzisimamia Wizara zake mbili (2) na Taasisi zilizopo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri huo, hata hivyo, kuna baadhi ya ushauri ambao Kamati imeona kuwa haujatekelezwa ipasavyo. Maeneo ambayo Kamati imeona ushauri wake haukutekelezwa ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Uwekezaji, Kamati iliitaka Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kupeleka fedha zilizosalia kwa ajili ya mradi wa *TAMCO* ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia itekeleze miradi ya aina katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchi.

(ii) Kuongeza kasi ya uwekezaji wa miundombinu wezeshi katika Mradi wa *Industrial Park Kibaha*.

(iii) Kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mradi wa *General Tyre* kwa vile kukamilika kwake kutaongeza mchango katika Pato la Taifa lakini kuongeza ajira pia. Hili suala la *General Tyre* limechukua muda mrefu tunaomba sasa Bunge liweze kutoa tamko rasmi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Kamati iliitaka Serikali kufanya yafuatayo;-

(i) Kuangalia upya Sheria za Misituni, Mazingira na Mifugo ili kuondoa mgongano wa kisheria katika utekelezaji na uhamasishaji wa usimamizi wa Mazingira. Mazingira ni suala mtambuka na usimamizi wake unazigusa Wizara na sheria tajwa hivyo ni vema zifanye kazi pamoja.

(ii) Tozo zinazotokana na shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira ni nyingi lakini zinakusanywa na Taasisi au Idara nyingine za Serikali. Kamati inashauri tozo hizo walau kwa asilimia 5 zingie katika Mfuko wa Mazingira. Mfano tozo ya magari chakavu, tozo ya mkaa, tozo ya mafuta na tozo ya magogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliirifiwa hatua mbalimbali za utekelezaji wa ushauri huo lakini haikuridhishwa na hatua hizo. Kamati inaishauri Serikalil kuongeza kasi ya kutekeleleza ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifanya ziara za ukaguzi wa ufanisi uliopo katika kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 14 hadi 19 Machi, 2018, Kamati ilitembelea miradi mitatu (3) inayotekelezwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni Mradi Na. 6260 – SIDO Mkoani Iringa, Shughuli za Usimamizi wa Mazingira

katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu – Mkoani Iringa na Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika maeneo ya Mgodu wa Wachimbaji Wadogo Mkoani Singida unaofahamika kwa jina la Sekenke One. Maelezo ya miradi hiyo, pamoja na maoni na mapendekezo ya utekelezaji wake yanapatikana katika taarifa ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wabunge wote wanayo, kwa sababu ya muda naomba nisyasome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Kamati kwa wadau wa Sekta ya Viwanda. Kamati ilipata fursa kwa mwiliko wa wadau wa viwanda kutembelea baadhi ya viwanda katika Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kujionea shughuli zinazofanywa na katika viwanda hivyo, mafanikio na changamoto zao ili tuweze kuishauri Serikali vema. Viwanda vilivyotembelewa na Kamati katika kipindi hicho vimegawanyika katika makundi matano, ambayo ni viwanda vinavyotumia malighafi ya chuma ili kuzalisha bidhaa za mabati, nondo; viwanda vya vinywaji baridi; viwanda vya vinywaji vikali; kiwanda cha sigara na kiwanda cha mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutembelea viwanda vyote hivyo, Kamati iliweza kubaini changamoto mbalimbali katika viwanda hivyo zikiwemo changamoto za bidhaa feki na changamoto ambazo mpaka leo hazijashughulikiwa na Serikali. Kuna shida kubwa ya bidhaa feki, Kamati imeshauri Serikali na taasisi zake kwa kushirikiana kuhakikisha kwamba ukaguzi wa mara kwa mara unafanyika katika eneo hili kuhakikisha kwamba bidhaa feki zinaondolewa sokoni haraka na kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukinzana kwa sheria zinazosimamia Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji zinasimamiwa na mamlaka mbalimbali za udhibiti, mamlaka hizi zimeanzishwa kisheria lakini sheria zinazoziongoza mamlaka hizo zinaonekana kukinzana katika mazingira halisi ya sasa ya biashara. Biashara imebadilika na uchumi wa dunia umebadilika, sheria zetu zingine zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukubwa wa gharama za uzalishaji. Wadau wamelalamikia gharama za uzalishaji nchini ni kubwa jambo ambalo linapelekea bei za bidhaa zinazozalishwa kuwa kubwa kuliko zile zinazolingia kutoka nje, hivyo kushindwa kushindana katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ugumu wa upatikanaji wa vibali vya kuingiza sukari ya viwandani (sukari ghafi). Upatikanaji wa vibali hivi umegubikwa na urasimu sana jambo linalosababisha baadhi ya viwanda kusitisha uzalishaji kwa muda kusubiri viwanda hivi viendeleo kupata tathmini ya Serikali na kusababisha ajira kusimama kwa muda. Tunaiomba Serikali kupitia Bunge lako Tukufu suala la sukari ya viwandani lifanyiwe kazi mapema ili kuhakikisha kwamba uhakiki ukifanyika vibali vitolewe kwa wakati ili uzalishaji usisimame na mapato ya Serikali yapatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano hafifu kati ya mamlaka mbalimbali za Serikali. Utendaji wa Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji, unahusiana na maamuzi ya Wizara nyingine kama Wizara ya Ardhi, kupata vibali vya ardhi; Wizara ya Nishati, kupata umeme; Wizara ya Maji, kupata huduma ya maji; Mamlaka ya Uhamiaji kupata vibali vya kuingia nchini; na Wizara ya Fedha katika kodi na tozo mbalimbali. Changamoto iliyopo ni mamlaka hizi kutofanya kazi kwa pamoja jambo linalokwamisha utekelezaji wa shughuli za viwanda, biashara na uwekezaji kwenda kwa kasi ambayo Mheshimiwa Rais ameionyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Kwanza, kodi ya kielektroniki ya ushuru wa stampu (*ETS*). Kamati inakubaliana na nia nzuri ya Serikali kuhusu kuanzishwa kwa ushuru wa stampu ili kuwadhhibiti wazalishaji wasiowaaminifu lakini kamati ina maoni na ushauri kwamba, pamoja na kwamba zoezi hili limeanza kwa baadhi ya viwanda, viwanda zaidi ya 37 vimeshafungiwa mashine hizi na hasa viwanda vya vinywaji vikali, vinywaji vya pombe na viwanda vya sigara, Kamati inashauri utekelezaji wa kodi hii ufanywe hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa *ETS* kama ulivyopendekezwa na Serikali mfumo huu ni ghali sana, wadau wako tayari kushirikiana na Serikali ili kubuni mfumo mwingine kwa gharama nafuu. Kwa kuanzia kwa kuwa mfumo umeanza, Kamati inaunga mkono juhudi hizi na tunashauri kwa upande wa bidhaa nyingine kama bidhaa za vinywaji baridi, soda na maji ambazo zinatumiwa na Watanzania wengi wenye kipato cha chini basi kodi hii ianze kwa hatua nyingine isuburi hatua ya kwanza ya mafanikio ya viwanda vilivyoanza vya pombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wa forodha wa asilimia 15 ambao unatozwa kwenye sukari ya viwandani (*industrial sugar*) ambao ushuru huu bado haujarudishwa katika viwanda hiyo. Kamati inashauri Serikali iangalie namna bora ya kuweza kuhakikisha kwamba fedha hizi zinarudi kwa wakati ili kuhakikisha wafanyabiashara mitaji yao inarudi na wanaendelea na uzalishaji. Kwa kuwa utekelezaji wa mfumo huu umeonekana kuwa kero, Serikali iondoe na badala yake ipendekeze adhabu kwa wote watakaoathirika kufanya udanganyifu au watakaodhihirika kufanya udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna urasimu unaochelewesha upatikanaji wa vibali, lakini bado kuna urasimu katika kulipa malipo haya, vitu vyote viwili hivi vinawakatisha tamaa wawekezaji katika eneo hili la viwanda vya vinywaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwepo kwa bidhaa bandia za bati na nondo sokoni. Serikali iongeze udhibiti katika bandari zake hususani banadari ya Dar es Salaam kwa kuimarisha ukaguzi wa bidhaa za bati na nondo kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya kufanyia biashara yamekuwa magumu jambo ambalo halitoi taswira nzuri kwa ustawi wa wawekezaji nchini. Kamati inashauri Serikali itafute kiini cha tatizo hili ili kujenga imani kwa wawekezaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wakati wa kuingia makubaliano ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa fedha za misaada au mikopo ya masharti nafuu. Serikali ijitahidi kuweka vifungu au utaratibu ambao utawaelekeza wakandarasi wanaopewa kazi kununua mahitaji yao kutoka ndani ya nchi mfano, mabomba, nondo, bati na kadhalika. Hatua hii itasaidia kuchochea ukuaji wa viwanda vya ndani na kulinda ajira za ndani bila ya kuathiri ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa sasa wa kununua bidhaa kutoka nje unawanufaisha zaidi wageni na kutoa ajira nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kama ilivyo ada, Kamati za Bunge za Kisekta hufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara zinazosimamia kwa mwaka wa fedha unaoishia na kufanya ulinganisho wa utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato kwa matumizi ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitekeleza jukumu hili kama linavyoelekezwa na Kanuni ya 98 ya Kanuni ndogo ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Maelezo ya utekelezaji wa jukumu hili ni kama inavyoonekana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara, pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Taasisi zilizoko chini yake. Kamati pia ilipokea kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali na utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Taasisi zinazokutana na Kamati hizo ni pamoja na *EPZ, TFC, SIDO, TBS, CARMATEC, TIC*, Bodi ya Stakabadhi ya Ghalani,

TEMDO, Kiwanda cha Urafiki, maelezo ya taarifa hizi kama yanavyoonekana katika taarifa ya Kamati ninawasilisha mezani, kutokana na changamoto ya muda naomba niwasilishe baadhi ya taarifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyobinafsishwa; Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, baada ya kuona uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo, aliamua kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao hayo kwa nia ya kuyaongezea mazao. Lakini alilenga kuchochea ukuaji wa uchimi na kutoa ajira. Viwanda vile vya kihistoria vilipitia ukuwaji tofauti, na hatua ya mwisho ilikuwa ni kuvibinafsisha na kviendeleza viwanda hivyo. Kuongeza ajira na mapato ya Serikali kupitia kodi na kuiruhusu Serikali ili sekta binafsi iweze kumiliki uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya ubinafsishaji hayakutekelezwa; baadhi ya viwanda viliendeshwa kwa muda mfupi na kufungwa na viwanda vingine havikuendelezwa kabisa jambo linaloilazimu Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuvirejesha Serikalini. Changamoto ipo katika utekelezajiwa zoezi la kufua viwanda vilivyobinafsishwa. Kamati hairidhishwi na hatua zinazochukuliwa kama inavyoolezwa katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi kwa lengo la kutimiza madhumuni ya waasisi wetu ya kuanzisha viwanda hivi. Lakini pia kutimiza azma ya nchi yenye uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo mwaka 2025. Kitabu changu cha hotuba ukurasa wa 49, 50 na 51 tumetoa taarifa yetu kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa ni viwanda 156, lakini vinasuasua na kuna udanganyifu mkubwa katika eneo hili la ubinafsishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Bunge lako tukufu liweze kuona hili na hatimaye kutoa ushauri kwa Serikali. Suala la ubinafsishaji wa viwanda ni suala ambalo limebeba nguzo kubwa ya uchumi wa Taifa. Viwanda vinavyofanya

kazi havizidi viwanda 20 ni viwanda vikubwa ambavyo navyo vinasaidia sana kutoa gawio la viwanda vingi ambavyo zaidi ya mia bado vinasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa sheria ya mazingira katika ngazi za Serikali za mitaa na changamoto zilizopo katika usimamizi wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na mikakati ya kuikabili. Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekeleza wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na changamoto zinazopatikana katika kutekeleza sheria hii. Baada ya kuchambua taarifa hiyo, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

Kwanza uelewa mdogo wa jamii juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira jambo linalopekea ukiukwaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kiasi kikubwa. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiwezesha Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kirasilimali fedha na watu ili waweze kuwafikia Watanzania wengi na kuwapatia elimu ya uhifadhi wa mazingira, faida ya kuyatunza na hasara ya kuyaharibu, kwani kwa sasa uelewa wa jamii nyingi kufanya usafi tu ndiyo kutunza mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo yameathiriwa na mabadiliko ya tabia ya nchi hivyo kusababisha vyanzo vya maji kusogea na kusababisha changamoto katika kusimamia utekelezaji wa mita 60. Kamati inaishauri Serikali kupitia NEMC na Wizara ya Maji kutafuta ufumbuzi wa haraka wa namna ya kutekeleza sheria ya mita 60 kwa lengo la kuondoa migogoro iliyoko. Lakini pia kuwanusuru watu ambao maeneo yao yamefikwa na vyanzo vya maji kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha kwa ajili ya kurejesha mazingira ya mgodi, kupelekewa na kuratibiwa na Wizara ya Nishati ambayo si Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa mazingira jambo ambalo linapelekea kutumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Kamati inashauri fedha hizo zipelekwe kwa Wizara yenye dhamana Ofisi ya Rais ya Makamu wa Rais (Mazingira). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 takribani miaka 22 sasa ambapo kuna mambo mengi yamekwishatokea na hayakuruhusiwa kwenye sera hii. Kamati inashauri Serikali kufanya mapitia Sera ya Taifa ya Mazingira na kuihusisha ili iendane na hali halisi ya mazingira ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa mafungu yote mawili, Fungu 44 na Fungu 60 liliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 143.3 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 43.3 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 100 kwa ajili ya maendeleo. Aidha, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliarifiwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2018 Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 26.7 kwa mafungu yote mawili, kiasi hili ni sawa na asilimia 18.63 ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni 6.4 tu ndiyo imetolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 6.4 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Utoaji wa fedha kwa maendeleo hauoneshi uwiano sawa na matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupeleka kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa lengo la kuwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Kwa upande wa makusanyo, hadi kufikia Disemba, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya bilioni 7.9 sawa na asilimia 39.5 ya kiasi ilichoipangia kukusanya kwa mwaka wa fedha 2018. Makusanyo hayo hayaonyesha uhalisia wa makadirio ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati; kwanza kabisa ni utekelezaji wa kufufua kiwanda cha

General Tyre umechukua muda mrefu miaka kumi na zaidi, Serikali imeshaweka fedha nyingi lakini hakuna ambacho kinaonekana.

Hivyo basi, Bunge linataka kujua kama Serikali imeshapata utaratibu mzuri wa kufufua kiwanda hicho na lini kiwanda kitafufuliwa na kufanya kazi. Sambamba na hilo Bunge linashauri kama hakuna utaratibu ambao uko tayari wa kufufua kiwanda hicho ni vyema eneo lingetumika kuendesha shughuli nyingine za uwekezaji, ukizingatia eneo hili liko kwenye eneo la mvuto wa biashara kwa maana ya *prime area*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala la vibali vya sukari ambalo tayari nimeshalizungumzia na changamoto la Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira. Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira limepewa jukumu la kisheria kusimamia masuala ya uhifadhi wa mazingira. Kwa kuwa Baraza limekuwa likishindwa kutekeleza majukumu yake kiufanisi kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha, kukosa wataalam wenye taaluma ya mazingira na kukosa vitendea kazi. Hivyo basi, Bunge linashauri Serikali kuzingatia madhumuni ya kuanzishwa kwa chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru wewe kwa uongozi wako pamoja na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati mmekuwa mkipata muda mzuri wa kusaidiana na Kamati, pia naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kipindi chote hiki kwa kufanya kazi pamoja kuanzia Machi hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe tena, lakini pia kuwashukuru wenzangu wote katika kufanikisha shughuli hii wakiwemo wataalam na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani maalum, naomba nichukue fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hatua na juhudi mbalimbali anazozionyesha kwenda kwa vitendo katika kuhakikisha azma ya kujenga Tanzania ya viwanda inafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais na itaendelea kusimamia kuishauri Serikali kuhakikisha kwa pamoja tunafanikisha azma hiyo. Kamati inaridhishwa na kauli zake na maagizo yake katika kuhakikisha kwamba Tanzania ya viwanda sasa inasonga mbele kwa vitendo. Kamati inasema hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu kwa hali ya juu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza kwa ushirikiano walioutoa katika kuandaa taarifa hii mpaka kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa majina yao yanayoonekana kwenye taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wizara zilizo chini ya usimamizi wa Kamati pamoja na Makatibu Wakuu, watendaji wote wa Wizara, taasisi zote zilizoko chini yao kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kufikia mbele katika kutoa ufafanuzi na pale ambapo wote walikuja pale walipohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, salamu za kipekee zimuendee Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa msaada kwa Kamati yetu katika maeneo mbalimbali ambayo Kamati inafanya kazi hususan katika mazao ya kilimo, mazao ya pamba, mazao ya korosho na mazao mengine yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati katika kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kikamilifu. Pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndugu Hussein,

Mkurugenzi Msaidizi wa Fedha, Makatibu wa Kamati, Ndugu Wilfred Magova, Ndugu Zainab Mkamba pamoja na wasaidizi wao pamoja na kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilioamba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI
YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA
NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA KUENZIA
MACHI, 2018 HADI JANUARI, 2019 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira naomba kuwasilisha taarifa inayoeleza shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2018 hadi Januari, 2019.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Nne ambapo, Sehemu ya Kwanza inaelezea Utangulizi, Sehemu ya Pili inaelezea namna Kamati imetekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha kuanzia Machi 2018, hadi Januari, 2019 na matokeo yaliyobainishwa, Sehemu ya Tatu inaelezea

Maoni na Mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

1.2 *Majukumu ya Kamati*

Kwa mujibu wa Fasili ya 6 (1) ya Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inajukumu la kusimamia shughuli za Sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira. Kwa muktadha huo na kwa kuzingatia matakwa ya Fasihi ya 7(1) ya Nyongeza ya Naane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Kamati hii inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji, na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;
- (ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo;
- (iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- (iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

1.3 *Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa lengo la kuisimamia na kuishauri Serikali Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji za Wizara na taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati; Taarifa hizi zilijumuisha taarifa za kawaida za utekelezaji wa majukumu ya wizara na taarifa za utekelezaji wa bajeti za wizara ambapo Kamati ilizipokea, kuzichambua na kuzijadili na hatimaye kuishauri Serikali kadiri Kamati ilivyoona inafaa;

- (ii) Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya ziara katika miradi mbalimbali kwa lengo la kubaini ufanisi uliopo katika kutekeleza Miradi hiyo;
- (iii) Vikao na wadau wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Kamati iliwatembelea pamoja na kuwaalika wadau hao mbele ya Kamati kwa lengo la kufahamu namna wanavyoendesha shughuli zao (mafanyakio na changamoto zao) kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha;
- (iv) Kamati ilihudhuria semina mbalimbali zilizoendeshwa na wadau wa sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira wa lengo la kuwajengea wajumbe uelewa juu ya sekta hizo.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2018 na Januari, 2019 Kamati iliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni katika kuzisimamia Wizara zake mbili (2) na Taasisi zilizopo chini yake.

Mheshimiwa Spika, majukumu yaliyotekelezwa na Kamati ni pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zinazoripoti kwa Kamati; Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka unaoishia pamoja na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka unaofuata; na Vikao na wadau wa Sekta zinazosimamiwa na Kamati kwa lengo la kusikiliza maoni yao; na kuhudhuria Semina za kujenga uelewa wa Wajumbe.

2.1 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri huo, hata hivyo kuna baadhi ya ushauri ambao Kamati imeona kuwa hayajatekelezwa ipasavyo. Maeneo ambayo Kamati imeona ushauri wake haukitekelezwa ni haya yafuatayo:-

i) Kwa upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Uwekezaji, Kamati iliitaka Serikali kufanya yafuatayo;-

a) Kupeleka fedha zilizosalia kwa ajili ya mradi wa TAMCO ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia itekeleze miradi ya aina katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchi.

b) Kuongeza kasi ya uwekezaji wa miundombinu wezeshi katika Mradi wa Industrial Park Kibaha.

c) Kuongeza kasi ya utekezaji wa Mradi wa General Tyre kwa vile kukamilika kwake kutaongeza mchango katika Pato la Taifa lakini kuongeza ajira pia.

ii) Kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Kamati iliitaka Serikali kufanya yafuatayo;-

a) Kuangalia upya Sheria za Misititu, Mazingira na Mifugo ili kuondoa mgongano wa kisheria katika utekelezaji

na uhamasishaji wa usimamizi wa Mazingira. Mazingira ni suala mtambuka na usimamizi wake unazigusa Wizara na Sheria tajwa hivyo ni vema zifanyekazi pamoja.

b) Tozo zinazotokana na shughuli zinazochangia uharibifu wa Mazingira ni nyingi lakini zinakusanywa na Taasisi au Idara nyingine za Serikali. Kamati inashauri tozo hizo walau kwa asilimia 5 ziingie katika mfuko wa Mazingira. Mfano tozo ya magari chakavu, tozo ya mkaa, tozo ya mafuta na tozo ya magogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa hatua mbalimbali za utekelezaji wa ushauri huo lakini haikuridhishwa na hatua hizo. Kamati inaishauri Serikalil kuongeza kasi ya kutekeleleza ushauri huo.

2.2 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifanya ziara za ukaguzi wa ufanisi uliopo katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama inavyoelekezwa na kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 14 hadi 19 Machi, 2018 Kamati ilitembelea miradil mitatu (3) inayotekelezwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Miradi hiyo ni Mradi Na. 6260 – *SIDO Institutional Support* Mkoani Iringa, Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu – Mkoani Iringa na Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Mgodu wa Wachimbaji Wadogo wa Sekenke One Mkoani Singida.

2.2.1 Mradi Na. 6260 SIDO Institutional Support

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembela **Mradi Na. 6260 - SIDO Institutional Support**, Mradi huu unatekelezwa nchi nzima lakini Kamati ilipata fursa ya kutembelea karakana ya SIDO-Iringa (kituo cha uendelezaji wa Teknolojia Iringa) na kujionea jinsi wanavyoendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, karakana ya SIDO – Iringa inaendesha shughuli za kubuni na kutengeneza mitambo mbalimbali ambayo hutumiwa na wajasiriamali katika kurahisisha shughuli zao za uzalishaji. Pamoja na kutengeneza mitambo hiyo, kituo kinaendesha mafunzo na kutoa ushauri kwa wajasiriamali kuhusu uzalishaji na matengenezo endelevu kwenye mitambo wanayowauza.

Mheshimiwa Spika, karakana ya SIDO - Iringa inakabiliwa na changamoto ya matumizi ya mitambo ya zamani (tangu miaka ya 1970) ambayo inapelekea kuwepo matumizi makubwa ya umeme na kusababisha bidhaa wanazozalisha kuuzwa kwa bei kubwa ikilinganishwa na washindani wao. Pia uchakavu wa mitambo unaosababisha kazi nyingi kufanyika kwa mikono hivyo kutumia muda mwingi kwa uzalishaji usio na tija.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni upungufu mkubwa wa watumishi (Karakana inawafanyakazi watatu (3) tu) hivyo kupelekea fundi mmoja kufanya kazi zaidi ya uwezo wake; pia miundombinu mibovu katika eneo la SIDO - Iringa jambo linalopunguza ufanisi wa kituo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo bado karakana ya SIDO-Iringa imefanikiwa kubuni na kutengeneza mitambo mbalimbali ikiwepo mtambo wa kusafishia mafuta ya Alizeti-Double refinery uliofungwa CHATO AMCOS Mjini Chato,

mtambo wa upepo na mvuke wa kukaushia chai kwa kiwanda cha Chai cha Kisogo, mtambo wa kusindika zao la Kakao na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali vya ufundi.

Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Institutional Support-SIDO Iringa

Mheshimiwa Spika, SIDO ni taasisi nyeti na muhimu sana katika kutekeleza azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda kwa kutengeneza vipuri kwa ajili ya viwanda vingine. Kamati inaishauri Serikali kuwa;-

- i) Kuwezesha Taasisi ya SIDO kikamilifu ili iweze kufufua karakana zake zote nchini;
- ii) Kuiwezesha SIDO kubuni teknolojia rahisi itakayo zalisha mashine na mitambo inayoendana na uhitaji wa soko; na
- iii) Kuajiri watumishi wenye weledi katika fani mbalimbali zinazohitajika katika karakana za SIDO.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya SIDO kupitia mfuko wa NEDF huwasidia wajasiriamali kwa kuwakopesha mitaji. Serikali imekuwa ikitenga bajeti ndogo isiyoendana na mahitaji halisi ya huduma za mfuko jambo linalopelekea kukwamisha ufanisi wa Mfuko. Kamati inaendelea kuishauri Serikali;-

- i) Kuongeza bajeti ya Mfuko wa NEDF, ili kuiwezesha kuwiana na mahitaji halisi. Hatua hii itauwezesha mfuko kuwafikia wananchi wengi zaidi, lakini pia itawezesha kutoa mikopo mikubwa zaidi kwa wajasiriamali tofauti na ilivyo sasa kiasi cha juu cha mkopo ni shilingi Million Tano (5,000,000); na

- ii) Fedha zinazopitishwa kwa ajili ya NEDF zipelekwe kwa wakati ili kuweza kutekeleza majukumu lililokusudiwa.

2.2.2 Ziara katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inatekeleza Mradi wa Usimamizi wa Ikolojia ya eneo la Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kurejesha mtiririko wa maji kwa kipindi cha mwaka mzima. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika Bonde na kujua mikakati ya Serikali katika kukabiliana na athari za kimazingira zilizojitokeza katika eneo la Bonde.

Mheshimiwa Spika, Bonde lote la Mto Ruaha Mkuu linajumuisha vyanzo vya mito mikuu Tisa (9). Kwa ujumla hali ya Bonde siyo ya kuridhisha na lipo katika **hatari ya kukauka** ndiyo maana **Mheshimiwa Makamu wa Rais**, aliamua kuiagiza Ofisi yake Idara ya Mazingira kuunda kikosi kazi cha kuhakikisha mto Ruaha unarudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Ruaha Mkuu linakabiliwa na chanagamoto zifuatazo;-

- i) Jamii kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo ya Bonde hivyo kusababisha uchepushaji mkubwa wa maji pasipo kuzingatia mahitaji ya watumiaji wengine hasa wakulima wa Mpunga Mbarali;
- ii) Ongezeko kubwa la idadi ya mifugo inayochungwa katika eneo la hifadhi;
- iii) Kupanuka kwa shughuli za binadamu hasa kilimo cha mpunga katika mashamba ya

Mbarali na kulima kando ya mikondo ya mito;
na

- iv) Kukinzana kwa baadhi ya Sheria katika kusimamia uhifadhi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu (Sheria ya Mita 60 na Sheria za usimamizi wa Mabonde chini ya Wizara ya Maji)

Mheshimiwa Spika, katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu, Kamati iliweza kubaini kubaini changamoto na kutoa ushauri kama ifuatavyo;-

- i) Bonde la Mto Ruaha linatumiwa na wadau mbalimbali, mfano shughuli za Uhifadhi wa wanyama (Ruaha National Park), uvuvi, kilimo na ufugaji hali inayopelekea Bonde hili kuelemea. Ili kupunguza madhara ya uchepushaji na upotevu mkubwa wa maji unaotokana na kutozingatia kanuni za Mazingira, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa Elimu ya matumizi sahihi ya maji hasa kwa jamii zinazoendesha shughuli zake katika eneo la Bonde; na
- ii) Waendeshaji wa miradi mikubwa ya uzalishaji umeme ambayo inategemea maji kutoka katika Bonde hili (Bwawa la Mtera, Kidatu na Mradi mpya wa *Stieglers Gorge*) watambue uhusiano mkubwa kati ya miradi yao na uhifadhi wa mazingira katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Itumike busara ya Miradi hiyo ya Umeme kuchangia katika kuhifadhi wa mazingira ya Bonde kwa uhai wa miradi yao.

2.2.3 Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Mgodini wa Wachimbaji Wadogo Sekenke One – Singida

Mheshimiwa Spika, shughuli mbalimbali za binadamu zimekuwa zikiendesha bila kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, miongoni mwa

shughuli hizo ni uchimbaji madini. Utekelezaji wa Sheria za Mazingira katika mgodi nchini bado siyo wakuridhisha, kwa mujibu wa kaguzi zilizofanyika hadi kufikia Disemba, 2017 kati ya **migodi 128** ni **migodi 5** tu sawa na **asilimia 4** ndiyo inayozingatia Sheria za Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa pia ya kutembelea mgodi wa wachimbaji wadogo wa Sekenke One Mkoani Singida kwa lengo la kujionea namna wanavyoendesha uchimbaji, hali ya mazingira katika eneo la mgodi na uzingatiji wa Sheria za Mazingira katika eneo la mgodi.

Mheshimiwa Spika, hali ya mazingira katika eneo la mgodi sio ya kuridhisha, Kamati ilijionea mambo yafuatayo;-

- i) Wachimbaji wadogo wakitumia kemikali hatari ya zebaki katika Kuchenjua dhahabu bila kuwa na vifaa vya kujikinga, kitendo hiki kinaathiri mazingira lakini pia afya za wachimbaji hao na jamii inayoishi eneo linalozunguka mgodi;
- ii) Matumizi ya teknolojia duni ikiwemo matumizi ya magogo katika kuzuia kingo za mashimo/migodi na kusababisha ukataji wa miti katika maeneo mengi nchini; na
- iii) Uchimbaji wa kubahatisha bila kuwa na uhakika wa kiasi cha madini kilichopo ardhini hivyo kunasababisha kuwepo na mashimo mengi ardhini.

Mheshimiwa Spika, katika mgodi wa Wachimbaji wadogo la Sekenke-One Kamati ilibaini changamoto nyingi na tukatoa ushauri katika mambo yafuatayo;-

- i) Ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa misitu hovyo kwa ajili ya kupata magogo yanayotumika katika zoezi la uchimbaji. Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zake za ufundi kubuni njia mbadala ambayo itakuwa rafiki kwa mazingira na afya kwa wachimbaji wadogo. Mfano badala ya kutumia magogo wanaweza kutumia chuma;
- ii) Wachimbaji wadogo nchini wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mitaji na hivyo kulazimika kutumia zana duni na kusababisha athari kubwa za mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuwasiliana na taasisi za fedha zinazoweza kuwakopesha fedha au vifaa kwa riba nafuu;
- iii) Wachimbaji wadogo wanatumia teknolojia duni katika uchimbaji na uchenjuaji, jambo linalopelekea kiasi kikubwa cha Dhahabu kubaki katika makinikia mwisho wa siku wanakuwa wametumia nguvu nyingi kuwanufaisha watu wengine (wachimbaji wadogo wanapata asilimia **30** tu na asilimia **70** inabaki kwenye makinikia ambayo wanauziwa wenye mitambo ya kuchenjulia). Kamati inaishauri Serikali iangalie namna ya kuwasaidia ili kuongeza tija kwa wachimbaji wadogo na kuongeza mapato kwa Serikali.

Mhesimiwa Spika, wajumbe walihoji kuhusu matumizi ya Zebaki katika uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo, Wizara yenye dhamana ya kusimamia mazingira iliiarifu Kamati kuwa Serikali

ipo katika mpango wa kutekeleza Mkataba wa *Minamata Convention* wenye lengo la kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini ili kupunguza madhara ya kemikali hii kwa afya za binadamu na mazingira kwa ujumla. Kamati inapongeza kwa jitihada hizo na inaendelea kuisisitiza Serikali iharakishe utekelezaji wa mpango huo kwa lengo la kuokoa maisha ya wachimbaji na jamii zinazoishi kuzunguka maeneo ya migodi.

2.2.4 Ziara ya Kamati kwa Wadau wa Sekta ya Viwanda Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea viwanda vitatu vinavyozalisha bidhaa za Mabati, Nondo na Mabomba, viwanda hivyo ni pamoja na kiwanda cha ALAF LTD ambao wanazalisha mabati, kenchi za chuma, masufuria na sahani za chuma; kiwanda cha MM Industries LTD ambao wanazalisha bidhaa za mabati, nondo, bomba za chuma, gypsum na matanki ya plasiki; na kiwanda cha Lodhia Steel Industries LTD wanaozalisha nondo, mabomba ya chuma, mabomba ya plastiki na matanki ya plastiki.

Mheshimiwa Spika, viwanda hivi vinakabiliwa na changamoto ya uwepo wa bidhaa za mabati na nondo nyingi sokoni zinazouzwa bei ndogo ikilinganishwa na bidhaa wanazotengeneza wao. Kinachopelekea hili ni pamoja na:-

- a) Uagizwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango kutoka nje ya nchi hususani mabati na kuuzwa bei ya chini ikilinganishwa na bei za mabati yanayozalishwa nchini.
- b) Ukwepaji kodi (*under declaration of tax liability*) hali inayopelekea kuuzwa bei ya chini sokoni. Wafanyabiashara wasiowaaminifu kwa kushirikiana na watendaji wasio waaminifu hushirikiana kuingiza mabati ambayo hupitia hatua zote za uzalishaji na kuyatoza kodi kama mabati ghafi (*semi processed*).

- c) Wakandarasi wanaotekeleza miradi mikubwa ya nchi ikiwepo miradi ya maji kutumia vifaa ambavyo huagizwa kutoka nje ya nchi wakati viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha malighafi hiyo.

i) Viwanda vya vinywaji baridi na Vinywaji vikali

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea viwanda vya vinywaji baridi ambapo ilitembelea kiwanda cha Coca Cola Kwanza ambao ni wazalishaji wa vinywaji baridi aina ya Coca Cola, Fanta, Mirinda na juice za matunda mbalimbali; kiwanda cha Bakhresa Food Products Mkuranga ambacho huzalisha juice za aina mbalimbali. Kwa upande wa vinywaji vikali Kamati ilitembelea Kiwanda cha Tanzania Breweries LTD (TBL) na Kiwanda cha Serengeti Breweries LTD (SBL) ambao ni watengenezaji na wasambazaji wa vinywaji vikali kama bia na pombe kali. Viwanda vinavyotengeneza vinywaji baridi na vikali vinakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Ushuru wa Forodha 15% (refundable import duty 15%)

Serikali iliongeza ushuru wa forodha kwa 15% kwa waagizaji wa Sukari ya viwandani nchini ili kuwadhibiti wafanyabiashara wasio waaminifu. Ushuru huu unapaswa kurejeshwa kwa wenye viwanda baada ya kuwasilisha matumizi TRA na kuhakikiwa.

Mheshimiwa Spika, tunatambua na kukubaliana na nia nzuri ya Serikali ya kuwadhibiti wafanyabiashara wasiowaaminifu lakini utekelezaji wake umegeuka kuwa ni kero. Takribani miaka mitatu sasa tangu utaratibu huu kuanzishwa, Serikali imeshindwa kurejesha fedha hizo.

b) Ushuru wa Stampu ya Kielekroniki (*Electronic Tax Stamp*)

Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilipitishwa kodi ya ushuru wa stampu (*Electronic Tax Stamp*), kwa ajili ya kuwadhibiti wamiliki wa viwanda wasio waaminifu wanaotoa taarifa za uwongo za uzalishaji na kulipa kodi kidogo.

Mheshimiwa Spika, mfumo uliopendekezwa na Serikali katika kukusanya kodi hiyo ni ghali mno, mfano wazalishaji wa Soda, bia na juice, sigara na pombe kali kodi kwa stempu moja ni kati ya shilling 8 mpaka 49, kiasi hicho ni kikubwa kuliko kodi ambayo inalipwa Serikalini. Aidha, Kiasi hicho kitalipwa kwa wakala wa mfumo na si Serikali.

c) Uwepo kwa pombe kali (spirits) bandia sokoni

Uwepo wa pombe kali bandia sokoni ambazo hutengenezwa katika maeneo mbalimbali yasiyo rasmi na kuuzwa kwa bei ya chini kuliko zinazotengenezwa na viwanda vyetu na kupelekea kua soko la bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kulipa kodi Serikalini.

d) Ongezeko la Kodi kwenye Pombe kali aina ya Valuer

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliogeza kodi katika pombe kali aina ya Valuer kutoka shilingi 200 mpaka shilingi 3215 kwa lita hivyo kuikosesha ushindani katika soko. Pombe hii ilikuwa inatengezwa na Kiwanda cha Bia Tanzania (TBL) ambacho kilisitisha uzalishaji wa bidhaa hii baada ya kukosa ushindani kwenye soko. TBL walikuwa wanunuzi wakubwa wa zabibu kwa ajili ya kuzalisha Valuer, kuanguka kwa bidhaa sokoni kutaleta athari kubwa kwa wakulima wa zao hili.

ii) **Kiwanda cha Sigara Tanzania (TCC Ltd)**

Mheshimiwa Spika, kamati ilipata fursa ya kutembelea kiwanda cha kutengeneza sigara, kiwanda hiki kinazalisha aina mbalimbali za sigara kwa kutumia tumbaku.

Mheshimiwa Spika, wamiliki wa kiwanda hiki wanalalamikia kuwepo kwa Kodi ya Stampu ya Kielektroniki jambo linalopelekea gharama za uzalishaji kuwa kubwa na na kupelekea kuongeza bei ya bidhaa zao. Aidha, uwepo wa Kodi ya Stampu ya Kielektroniki kutaongeza ugumu katika kupanga bei mpya ya sigara mfano, kwenye mzunguko wa fedha hakuna shilingi 15/=, 20/=, 25/= n k. Sambamba na hilo wanalalamikia ugumu wa mazingira ya kufanya biashara nchini jambo linalopelekea kuendelea kufungwa kwa biashara nchini na kushuka kwa mauzo.

iii) **Kiwanda cha mafuta ya kula cha Murza Wilma**

Mheshimiwa Spika, wamiliki wa kiwanda hiki wanalalamikia ongezeko la kodi katika mafuta ghafi yaingiayo kutoka nje kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 25. Ongezeko hili la kodi limesababisha uingizaji wa mafuta hayo kwa njia za panya kuwa mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kuongeza kodi hii ili kuvilinda viwanda vya ndani ni njema sana lakini haitafanikiwa kwa kuwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaendelea kuingiza mafuta kwa njia za panya na mafuta hayo yataendelea kuuzwa kwa bei ya chini kuliko yanayozalishwa nchini. Kamati inaishauri Serikali kujitahidi kudhibiti mipaka yetu pamoja na bandari bubu kwa lengo la kuzuia uingizaji mafuta usio rasmi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ziara hii Kamati iliona kuna haja ya kuwaalika wadau wengine wa Sekta

ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji chini ya Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenyeviwanda Tanzania (CTI) mbela ya Kamati ili kuwasikiliza maoni yao juu ya mazingira ya biashara nchini lengo likiwa ni kupata maoni ya wadau wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, wadau waliofika mbele ya Kamati waliwasilisha changamoto zilizofanana na zile zilizowasilishwa na wenye viwanda wakati wa ziara ya Kamati. Wadau hao waliongezea baadhi ya changamoto ambazo ni pamoja na;-

- a) **Kukinzana kwa Sheria zinazosimamia Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji**, Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji zinasimamiwa wa Mamlaka mbalimbali za udhibiti. Mamlaka hizi zimeanzishwa kisheria lakini Sheria zinazoziongoza mamlaka hizo zimeonekana kukinzana na mazingira halisi ya sasa ya biashara.
- b) **Ukubwa wa Gharama za uzalishaji**, Wadau wamelalamikia gharama za uzalishaji nchini ni kubwa jambo linapelekea bei ya bidhaa zinazozalishwa kuwa kubwa kuliko zile zinazolingia kutoka nje, hivyo kushindwa kushindana katika soko.
- c) **Ugumu wa Upatikanaji wa Vibali vya kuingiza sukari ghafi nchini**, Upatikanaji wa vibali hivi umegubikwa na urasimu sana jambo linalosababisha baadhi ya Viwanda kusitisha uzalishaji kwa muda na vingine kufikiria kufunga viwanda.
- d) **Mawasiliano hafifu kati ya mamlaka mbalimbali za Serikali**, Utendaji wa Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji unahusiana na maamuzi Wizara nyingine kama wizara ya Ardhi kupata vibali vya ardhi, Wizara ya

Nishati kupata umeme, Wizara ya Maji kupata huduma ya maji, Mamlaka ya Uhamiaji kupata Vibali vya kuingia nchini, Wizara ya Fedha katika kodi na tozo mbalimbali. Changamoto iliyopo ni Mamlaka hizi kutofanya kazi kwa pamoja jambo linalokwamisha utekelezaji wa shughuli za viwanda, biashara na uwekezaji.

Maoni na Ushauri wa Kamati juu ya Hoja za Wadau wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji:

a) Kodi ya Kieletroniki ya Ushuru wa Stamp:

Mhesimiwa Spika, Kamati inakubaliana na nia nzuri ya Serikali kuhusu kuanzishwa kwa kodi ya ushuru wa stampu ili kuwadhibiti wazalishaji wasio waaminifu, lakini Kamati ina maoni na ushauri ufuatao;

- i) Utekelezaji wa kodi hii utapelekea kupandisha bei na kusababisha kupungua kwa mauzo kwa kiasi kikubwa hali inayoweza kusababisha kupunguzwa wafanyakazi na kupungua mapato ya Serikali kutoakana mishahara (PE) na kodi ya mapato (*Business Income*);
- ii) Mfumo wa ETS kama unavyopendekezwa na Serikali ni ghali sana. Wadau wapo tayari kushirikiana na Serikali ili kubuni mfumo mwingine kwa gharama nafuu kwa manufaa ya pande zote ni vema Serikali ikakaa na kushauria na wadau hawa;
- iii) Utekelezaji wa kodi hii utawalazimu wenye viwanda kuongeza bei ya kila bidhaa kwa Shilingi 100/= kwa sababu Sarafu nyingine hazipo kwenye mzunguko hivyo kuzifanya kushindwa kushindana katika soko.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaikumbusha Serikali kuwa, wajibu wa msingi wa wafanabiashara ni kulipa kodi lakini gharama za ukusanyaji wa kodi ni za Serikali.

Utekelezaji wa Mfumo huu wa kodi utawalazimu wadau kuweka miundombinu ya ukusanyaji wa kodi ambalo si jukumu lao, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia haya.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Viwanda ambavyo vilitakiwa kuwa mfano kwa kuanza kutekeleza mfumo huu wa kodi, viwanda hivyo ni viwanda vinavyozalisha pombe kali na viwanda vya Sigara. Viwanda hivyo vimekwisha anza utekelezaji wa agizo hili, takribani mitambo 37 imekwishafungwa katika viwanda mbalimbali na changamoto zilizohisiwa kuambatana na mfumo huo wamekutana nazo ikiwemo changamoto ya kupunguza kasi ya mitambo ya uzalishaji (*slow down production*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa viwanda hivi vilitumika kama mfano, Kamati inaishauri Serikali kuwatembelea wenye viwanda hivyo na kushauriana nao kwa lengo la kuboresha kabla ya mfumo huu kuanza kutumiwa na wadau wote.

b) Ushuru wa Forodha 15% (refundable import duty 15%)

Mheshimiwa Spika, Serikali bado haijarejesha kiasi kikubwa cha tozo hii kwa wenye viwanda wanaotumia Sukari ghafi nchini jambo linalopelekea viwanda hivyo kushindwa kujiendesha kutokana sehemu kubwa ya mitaji yao ipo Serikalini. Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo;

- i) Kurejesha fedha hizo kwa wakati kwa kuwa nyingi ni mikopo kutoka katika taasisi za fedha hivyo kusababisha malimbikizo ya riba na marejesho. Aidha, viwanda hivi vinashindwa kujiendesha kutokana na kiasi kikubwa cha mitaji yao kuwa Serikali, hali hii ikiendelea watalazimika kusitisha uzalishaji.
- ii) Kwa kuwa utekelezaji wa mfumo huu umeonekana kuwa kero, Serikali iuondoe na

badala yake ipendekeze adhabu kwa wote watakaodhihirika kufanya udanganyifu;

Mheshimiwa Spika, bado kuna urasimu unaochelewesha upatikanaji wa vibali vya kuagiza sukari ghafi nchini, hivyo kusababisha viwanda kuzalisha kwa msimu. Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali hivyo kwa wakati na kwa wale wanaofanya udanganyifu wachukuliwe hatua stahiki.

c) Kuhusu kuwepo kwa bidhaa bandia za Bati na Nondo Sokoni:

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze udhibiti katika Bandari zake hususani Dar es Salaam kwa kuimarisha ukaguzi wa bidhaa za Bati na Nondo kutoka nje ya nchi;

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kufanyia biashara yamekuwa magumu jambo ambalo halitoi taswira nzuri kwa ustawi wa wawekezaji nchini. Kamati inaishauri Serikali itafute kiini cha tatizo hili ili kujenga imani kwa wawekezaji;

Mheshimiwa Spika, aidha, wakati wa kuingia makubaliano ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa fedha za misaada au mikopo ya masharti nafuu, Serikali ijitahidi kuweka vifungu/utaratibu ambao utawaelekeza wakandarasi wanaopewa kazi kununua mahitaji yao kutoka ndani ya nchi mfano, mabomba, nondo, bati n.k. Hatua hii itasaidia kuchochea ukuaji wa viwanda na kulinda ajira za ndani bila kuathiri suala ubora. Utaratibu wa sasa wa kununua bidhaa hizo kutoka nje unawanufaisha zaidi wageni na kutoa ajira nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupunguza kodi ya pombe kali aina ya valuer,

ambayo hutengenezwa kutokana na matunda ya mizabibu, kwa lengo la kusaidia wakulima kuwa na soko la Zabibu la uhakika na kuchochea ukuaji wa kilimo hicho nchini hasa hapa Dododma ambapo Mheshimiwa Spika wapiga kura wako ni wakulima wazuri za Zabibu;

2.3 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati za Bunge za Kisekta hufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazosisimamia kwa mwaka wa fedha unaoishia na kufanya ulinganisho wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha unaofuata. Jukumu hili limeainishwa katika Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

2.1.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Katika kufanya uchambuzi huu, Kamati ilizingatia makusanyo ya maduhuli, fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Chanzo cha taarifa hizi ni taarifa zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati na majadiliano yaliyofanyika na hatimaye kupata taarifa hizi muhimu.

a) **Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Fungu 44 na 60**

i) **Makusanyo ya Maduhuli**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizopo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **28,000,000,000** kutoka katika makusanyo ya ada za leseni, mauzo ya nyaraka za zabuni na faini ya kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara. Hadi kufikia kufikia Desemba, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi **8,598,083,500.07** kiasi ambacho ni sawa na asilimia **30.7** tu ya lengo lililo kusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa, Desemba, 2017, takribani miezi sita (6), ya utekelezaji kwa mwaka 2017/2018, ni asilimia 30.7 tu ya lengo ndio ilikuwa imekusanya, jambo linaloashiria uwezekano mdogo sana wa kufikia lengo lililokusudiwa. Kamati iliishauri Serikali kupanga bajeti ya makusanyo maduhuli kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vyake vya mapato ili kuwa na uhakika wa kufikia malengo.

ii) **Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2017/2018**

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha **2017/2018**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa na kuidhinishiwa jumla ya shilingi **122,215,109,750.00** kati ya fedha hizo Shilingi **80,190,377,000.00** ikiwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na Shilingi **42,024,732,750.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yake yote mawili

Fungu 44 Viwanda na **Fungu 60** Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Fungu 44 Viwanda lilitengewa shilingi **98,012,870,000.00** Kati ya fedha hizo Shilingi **73,840,377,000.00** zilikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **24,172,493,000.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Na Fungu 60 Biashara na Uwekezaji lilitengewa Shilingi **24,202,239,750.00**, kati ya hizo Shilingi **17,852,239,750.00** ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **6,350,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

iii) **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa, hadi kufikia Machi, 2018, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi **37,447,911,373.33** kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **30.64** tu ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mafungu yote **44** na **60**. Kamati ina maoni kwamba, kuchelewa kutolewa kwa wakati fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kumekuwa kikwanzo kikubwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini mambo yafuatayo;-

- Asilimia kubwa ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, (Shilingi **29,447,911,373.33** ambazo ni asilimia **78.6** ya fedha zote zilizopokelewa zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengine) ambapo pia

asilimia kubwa ya fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya Mishahara. Mwenendo huu wa utoaji wa fedha kutoka Hazina unaashiria kuwa hakuna uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na fedha za Miradi ya Maendeleo;

- Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, kati ya Shilingi **80,190,377,000.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi bilioni **8** tu ndizo zilikuwa zimepokelewa kwa mafungu yote mawili **44** na **60** kutoka bajeti ya Fedha za Ndani, kiasi hiki ni sawa na asilimia **9.97** ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo. Hali hii imekwamisha utekelezaji wa miradi mingi kwa wakati hali inayopelekea kupanda kwa gharama mwaka hadi mwaka; na
- Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kiwango kikubwa unaonyesha kuwa Serikali inapanga matumizi makubwa yasiyoakisi uhalisia wa vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa siyo wakuridhisha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

b) *Makisio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha unaoishi Kamati hufanya ulinganisho wa Makisio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa

Fedha unaofuata kwa lengo la kupata uhalisia wa kiasi kinachooombwa ukilinganisha na utekelezaji wa mwaka ulioisha katika kipengele cha ukusanyaji wa Maduhuli na kipengele cha maombi ya fedha.

i) Makisio ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepanga kukusanya Shilingi **20,006,300,000.00** kwa **Fungu 44 na 60** kutokana na uzaji wa nyaraka za zabuni, leseni za biashara, faini kutokana na kukiuka masharti ya leseni pamoja na marejesho mishahara endapo mtumishi ataacha kazi.

Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **28.5** ya Shilingi **28,000,000,000.00** kiasi kilichokadiriwa katika ya Mwaka wa Fedha **2017/2018**. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kujikadiria kwa kuzingatia uwezo wao halisi wa Makusanyo.

ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mafungu yote Mawili (Fungu **44 na 60**) ilitengewa Shilingi **143,334,153,648.00**. Kiasi hiki ni zaidi kwa asilimia **17.28** ya shilingi **122,215,109,750.00** ya bajeti iliyotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kati ya fedha zinazooombwa, Shilingi **43,309,628,648.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **100,024,525,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka (ongezeko la asilimia **17.28**) ambalo ni jambo jema na la kupongezwa. Changamoto inakuja katika upatikanaji wa fedha hizo kutoka Hazina ambao si wakuridhisha mfano halisi ni bajeti ya mwaka 2017/2018 hadi kufikia Machi, 2018 ni asilimia **30.64** tu ndiyo ilikuwa imepokelewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuwa fedha zinachoidhinishwa na Bunge zitolewe tena kwa wakati kwa lengo la kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

2.3.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ua Ofisi ya makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya Ofisi.

a) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2017/2018

i) Makusanyo ya Mapatato

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira hufanya Makusanyo kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira - NEMC. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Baraza lilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi

15,683,161,500.00 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 8 Machi, 2018 Baraza lilikuwa limekusanya Shilingi **6,700,911,516.00** tu sawa na asilimia **42.7** ya makadirio yake, makusanyo haya yaliashiria ugumu wa kufikia lengo. Kamati inaendelea kusesitiza kuwa lengo la maduhuli linapaswa kupangwa kwa umakini mkubwa na kuzingatizingatia hali halisi.

ii) **Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka fedha 2017/2018**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha **2017/2018** Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira iliidhinishwa jumla ya Shilingi **9,634,020,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,845,568,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (mishahara na matumizi mengineyo ambayo ilijumuisha na ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira) na Shilingi **5,788,452,437.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya Shilingi **9,634,020,437.00**, zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira ni Shilingi **4,369,633,141.30** tu ndizo zilikuwa zimetolewa hadi kufikia 8 Machi, 2018. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **45.3** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi kabisa na mwenendo wa upatikaji wa fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, Idara ya Mazingira. Utoaji huu wa fedha unakwamisha utendaji wa Ofisi hii muhimu katika uratibu wa masuala ya Mazingira. (kati

ya Shilingi **3,845,568,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili matumizi ya kawaida ni Shilingi **1,875,032,651.30** tu ndizo zilizokuwa zimetolewa sawa na asilimia **48.4** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida)

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/2018 (8 Machi, 2018) fedha za Miradi ya maendeleo, kati ya Shilingi **5,788,452,437.00** zilizotengwa ni Shilingi **2,494,600,490.00** tu ndizo zilizopokelewa ambazo pia ni fedha za nje na hakuna fedha za ndani zilizoidhinishwa Bunge zilizokuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, ikitokea wahisani wakaamua kusitisha ufadhili wao kwa miradi ya uhifadhi wa mazingira nchi itakuwa katika hali mbaya. Kamati inaishauri Serikali kulipa uzito suala la Uhifadhi wa Mazingira kwa kuongeza Bajeti ya Uhifadhi wa Mazingira na kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinatolewa tena kwa wakati.

b) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

i) Makisio ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi Mazingira (**NEMC**) imepanga kukusanya shilingi **18,877,446,995.00** kutokana vyanzo vyake vya ndani. Makisio ya mwaka wa fedha **2018/2019** ambayo ni zaidi kwa asimia **20.4** ikilinganishwa na Shilingi **15,683,161,500.00** mwaka **2017/2018** ambazo hazitafikiwa, hivyo makadirio haya hayana uhalisia.

ii) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Idara ya Mazingira katika mwaka wa fedha **2018/2019** iliomba kuidhinishiwa Shilingi **8,118,494,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **15.7** ikilinganishwa na Shilingi **9,634,020,437.00** kwa bajeti ya mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,524,540,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **4,593,954,000.00** ni matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Raisi kwa ujumla wake na kubaini kuwa mahitaji ya bajeti ya usimamizi na hifadhi ya mazingira ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa. Kamati hairidhishwi na ukomo wa Bajeti ya Mazingira hivyo ni maoni ya Kamati kwa Serikali iangalie upya ukomo wa bajeti ya Ofisi hii muhimu.

2.4 TAARIFA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Machi 2018 hadi Januari, 2019, Wajumbe walipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira taarifa hizo ni kama zifuatavyo:-

- a) **Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Maudhui ya Mwongozo wa Mageuzi ya Udhubiti ili kurahisisha Mazingira ya kufanya Biashara nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*)**

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*) ni matokeo ya malalamiko ya muda mrefu ya wawekezaji wenye viwanda na wafanyabisahara juu ya mazingira mabovu/ magumu ya kufanyia biashara nchini. Andiko hili limetoa mapendekezo ya maboresho kwenye mazingira ya biashara hususani mfumo wa udhibiti wa biashara na kuondoa mgongano baina ya mamlaka hizo, pia limeweka utaratibu wa kutekeleza sheria na sera mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, maeneo mahususi yaliyoguswa katika mpango huu ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kwa muda mrefu ni pamoja na gharama kubwa za kuanzisha na kuendeleza biashara zinazotokana na wingi wa tozo; wingi wa mamlaka za Udhhibiti ambazo majukumu yake yanaingiliana; na migongano ya sheria, kanuni na taratibu katika mamlaka mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mazingira magumu ya kufanyia biashara yamekuwa yakiathiri ufanisi kwenye biashara na mwisho wa siku kupunguza utayari/ari kwa wawekezaji. Sambamba na hilo yamekuwa yakishawishi uvunjaji wa sheria na taratibu na kuleta vitendo vya rushwa na ufiadini kwa baadhi ya watendaji na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inajielekeza katika kujenga Uchumi wa kati kupitia Ujenzi wa Viwanda ifikapo 2025 lakini mazingira ya kufanyia biashara yamekuwa magumu. Ugumu wa Mazingira ya kufanyia biashara umepelekea biashara nyingi kufungwa, hali hii inaashiria hata bidhaa zitakazoenda kuzalishwa katika viwanda

tunavyoendelea kuvianzisha zitakosa soko na mwisho wa siku viwanda hivyo vitafungwa.

Mheshimiwa Spika, tumendelea kushuhudia nchi yetu ikizidi kushuka na kushika nafasi ya chini katika orodha ya nchi zilizokuwa na urahisi wa kufanya biashara (easy of doing business) kutoka nafasi ya 132 mwaka 2016 hadi nchi ya 144 mwaka 2019. Hali hii si nzuri na jitihada za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kujinusu na uporomokaji huo.

Mheshimiwa Spika, matumaini ya Kamati pamoja na Wadau wote wa Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji yapo katika Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*). Kamati inaiomba Serikali kukamilisha mpango kazi wa utekelezaji mpango huu na utekelezaji wake uanze haraka iwezekanavyo. Sambamba na hilo Mpango huu uwe *flexible* kufanyiwa maboresho kadiri changamoto zinavyoendelea kujitokeza katika mazingira ya kufanyia biashara.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mpango huu wa Serikali, pia tunatakiwa kutambua kuwa mazingira ya biashara yanajumuisha pia nchi za jirani, hivyo basi ili kuviwezesha viwanda na wafanyabishara wetu kushindana katika soko ni vyema wakati wa kupanga kodi/tozo na kutunga sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamia biashara tuzingatie nchi jirani wanafanya nini/vipi. Hatua hii itatatua changamoto ya sisi kuwa soko la biadhaa za wenzetu lakini pia itaziwezesha bidhaa zetu kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mipango mizuri ambayo hutuaminisha kuwa italeta mabadiliko katika mazingira ya kufanyia biashara ikiwepo

Mpango wa kuboresha Mazingira ya Uwekezaji (*Business Environment Strengthening for Tanzania - BEST2000*) na Programu ya kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (*Roadmap for Improving Investment Climate*, 2009) lakini ufuatiliaji wake umekuwa mgumu kutokana na kutokuwa na muda maalumu wa utekelezaji wake (time frame). Kamati inashauri Serikali ipange muda maalumu (time frame) ya utekelezaji wa *Blueprint* kwa lengo la kuweza kupima ufanisi wake na kuainisha changamoto ambazo zimetatuliwa baada ya kipindi hicho kupita;

- b) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Shughuli zinazofanywa na Mamlaka ya EPZ pamoja na jitihada za Serikali katika kuhamasisha wazawa kuwekeza katika maeneo ya EPZ.**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya EPZ ni mamlaka ya Serikali iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge (EPZ.Act, 2006) pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2008 na 2012 kwa lengo la kuandaa mazingira ya sekta ya Viwanda ambayo yataiwezesha Tanzania kuzalisha bidhaa ambazo zitaweza kushindana katika soko la kimataifa. Mamlaka ya EPZ imepewa jukumu la kusimamizi na kutekeleza Sheria na program za *Export Processing Zone (EPZ)* na *Special Economic Zone SEZ*.

Mheshimiwa Spika, EPZ ni maeneo maalumu ya uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya soko la nje, na ilianzishwa kwa madhumuni ya kujenga na kukuza Sekta ya Viwanda, kukuza mauzo ya nje, kuongeza ajira, kukuza teknolojia, kuunganisha bidhaa zetu na masoko ya kimataifa na kuongeza thamani malighafi za ndani. SEZ ni mkakati wa kutekeleza 'Mini Tiger Plan 2020' na inalenga kuhamasisha ukuaji wa uchumi na kupunguza

umasikini, SEZ ilianzishwa kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kukuza ushindani, kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuongeza pato na fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, jukumu mahsusi la Mamlaka ya EPZ ni kuainisha, kutwaa, kuendeleza na kusimamia Kanda maalumu za Kiuchumi. Baada ya kutwa maeneo maalumu ya kiuchumia, huyaendeleza kwa njia tatu ambazo ni Mamlaka ya EPZ kumiliki maeneo kwa niaba ya Serikali, kuhaulisha au kukodisha maeneo kwa wawekezaji na EPZA kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuyaendeleza maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vilivyopo ndani ya EPZ na SEZ vinapata fursa za:-kusamehewa kodi ya mapato ya makampuni (*Corporate tax*) kwa miaka 10 ya mwanzo; msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani - VAT na ushuru wa forodha kwa malighafi, vifaa, mashine na vifaa vya ujenzi vinavyonunuliwa hapa ndani ama kuagizwa kutoka nje; Msamaha wa kodi na ushuru unaotowwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka 10 ya mwanzo; na faida nyingine za kiutaratibu kama vile kuwepo na huduma za TRA karibu, urahisi wa upatikanaji wa vibali vya kazi kwa watumishi watano wenye asili ya nje na kupata huduma zote muhimu chini ya mwamvuli wa EPZA.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manuafaa na umuhimu mkubwa wa Mamlaka ya EPZ wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha kulinganisha na mahitaji halisi ya mamlaka jambo linalopelekea kukwamisha uendeshaji wa program za EPZ na SEZ; Ushirikiano hafifu kati ya Mamlaka ya EPZ na Taasisi/idara nyingine za Serikali katika kukamilisha baadhi ya shughuli mbalimbali za mamlaka; na Mamlaka ya

EPZ msimamizi mkuu wa utekelezaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati katika maeneo maalumu ya uwekezaji lakini inakabiliwa na changamoto wa upungufu wa wataalamu wa fani muhimu jambo linalokwamisha ushiriki wao katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mhesimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya Mamlaka ya EPZ na kubaini kuwa Sheria ya Mamlaka ya EPZ inaweza kuwa kikwazo. Sheria hii inamtaka Muwekezaji kuuza asilimia **80** ya bidhaa anazozalisha nje ya nchi na asilimia **20** tu kuuzwa ndani, Sheria hii inaweza kuwa kikwazo kwa wawekezaji kwa sababu moja ya vivutio vya wawekezaji kutaka kuja Tanzania ni kupata soko pia. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha sheria hii na kuongeza walau asilimia chache za kuuza ndani hatua hii itawavutia wawekezaji wengi sababu soko lao litaongezeka;

Mhesimiwa Spika, aidha, Mamlaka ya EPZ imepewa jukumu la kutwaa maeneo, kuyalipia fidia na kuyaendeleza kimiundombinu kuhakikisha yanakuwa tayari kwa ajili ya uwekezaji, lakini upatikanaji wa fedha za maendelo kwa Mamlaka ya EPZ si wa kuridhisha (mfano katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilipokea asilimia 3 tu) jambo linalopelekea kukwamisha utekelezaji wa mamlaka hii. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hii zinapatikana tena kwa wakati ili kufanikisha jukumu hili kubwa;

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Maeneo yaliyotwaliwa na Mamlaka ya EPZ lakini mpaka sasa hayajalipwa fidia jambo linalowakwamisha wenye maeneo yao kujiendeleza katika maeneo mengine. Kamati inaishauri Mamlaka kutwaa maeneo machache ambayo itakuwa na uwezo wa kulipa fidia kwa wakati; Sambamba na hili

Mamlaka ya EPZ ising' ang' anie kutwaa maeneo ya mjini ambayo yamegubikwa na migogoro, ijaribu kutwaa maeneo ya nje ya miji na kuyaendeleza kimiundombinu na kuyawekea vivutio ambavyo vitawavuta wawekezaji kwenda kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Miradi chini ya Mamlaka ya EPZ utekelezaji wake umechukua muda mrefu sana, mfano Mradi wa Kurasini Logistic Centre unatekelezwa kwa takribani miaka Kumi (10) sasa na Serikali imekwishawekeza fedha nyingi shilingi 191 (ambazo zimeshalipwa kama fidia), lakini bado hayajaanza kuwekezwa hivyo fedha zilizowekwa pale ni kama zimetelekezwa tu. Kamati inaishauri Serikali kuja na mpango wa haraka wa kuutekeleza mradi huu ili Taifa liweze kunufaika;

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wawekezaji chini ya mradi wa EPZ na SEZ wamekabidhiwa maeneo na wana nia ya kuyaendeleza lakini wamekuwa wakikumbana na mikwamo kutoka kwa mamlaka nyingine za Serikali na hivyo kupelekea kuchelewa kuyaendeleza. Kamati inaishauri Mamlaka ya EPZ kuweka utaratibu wa kuwatembelea wawekezaji mara kwa mara kwa lengo la kuwasikiliza changamoto zao na kuwasidia kuzitatua. Hatua hii itawavutia wawekezaji wengi kuwekeza nchini kwa kuona kuwa Serikali inawajali.

- c) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Uendeshaji wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC);**

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) ilianzishwa mwaka 1968 chini ya Sheria ya Makampuni (*Companies Ordinance 212*) ikiwa ni

ubia kati ya Serikali ya Tanzania chini ya NDC na Kampuni ya Kijerumani ya *Messrs Klockner INA* na kupewa jukumu ya kuendesha kiwanda cha kutengeneza mbole kilichokuwa Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kilianza kazi mwaka 1972 na kufanya kazi mpaka mwaka 1991 ambapo kilipata hitilafu na kusimama uzalishaji. Baada ya hitilafu hiyo Kampuni ya kijerumani ilijitoa na kukabidhi hisa zake kwa Serikali hivyo kufanya Serikali kuwa mmilikiwa wa kiwanda kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hitilafu ya mwaka 1991 TFC haikufanya kazi ya uzalishaji hadi kilipofungwa rasmi mwaka 1996 kupitia waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 6 ambao ulieleza sababu ya kufungwa ni kutokana na kiwanda hicho kuwa katika eneo la makazi ya watu. Waraka ulielekeza kuwa kiwanda kifungwe na mali zote za kiwanda ziuzwe. Pia ulielekeza kuwa kitengo cha biashara kibaki na kitafanya kazi ya kuagiza na kusambaza mbole.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa ya TFC kamati ilibaini kuwa TFC inajiendesha kibiashara lakini kwa miaka mitatu mfululizo ilikuwa ikipata hasara. Kamati inaishauri Wizara kukifanyia tathimini na kubainisha kuwa kama ina umuhimu wa kuendelea kuwepo au kutokuwepo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kujitoa katika uendeshaji wa TFC na kuibinafsisha kampuni hii, hatua ya kubinafsisha TFC itasaidia kupata uhakikika wa mbole, tutapata kodi na watanzania watapata ajira.

Mheshimiwa Spika, sheria, sera na miongozo ya usimamiazi wa masuala ya mbolea nchini yameonekana kuwa na ukakasi katika utekelzaji wake, Kamati inaishauri Serikali kuzipitia upya na

kubaini dosari zilizopo na kuzirekebisha kwa manufaa ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imechaguliwa kuwa *Food Basket* wa kutekeleza mpango wa Chakula wa *Food Security* wa Afrika Mashariki. Maboresho ya sheria, sera na miongozo ya usimamizi wa mbolea itasaidia wakulima kuwa na uhakika wa mbolea na hatimaye tutapata mazao mengi na yenye ubora ili kukidhi mahitaji ya mpango huu;

Mheshimiwa Spika, utendaji wake TFC unahusiana moja kwa moja na shughuli za kilimo, kwa kulitambua hilo Kamati yangu ilishauri Serikali kuihamishia TFC chini ya usimamizi wa Wizara yake mama ya Kilimo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kupokea ushauri huu na sasa TFC imehamishiwa Wizara ya Kilimo.

- d) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Mkakati wa Serikali wa kuliwezesha Shirika la SIDO kuhakikisha linafikisha huduma zake kwa watanania wengi zaidi;**

Mheshimiwa Spika, Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge namba 28 ya mwaka 1973 kwa lengo la kujenga msingi mzuri wa kuanzisha viwanda vidogo. SIDO imepewa jukumu la kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya SIDO ni kuishauri Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu maendeleo ya viwanda vidogo na kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo nchini, kupanga na kuratibu shughuli zote za miradi ya viwanda vidogo nchini, kufanya utafiti wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vidogo, kutoa

huduma na mafuzo ya kiufundi kwa viwanda vidogo nchini

Mheshimiwa Spika, tunahamasisha wazawa kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kuna muitikio mzuri hususani wakinamama wamekuwa wakijishughulisha na shughuli mbalimbali za ujasiriamali ikiwemo kuongeza thamani mazao hususani usindikaji. SIDO ndio ina jukumu la kuwasaidia wajasiriamali hawa lakini inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Bajeti inayotengwa kwa ajili ya SIDO hailingani na mahitaji halisi, pamoja na udogo wa bajeti hiyo bado haipelekwi kwa wakati hivyo kukwamisha utekelezai wa majukumu ya SIDO. Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya Shirika hili lakini pia kiasi kinachotengwa na kuridhiwa na Bunge kipelekwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wetu wanaanza kuendelea kwa kuanza kutumia mashine na mitambo katika kufanya shughuli zao hususani za uongezaji thamani mazao, lakini Shirika linashindwa kutengeneza mashine zinazoendana na mahitaji ya soko. Hili linasababishwa na mitambo iliyopo katika karakana za SIDO ni ya zamani sana na inatumia teknolojia ya zamani. Kamati inaishauri Serikali kupitia SIDO kushirikiana na Taasisi/wadau wengine kuingia Ubia (Joint Venture) na sekta binafsi ili kununua mitambo ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wanaojishughulisha na usindikaji wanakumbana na changamoto ya vifungashio, wamekuwa wakitegemea kuagiza vifungashio kutoka nchi ya Kenya ambavyo vinakuwa ghali na upatikanaji wake sio wa uhakika. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea nguvu SIDO kwa kuipatia fedha na teknolojia stahiki ili iweze kuwekeza katika uzalishaji

wa vifungashio kwa wajasiriamali wetu ili waweze kuvipata kwa urahisi na uhakika.

e) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Uendeshaji wa Taasisi ya TBS na Mkakati wa Serikali katika kuhakikisha TBS inafikisha huduma zake kwa watanzania wengi Zaidi**

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linaendeshwa na Sheria Na. 2 mwaka 2009 na limepewa jukumu la kukuza matumizi ya viwango na kuinua ubora wa bidaa na huduma nchini kwa lengo la kupanua na kuimarisha soko la ndani na nje ya nchi. Sambamba na hili shirika linasimamia shughuli za utayarishaji wa viwango, udhibiti na uthibiti wa ubora wa bidhaa kutoka sehemu mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazoweza kuchukuliwa mara baada ya kubaini uwepo wa bidhaa hafifu sokoni zimebainishwa katika Sheria ya Shirika la Viwango Tanzania ambazo ni kuziondoa sokoni; kuweka utaratibu wa kiziharibu au kuzirudisha zilikotoka; kumtoa faini muuzaji/msambazaji; na kusitisha leseni au cheti cha ubora wa bidhaa cha mzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kupitia uhakiki wa ubora wa bidhaa tutaweza kuisaidia nchi yetu kutimiza azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda kwani bidhaa zetu zitakuwa na ubora wa kimataifa na hivyo kupata soko ndani na nje ya nchi. Katika harakati za kujenga Tanzania ya Viwanda tunategemea uwekezaji mpya unakuja kufanyika lakini TBS bado haina uwezo wa kutoa viwango vya bidhaa hizo (mfano Viwanda vya magari). Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha TBS kupata mafunzo stahili ambayo yataliwezesha Shirika

kuwa na uwezo wa kukagua uwekezaji mpya unaoendelea kufanyika;

Mheshimiwa Spika, TBS imepewa jukumu la kuinua ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini lakini tumeshuhudia wajasiriamali wengi wadogo wamekuwa wakipata changamoto za masoko ya bidhaa zao kwa sababu ya kukosa viwango (hali hii inachangiwa na kukosa elimu viwango). Kamati inaishauri Serikali kuwasadia wazalishaji wa ndani kwa kuwapatia elimu ya viwango na kuhakikisha wanazalisha bidhaa zinazoweza kushindana kwa ubora katika soko;

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wamekuwa wakitumia bidhaa zisizokidhi viwango, jambo hili hutokana na kuendelea kuwepo kwa bidha hizo katika soko lakini pia kutokana na unafuu wa bei za bidhaa. Kamati inaishauri Shirika kuongeze kasi katika kutoa elimu juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora. Hatua hii itasaidia kuepuka madhara lakini pia itachochea ushindani wa haki.

Mheshimiwa Spika, TBS imekuwa ikitumia mawakala wa Pre-Shipment Verification of Conformity (PVOC) kufanya ukaguzi wa bidhaa kabla hazijaingizwa nchini. Taarifa zilizopo ni kwamba mawakala wa PVOC wamekuwa na tabia ya kutokagua mizigo, wanachokifanya wanaangalia cheti cha TBS cha kiwanda kilipotoka bidhaa na kutoa cheti kama imeukagua na kuthibitisha mzigo. Kamati inatambua nia njema ya Serikali kuamua kutumia mfumo wa PVOC kwa lengo la kupunguza msongamano bandarini lakini kutokana na urasimu unaoendelea katika mfumo huu, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya namna ya kuachana na PVOC na kuamua kuendelea na utaratibu wa bidhaa kukaguliwa hapa nchini tu.

Mheshimiwa Spika, TBS haina kiwango kimoja cha gharama kwa huduma ya aina moja jambo ambalo linanatoa picha ya urasimu na kupelekea baadhi ya wafanyabiashara kuamua kutumia njia za panya kwa lengo la kuwakwepa TBS. Matokeo ya ukwepaji huu ni kukosa kodi lakini pia kuendelea kuwa na bidhaa zisizokidhi viwango sokoni. Kamati inaishauri Serikali *kuestablish* gharama za huduma zao TBS ambayo itakuwa sawa kwa huduma za aina moja.

f) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Mpango wa Serikali katika Kufungamanisha shughuli za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda.**

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa nafasi za ajira Viwandani zimechukuliwa na kutekelezwa na mitambo ya roboti (*robotic machine*), kwa kuzingatia hilo Serikali inatakiwa kuchukua jitihada za makusudi za kufungamanisha shughuli za kilimo, ufugaji uvuvi na ujenzi wa Viwanda kwa lengo la kuongeza ajira ukizingatia kuwa shughuli hizi ndio kimbilio na tegemeo la Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) umeelezea nia ya kuanzisha viwanda vitakavyo ajiri watu wengi, kuanzisha viwanda vinavyotumia malighafi nyingi zinazopatikana nchini na kutoa ajira, kuanzisha viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika kwa wingi nchini. Utekelezaji wa mpango huu unapaswa kwende sambamba na kufungamanisha shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji na ujenzi wa viwanda nchini kwa lengo la kuimarisha sekta hizi sambamba na kuimarisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi kutoka kwa sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia mazao yetu mbalimbali yakikumbana na changamoto ya kupata masoko jambo lililopelekea mpaka kushuka thamani kwa mazao. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuhamasisha ujenzi wa viwanda ambavyo vitaenda kuchakata mazao yetu hususani mazao ya kipaumbele. Sambamba na kuhamasisha ujenzi wa viwanda hivyo, tuwahamasishe wakulima wetu kufanya kilimo cha kisasa kwa lengo la kupata mazao mengi na yenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mazao yetu yamekumbwa na changamoto ya bei na masoko mfano mazao ya mahindi, mihogo, korosho, mtama, pamba, kahawa chai, pareto na tumbaku. Kwa mazao ya mahindi, mabibo na mihogo yanaweza kutumika kuzalisha nipa, ambayo inatumika katika kuzalisha pombe kali. Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali vya kutumia mazao ya mahindi, mabibo na mihogo kuzalisha nipa kwa lengo la kuwasaidia wakulima wa mazao haya kupata soko la bidhaa zao lakini pia kuongeza ajira kupitia kilimo cha mazo hayo na wenyeviwanda kupata malighafi (nipa) kiurahisi na kwa gharama nafuu na kusaidia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni;

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebarikiwa kuwa nchi ya pili Barani Afrika kwa wingi wa mifugo hivyo kutuweka kwenye nafasi ya kuwa na malighafi ya ngozi ya kutosha. Pia, mahitaji ya bidhaa za ngozi nchini ni makubwa (viatu, mikoba, mabegi, makoti na mikanda). Uwepo wa malighafi na mahitaji ya bidhaa za ngozi inatuweka katika nafasi nzuri ya kunufaika na hatua ya kufungamanisha viwanda na shughuli za ufugaji, Kamati inaishauri Serikali kuhamasishwa uwekezaji katika viwanda vya bidhaa za ngozi.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya ngozi katika soko la Dunia yamekuwa makubwa kwa kuwa kuna baadhi ya nchi huitumia kama chakula, Kamati inatambua nia njema ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvilinda viwanda vya ndani kwa kuweka *export levy* ya 80% kwa Dolla 37 kwa tani moja. Kamati inaishauri Serikali kutambua mahitaji ya viwanda vya ndani kisha kuruhusi kiasi kilichobaki kuuzwa nje ya nchi, sambamba na hilo Serikali iangalie namna ya kuishawishi Jumuiya kupunguza *export levy* kwa lengo la kutoa fursa kwa wafugaji wetu kuuza ngozi ambazo kwa sasa zimekuwa zikitupwa na kuchafua mazingira (Tanzania ndio wahanga wakubwa wa kodi hiyo kwa kuwa sisi ndio wazalishaji wa kubwa wa ngozi katika Jumuiya ya EAC).

Mheshimiwa Spika, zao la alizeti limeonekana kuwa zao mkombozi kwa wakazi wa ukanda wa Singida na Dodoma. Pamoja na kuwa na viwanda vidogo vidogo vingi katika ukanda huo bado tumeshuhudia wajasiriamali wadogo wadogo wakijipatia riziki kupitia kilimo cha alizeti na shughuli za kukamua mafuta na kuyauza barabarani. Wajasiriamali hawa hawana eneo maalumu la kufanyia shughuli zao za ukamuaji mafuta pia wanatumia teknolojia duni hivyo kuyafanya mafuta yao kukosa ubora unao stahili. Kamati inaishauri Serikali kuangalie namna nzuri ya kuwaunganisha wazalishaji wadogo wa mafuta ya alizeti kwa kuwapatia eneo maalumu la uzalishaji na uuzaji wa bidhaa zao. Sambamba na hilo iwawezeshe kupata mashine ya kuchuja mafuta kwa lengo la kuongeza ubora na thamani ya mafuta ya alizeti, hatua hii itarahisisha pia Serikali kupata mapato stahiki;

Mheshimiwa Spika, kilimo ni kimbilio na tegemeo la Watanzania walio wengi hivyo juhudi za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kuimarisha

shuguli za kilimo nchini. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango wa kuwahamasisha na kuwasaidia wakulima wetu kupata na kutumia mbegu bora kwa lengo la kupata mazao mengi na yenye ubora unaokidhi soko.

- g) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC) na Mipango ya CAMARTEC katika kutengeneza zana za kilimo zinazoendana na mahitaji ya wakulima vijijini;**

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC) ni muunganiko wa Taasisi ya Majaribio ya zana za kilimo- (TAMTU) na Mradi wa Uendeshaji wa Taknolojia Arusha – AATP ambao ulilenga kuboresha maisha ya wananchi kupitia uendeshaji na uhaulishaji wa teknolojiji za zana za kilimo, nishati, maji safi na taka, vifaa vya ujenzi na majengo vijijini.

Mheshimiwa Spika, CAMARTEC inatazamiwa kutoa teknolojia zenye kuleta maendeleo ya kilimo kwa jamii za vijijini nchini. Katika kutekeleza hili CAMARTEC inatekeleza majukumu ya kufanya utafiti katika zana za kilimo na teknolojia zinazofaa kutumika vijijini kwa lengo la kuleta maendeleo ya kilimo kwa wananchi waishio vijijini; kutengeneza sampuli kifani (*prototype*) zilizothibitishwa na kisha kuzitathimini ili kubaini ubora na uwezo wa kutumika katika mazingira ya Tanzania; kurekebisha (*adapt*) teknolojia za kigeni za zana za kilimo ili ziweze kuendana na mazingira ya Tanzania; kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya nadharia na vitendo yanayohusu zana za kilimo na teknolojia; kutoa huduma za ushauri elekezi juu ya ubunifu, majaribio ya kiufundi kuhusu zana za kilimo; na kuwa muwakilishi wa Taifa na katika

majukumu ya kituo katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, CAMARTEC imefanikiwa kubuni na kuunda trekta aina ya *CAMARTEC Fastrucktor-CFT* sambamba na kulifanyia majaribio na kufanya ufuatiliaji wa utendaji wake; kubuni na kuunda kipandio (*planter*) cha mbegu za pamba; kubuni na kuunda mashine za kipura mazao ya kilimo (mashine ya kupura na kupeta mtama, uwele, maharage, alizeti, dengu, ngano na mpunga); mashine ya kukata na kufunga majani ya malisho ya mifugo. Aidha, Kituo kimekuwa na miradi mbalimbali ya ujenzi wa mitambo ya nishati mbadala (biogesi) katika taasisi na kaya mbalimbali. Pia kituo kinajihusisha na tafiti za maeneo ya nishati ambapo kwa sasa inashirikiana na Tanzania Breweries Ltd (TBL) kafanya tafiti katika chachu ya bia iliyotumika kwa nia ya kuzalisha biogesi.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo wa watanzania wengi uwepo wa taasisi hii utawasaidia wakulima wetu kwa kuwarahisishia kazi kuanzia kwenye hatua ya kulima, kupanda na kuvuna. Kamati inashauri Wizara kukitengea kituo bajeti ya kutosha na fedha zipelekwe kwa wakati ili kiweze kufikisha huduma zake kwa wahitaji wengi zaidi hatimaye kuwasaidia wakulima wetu kuzalisha kwa kiwango kikubwa tena mazao bora yatacakayokidhi mahitaji ya soko;

Mheshimiwa Spika, kituo kinatumia teknolojia duni sana jambo linalopelekea kuzalisha mashine zinazohusisha nguvu nyingi katika kuzitumia, Kamati inaishauri Serikali kukiwezesha kituo hiki kupata teknolojia mpya ambayo itawawezesha kuzalisha mashine ambazo zipo *softicated* kidogo kwa lengo la kuwarahisishia wakulima wetu kazi;

Mheshimiwa Spika, kilimo ni shughuli inayotegemewa na kufanywa na watanzania walio wengi hususani wa hali ya chini, Kamati inaishauri Wizara kutenga bajeti ya kituo ambayo itawawezesha kutosheleza gharama za uzalishaji na kukiwezesha kituo kuuza zana zao kwa gharama nafuu na kuwanufaisha watu wa hali zote;

- h) **Utendaji wa Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO); na Mipango ya TEMDO katika kuwezesha upatikanaji wa vifaa/ zana zinazoendana na mnyororo wa kuongeza thamani kwenye mazao mbalimbali.**

Mheshimiwa Spika, mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka mitano (1975/76 – 1979/80) ulitilia mkazo uanzishaji wa viwanda vya msingi. Mpango huu ulipelekea kuundwa kwa Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO) kwa lengo la kulijengea taifa uwezo katika kubuni, kusanifu na kuunda mashine na mitambo kwa ajili ya sekta mbalimbali za uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya TEMDO ni pamoja na; kutafiti, kubuni na kuunda mitambo, mashine teknolojia pamoja na vifaa mbalimbali na kuhamasisha utengenezaji vilivyobuniwa kibiashara; kutoa huduma za kihandisi kwenye viwanda vikubwa, vya kati na vidogo kwa lengo la kuongeza ufanisi, matumizi bora ya rasilimali, ubora wa bidhaa na uwezo wa ushindani; na kutoa mafunzo kwa wahandisi na mafundi mchundo viwandani ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Shirika linakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa fedha jambo ambalo linapelekea Shirika kushindwa kujitangaza

na kusambaza mitambo na mashine zilizoalishwa na shirika kwa kiwango cha kuwafikia walengwa. Pia, Shirika halina mazingira ya mazuri ya kufanyia kazi pamoja na vitenda kazi vya kutosha katika kuendeleza shughuli za ubunifu na undelezaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, TEMDO imejipanga kubuni na kutengeneza zana kulingana na mahitaji ya tathimini iliyofanywa na kubaini zana zinazohitajika kwa sasa katika mfumo mzima wa uongezaji thamani mazao yetu kwa lengo la kuwarahisishia wakulima wetu katika zoezi zima la kulima, kupanda na kuvuna;

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa bajeti imekuwa tatizo sugu kwa taasisi zetu za utafiti (CAMARTEC, TEMDO, SIDO, TIRDO) jambo linalowakwamisha kujitangaza na kufikisha huduma zao kwa watu wengi. Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi hizi ziweze kuungana (*team up*) na kuandaa matangazo na kufanya semina kwa pamoja. Hatua hii itawawezesha kujitangaza zaidi kwa kutumia rasilimali ndogo waliyonayo ukizingatia kuwa taasisi hizi zinafanya kazi zinazoendana haitakuwa ngumu. Aidha, Kamati imevielekeza vituo hivi kuwasiliana na Halmashauri zote nchini kupitia kitengo cha Biashara katika kutoa elimu ya huduma wanazozitoa;

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa mashirika mengine ya utafiti chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara TEMDO pia inatumia teknolojia duni/ya zamani sana jambo linalosababisha kuzalisha mashine ngumu (zakizamani sana) kulingana na mahitaji ya soko la sasa. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha TEMDO kupata teknolojia ya kisasa ili iweze kuzalisha mashine *softicated* kwa lengo la kuwarahisishia kazi watumiaji.

i) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC); na Mpango wa Serikali katika kuvutia uwekezaji kwenye Sekta zinazofungamanishwa na Ujenzi wa Viwanda.**

j)

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania - TIC kiliundwa Septemba, 1997 baada ya kufutwa kwa iliyokuwa Taasisi ya Kuhamasisha Uwekezaji - IPC ya mwaka 1990. TIC inaendeshwa na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997, na ina jukumu kuu la kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha, kuwezesha na kuishauri Serikali kuhusu Sera sahihi na mambo mengine yanayohusu uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya TIC yameainishwa katika kifungu cha 5 cha sheria ya Uwekezaji ambayo ni pamoja na Kubuni mbinu za kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini kwa lengo la kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi; kusaidia wawekezaji kupata vibali mbalimbali na hati za kisheria; kuandaa na kusambaza taarifa sahihi kuhusu fursa za uwekezaji na upatikanaji wa mitaji na wabia; kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta muhimu zitakazokuza uchumi kwa haraka; na kushirikiana na Serikali kutafuta maeneo ya uwekezaji na kuyatayarisha kwa muwekezaji kuja na kuanza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuhusu mpango wa Serikali katika kuvutia uwekezaji kwenye sekta zinazofungamanishwa na ujenzi wa Viwanda, mpango huo umejielekeza katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ambao unaelekeza kuendeleza na kuhamasisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kama vile nguo, ngozi, mafuta ya kula, katani, sukari, matunda; kuimarisha programu za uhamasishaji na uwekezaji kupitia taasisi

zinazosimia uwekezai (TIC, EPZA na Tantrade); kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi; na kusimamia upatikanaji wa mitaji.

Mheshimiwa Spika, TIC inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Uwekezaji, mabadiliko ya kila mwaka ya Sheria ya Fedha yamekuwa yakiathiri utekelezaji wa Sheria ya Uwekezaji hususani katika kipengele vivutio vya uwekezaji na kodi. Kamati inashauri Wizara ya Fedha wakati wa kufanya Mapitio na Mabadiliko katika Sheria ya Fedha ikae pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania-TIC na kupitia Sheria ya Uwekezaji kwa lengo la kupata makubaliano yenye faida kwa pande zote mbili;

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria za uwekezaji hazikidhi matakwa ya sasa ya kuvutia na kuhudumia wawekezaji, kuna badhi ya maeneo yanahitaji maboresho. Maeneo yanayohitaji maboresho ni pamoja na kuizuia Sheria ya Uwekezaji kuathiriwa na mabadiliko ya sheria nyingine ikiwepo Sheria ya Fedha, Vivutio vya uwekezaji kwa kuingizwa kwenye Sheria ya Uwekezaji badala ya Sheria ya Fedha na kuimarisha huduma za *One stop shop*.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji umekuwa na mlolongo mkubwa na hata pale inapopatikana imekuwa na migogoro mingi kati ya wawekezaji na wakazi wa aneo husika, aidha mchakato wa kuhaulisha ardhi kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya jumla unachukua muda mrefu sana kati ya miaka miwili hadi mitatu (kwa wawekezaji wa nje hata wa ndani) jambo linalopelekea wawekezaji walio wengi kushindwa kuvumilia kuendelea kusubiri. Kamati inashauri kuwa katika kutenga maeneo ya uwekezaji tuangalie maeneo ya nje ya miji ambayo hayamilikiwi na watu hivyo kukwepa

suala la fidia na mivutano na wananchi. Pia, itolewe elimu kwa wananchi juu ya umuhimu na faida za uwekezaji hatua ambayo itapunguza migogoro kati yao kwa kuwaona wawekezaji ni wanyonyaji lakini pia itawawezesha kushiriki katika shughuli za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingi za uwekezaji zimekuwa zikifanyika katika maeneo ya miji, jambo hili kwa kiasi kikuwa linasababishwa na kukosekana kwa huduma mbalimbali (maji, umeme, barabara n.k) katika maeneo ya nje ya miji. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna katika Sheria yake ya Uwekezaji kuweka *Modal* ambayo itawaruhusu Wawekezaji kuvuta Huduma hizo katika maeneo yao kisha gharama wanazotumiwa zifidiwe katika bili ya matumizi watakazofanya;

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na matamko mbalimbali kutoka kwa viongozi wa Mamlaka wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo utekelezaji wake unaathiri hali ya Uwekezaji Nchini. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na TIC Kuandaa miongozo mbalimbali ambayo itawasimamia Viongozi hao katika kusimamia mambo ya Viwanda na uwekezaji;

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Kituo cha Uwekezaji Tanzania- TIC kimehamishiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

- k) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani (WRRB); na Mpango wa Serikali katika kutatua changamoto za uendeshaji wa maghala.**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani (WRRB) ni Taasisi ya Serikali

Iliyoazishwa kwa Sheria ya Stakabadhi Ghala Na.10 ya mwaka 2005. Mfumo wa Stakabadhi Ghala ni aina ya biashara ambapo bidhaa zinahifadhiwa ndani ya ghala lenye leseni na mmiliki wa bidhaa anapewa stakabadhi inayoonyesha umiliki mahsusi, thamani, aina, idadi na ubora wa bidhaa iliyowekwa ghalani. Mfumo huu unalenga kurasimisha mfumo ya masoko kwa lengo la kutafuta mazao ya kilimo, lakini pia kupunguza vipingamizi mbalimbali vinavyokinzana na uzalishaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Taasisi hii ni kutoa leseni kwa waendesha ghala; kutoa leseni kwa wakaguzi wa ghala; kuendesha mfumo wa kisasa na makini wa Stakabadhi ghaha; kutangaza mfumo wa Stakabadhi ghala; kuratibu shughuli za wadau wa mfumo wa stakabadhi ghala; kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa za mfumo wa Stakabadhi ghala kwa wadau; kushirikiana na vyombo vingine vya kitaifa na kimataifa vinavyofanya kazi kama za Bodi; na kuishauri na kuiwakilisha Serikali kwenye mikutano au makongamano yanayojadili mfumo wa Stakabadhi ghala;

Mheshimiwa Spika, watumiaji wa mfumo huu wananufaika na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wamiliki wa stakabadhi ghala kuzitumia stakabadhi zao kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha; kuongeza ushiriki wa wafanyabishara wa bidhaa za mazao katika biashara za kimataifa; kuongeza upatikanaji wa sehemu za kuhifadhi mazo zilizo bora, kupunguza hasara za baada ya kuvuna na kuimarisha uhakika wa chakula; kuunganisha mfumo mdogo wa ugani na pembejeo; kupata taarifa za soko na mauzo za kuaminika kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu na faida zipatikanazo kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi Ghala, bado Bodi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha, watu na vitendea kazi hivyo kukwamisha bodi kufika kwenye maeneo mengi lakini pia kushindwa kuhudumia mazao mengi; uhaba wa maghala bora ya kuhifadhi mazao, maghala mengi yaliyopo yanamilikiwa na watu binafsi hivyo uhakika wa kumnufaisha mkulima kwanza inakuwa changamoto; uelewa mdogo juu ya mfumo wa stakabadhi ghala hali inayopelekea baadhi ya wadau walanguzi kuwapotosha wananchi kwa maslahi yao binafsi;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa mpango ya Serikali katika kutatua changamoto za uendeshaji ghala utahusisha kushirikiana na soko la bidhaa kutengeneza mfumo wa kielektronic wa stakabadhi ghala na soko la bidhaa; kushirikisha taasisi/wadau wa sekta ya umma katika kutoa elimu ya Mfuko wa Stakabadhi Ghala; katika kutatua changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha Bodi imeandika maandiko mbalimbali na kuyatuma katika mashirika ya wafadhili kama Common Fund for Commodities na Agricultural Market Development Trust (AMDT);

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuiwezesha Bodi hii muhimu kwa kuipatia rasilimali watu na fedha ili kuweza kuhudumkia mazao mengi zaidi na hatimaye kuongeza ajira kupitia kilimo kwa kuwa watakuwa na uhakika wa soko. Aidha, Kamati inaomba kuona uwezeshaji wa Bodi hii unafanyika katika Bajeti ijayo ya Wizara yani Mwaka wa Fedha 2019/2020;

Mheshimiwa Spika, pamoja na huduma nyingine zitolewazo na Bodi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Bodi hii isaidie kuwapatia wakulima wetu

elimu ya huduma za kifedha, hatua hii itasaidia kuwaepusha kuchukuwa fedha (mikopo) kwa walanguzi na mwisho wa siku faida wanayoipata inaishia kulipa madeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Bodi ya Stakabadhi Ghala kwa lengo la kufanikisha kuunganisha Ujenzi wa Viwanda Nchini na Shughuli za Kilimo ambazo ndio shughuli kuu ya watanzania walio wengi. Tutumie Bodi kukusanya mazao ya wakulima na kuleta uhakika wa malighafi kwa viwanda vinavyotumia mazao ya kilimo. Suala hili liende sambamba na kujenga maghala mengi zaidi kwa lengo la kuhakikisha angalau asilimia kuwa ya mazao/wakulima wanaohitaji huduma hii ya Stakabadhi Ghalani wanaipata;

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Stakabadi Ghala inasimamia mazoa ambao usimamizi wake upo chini ya Wizara ya Kilimo na kwa upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara jukumu lao kubwa ni kutoa leseni tu kwa maghala na wawendesha maghala. Kamati inashauri usimamizi wa Bodi hii uhamishiwe kwa wizara mama ambayo ni Wizara ya Kilimo.

l)Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Kiwanda cha URAFIKI;

Mheshimiwa Spika, URAFIKI ni kiwanda cha ubia kati ya Serikali ya Tanzania (49%) na Serikali ya China kupitia kampuni ya *Chanzhou State Owned Textile Assets Operations Company Limited* (51%). Kiwanda kinazalisha nguo kuanzia hatua ya uchakataji wa pamba hadi kitambaa kilichotiwa rangi. Kiwanda hiki kilianza uzalishaji kama Shirika la uma miaka ya 1968 na uwezo wa uzalishaji ulikuwa mita milioni 33 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika miaka 22 ya Ubia (1996 hadi 2028) Kiwanda cha URAFIKI kimekuwa kikipata hasara, hasara ya kiwanda hiki inatokana na kuzalisha chini ya uwezo wa kiwanda ambao unatokana na kutumia teknolojia na mitambo ya zamani sana. Kamati inatambua uchakavu wa teknolojia ya miaka 1968 lakini inatambua pia lengo la kuingia Ubia lilikuwa ni kuongezaa nguvu katika kiwanda lakini pia kuleta teknolojia mpya.

Mheshimiwa Spika, aidha, kati ya miaka ya 1996 na 2008 kiwanda kimechukua mikopo ya jumla ya Yuan 217,150,000 kwa malengo tofauti tofauti ikiwemo la kuboresha Teknolojia ya kiwanda. Kamati haifahamu mkopo huo ulitumika kufanya nini kwa kuwa changamoto ya teknolojia duni ya kiwanda bado ipo mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia bidhaa za kiwanda cha URAFIKI zikipendwa sana sokoni, lakini uzalishaji wa kiwanda hauendani na mahitaji ya soko hivyo kutoa mianya wafanyabishara wasio waaminifu kuingiza sokoni kopi ya bidhaa za URAFIKI jambo ambalo si haki. Kamati inaishauri Serikali kufanya upembuzi yakinifu kwa kiwanda na kubaini changamoto hasa ya kiwanda ni nini. Sambamba na hilo atafutwe muwekezaji mwingine mwenye nia njema ya kutaka kuwekeza katika kiwanda chetu.

Mheshimiwa Spika, asili ya shughuli katika viwanda vya nguo husababisha viwanda hivyo kuajiri watu wengi zaidi, mfano ni hiki kiwanda cha URAFIKI kilikuwa kimeajiri watu elfu mbili (2000). Kwa sasa ajira zipo chini ya mia nne (400), kufufuka kwa kiwanda hiki na kukiwezesha kuzalisha kwa uwezo wa kiwanda kutatoa ajira kwa watanzania. Kamati inashauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kiwanda huki kinafufualiwa.

Mheshimiwa Spika, nikweli kuwa kiwanda kilianza kufanya vibaya kabla ya kuingia ushirika na Nchi ya China lakini baada ya ushirika kiwanda kimefanya vibaya zaidi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia jambo hili kwa ukaribu zaidi, sambamba na hilo jitihada za makusudi zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa tunaendelea kulitawala soko kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

- m) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Mpango wa Serikali wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa; na Jitihada za Serikali katika kuviridisha Serikalini viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo wamiliki wake wameshindwa kviendeleza.**

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira walipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Mpango wa Serikali wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa; na Jitihada zinazochukuliwa katika kuvirudisha Serikalini viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo wamiliki wake wameshindwa kviendeleza. Uchambuzi wa Kamati ulibaini taarifa ile haikuwa na maelezo ya kujitosheleza hivyo inahitaji maboresho kwa lengo la kuongeze uelewa wa Wajumbe na kuwawezesha kuisahuri Serikali. Maeneo yaliyohitaji maboresho ni pamoja na;-

- i) Sababu zilizobainishwa kupelekea viwanda kutokufanya kazi hazina uhalisia kwani Viwanda vyote viliuzwa kwa kuzingatia Mpango wa kibiashara (*Business plan*) lakini pia wamiliki walipewa mikataba yenye masharti ya kviendesha viwanda vile. Kamati inataka kujua kinachokwamisha Serikali kuwachukulia hatua wale wote waliokiuka Mikataba na masharti kwa kuwa mikataba tayari ilikwisha wafunga;

- ii) Kuna idadi ya Viwanda 156 vilivyobinafsishwa, Kamati inataka kujua ni Viwanda vingapi vinaweza kurudishwa/kufufuliwa na kuweza kufanya kazi na vingapi haviwezekani kufufuliwa ili vitoke katika idadi ya viwanda vilivyopo nchini; na nini Mpango wa Serikali wa kuyatumia maeneo ya viwanda vilivyo shindikanika kwa shughuli nyingine za maendeleo.
- iii) Kuna baadhi ya mikataba iliyotumika kubinafsisha Viwanda hivi haikuwa na kipengele kinachotoa nguvu ya kuvirudisha Serikalini. Kamati inahitaji kujua mikataba hii ilisainiwa vipi bila kuwa na kipengele hicho na hatua gani zinachukuliwa kutatua changamoto ya mikataba hii;
- iv) Kuna baadhi ya Viwanda vimetajwa kuwa chini ya uangalizi wa Serikali, hakuna maelezo ya namna Serikali inafanya uangalizi kwa kiwanda hivyo;
- v) Toka Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na Viwanda umefanyika ni takriban miaka 20 sasa, katika kipindi chote hicho kuna baadhi ya Viwanda havikuwahi kufanya kazi tarajiwa kabisa. Kamati inataka kujua ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali dhidi ya wamiliki wa viwanda hivyo.
- vi) katika zoezi la kuhamasisha kufufua viwanda vilivyobinafsishwa, kuna baadhi ya wewekezaji wameitikia wito wa Serikali wa kufufua viwanda walivyobinafsishiwa, walivifufua na kufanikiwa kuviendeleza lakini ndani ya mwaka mmoja tu wamevifunga. Kamati inataka kujua ni hatua gani za zaidi zimeendelea kuchukuliwa na Serikali katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, katika viwanda vilivyobinafsishwa kuna viwanda kumi (10) vinafanya kazi vizuri ikiwepo kiwanda cha Sigara

(TCC), kiwanda cha mabati cha ALAF, Kiwanda cha bia TBL n.k. Kamati inaishauri Serikali kuvienzi viwanda hivi vya kihistoria, sambamba na hilo tubainishe changamoto zinazovikabili viwanda hivi na kuzishughulikia kwa lengo la kuviondoa katika hatari ya kufungwa kama vyenzi;

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, baada ya kuona kuna uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo aliamua kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao hayo kwa nia ya kuyaongezea thamani mazao lakini pia alilenga kuchochea ukuaji wa uchumi na kutoa ajira. Viwanda vile vya kihistoria vilipitia hatua tofauti tofauti na hatua ya mwisho ilikuwa ni kuvibinafsisha kwa lengo la kviendeleza viwanda hivyo, kuongeza ajira na mapato ya Serikali kupitia kodi na kuiruhusu sekta binafsi kumiliki uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, jitihada za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa kwa lengo ka kutimizi madhumuni halisi ya ubinafsishaji.

- n) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa KAIZEN; Mpango wa Serikali katika kutumia falsafa ya KAIZEN; Namna Serikali inavyoishirikisha Sekta Binafsi (CTI, TPSF na TCCIA n.k) katika utekelezaji wa Mradi wa KAIZEN.**

Mheshimiwa Spika, KAIZEN ni neno lililotoholewa katika lugha ya kijapani linalomaanisha *Change for Better*, KAIZEN ni mfumo wa kuweka hali ya maelewano na ushirikiano miongoni mwa watumishi na uongozi katika kutumia mbinu bunifu kwa lengo la kuleta mabadiliko chanya katika kuimarisha ubora, uwajibikaji na tija endelevu kwenye kampuni au kiwandani katika mlolongo mzima wa uzalishaji ili kukidhi ushindani.

Mheshimiwa Spika, falsafa ya KAIZEN inalenga kuleta mabadiliko ya mtizamo wa watendaji wa viwanda ili kuongeza ufanisi, tija na ubora wa bidhaa. Zimeandaliwa programu mbalimbali za kufundishia chini ya KAIZEN ambapo mkufuzi kufikisha elimu kupitia programu hizo, mkufunzi pia huzungukia eneo la kiwanda na kubainisha changamoto za kiwanda kwa lengo wa kuwapatia huduma hiyo kulingana na mazingira halisi ya kiwanda chao. Tija ya utekelezaji wa falsafa hii huanza kuoneka mara baada ya mafunzo ambapo mabadiliko makubwa hupatikana kuanzia katika ari ya wafanyakazi, mahusiano ya wafanyakazi na waajiri na hata katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa utekelezaji wa falsafa hii umehusisha Sekta binafsi ambapo wanaanza kushirikishwa kuanzia kwenye Kamati ya Kitaifa ya kusimamia Mradi kama wajumbe wa kamati. Kamati hii inajukumu la kuidhinisha mpangokazi wa mradi wa mwaka, mkakati wa utekelezaji wa mradi, taarifa za utekelezaji wa mradi na kushauri kuhusu uboreshaji wa utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa KAIZEN upo katika awamu ya pili na unatekelezwa kupitia ufadhili wa nchi ya Japan, changamoto ya miradi inayotekelezwa na wafadhili haina *guarantee* ya utekelezaji wake kuendelea. Mipango ya Wizara ya kuiendeleza falsafa ya KAIZEN pindi ufadhili utakapoisha ni kuanza kuwatoza ada wahitaji ili waweze kuuendeleza jambo ambalo litakuwa si jema sana kwa waratibu lakini pia wahitaji wa huduma kwa kuwa walishazoea kuipata bure. Kamati inaishauri Serikali kujipanga kuuendeleza mradi huu kwa fedha zake ili kuonyesha wadau mapenzi/ushiriki wa Serikali katika kujenga na kuimarisha Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Spika, falsafa ya KAIZEN inatekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, na jukumu la kusimamia kiwanda cha URAFIKI lipo chini ya Wizara hiyo, falsafa hii imevisaidia/nufaisha viwanda vingi na kuhakikisha vinafanya kazi kufikia uwezo wake. Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kabla awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi haijaisha wanakisaidia kiwanda chetu cha URAFIKI.

Mheshimiwa Spika, falsafa ya KAIZEN ni nzuri sana imekuwa ikisaidia viwanda vingi lakini inafahamika kwa watu wachache tu. Kamati inaishauri Wizara kuitangaza katika vipindi vya redio na televisheni ili kukuza uelewa wa huduma hii nzuri.

- o) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Sera zinazosimamia Ujenzi wa Viwanda;-**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara inasimamia na kuratibu Sera kuu nne (4) ambazo ni Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996-2020, Sera ya Maendeleo ya Viwanda vidogo na Biashara ndogo ya mwaka 2003, Sera ya Taifa Biashara ya mwaka 2003 na Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo ya mwaka 2008. Kabla Sekta ya Uwekezaji kuhamishiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ilikuwa inasimamia Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, Sera hizi mahsusi za usimamizi wa ujenzi wa Tanzania ya Viwanda ni za muda mrefu sana zina umri takribani **miaka 11 hadi 22**, kwa mazingira ya sasa ya biashara zinaonekana kupitwa na muda. Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya sera hizi na kuziboresha ili

kuhakikisha zinaendana na mazingira ya sasa ya kufanyia biashara. Sambamba na Sera, Sheria za usimamiza wa biashara pia zimepitwa na wakati haziendani na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Sera, Sheria zinazosimamia sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (hususani sheria zilizounda mamlaka za udhibiti) ni nzuri lakini ziliandaliwa kuendana na mazingira ya biashara ya wakati huo. Kamati inasisitiza Serikali kuzipitiwa upya sheria hizi na kuboresha kwa lengo la kuziwezesha kuendana na mazingira ya sasa ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda lakini tunaenda kujenga viwanda ambavyo havitakuwa na uhai mrefu, kinachopelekea kuuu viwanda vyetu vya ndani ni gharama kubwa za uzalishaji kuanzia hatua ya uzalishaji mpaka kufika Sokoni. Hatua hii inapelekea bidhaa zinazozalisha nchini kuwa kubwa na kushindwa kushindana katika soko matokeo nchi yetu imekuwa soko la bidhaa kutoka nche. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa kuna haja ya Serikali kukaa chini na wazalishaji wa ndani na kubainisha gharama zao za uzalisha na Serikali kuangalia namna ya kuwapunguzia mzigo huo, hatua hii itawasaidia wazalishaji wa ndani kuzalisha kwa gharama nafuu na kuweza kushindana katika soko.

- p) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2018**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mafungu yote Mawili (Fungu **44** na **60**) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **143,334,153,648.00**

kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **43,309,628,648.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **100,024,525,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **20,006,300,000.00**

Mheshimiwa Spika, Kamati iliarifiwa kuwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018 Wizara ilikuwa imepokea shilingi **26,703,462,562.00** kwa mafungu yote mawili, kiasi hiki ni sawa na asilimia **18.63** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zilizopokelewa ni shilingi **6,477,221,314** tu ndio imetolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, kiasi hichi ni sawa na asilimia **6.47** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Utoaji huu wa fedha za maendeleo haouonyeshi uwiano sawa wa matumizi ya kawadi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inendelea kuishauri Serikali kupeleka kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa lengo la kuziwezesha wizara zetu kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makusanyo hadi kufikia Disemba, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **7,900,492,248.00** sawa na asilimia **39.5** ya kiasi ilichoipangia kukusanya kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kwa mahesabu ya kawaida Wizara ilipaswa kuwa imekusanya asilimia 50 ya lengo iliyokuwa imejipangia lakini imekusanya asilimia **39.5** tu. Kamati inaishauri Serikali kuangalia changamoto zilizokwamisha kufikia lengo lililokusudia na kuzitatua, hili liende sambamba na kuangalia kama ilijipangia makusanyo yanayoendana na uwezo wake halisi wa kukusanya.

2.5 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inasimamia na kushauri kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu masuala ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha Machi, 2018 hadi Januari, 2019 ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii. Taarifa hizo ni kama ifuatavyo:-

- a) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Mikakati ya Serikali katika kutekeleza kaulimbiu yake ya Wiki ya Mazingira ambayo ni “Mkaa ni gharama tumia Nishati mbadala”.**

Mheshimiwa Spika, ripoti ya pili ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2014 imebainisha kuwa kasi ya uharibifu wa misitu ni kubwa ambapo kila mwaka zaidi ya hakta 372,000 zinapotea. Moja ya jambo linalochangia upotevu wa misitu kwa kiasi kikubwa ni ukataji wa misitu kwa ajili ya kupata nishati ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, Biashara ya kuni na mkaa ni chanzo cha mapato lakini pia inatoa ajira kwa jamii wananchi wanaojihusisha na biashara hiyo. Changamoto inakuja katika zoezi la kuzalisha bidhaa hii ambapo kwa kiasi kikubwa linaendeshwa kinyume na taratibu na sheria za kuendesha biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya jamii haziwezi kabisa kuacha matumizi ya kuni na mkaa, na hii ni kutokana na asili ya shughuli zao. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango wa kuzielimisha jamii hizi kuhusu uvunaji endelevu wa misitu yetu kwa ajili ya mkaa, hatua ambayo

itakuwa ya faida kwa wote ambapo Serikali kuendelea kukusanya kodi ya zao la mkaa, wazalisha na wauza mkaa watajipatia kipato na watumiaji watapata bidhaa;

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna taasisi zisizo za kiserikali (NGO's) mbalimbali zinaunga mkono matumizi ya mkaa, lakini zinahimiza kutumia uvunaji endelevu wa misitu yetu. Kamati inaishauri Serikali kuzitambua taasisi hizo na kufanya nazo kazi katika kusambaza elimu ya uvunaji endelevu.

Mheshimiwa Spika, kutegemea gesi ya LPG kama nishati mbadala ni kuwaumiza watanzania kwa kuwa bei ya nishati hii ni kubwa na inaendelea kupanda. Kamati inapongeza mpango wa Serikali wa kutaka kuanza kusindika gesi asili ili iweze kutumika majumbani, utekelezaji wa mpango huu ufanyike haraka ili kuiokoa misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, Nishati ya kuni na mkaa ni tegemeo la watu wengi na takwimu zinaonyesha takribani asilimia 90 ya watanzania wanatumia nishati hiyo kutokana na kuwa inapatikana kwa bei nafuu. Kamati inashauri ufanyikie utafiti wa kutosha ili kupata nishati mbadala ambazo zitakuwa za kudumu na bei nafuu, upatikanaji wa nishati mbadala ya bei nafuu itasaidia kupunguza matumizi ya nishati ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Spika, kuna matumizi makubwa ya nishati ya mkaa na kuni katika taasisi za Serikali hususani Magereza na shule za bweni nchini jambo linalopelekea ukataji misitu kwa kiasi kikubwa na kupelekea maeneo mengi kuwa na hali ya jangwa. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mahsusi kwa ajili ya kuzipatia taasisi hizi nishati mbadala ili kuokoa kiasi kikubwa cha miti inayokatwa kwa ajili ya kuni na mkaa. Sambamba

na hilo taasisi hizi zihimizwe kuwa na mashamba ya miti, kuzalisha na kutumia biogas na majiko banifu.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Uvunaji wa miti zimekuwa kikwazo katika baadhi ya maeneo, mfano mkulima akitaka kusafisha eneo kwa ajili ya kilimo na akavuna miti iliyopo katika eneo hilo, hutozwa tozo kama wavunaji miti ya mkaa. Hatua hii hupelekea baadhi ya wakulima kuamua kuteketeza kwa moto maeneo hayo ili wasikutwe na miti. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia tena Sheria hii ili itoe maelekezo ya namna itakavyotumika kwa baadhi ya maeneo.

- b) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa kupambana na kuenea kwa Hali Jangwa na Ukame.**

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 61 ya nchi yetu ya Tanzania ipo hatarini kugeuka jangwa, mikoa iliyoathirika zaidi ni pamoja na Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara na baadhi ya maeneo ya MKoa wa Kilimanjaro. Juhudi za makusudi zinahitajika katika kupambana na hali hii ili kujinusu na balaa la jangwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali katika kipambana na balaa la kuenea kwa hali ya jangwa na ukame ni pamoja na kujiunga katika Mikataba mbalimbali inayohusiana na uhifadhi wa Mazingira ambapo kwa sasa Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na imekuwa ikishiriki katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali chini ya Mkataba huu ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi inayolenga matumizi bora na endelevu ya ardhi, kushiriki

mikutano ya nchi wanachama na kuandaa mpango kazi wa kitaifa katika kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, kama nchi mwanachama wa Mkataba huu Tanzania imeweza kunufaika na ufadhili wa kutekeleza miradi na mbalimbali ambapo mpaka sasa tumefanikiwa kutekeleza miradi minne (4) ambayo ni Mradi wa kujenga uwezo wa kitaasisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira; mradi wa kuokoa maeneo yaliyoharibika ya miinuko ya Kilimanjaro; Mradi wa kuhifadhi Misitu ya Miomboi Tabora na Katavi; na program ya kuandaa shabaha ya kuzuia uharibifu wa ardhi. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuridhia kuwa Mwanachama wa Mkataba huu muhimu ambao umetuwezesha kupata manufaa.

Mheshimwa Spika, kwa nia ya kupunguza athari ya kuenea kwa hali ya jangwa na Ukame. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ambapo itabainisha kila aina ya shughuli itakayofanyika katika eneo husika na jamii zijengee uelewa juu ya matumizi bora ya ardhi. Sambamba na hilo Serikali iongeze juhudi katika kulinda maeneo yaliyohifadhiwa kama ardhi owevu, misitu, mbuga za wanyama na mapori endelevu. Aidha, jamii ipatiwe elimu juu ya faida zipatikanazo katika kuhifadhi maeneo husika, hatua ambayo itazifanya jamii kuwa miongoni mwa walenzi wa hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina faida ya kuwa na maeneo mengi yaliyohifadhiwa lakini pia zinafanyika jitihada kubwa za kutunza mazingira, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango wa kutambua fedha na nguvu kazi (*shadow prising*) inayotumika katika maeneo ya hifadhi, ili kubainisha juhudi za nchi katika kupambana na hewa ukaa jambo litakalotuwezesha kupata

ufadhili zaidi kutoka katika mifuko ya usimamizi wa mazingira ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kampeni za Serikali za Upandaji miti zitekelezwe kwa kuzingatia maeneo yaliyoathirika zaidi na ukame lakini pia miti inayopandwa izingatie asili ya eneo husika ilikupata matokeo mazuri. Sambamba na hilo Serikali ifuatilie miradi ya maji iliyoanzishwa kwa ajili ya umwagiliaji vitalu hatua hii itasidia ufanisi wa Kampeni hizi.

Mheshimiwa Spika, katika kuilinda misitu yetu Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira ishirikiane na Wizara yenye dhamana ya misitu kuandaa mpango wa usimamizi na uvunaji wa misitu yetu, pia kutengwa maeneo ya hifadhi na maeneo ya kuvuna miti.

- c) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Juhudi za Kuhifadhi Ziwa Manyara na Ziwa Jipe ambayo yapo katika hatari ya kutoweka.**

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeneemeka takribani asilimia 10 ya eneo la nchi yetu limefunikwa na ardhi owevu ambayo inajumuisha maziwa, bahari, mito, mabwawa n.k. Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004 zinaelekeza na kusisitiza umuhimu wa kutunza na kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Maziwa, Mito, Mabwawa pamoja na vyanzo vya maji kwa kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali ikiwemo jamii. Serikali za Mitaa zimepewa wajibu wa kuhakikisha rasilimali maji zilizopo katika maeneo yao zinalindwa na kutunzwa.

Mheshimiwa Spika, maziwa ikiwemo ziwa Manyara na Jipe yana manufaa makubwa

ambayo ni pamoja na kuboresha afya na kipato cha wakazi wa eneo linalozunguka ziwa kwa shughuli za uvuvi; kuboresha hali ya hewa na kuleta mandhari nzuri; ardhi ya kando kando ya ziwa huwa na rutuba nyingi hivyo kuvutia shughuli za kilimo; na pia wanyama, ndege na bioanuai zinazopatikana katika maeneo ya maziwa huvutia shughuli za utalii hivyo kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa yapatikanayo katika maeneo ya hifadhi za maziwa lakini bado kuna uharibifu mkubwa unaofanyika kutokana na shughuli za binadamu za kiuchumi (mfano Uvuvi, Kilimo kuzunguka eneo la ziwa na vyanzo vya maji vya ziwa, unyweshaji wa mifugo n.k). Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa jamii wanaozunguka maeneo ya hifadhi za maziwa kuhusu ya athari za kuharibu mazingira hayo, pia jamii ifundishwe namna bora ya utekelezaji wa shughuli zao bila kuathiri hifadhi ya maziwa pamoja na vyanzo vyake vya maji.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Manyara na Jipe yanapatikana katika mipaka ya nchi yetu na nchi ya Kenya lakini jitihada za uhifadhi wa maziwa haya zinaonekana kuwa za upande mmoja yani Tanzania tu. Kamati inaishauri Serikali kukutana na nchi husika na kurejea makubaliano ya Uhifadhi waliyowekeana kwa lengo la kuongeza uhifadhi wa maziwa haya.

Mheshimiwa Spika, asilimia 51 ya ziwa Manyara ipo katika hifadhi ya Taifa na 49 iliyobaki ipo katika usimamizi wa Serikali za Mitaa ambao wameonekana kutotilia uzito uhifadhi wa sehemu waliyopewa. Kamati inashauri Serikali kubadilisha umiliki huo na asilimilia 100 ya eneo la Manyara zote ziwekwe chini ya hifadhi kwa kuwa

Halimashauri haijalipa kipaumbele uhifadhi wa sehemu ya Ziwa waliyoachiwa.

d) **Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Basel kuhusu Udhhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu.**

Mheshimiwa Spika, ongezeko la uzalishaji taka hatarishi na zenye sumu katika nchi zenye viwanda kulipelekea uhitaji wa kuwa na utaratibu wa kudhibiti usafirishaji wa taka hizo na utupaji wake kwa namna ambayo haina madhara kwa mazingira, watu na viumbe wengine. Majadiliano yalifanyika chini ya Umoja wa Mataifa na hatimaye mkataba wa Basel ulipitishwa. Mkataba wa Basel unahusu Udhhibiti wa Usafirishaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na utupaji wake.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa Mkataba huu ilikuwa ni kwa ajili ya kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa kudhibiti uzalishaji, usafirishaji na utupaji wa taka zenye sumu. Kwa nchi ya Tanzania Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa kushirikian ana Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira - *NEMC* pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ndio inasimamia utekelezaji wa Mkataba huu ambapo kila mmoja amepewa majukumu yake kuhusiana na utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya teknolojia yamewezesha urejeleshaji wa taka hatarishi kwa lengo la kupata malighafi au kuongeza thamani na kupata mali nyingine hatua ambayo imechochea kwa kiasi kikubwa ukusanyaji, usafirishaji na biashara ya taka ikiwemo chuma chakavu, betri mbovu, mafuta na vifaa chakavu vya kielektroniki. Hivyo hatua ya Serikali ya kuridhia mkataba huu ilikuwa njema ukizingatia nchi yetu

bado haijawa na miundombinu na teknolojia ya urejeleshaji wa taka hatarishi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa taka hatarishi hapa nchini unakabiliwa na changamoto ikiwemo uelewa mdogo wa wadau wanaojihusisha na ukusanyaji, utunzaji na usafirishaji wa taka hizo. Madhara yanayopatikana kutokana na *kumis-handle* taka hizi ni makubwa, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wadau wanaojishughulisha na shughuli hizo ili kuinusuru nchi na madhara yanayoweza kupatikana.

Mheshimwa Spika, nchi yetu bado haina miundombinu na teknolojia ya urejeleshaji wa taka hatarishi jambo ambalo tunalazimika kuzisafirisha nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji kutafuta wawekezaji ambao watakuwa tayari kuwekeza katika shughuli za urejeleshaji wa taka hatarishi hatua ambayo itatusaidia kupunguza gharama za kuzisafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali za kuwa mwanachama wa mikataba mbalimbali ya uhifadhi wa Mazingira, lakini inatoa angalizo kwa Serikali kuhakikisha nchi inapata manufaa stahiki yatokanayo na mikataba hiyo. Serikali ipitie upya mikataba yate iliyowahi ingia kisha kuandaa mpango mkakati wa kuitekeleza kwa manufaa ya nchi.

- e) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika Ngazi ya Serikali za Mitaa; na Changamoto zilizopo katika Utekelezaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na mikakati ya kuzikabili.**

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ilipitishwa na Bunge Mwaka 2004 na kupewa jukumu la kuweka mfumo wa kitaasisi ambao utakuwa na mipango endelevu ya kutunza na kuhifadhi mazingira. Sheria hii inatamka kuwa mazingira ni urithi wa kizazi kilichopo na vijavyo na inampa kila mtu anayeishi Tanzania haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uasimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 imebainisha majukumu na wajibu wa kila Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia masuala ya Uhifadhi wa Mazingira. Aidha, Sheria hii imezielekeza Halmashauri za Jiji, Manispaa, Wilaya na Mji kuteua au kuajiri Ofisa Usimamizi wa Mazingira ambaye ndio huwa msimamizi mkuu wa masuala ya mazingira katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, Ofisa Mazingira ambae ni muajiriwa katika ngazi ya Serikali za Mitaa amepewa majukumu ya kusimamia masuala yote ya mazingira katika eneo lake na kuhakikisha yanatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Pia Sheria inamuelekeza kushauri Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya eneo lake kuhusu masuala yote ya mazingira; kuandaa taarifa kuhusu hali ya mazingira ndani ya eneo husika; na Kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC kuhusu utekelezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira unakumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa watumishi hasa wa fani ya Maafisa Mazingira; masuala ya usimamizi wa mazingira katika ngazi ya serikali za mitaa kutopewa umuhimu na kuchukuliwa kama kufanya usafi; Bajeti kidogo

inayotengwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika shughuli za Mazingira; Uelewa mdogo wa wananchi na watendaji katika ngazi mbalimbali juu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira; Upungufu wa vitendea kazi ambao hukwamisha shughuli za uratibu wa kazi mazingira; Ushiriki mdogo wa Serikali za Mitaa katika kuandaa mipango ya hifadhi ya mazingira na usimamizi wa Sheria ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, jamii inaelewa mdogo juu ya umuhimu wa utunzaji mazingira jambo linalopelekea ukiukwaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kiasi kikubwa. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiwezesha Ofisi ya Makamu Rais-Mazingira kirasilimali fedha na watu ili waweze kuwafikia watanzania wengi na kuwapatia elimu ya Uhifadhi wa Mazingira (faida za kuyatunza na Hasara ya kuyaharibu) kwani kwa sasa uelewa wa jamii nyingi kuwa kufanya usafi tu ndio kutunza mazingira;

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya utekelezaji wa Sheria ya Mita 60, baadhi ya maeneo yameathiriwa na Mabadiliko ya Tabia nchi hivyo kusababisha vyanzo vya maji kusogea mpaka kwenye maeneo ya wakazi au wanapoendeshea shughuli zao za kijamii. Kamati inaishauri Serikali kupitia NEMC na Wizara ya Maji kutafuta ufumbuzi wa haraka wanamna ya kutekeleza Sheria ya Mita 60 kwa lengo la kuondoa migogoro iliyopo lakini pia kuwanusuru watu ambao maeneo yao yamefikwa na vyanzo vya maji kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi;

Mheshimiwa Spika, shughuli za uchimbaji madini zimekuwa zikichafua mazingira kwa kiasi kikubwa ndio maana Sheria ya Madini iliweka kifungu ambacho kinamlazimu muwekezaji kutenga

fedha kwa ajili ya kurejelesha mazingira ya mgodi baada ya kufungwa. Changamoto ni fedha zilizotengwa hupokelewa na kuratibiwa na Wizara ya Nishati ambayo si Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa Mazingira, na mwisho wa siku kutumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Kamati inashauri fedha hizo zipelekwe kwa Wizara yenye dhamana ya Mazingira, sambamba na hili sheria za ufungaji wa migodi iwekwe kipengele kinachotoa fursa kwa wakazi wa eneo husika kushirikishwa/kushauri katika zoezi la kufunga mgodi ambapo watashauri nini kifanyike katika eneo lao kwa kuzingatia shughuli za maendeleo za eneo husika;

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Mazingira ni ya Mwaka 1997 takribani miaka 22 ambapo kuna mambo mengi yamekwishatokea na hayakuhusiswa kwenye Sera hii (mfano mabadiliko ya Tabia nchi na viumbe vamizi). Sambamba na hilo Sera hiyo inatekelezwa kutumia Sheria ya mwaka 2004 ambayo imehusisha mabadiliko mbalimbali ambayo hayapo kwenye Sera. Kamati inaishauri kufanya mapitio ya Sera ye Taifa ya Mazingira na kuihuisha ili iendane na hali halisi ya mazingira kwa sasa.

- f) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utendaji wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (National Environmental Management Council – NEMC)**

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni taasisi ya Serikali inayotekelaza majukumu yake chini ya usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Baraza hili lilianzishwa chini ya Sheria Namba 19 ya Mazingira mnamo mwaka 1983 ambapo ilikuwa

na jukumu la kutoa ushauri kwa Serikali na wadau kuhusu masuala ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutungwa kwa Sheria ya Usimamizai wa Mazingira ya Mwaka 2004 majukumu ya baraza yalihuwishwa na kuwa ni kuratibu utekelezaji wa sera na sheria ya mazingira katika Nyanja kuu nne ambazo ni kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa mazingira; kusimamia mchakato wa tathimini ya athari za mazingira; kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya maamuzi yanayohusu mazingira; na kusimamia kwa ujumla mambo yote yanayohusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Majukumu yake Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira linakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watumishi wenye fani ya mazingira katika Baraza ukilinganisha na majukumu ya baraza kitaifa; uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sheria za mazingira jambo linalopelekea kutokuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira; na ushirikiano mdogo wa wadau wengine katika kusimamia utekelezaji wa sheria ya mazingira wakati sheria hiyo imempa kila mdau majukumu yake;

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira linadhamana kubwa ya kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira lakini kuna baadhi ya maamuzi ni lazima yafanywe na Waziri mwenye dhamana. Kamati inashauri NEMC wapewe mamlaka kamili, badala ya kuwa Baraza iwe Mamlaka ya Taifa ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, hatua hii itaipaa mamlaka kamili ya kusimamia masuala ya Mazingira na pia tutampunguzia Waziri majukumu.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wengi huwa hawaweki uzito katika suala la vibali vya mazingira, huanza kutafuta vibali hivi dakika za mwisho wakati ambapo wamesha pata vibali vingine vya uwekezaji na kutegemea kupata cheti cha mazingira kwa muda mfupi jambo ambalo haliwezekani kwa kuwa EIA ni mchakato mrefu kidogo. Kamati inaishauri Serikali kupitia mamlaka zake zinazoratibu uwekezaji, kuwashauri Wawekezaji kufuatilia kibali cha mazingira sambamba na vibali vingine ili kutoa nafasi kwa mchakato wa EIA kukamilika;

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kukasimisha jukumu la kusaini na kutoa vyeti cha EIA kwa NEMC ambao ndio wasimamizi wakuu wa zoezi hili, kwa sasa cheti ni mpaka kinasainiwa na Waziri mwenye dhamana ya mazingira ambae anamajukumu mengine mengi;

Mheshimiwa Spika, mipango miji yetu ni ya zamani sana jambo ambalo linaleta mgongano katika matumizi ya ardhi, kuna baadhi ya maeneo viwanda vimejengwa katika makazi na kwingine makazi yamejengwa maeneo ya Viwanda, na maeneo mengine machinjio yapo katika maeneo ya makazi. Kamati inaishauri Serikali kuipitia upya ramani za mipango miji na kuiboresha kwa lengo la kuondoa migogoro inayoendelea;

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi nchini hayana vituo vya kuteketeza taka hatarishi jambo ambalo linalazimu wazalishaji taka hizo kuzisafirisha mpaka Dar es Salaam jambo ambalo si salama kwa kuwa zimekuwa zikianguka mabarabarani na kuhatarisha afya za wapiti njia. Kamati inaishauri Serikali kupitia NEMC kushawishi wawekezaji wengi zaidi kuwekeza katika maeneo mengi zaidi ili kuondoa hii adha ya kuzisafirisha kwenda Dar es Salaam;

g) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Changamoto za Viumbe Wageni vamizi katika Mazingira**

Mheshimiwa Spika, Viumbe Wageni/Vamizi ni Kiumbe chochote kigeni katika mazingira ambacho uwepo wake huleta madhara kwa mazingira, uchumi, baionuai, afya ya jamii, mifugo na mimea. Chanzo cha Viumbe vamizi ni Shughuli za kibinadamu ambazo huwaleta viumbe maeneo mapya, shughuli hizo ni pamoja na majaribio ya mazao ya kilimo, misitu na mifugo; mizunguko ya mifugo toka eneo moja na jingine; mabadiliko ya tabianchi; viumbe kubadili tabia kukabiliana na mabadiliko yeyote; maendeleo ya mifumo ya usafiri duniani (mf. Safari za meli); na Mifumo ya asili kama Upepo.

Mheshimiwa Spika, madhara ya Viumbe Vamizi yameanza kuonekana tena kwa kasi katika Mazingira, madhara hayo ni pamoja na kupungua kwa bionuai na kuharibu vyanzo vya maji; kiuchumi hupunguza uzalishaji kilimo na kuathiri shughuli za utalii; kiafya na jamii husababisha kueneza magonjwa na kupunguza uzalishaji chakula. Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kina na kubaini Viumbe wageni/vamizi waliopo nchini na maeneo wanapopatikana, hatua hii itatoa picha ya ukubwa wa tatizo na kujipanga namna ya kulitatua;

Mheshimiwa Spika, Kuna baadhi ya mimea ni migeni na vamizi lakini yaweza kuwa na faida, Kamati inashauri Serikali ifanye utafiti kuhusu mimea hii vamizi na kubaini faida na madhara yake kisha ndio ifanye uamuzi wa kuyateketeza;

Mheshimiwa Spika, Kuna baadhi ya viumbe wageni/vamizi ambayo athari zake katika mazingira zimekwishaonekana na zinaenea kwa

kasi sana mfano gugu karoti ambalo pia ni sumu, Kamati inashari zichukuliwe hatua za haraka katika kuteketeza mmea huu;

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nchi haina mpango mkakati wala miongozo ya kushughulikia changamoto ya Viumbe vamizi jambo linalopelekea ugumu kutatua changamoto hii. Kamati inatambua kuwa kuna kikosi kazi kimeundwa kwa ajili kushughulikia changamoto ya viumbe wageni vamizi, Kamati inaomba kushirikishwa kabla taarifa hiyo kabla haijawa *final* kwa lengo la kushauri tu.

- h) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Uhifadhi wa maeneo lindwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira; na Jitihada za Serikali katika kuyahifadhi maeneo lindwa.**

Mheshimiwa Spika, takribani asilimia 30 ya eneo la nchi hii imehifadhiwa kisheria kwa namna moja ama nyingine, maeneo hayo yanajumuisha mbuga za taifa, mapori ya akiba ya wanyama pori, hifadhi ya bahari, misitu ya akiba.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya mazingira sura ya 191 katika kusimamia maeneo lindwa imempa Waziri mwenye dhamana ya mazingira mamlaka kutangaza eneo lolote la ardhi linaloweza kuharibika upesi kiikolojia au eneo nyeti, kuwa eneo lindwa lakini anapaswa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Mazingira. Sheria hii pia imeweka usimamiazi wa maeneo lindwa chini ya Mamlaka ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya kuanzisha maeneo lindwa au nyeti ya Mazingira ni pamoja na kukuza na kuboresha sekta ya utalii, vyanzo

vya maji na umeme, hifadhi ya bioanuai (wanyama, wadudu, ndege)

Mheshimiwa Spika, Sheria za kusimamia maeneo lindwa zinajitoshleza sana tatizo lipo katika usimamizi wa maeneo hayo, ambao unasababishwa na ufinyu wa rasilimali fedha na watu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya wizara hii muhimu na kutoa vibali vya kuajiri maafisa mazingira wenye taaluma ya mazingira kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mazingira;

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mazingira unadhamana ya kubwa ya kusimamia mazingira lakini unakumbana na changamoto ya fedha, Kamati inaishauri Serikali kuuwezesha mfuko wa mazingira na kuupatia kibali cha kukusanya asilimia chache ya tozo zinazohusiana na mazingira, kuimarika kwa Mfuko huu kutaiwezesha Wizara ya Mazingira kutekeleza majukumu yake bila kutegemea fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali;

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuzieliisha jamii juu ya uhifadhi wa maeneo lindwa, lakini elimu hii izingatie wahusika wa eneo, aina ya maisha na shughuli wanazofanya ukihusianisha na aina ya uharibifu wa mazingira wanaofanya ili kuhakikisha wanapata elimu stahiki (mkulima, Mfugaji, mvuna mkaa hawa wanafanya shughuli tofauti na utaribifu tofauti) hatua hii itasaidia kupunguza migogoro inayotokea kati ya maafisa mazingira na jamii;

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo lindwa yapo katika umiliki wa watu Binafsi (mfano eneo la kuzunguka ziwa Chale hivyo faida za utalii katika ziwa chale zinaenda kwa mtu binafsi) na Wizara yenye mamlaka ya kusimamia mazingira hana mamlaka ya kuingia katika maeneo hayo.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha maeneo yote ya Vivutio na Lindwa yanawekwa chini ya Umiliki wa Serikali ili kuhakikisha manufaa ya maeneo hayo yanakuwa ya nchi na sio watu binafsi.

i) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kuhusu Muongozo wa Taifa wa Tathimini ya Mazingira kimkakati (SEA).**

Mheshimiwa Spika, Tathimini ya Mazingira Kimkakati (TMK) ni utaratibu wa kuhusisha au kutathimini masuala ya mazingira ili kuleta dhana ya uendeleu katika ngazi ya miswada, kanuni, sera, mikakati, progamu na mipango ikihusisha masuala ya usimamizi wa mazingira. Utaratibu huu ulianzishwa miaka ya 1960 baada ya mapinduzi ya Viwanda, kwa Tanzania ulianza kutumika rasmi baada ya kuanzishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kabla ya hapo TMK ilikuwa inafanyika kihiyari tu.

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Tathimini ya Mazingira Kimkakati unaelekeza hatua na ngazi mbalimbali za kufuatwa katika kusimamia TMK lengo likiwa ni kuhakikisha masuala ya mazingira yanajumuishwa mapema katika mipango ya maendeleo ili kuleta maendeleo endelevu na kubainisha fursa na vikwazo vinavyoweza kuathiri au kuathiriwa na sera, miswada, kanuni, mikakati, mipango na program.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kufanya Tathimini ya Mazingira Kimkakati kwani husaidia kutambua mibadala ya maendeleo mapema na kutoa miongozo stahiki katika hatua ya sera, miswada, mipango na mikakati; kushirikisha wadau wote katika hatua ya mwanzo ya mipango ya maendeleo; kuwezesha ushirikiano wa nje ya mipaka ya nchi katika usimamizi wa maliasili za pamoja;

Tathimini ya Mazingira Kimkakati pia inaweza kusaidia kutambua na kushughulikia maeneo yanayoweza kuwa na migogoro au utofauti katika hatua za awali za kutunga sera mpya, miswada, kanuni, mikakati, mipango na programu; na hivyo kuzuia makosa yatacakayogharimu.

Mheshimiwa Spika, kufanya Tathimini ya Mazingira Kimkakati ni takwa la kisheria, kifungu Namba. 104 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kinaelekeza wakati wa kuandaa muswada ambao una uwezekano wa kuwa na athari katika usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira au usimamizi wa endelevu wa maliasili TMK inapaswa kufanyika na kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira. Sambamba na hilo, kifungu Namba 105 kinalekeza kufanya TMK katika maliasili ya madini, petrol, vituo vya kufua umeme wa maji na miradi mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuwa na Tathimini ya Mazingira Kimkakati ni kuhakikisha kunakuwa na ushiriki wa kipengele cha uhifadhi wa mazingira katika hatua za awali za utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo kwa namna moja ama nyingine itahusisha masuala ya mazingira (hususani miradi mikubwa ya maendeleo). Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha miradi yote mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali inapitia hatua za Tathimini ya Mazingira Kimkakati kwa lengo la kuhamasisha wadau binafsi kutekeleza TMK.

j) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa Nchini;**

Mheshimiwa Spika, Bioteknolojia ya Kisasa (Third generation biotechnology) - ni teknolojia inayohusisha uhamishaji wa viini tete/vinasaba

vya uhai kutoka kiumbe kimoja kwenda kiumbe kingine kisichohusiana nacho kinasaba (genetic engineering) yani jeni inaweza kuhamishwa kutoka Samaki kwenda Mimea au Kuku kwenda Nyanya.

Mheshimiwa Spika, Bioteknolojia ya Kisasa inaweza kutumika katika sekta mbalimbali kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kuleta tija kwa maendeleo endelevu. Mfano inaweza tumika katika sekta ya kilimo kuongeza uzalishaji na uboreshaji wa mazao ya kilimo; sekta ya afya kwa kutengeneza madawa na chanjo; viwandani katika kutengeneza bidhaa zinazotokana na viumbe au sehemu za viumbe pia katika kufanya urejeleshaji wa taka sumu za viwandani kabla ya kuziruhusu kutupwa.

Mheshimiwa Spika, athari zinazoweza kutokana na matumzi ya GMOs ni pamoja na uharibifu wa bioanuai na uoto wa asili wanaotumika katika majaribio; usugu wa dawa kwa matibabu ya magonjwa; kujitokeza kwa magugu na wadudu sugu; na kupotea kwa mbegu za asili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais mratibu namsimizi wa masuala yote yanayohusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa nchini. Katika kutekeleza hilo Ofisi hutoa elimu kwa umma na kujenga uwezo wa wataalaam na taasisi za utafiti na udhibiti, kusimamia usalama wa utafiti na usafirishaji wa bidhaa /mazao yanayotokana na bioteknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa nchi katika kudhibiti madhara yatokanayo na teknolojia hizi bado ni mdogo, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kuingia mikataba ya uingizaji wa bioteknolojia mpya nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nchi inakabiliwa na changamoto ya viumbe vamizi ambao wengi wa viumbe hivyo chanzo chake ilikuwa ni haya majaribio ya bioteknolojia. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini sana katika kuridhia bioteknolojia zinazolingia nchini kuwa lengo la kuepuka kufanywa nchi ya majaribio ya teknolojia hizi.

k) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Usimamizi wa Mazingira katika Sekta ya Mafuta na Gesi.**

Mheshimiwa Spika, nishari ya gesi na mafuta ni nyenzo muhimu sana katika maendeleo ya uchumi wanchi, nchi yetu imebarikiwa rasilimali ya gesi ambapo ugunduzi uliofanyika katika maeneo mbalimbali umebaini akiba ya futi za ujazo 55.098 trilioni ya gesi asilia. Gesi asilia ni nishati rafiki wa mazingira na inaweza kutumika kama nishati mbadala wa kuni, mkaa, pamoja na mafuta.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya nishati ya gesi yakisimamiwa vizuri yatachangia sana kwenye hifadhi ya mazingira. Hatua hii itasaidia kupunguza ukataji wa misitu kwa ajili ya mkaa, uzalishaji wa gesi zinazochangia uchafuzi wa hewa utapungua hatimaye mabadiliko ya tabianchi yatapungua.

Mheshimiwa Spika, Baraza limepewa mamlaka na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ya kufanya ukaguzi, utafiti na uchunguzi utakaosaidia katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Kwa muktadha huo NEMC ndio chombo tunachokitegemea katika kusimamia masuala ya mazingira katika sekta ya gesi na mafuta.

Mheshimiwa Spika, NEMC inashindwa kusimamia kikamilifu sekta ya Gesi kwa kuwa haina utaalumu na wataalamu katika sekta ya mafuta na gesi (TAM). Pia, changamoto ya upungufu wa vitendea kazi kwa ajili ya kufanya uperembaji na ufinyu wa rasilimali fedha jambo linalosababisha ishindwe kuasimamia Sekta ya gesi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mafuta na Gesi ni sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi, lakini kama zisiposimamiwa na kuratibiwa kiukamilifu katika hatua ya uziduaji ni sekta zinazoharibu mazingira kwa kasi. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha NEMC kutekeleza jukumu la kusimamia Sekta ya Mafuta na gesi kwa kuwajengea uwezo wa kitaasisi (wataalamu na utaalumu), rasilimali fedha na vitendea kazi ili waweze kusimamia sekta hii kikamilifu.

- l) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2018.**

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira katika Mwaka wa Fedha **2018/2019** waliidhiniwa shilingi **8,118,494,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,524,540,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **4,593,954,000.00** ni matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018 nusu ya Mwaka wa Fedha **2018/2019** ni shilingi shilingi **5,020,282,003.28** ambapo shilingi **4,481,482,003.00** zilitolewa kwa ajili ya Mishara na matumizi mengineyo na kiasi kilichobaki shilingi **538,800,000.00** ndio ilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya inayotengwa kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira haitoshi kupambana na uharibifu wa mazingira ambao umendelea kufanyika hususani changamoto ya Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, bajeti hii ndogo imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka jambo linaloashiria Serikali yetu kutotoa umuhimu kwa suala la uhifadhi wa mazingira. Kamati kuishauri Serikali kutoa uzito unaostahili katika suala la uhifadhi wa mazingira na ianze kwa kutenga fedha za kutosha za usimamizi wa mazingira na fedha hizo zitolewe kwa wakati.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 *Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote cha kuanzia Machi, 2018 hadi Januari 2019 Kamati ilitekelza majukumu yake ya kikanuni katika kuzisimamia Wizara pamoja na Taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati. Sasa naomba nitumie fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati na niliombe Bunge lako Tukufu liazimie kuwa Maazimio ya Bunge.

3.1.1 Upokeaji wa Fedha kutoka Hazina

KWA KUWA, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina,

NA KWA KUWA hali hiyo huchangia kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hususani Miradi ya Maendeleo,

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kujipangia Bajeti inayoakisi makusanyo halisi ya Nchi. Sambamba na hilo Kamati inashauri Serikali kujipangia miradi

michache ambayo itatekelezwa kwa wakati na kuanza nufaika na miradi hiyo kuliko kuwa na miradi mingi ambayo huishia kupatiwa fedha kidogo kidogo na utekelezaji wake unakuwa hauna tija.

3.1.2 Mradi wa Chuma wa Liganga na Mradi wa Makaa ya mawe wa Mchuchuma

KWA KUWA utekelezaji wa Miradi hii umekuwa ukisuasua na kuchukua muda mrefu sana,

NA KWA KUWA, Serikali imeonyesha wasiwasi katika mikataba ya uwekezaji kwenye miradi hii,

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kutafuta mbobezi (*expert*) ambaye atafanya utafiti katika eneo la mgodi kwa lengo la kubaini aina ya madini, kiasi cha madini kilichopo na thamani ya miradi. Utafiti huo utaipatia Serikali taarifa ambazo zitaiongoza wakati wa kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi hii. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mawazo tofauti ya utekelezaji wa Miradi hii, ambapo inaweza kufikiria kuuza chuma kama malighafi au kumtafuta muwekezaji atakaejenga kiwanda cha uchenjuaji. Sambamba na hilo Kamati inaishauri Serikali kuonyesha nia yake ya kutekeleza miradi hii kwa kuanza walau kujenga miundombinu itakayowezesha kufika katika eneo la mradi.

3.1.3 Mradi wa Kufufua Kiwanda Cha General Tyre

KWA KUWA, utekelezaji wa mradi wa kufufua kiwanda cha General tyre umechukua muda mrefu (miaka kumi) na Serikali imekwisha weka fedha nyingi lakini hakuna ambacho kinaonekana kufanyika,

HIVYO BASI, Bunge linataka kujua kama Serikali imeshapata utaratibu mzuri wa kufufua kiwanda hicho na lini kiwanda kitafufuliwa na kufanya kazi. Sambamba na hilo Bunge linashauri kama hakuna

utaratibu ambao uko tayari kwa ajili ya kukufufua kiwanda hicho ni vema eneo la kiwanda lingetumika kuendesha shughuli nyingine za uwekezaji ukizingatia eneo la kiwanda ni eneo lenye mvuto wa kibiashara (*prime area*).

3.1.4 Shirika la Maendeleo la Taifa – NDC

KWA KUWA NDC imepewa majukumu ya kusimamia miradi mingi ya maendeleo hasa ile ya kimkakati ambayo utekelezaji wake utachochea ukuaji wa sekta mbalimbali,

NA KWA KUWA, Shirika hili muhimu limekuwa likipangiwa na kupatiwa bajeti ambayo haiakisi mahitaji yake halisi,

HIVYO BASI, Bunge linaishauri NDC kwa kiasi kidogo cha fedha inachotengewa na kupatiwa ni vema katika kila Mwaka wa Fedha ikaamua kujikita na mradi mmoja ili kuutekeleza kikamilifu.

3.1.5 Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo – SIDO

KWA KUWA Serikali imeonyesha nia nzuri ya kutaka kuwashirikisha wazawa katika kujengwa uchumi wa Viwanda, watanzania wameitikia wito wa Serikali yao lakini wengi wao bado ni wajasiriamali wadogo,

NA KWA KUWA, Shirika la Viwanda vidogo – SIDO ndio limepelewa jukumu la kuweka mazingira ya msingi ya kukuza viwanda vidogo na biashara ndogo,

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali

- a) Kulingezea nguvu Shirika hili ili kuhakikisha huduma zake kuanzia elimu ya uzalishaji, masoko pamoja na mitaji vinapatikana na kuwanufaisha watanzania wengi zaidi kwa lengo la kuongeza ushiriki wao katika ujenzi wa

- uchumi wa nchi badala ya kutegemea wawekezaji kutoka nje tu; na
- b) Kuziwezesha karakana za SIDO kupata teknolojia mpya kwa lengo la kuzalisha mashine zinazoendana na mahitaji halisi ya soko ya sasa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Bunge linataka kujua kama Serikali lilifanya utafiti na kubaini kuwa mahitaji ya sasa katika maeneo ya SIDO ni kujenga mabanda (*shades*). Maana kuna baadhi ya maeneo *shades* hizo zimekuwa zikitumika kama magodauni kinyume na lengo lililokusudiwa, (mfano SIDO Iringa).

3.1.6 Utakelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo Wa Udhibiti Wa Biashara Nchini

KWA KUWA Serikali imeiaminisha Kamati pamoja na wafanyabiashara kuwa suluhisho la changamoto zote zinazoonekana na kusababisha mazingira ya kufanyia biashara kuwa magumu litapatikana katika Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*), ulioandaliwa na Serikali,

NA KWA KUWA mpango huo pamoja na mpango kazi wa utekelezaji wake vimekamilika,

HIVYO BASI Kamati linashauri Serikali kuanza utekelezaji wa mpango huu haraka iliwekanavyo. Sambamba na hilo Serikali ipange muda maalumu (*time frame*) ya utekelezaji wa mpango huu kwa lengo la kupima ufanisi wake na kuainisha changamoto ambazo zimetatuliwa baada ya kipindi hicho kupita.

3.1.7 Mazingira ya Kufanyia Biashara Nchini

KWA KUWA, mfumo wowote wa Uzalishaji unamlenga mlaji wa mwisho (*final consumer*),

NA KWA KUWA, mazingira ya kufanyia biashara yamekuwa magumu na ugumu huo kwa kiasi kikubwa unasababishwa na utekelezaji wa sheria za kodi ambazo nyingi tumezinakili kutoka kwa wenzetu walioendelea na haziendani na mazingira yetu,

NA KWA KUWA hali hiyo imepelekea baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kufunga biashara jambo ambalo halitoi taswira nzuri kwa ustawi wa watanzania lakini pia wawekezaji nchini,

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuzipitia upya na kuziboresha sheria za kodi ili ziweze kuendana na mazingira halisi ya nchini kwetu, hatua hii itachoche uwekezaji lakini pia itasaidia kumlinda mlaji.

3.1.8 Uwepo wa Bidhaa Feki Sokoni,

KWA KUWA, uwepo wa bidhaa feki sokoni unadhihirisha kuwa nchi bado haijafanikiwa kulinda mipaka yake na watendaji wasio waaminifu wanaendelea kufanya vitendo vya rushwa,

NA KWA KUWA Serikali ilitambua madhara ya bidhaa feki na kuamua kuanzisha Mamlaka za Udhibiti ambayo zina dhima ya kudhibiti na kuthibiti ubora wa bidhaa kutoka sehemu mbalimbali za ndani na nje ya nchi na kuleta ushindani sawa sokoni,

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuziongezea nguvu mamlaka hizi kwa kuzipatia rasilimali fedha na watu ili iweze kuimarisha ukaguzi wake nchi nzima. Vile vile kwa watendaji wanaojihusisha na vitendo vya rushwa wachukuliwe hatua stahiki ili kukomesha vitendo hivyo.

3.1.9 Vibali vya kuingiza Sukari Nchini

KWA KUWA, vibali vya kuingiza sukari vimekuwa vikitolewa bila kuzingatia *Gap Sugar* iliyopo kwa

wakati husika jambo linalotoa mianya kwa wafanyabiashara wasio waaminifu kuamua kupunguza uzalishaji na kuingiza sukari zaidi kutoka nje ya nchi,

KWA KUWA, hatua ya kupunguza uzalishaji inamadhara katika ajira,

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kabla ya kutoa vibali kwa mwaka 2019 ifanye tathimini upya kwa lengo la kubaini uwezo wa viwanda vya ndani na *Gap Sugar*, hatua ambayo itasaidia kubaini mahitaji halisi lakini pia kujua sifa za waombaji na kuondoa hali ya sintofahamu inayoendelea sasa.

3.1.10 Changamoto za Baraza Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira

KWA KUWA Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira limepewa majukumu ya kisheria ya kusimamia masuala ya kuhifadhi mazingira

NA KWA KUWA Baraza limekuwa likishindwa kutekeleza majukumu yake kiufanisi kutokana na ufinyu wa rasiliamali fedha, kukosa wataalamu wenye taaluma ya mazingira na kukosa vitendea kazi,

HIVYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuzingatia madhumuni ya kuanzishwa kwa chombo hiki

3.1.11 Ufinyu wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

KWA KUWA Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira imepewa jukumu kubwa la kuratibu na kusimamia masuala yote uhifadhi wa mazingira hapa nchini,

NA KWA KUWA upatikanaji wa fedha ndio nguzo ya kupata matokeo yaliyokusudiwa

HIVYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutenge Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza jukumu ya uhifadhi wa mazingira.

3.1.12 Tozo za Mazingira kuingizwa katika Mfuko wa Mazingira

KWA KUWA mfuko wa Mazingira ulianzishwa kwa madhumuni ya kuisaidia wizara yenye dhamana ya Kusimamia masuala ya mazingira kutafuta fedha kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi,

NA KWA KUWA tumeshuhudia hali ya utengaji fedha kwa ajili ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maizngira sio wa kuridhisha,

NA KWA KUWA Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilikwisha kamilisha mapendekezo ya vyanzo vya mapato na viwango vya uchangiaji kwa sekta nyingine katika Mfuko wa Mazingira na kuviwasilisha Serikalini.

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Mazingira ambavyo vimeainishwa na kuwasilishwa Serikalini vinapata kibali na kuanza kuchangia katika Mfuko huu kwa lengo la kuuwezeshwa kufanya kazi yake iliyokusudiwa.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa uongozi wako uliotukuka na kwa ushirikiano ambao umekuwa ukiipatia Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake. Na pia, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kuanzia Machi 2018 hadi kufikia Januari, 2019.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa **Mheshimiwa John Pombe Magufuli**, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua na juhudi mbalimbali anazozionyesha tena kwa vitendo katika kuhakikisha **Azma ya Kujenga Tanzania ya Viwanda** inafanikiwa. Kamati inaunga mkono juhudi zake na itaendelea kuisimamia na kuishauri Serikali kuhakikisha kwa pamoja tunafanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza kwa ushirikiano walioutoa katika kuandaa taarifa hii mpaka kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

i.	Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb	Mwenyekiti
ii.	Mhe. Kanal (Mst.)Masoud Ali Khamis,Mb	M/Mwenyekiti
iii.	Mhe. David Cecil Mwambe, Mb	Mjumbe
iv.	Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
v.	Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
vi.	Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
vii.	Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
viii.	Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
ix.	Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
x.	Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
xi.	Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
xii.	Mhe. Kmamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe
xiii.	Mhe. Zainab Mdolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xiv.	Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xv.	Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xvi.	Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe

xvii.	Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xviii.	Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb	Mjumbe
xix.	Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	Mjumbe
xx.	Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb	Mjumbe
xxi.	Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
xxii.	Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote wa Wizara zilizochini ya usimamizi wa Kamati, pamoja na Makatibu Wakuu, Watendaji wote wa Wizara na Taasisi chini ya Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara walipohitajika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati na kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kiukamilifu. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba pamoja na wasaidizi wa Kamati Ndg. Modester Kipiko, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujiadili taarifa hii na hatimaye kukubali **maoni, ushauri** na **mapendekezo** ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA VIWANDA,
BIASHARA NA MAZINGIRA**

4 Februari, 2019

MHE. OMAR M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono. Sasa tunaanza uchangiaji tunaanza na Mheshimiwa Cecil Mwambe, ajiandae Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Kiteto Zawadi na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa kunipa nafasi kwa kuwa mtu wa kwanza kuchangia ili tujaribu sasa kulielekeza Taifa kwenye mambo ya msingi kabisa ambayo sisi tulitamani tuyaone yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuunga mkono, Taarifa ya Kamati ambayo imejaribu kuonesha upungufu mbalimbali ulioko kwenye utekeleza wa azma ya Mheshimiwa Rais inayohusiana na masuala ya viwanda na niishauri meza yako moja kwa moja kabla sijaenda mbali kwamba kwa kweli kwenye suala la viwanda kama ambavyo taarifa yetu ya Kamati imeonesha kuna matatizo makubwa sana, hasa zaidi kwenye utekelezaji wa hili wazo la kuwa na viwanda, lakini pia ukienda kwenye suala la viwanda vilivyobinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliwaita wawekezaji kwenye sekta ya madini, lakini pia Mheshimiwa Spika naye aliunda hapa tume maalum ya kuchunguza masuala yanayohusiana na madini na makinikia na majibu yaliletwa humu ndani. Sasa nipendekeza kama inawezekana Mheshimiwa Spika naye afikirie kutengeneza tume maalum ya Kibunge ambayo itakwenda kufanya uchunguzi na kuleta majibu yanayohusiana na masuala ya viwanda zaidi ya 150 vilivyobinafsishwa kwa sababu kimsingi hakuna chochote kinachoendelea kwenye hivi viwanda, viwanda pekee vinavyofanya kazi ni viwanda kumi tu kwa hiyo tunamrudisha nyuma sana Rais kwenye wazo lake la viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukifuatilia kabisa michango inayotolewa na Wabunge, lakini na michango mbalimbali maeneo mengi inaonesha kabisa la Rais la kutaka kuwa na viwanda kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda, linakwenda kufeli. Miaka ya 1980 na huko chini kama tunavyoongea hapa tulikuwa na viwanda zaidi ya 150 vya Serikali vilifeli. Sasa sidhani kama kuna utafiti uliofanyika unaoonesha kinaga ubaga ni kwa nini viwanda hivi vilifeli ambavyo Rais anasimama navyo na tumetumia kama ndio sera ya nchi yetu kuhakikisha tunakwenda kuboresha viwanda. Vinginevyo kama hatutafanya haya, vile viwanda vinavyotajwa 3000, viwanda vinavyotajwa 4000 na vyenyewe vitakwenda kufeli kama ambavyo vimefeli hivyo viwanda vingine huko nyuma, tena vilikuwa vichache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe kushauri kwamba tufanye mabadiliko ya makusudi kabisa ya sera ya viwanda, tufanye mabadiliko makusudi kabisa na utafiti kuona hivi viwanda tunavyovijenga masoko yake yako wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa 16 kwenye taarifa ya Kamati hii ambayo iko hapo mbele yako, kwenye ukurasa wa 16 wanaongelea hapa habari ya *import duty* zaidi sana kwenye sukari ya viwanda. Hawa wenye viwanda wana lalamika kwamba Serikali imekuwa ikiwatoza wao pesa kwa ajili ya kuingiza sukari ya viwanda inayotumika kuzalisha soda na vinywaji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya sana kwa miaka mitatu sasa Serikali hajjarudisha hii pesa kwao na inaonyesha wazi kabisa na labda Waziri aje kutuambia hapa baadae kwamba Serikali haina mpango wa kurudisha hizi pesa za watu wenye viwanda. Sasa badala ya kuwazungusha kila siku ni bora watuambie moja kwa moja kwamba hizo pesa hazitapatikana kwa sababu hazipo kwenye mfuko wowote na kwa ufupi Serikali haina hiyo pesa ambayo inatakiwa irudishwe kwa watu wenye viwanda kutokana na hii pesa yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa vyovyote vile mpaka sasa hivi Serikali haina nia ya kufanya hicho kitu na badala yake imeamua kuwazungusha watu walio-*deposit* kule pesa, kwa hiyo, iamue kuacha au kutokuendelea na kukusanya hii pesa kwa sababu haina uwezo wa kurudisha na tunasababisha viwanda vinakufa, watu wanashindwa kuendeleza na kufanya mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa wa 20 kwenye hili jambo tunalosema Mheshimiwa Rais ana nia njema ya kutaka kuhakikisha Tanzania inakuwa ya viwanda. Lakini soma tu pale, kwamba katika pesa za maendeleo zilizotengwa bilioni 80 zimekwenda bilioni nane tu ambayo ni sawa sawa na asilimia tisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi na ninyi tujiulize kwamba Mheshimiwa Rais anataka Tanzania iwe ya viwanda, lakini pesa za viwanda ambazo zinatakiwa zitolewe na Hazina, pesa za maendeleo haziendi. Kwanza zinakwenda kidogo, tunaambiwa hapa ni asilimia tisa tu. Hata hivyo katika hiyo asilimia tisa na yenyewe haiendi kwa wakati, matokeo yake, watu wanashindwa kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea hapa habari za *SIDO*, *SIDO* ndio tunataka iwe sehemu kubwa ya chachu ya viwanda Tanzania tuwaongezee *SIDO* nguvu, ili waweze hii sera ya viwanda iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kimsingi hakuna lolote linalofanyika na awamu hii kuhusiana na masuala ya viwanda kwa sababu hawakujiandaa, wameamua kuja na kitu ambacho utekelezaji wake ni hauwezekani, labda waamue kutafuta namna nyingine ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yanayohusiana na viwanda turudi sasa kwenye viwanda vikuu; na tumejadili hapa mambo mengi, nimeona watu wanajadili masuala ya korosho, Mheshimiwa Waziri pale naye kajibu. Sasa ukiingia upande wa biashara, kwa sababu

tunajadili masuala ya viwanda, pamoja na biashara, kimsingi Mawaziri hawa hawa ambao leo wanatoa maelezo kuhusiana na masuala ya viwanda vya korosho pamopa na bei za korosho kwa ujumla ndio hao ambao walikuja ndani ya Kamati. Juzi hapa Mheshimiwa Hasunga alikuwa anamjibu Mheshimiwa Bobali, anamwambia kwamba uzalishaji wa korosho gharama yake mpaka sasa hivi, kwa hiyo hata wakiuza kwa shilingi 4,180 haina maana kwamba wao wanapata faida kubwa. Ni Waziri huyu huyu na kitabu ni hiki, alipokuja ndani ya Kamati alisema hivi, kwamba mpaka sasa hivi wamepata watu wanaotaka kununua korosho kwa shilingi 3,500 lakini wamewakatalia, kwa sababu gharama za utaratibu wa uendeshaji wa zao la korosho kwa kilo moja mpaka sasa hivi, imefikia shilingi 3,850. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika shilingi 3,850 wao wanakwenda kuuza shilingi 4,180. Sasa tunataka watueleze ile gap kati ya shilingi 3,850 au shilingi 3,300 mpaka shilingi 4,180 hii pesa iliyozidi nani anakwenda kupewa? Kwa sababu haioneshi nia ya kutaka kuwarudishia Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa tulisema pia, tunachofanya sisi ni biashara na Serikali imeamua kufanya biashara kupitia benki zake hapa. Wanasema wenyewe kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko Serikali imeamua kufanya biashara ya Korosho sasa wanawazuia. Kilichokuwa kinafanyika mwanzoni, tuseme labda kwenye hili suala la Kangomba ambalo watu wanafikiri ni dhambi kubwa sana, na mimi sioni kama kuna dhambi yoyote inafanyika. Kangomba ni *facillitators* kama walivyo *facillitators* kama walivyo *facillitators* wowote kwenye mazao ya biashara, sawa sawa na watu walivyo kwenye pamba, sawa sawa walivyo watu kwenye mahindi, hata kwenye nyanya, wanasema wafuate mfumo unaotakiwa, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajuliza hivi kutoa nyanya kwa Mkulima na kuipeleka sokoni ni dhambi? Kutoa mahindi kwa mkulima mmoja mwenye uwezo wa kuvuna wa gunia tatu, akaja kuniulizia mimi mwenye uwezo wa kujikimu

pesa ya maisha lakini naweza kuvuna hata gunia mia nikazipeleka kwenye maghala makubwa, hii ni dhambi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndicho kinachofanyika kwa wauzaji au Wafanyabiashara wa korosho. Serikali kabla haijapeleka pesa maghala yanafunguliwa kuanzia mwezi wa kumi, korosho inaanza kuvunwa miezi ya nane, mwezi wa saba, wakati huo wote haya yote yanafanyika Serikali haijapeleka pesa. Sasa mtu anapoamua kujikimu kwa kutumia mali yake mwenyewe iliyoko ndani, anachukua korosho anapeleka kwa baba mwenye duka kijijini kwetu anakwenda kubadilishana na unga, anakwenda kubadilishana na sukari, anakwenda kuchukua pesa ili aweze kumtibu mtoto wake, leo Serikali hii sikivu inasimama hapa na kusema hawa watu ni wezi, tuwaombe radhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaombe radhi wachuuzi wa korosho kwa sababu wao sio wezi, kinachotakiwa kufanyika ni kurasimisha huu mfumo, na yatambulike kwenye mifumo huru. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inasema inakusanya korosho kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko, na wanakwenda kuziua ni lini watakwenda huko chini? Sasa kwa nini tusirasimishe hawa kangomba wakakusanya korosho kidogo kidogo kutoka kwa watu wetu ...

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MHE. CECIL D. MWAMBE: ... wanaozalisha kidogo, wakapeleka kwenye maghala

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Cecil subiri.

TAARIFA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nataka nimpe taarifa Kaka yangu anayechangia kuwa asilipotoshe Bunge. Kangomba ni sawa sawa na wale wakopeshaji wa fedha mtaani, anakopesha shilingi 1,000 riba shilingi 1,500; ndiyo sawa sawa na hao watu wa kangomba wananunua mashamba yakiwa na maua kwa pesa ndogo, na wao wanakuja kuuza kwa bei, kubwa kwa hiyo asipotoshe Bunge naye akiwa mmojawapo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Cecil.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja hapa kidogo kwenye suala hilo hilo kangomba, naomba niendeleo kwamba tafsiri anayoitoa Mheshimiwa Mlinga ninamuomba kwa makusudi kabisa akae na wazee akiwemo Mzee Mkuchika na wengine wote wanaotokea upande huu, ukanda huu unaolima korosho halafu wamwambie kangomba kwa uhalisia ni nini, na si hicho anachokisema yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama kangomba ni dhambi wasimame hapa watuambie, kwamba kufanya kangomba ni dhambi na kwamba hairuhusiwi. Vinginevyo kinachotokea ni kwamba Serikali inataka kwenda kufanya dhuluma kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa korosho; na ni kwa nini, korosho ...

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti
Taarifa

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Zitto.

TAARIFA

MHE KABWE R. Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji, kwamba kwenye sekta ya pamba Serikali inaruhusu wafanyabiashara kuingia kilimo cha mikataba na wakulima wa pamba na wao wananunua

mazao yote hata kabla hayajapandwa. Sasa hii inatofauti gani na kangomba ambayo watu wanaenda kuzungumza na wakulima na wananunua na kangomba ni *broker* kama *broker* mwingine yeyote. Mzungumzaji atakubaliana na mimi kwamba tulatele hoja ili langomba arasimishwe rasmi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa, Mheshimiwa Cecil.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Zitto kwanza kwa kunikumbusha, na kuiomba Serikali ilete hoja Bungeni ya kurasimisha biashara hii na hawa watu wa katikati ambao wao watakwenda ku-*bridge* kati ya mkulima pamoja na mnunuzi mkubwa ambaye ni Serikali, kwa sababu wameamua wakafanye hiki kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe tu angalizo kwenye hili jambo

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa sasa hivi Wakulima wanapewa adhabu...

MWENYEKITI: Taarifa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Cecil.

TAARIFA

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe tu taarifa mzungumzaji ambaye anazungumza, anachangia vizuri, lakini naomba tu nimweleze kwamba *brokers* wanasajiliwa na wana leseni, kangombas hawana leseni, hawana *TIN* namba na hawalipi kodi.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu*)

MWENYEKITI: *Order, order, order in the Parliament.*

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kitu chochote ambacho ni halali lazima kisajiliwe...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magereli *order*.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

WAZIRI WA KILIMO: ... lazima kwanza

MWENYEKITI: Waheshimiwa, sikilizeni majibu yawaingie,

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kangomba hawajasajiliwa, hawana leseni, hawalipi kodi, kwa hiyo ni walanguzi, kwa hiyo hao kwa mujibu wa sheria za biashara hawaruhusiwi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Cecil.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kujua tatizo la msingi linalozalisha kangomba Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa niombe Wizara yake ikatole leseni, ikarasimisha hizo biashara ili wawashauri hao watu walipe kodi, ndilo suluhisho la hili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu elimu hii hamkuitoa wakati unaotakiwa muitoe niwaombe na Serikali hapa itoe tamko, korosho zote mlizozikusanya mzirudishe badala ya kuwadhulumu kwa sababu hamkwenda kuwaeleza kwamba wanatakiwa kuwa leseni. Kosa hili limeanzishwa na Serikali na mkiliacha litaendelea kujitokeza

kwa sababu kangomba ni jina la kilugha la Kimakonde, Kiyao ni mchanganyiko, lakini kiingereza chake hawa watu ndio *brokers*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mlichokifanya Serikali kwa kumwita yule *INDO* kampuni ambayo mnasema ni ya Kikenyia inayomilikiwa na kijana wetu Mtembei ambaye ni muhaya wa Tanzania, anachokifanya yeye ni *brokerage* kwa sababu Serikali imeshindwa kutafuta masoko ya korosho na yeye anakwenda kuziua hizi korosho nchi za nje, jukumu ambalo lilikuwa lifanywe na Wizara ya Viwanda na Biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo mmemruhusu kangomba *INDO* afanya hiyo kazi muwaruhusu na wale kangomba wengine, lakini kwa kuanzia hakikisheni kwanza korosho zao mlizokusanya mwaka huu mnazirudisha kwa sababu wao si *wezi*, *there is no logic*. Nimeona hapa kwene mtandao inasambaa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Newala amekamata wafanyabiashara na wakulima, wa upande wa Mozambique kuja kuuzia Korosho zao Newala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhambi gani walikuwa wanafanya kwenye uchumi wetu? Hivi mtu kutoa mali nje na kuzileta hapa ni dhambi? Watu wa kwetu sisi wa mipakani, mpaka wa Mozambique na Tanzania tunatenganishwa na mto Ruvuma, watu wa kwetu wanalima upande wa pili na watu wa huko Mozambique wanasoma upande wa huku, wanaita ng'ambo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyejua hapa; Mkuchika na wengine...

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. CECIL D. MWAMBE: ...babu zake walikuwa wanalima huko, wanakwenda kulima ng'ambo wanarudisha mazao yao pale.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecil kaa kidogo. Mheshimiwa Selasini, tulieni, Mheshimiwa Millya.

MHE. JAMES O. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Millya ni mwanasheria.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MHE. JAMES O. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Millya.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MHE. JAMES O. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto...

MWENYEKITI: Waheshimiwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

T A A R I F A

MHE. JAMES O. MILLYA: Mheshimiwa Zitto anatoka Kigoma, hamna korosho, lakini amechangia, sasa sijui hawa watu ambao *national figure* kutoka Kigoma.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JAMES O. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge,...

MHE. JAMES O. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojaribu kusema ni kwamba

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kubenea kaa chini.

MHE. JAMES O. MILLYA: Taarifa ninayotaka kumpa mzungumzaji...

MWENYEKITI: Kubenea kaa chini.

MHE. JAMES O. MILLYA: ..ni kwamba

MWENYEKITI: Waheshimiwa tutaanza kuandika majina.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MHE. JAMES O. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mzungumzaji anatetea wauzaji wa Mozambique kuja kuuza korosho kwetu kwa sababu Serikali ya Magufuli imetoa bei nzuri, hao hao ndio wanasema haya makosa yaendelee. Wakati Serikali ya Magufuli inatoa bei nzuri kwa ajili ya wakulima wa korosho Lindi na Mtwara yeye anawatetea wa Msumbiji wakati Rais wetu anawatetea Watanzania, wewe ni mtu wa namna gani? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kweli kabisa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Cecil, hebu subiri kwanza.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: ...subiri, kwanza, mimi si ndiye *referee* hapa? Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Magereli, hii ni mara ya mwisho mtatoa sauti zenu bila utaratibu humu ndani, niko *very serious*.

MBUNGE FULANI: Taarifa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: ...mjadala ni mzito kwa pande zote mbili. Ukitaka jambo lako Mbunge unasimama kwa mujibu wa Kanuni. Ukifikiri hapa ni kwenye viwanja vya michezo hapa sipo na tunaingia kwenye lala salama, nikikutoa hapa hutarudi mpaka mwaka ujao. Mheshimiwa Cecil! (*Makofi/Kicheko*)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Millya kwa kuliona tatizo linalofanywa na Serikali naipokea taarifa yake (*Vicheko*)

MBUNGE FULANI: Taarifa Mwenyekiti.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni kwamba hata hiyo Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo *broker* waliyompa kuuza hizo korosho

T A A R I F A

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkuchika.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa

Mwenyekiti, hili Bunge ni jengo linaloheshimika sana, ndiyo maana kabla hatujaanza kazi tunakula kiapo tutafanya kazi, tena tunamalizia Ee Mungu nisaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema uongo katika jengo kama hili, ni jambo la hatari. Mimi ni mkulima wa korosho, nina shamba la korosho. Neno kangomba ni neno la Kimakonde, mimi ni mzee wa Kimakonde, nimesimama hapa nieleze nini maana ya neno kangomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kangomba ni ununuzi wa korosho kwa kutotumia kapani au kipimo kinachotambulika na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge Wanaopinga Rushwa. Jumamosi iliyopita, acha hii ya jana, tulikuwa na semina pale *Dodoma Hotel* inayohusu *weights and measures*; umuhimu wa vipimo katika biashara ya mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao kile kililaani kangomba kwa sababu kangomba anasema tu kwamba bakuli hii ni shilingi saba, yule ambaye ana shida anayefanya biashara ya kangomba ni mtu ambaye ananunua korosho kwa mkulima, kwa kipimo ambacho si kidogo, ni kidogo ambacho anamnyonya ili baadae yeye aende apate faida kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutegemea mtu anayetoka eneo la korosho, anavyojua wapiga kura wake wanavyoichukia kangomba kule nyumbani, sikutegemea awepo hapa mtu anayetoka eneo la korosho anasema kangomba ni halali; *kangomba is corruption*, ndiyo maana Serikali inaipiga vita, na tutaendelea kuipiga vita... (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa wameshakuelewa, Mheshimiwa Cecil malizia dakika yako moja.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimwambie tu mzee wangu Mkuchika, namheshimu alisoma na baba yangu, kwamba...

MWENYEKITI: Changia suala ambalo liko kwenye mjadala.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, si najenga hoja.

MWENYEKITI: Haya endelea.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka nimweleze ni kwamba mpaka sasa hivi hiyo Wizara ya Kilimo, wana kesi ngapi Mahakamani za watu waliokwenda kulalamikia kangomba? Na anachokisema mzee si kwamba kangomba haifanyiki, ukimsikiliza kwa nyuma kwa nyuma anachosema irasimishwe ili wakae na mzani wakati wa kununua, ndicho anachokisema pale. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na mimi nipokee taarifa yake na nimshukuru na ameliona hili wazo kwamba kinachofanyika watu wanakwenda kununua kwa vipimo visivyo sahihi. Kwa hiyo, ameshauri Serikali kwamba sasa hivi ipeleke mizani kwa wanunuzi wadogo wadogo vijijini ili waweze kuweka hili jambo likae sawa na ndicho kilio chetu, hicho ndicho kilio chetu. Sawa sawa na lile la Mheshimiwa Millya alikuwa analisema pale... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Eheeh.

MWENYEKITI: Nlikuongeza dakika tatu, ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, ajiandae

Mheshimiwa Kiteto Zawadi, ajiandae Mheshimiwa Musukuma.
(*Makofi*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Kamati hii ya Viwanda na Biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Wataalamu wote, pamoja na Wabunge wote wa Kamati hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila, nachukua nafasi hii ingawa si Wizara yake, kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kuruhusu wachungaji na wafugaji pamoja na wakulima wanaokaa karibu na Hifadhi za Serikali kwa kuwaruhusu maeneo ambayo yana mapori ambayo hayana wanyama ili wananchi waweze kuyatumia wakati wa dharura, vilevile na vijiji 300 ambavyo vimeruhusiwa virasimishwe. Namshukuru sana kwa kupokea kilio cha wakulima na wafugaji cha muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono mapendekezo ya Kamati, ila nina mawazo mawili/matatu ambayo yamo kwenye Kamati ningependa kuyafafanua na kuyaelezea vizuri, kama yataweza kuchukuliwa na kuwa msingi mzuri wa kuelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni suala hili la Liganga na Mchuchuma. Suala hili la Liganga na Mchuchuma lina takribani zaidi ya miaka 50 na kinachoonekana tunaweza tukaenda tena miaka mingine 50 kama hatukupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuma ni bidhaa kama bidhaa zingine na ndani ya chuma cha Liganga kuna mchanganyiko wa madini mbalimbali. Kwenye mkutano wa madini Mheshimiwa Rais alieleza na *analysis* zilizomo kwenye mchanga ule. Pendekezo tulilionalo ni kwamba Serikali ichukue *analysis* za gharama za uzalishaji kama itajenga Kiwanda cha Chuma, ichukue *analysis* ya mali iliyomo mule

ndani ya chuma ione kama inaweza kuu-peg ule mchanga kwa bei ili wanunuzi waweze kununua kwa kulipia Serikalini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya kuongea hili ni kwamba, wenzetu Waganda leo wanachimba *crude oil* kutoka Uganda wanapeleka Tanga kupitia hapa lakini wananunua petroli na dizeli kutoka nje kwenda Uganda. Ni kwamba ndani ya *crude* ile kuna vitu ambavyo kama watachenjua hiyo *crude oil* kule Uganda hawawezi kuisafirisha au hawawezi kutumia ile *material* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi kwa Liganga ni vizuri Serikali ikafikiria upya. Sababu nyingi za msingi ni kwamba chuma ni bidhaa kama bidhaa nyingine. Tunapongea leo bei ya chuma duniani inaendelea kuanguka na hatujui ndani ya miaka kumi bei ya chuma itakuwaje maana chuma ni bidhaa ambayo inatumika na inakuwa *recycle*, sio kama chakula. Kwa hiyo hata kama tutang'ang'ania tunajua nini kitatokea baada ya miaka kumi. Ni vizuri Serikali ikafikiria kufanya *analysis* na kuanza kuruhusu chuma hicho Serikali iuze ili iweze kununua chuma kipya na kutumia au kupata pesa kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni kwamba ndani ya chuma au ndani ya bidhaa zozote kama unataka kuzalisha hapa lazima uangalie matumizi ya yale makapi. Inawezekana sisi tunataka kutengeneza kweli hicho kiwanda, lakini kuna makapi na bidhaa nyingine ambazo huenda tukawa hatuna matumizi nazo au soko la kuziua au ubebaji wake zikishanyofolewa mle ndani ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la msingi ni kwamba wataalamu waangie, kama uamuzi unaweza kufanyika ili kwa mara ya kwanza baada ya miaka hamsini hiyo bidhaa tunayosema chuma iweze kutusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wasukuma mtu akija kununua mpunga kwao, unachouliza kitu cha kwanza ni bei ya mchele, ukijua bei ya mchele ndipo unajua kwamba niuze

mchele au niuze mpunga; lakini utaangalia gharama zako, waste na nini, ndiyo utatoa bei ya mpunga. Kwa hiyo hata hili nafikiri wataalamu wajaribu kufanya *vice versa* waone kama mtu anataka chuma waangalie bei ya gharama zao na waangalie bei ya *waste* na nini ili waamue kama wanaweza kuuza ni vizuri Serikali ikauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hili tatizo la bidhaa ya mazao mbalimbali. Nimesikia wachangiaji, Waheshimiwa Wabunge hapa wameongea sana suala la mihogo kwenda kutafuta wateja China, kufanya nini; lakini mimi nilikuja hapa na wazo na kwenye Kamati tulijaribu kulingea na kuliingiza. Lugha niliyotumia ilileta mtafaruku kidogo niliposema kwamba wananchi waruhusiwe kutengeneza gongo kutokana na mahindi, muhogo na mtama. Maana yangu, gongo ni kama kusema kitimoto kwenye nguruwe, lakini maana yangu ni *spirit*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gongo ni neno la mtaani kama vile kitimoto, lakini maana yake ni *spirit*. Pombe zote kali tunazokunywa hapa ni *spirit*. Hata tukiwauzia Wachina mahindi au muhogo, wakatengeneza *spirit* ile ile wataturudishia sisi. Kwa hiyo, sasa hivi sisi tunachokunywa ni *spirit* kutoka kwenye mahindi ya watu wa nje. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sawa sawa.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna ubaya gani Serikali isiruhusu gongo, iruhusu *spirit* itengenezwe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iruhusu *spirit* kutoka kwenye mazao ya chakula ili iweze kusaidia na kuinua bei ya mazao. Najua kuna wachangiaji wengi kwenye mtandao wanajaribu kusema kwamba bei ya vyakula itapanda, lakini leo hatuna njaa ya chakula, njaa yetu kubwa ni pesa. Maana yake vyakula vimebadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchele, leo tuna *competition* kubwa sana ya *chips*. Tunalia sana mikoa

inayozalisha mchele, maana yake watu wameanza kula viazi vitamu ambavyo ni *chips*. Na sisi watu wa Mwanza na Shinyanga hatuwezi kulalamika kwa kuwa watu wameanza kula *chips*, ni pamoja na sisi wenyewe; na bahati nzuri watoto wameipenda *chips*. Sasa sisi wenye mchele tutafanya nini? Ni lazima tutafute *option* nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri wataalam wetu wajaribu ku-*review* kidogo mawazo, itatusaidia sana. Maana yake elimu tunayotumia imeandikwa zaidi ya miaka 50 na dunia inakwenda haraka: Je, wataalam wanajaribu kweli ku-*review* mawazo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kumaliza kwa kuongea, suala hili limetusumbua sana hasa kwenye Kamati yetu ya Madini tulivyokuwa juzi kwenye kikao. Mheshimiwa Rais ame-*invest* pesa nyingi sana kwenye ndege zaidi ya shilingi trilioni moja. Ndege hizo tunatarajia ziende nje zikalete watalii na watalii watuletee dola. Hata hivyo, dola sisi hatui-*charge tax*, lakini dhahabu tunai-*charge tax* na dhahabu ni *currency*. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Ni fedha!

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, dhahabu ni pesa na ni pesa ya kwanza kabla ya pesa hizi tunazozitumia za karatasi. Nafikiri kwa nyie wenzetu wasomi mnaelewa, pesa ya kwanza duniani ni dhahabu, lakini kwa nini tutumie gharama ya shilingi trilioni moja kufuata dola kwa Mchina Uchina? Tunakataa *currency* ya mtu ambaye hana viatu wala kitu chochote, hajaomba huduma ya Serikali, anatumia dhahabu; na leo tunalia na Mheshimiwa Mpango, tuna *deficit* ya dola; lakini dola zipo mlangoni na watu walionazo hawana tatizo lolote. Tunataka *tax* ya nini? Mbona dola hatui-*charge tax*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda na dola kwenye benki, unachoulizwa zaidi ni kwamba unazo nyingi tukuongeze bei? Mbona huyu wa dhahabu haambiwi kwamba unazo tukuongeze bei? Badala yake anaambiwa

tutakukata. Ukimwambia utamkata, anakataa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wataalam wetu wajaribu sana ku-*review*, maana yake elimu wanayotumia, hatukatai, lakini elimu isiwe kama Biblia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hata Baba Mtakatifu anafanya marekebicho kwenye Kanisa Katoliki ili kusudi Kanisa lisiwe gumu na Walokole wasimalize wafuasi. Maana yake kwa ajili ya ugumu ule, Walokole wameendelea kuchukua wafuasi.

Kwa hiyo, tunaomba na ndugu zetu; Mheshimiwa Mpango, jaribu kidogo kuchukua na elimu ya Mtaani ili ijaribu kutuina kwenye uchumi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kiteto Zawadi.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika kujadili Taarifa ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kupongeza juhudi za Serikali za awamu zote kwa kuhakikisha kuwa nchi yetu inakuwa ni nchi ya uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu iliyopelekea nchi yetu kubinafsisha viwanda ni kuleta tija. Kama nchi, tuliamini ya kwamba kubinafsisha viwanda kutaleta tija, kuongeza uzalishaji, pia kuongeza ajira, kuweka teknolojia mpya, kuongeza ubora na thamani ya bidhaa ambazo zinazalishwa katika viwanda hivyo tulivyovibinafsisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaendelea kuamini kwamba viongozi waliopita walikuwa na nia njema ya kubinafsisha viwanda vyetu. Ila nia hiyo njema iliharibiwa na baadhi ya Watendaji na Wawekezaji ambao walikuwa na dhamira ya kupotosha dhamira kubwa ya kubinafsisha viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulibinafsisha viwanda yapata 156, lakini leo hii viwanda vinavyofanya kazi na hata taarifa ya Kamati inaonyesha ni viwanda 16 tu peke yake katika viwanda 156. Suala hili siyo suala la kulifumbia macho, lakini kwa sababu tumeshateleza, hatuna budi kuendelea kuishauri Serikali ili kuona ni kwa namna gani wanaweza wakarudisha nia ya madhumuni ambayo yalikuwa ni mema ya ubinafsishaji wa viwanda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali katika maeneo mawili; eneo la kwanza, kuhakikisha ya kwamba inapitia mikataba yote ambayo ilihusika katika ubinafsishaji wa viwanda. Wakati zoezi zima la ubinafsishaji wa viwanda linafanyika, kulikuwa kuna mikataba ambayo ilikuwa ni ya ovyo, mikataba ambayo iliifanya Serikali kutokuwa na nguvu ya kuweza kuwanyang'anya viwanda wale ambao walivitumia vibaya na kuweza kuvirudisha kwa wale ambao sasa wana uwezo wa kuvifanya viwanda hivi kuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naishauri Serikali, kama itampendeza Mheshimiwa Spika kuunda Kamati Maalum ya Kibunge ili waweze kufuatilia mikataba ambayo Serikali iliingia na ili kuweza kuipa Serikali nguvu ya kuweza kuvitwaa viwanda ambavyo havifanyi kazi kama vile unavyoona kwamba katika viwanda 156 ni viwanda 16 peke yake ambavyo vinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naishauri Serikali kuangalia namna ya kuviondoa katika orodha ya viwanda, viwanda vile ambavyo havifanyi kazi. Hii ni kwa sababu ukiangalia kwenye taarifa yetu ya Kamati; na Kamati imesisitiza kwamba vile viwanda ambavyo havifanyi kazi vizuri

viondolewe basi kwenye orodha ili kuepuka mgongano wa mawazo wa kusema kwamba tuna viwanda vingi na vinafanya kazi, tukiendelea kuamini kwamba vinafanya kazi wakati havifanyi kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuondoa hiyo *notion* ya kuwafanya Watanzania waamini kwamba tunavyo viwanda vikubwa na vingi ambavyo vinafanya kazi, ni vyema tukaondoa vile viwanda ambavyo havifanyi kazi katika orodha ya viwanda ambavyo vimebinafishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuangalia katika suala zima la upelekaji wa fedha. Katika taarifa ya Kamati tumeona upelekaji wa fedha katika Wizara ya Viwanda na Biashara wamepelekewa fedha kwa asilimia 18 hadi kufikia Desemba, 2018. Katika hiyo asilimia 18, ni 6% peke yake ambayo ilikuwa imeenda kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini nia njema ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ambayo anatangaza kila mara kwamba anataka kuona uchumi wa viwanda katika nchi yetu ya Tanzania. Ninaamini Mheshimiwa Rais anayo nia njema kabisa, lakini je, nia njema aliyonayo Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, itafikiwa vipi kama tu hata upelekaji wa fedha katika Wizara ni kwa asilimia ndogo namna hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuangalia kwamba kama tunataka kweli kwenda katika uchumi wa viwanda, tuhakikishe tunatenga fedha za kutosha lakini zile fedha tunazozitenga tuhakikishe zinaenda kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kuweza kusaidia kuleta tija katika suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Wizara ya Mazingira, ninaamini kwamba ni Wizara nyeti, ina mambo mengi sana ya kuyaangalia. Kwa mfano, katika hiki kipindi cha hivi karibuni, maeneo mengi sana yanaonekana kwenda kuwa na jangwa na kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira, lakini Wizara hii imekuwa ikitengewa fedha ndogo;

na hizo fedha kiasi kidogo ambacho kinatengwa pia kinaenda kidogo. Kwa maana hiyo, Wizara hii tunaizorotesha na kuifanya ishindwe kufanya kazi yake ya kuweza kuyatunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku ya leo baada ya kuyasema hayo, ninaomba Serikali iweze kupitia maoni ambayo yametolewa na Kamati ya Viwanda na Biashara, lakini pia niendeleo kupongeza juhudi ambazo zinafanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ili kuhakikisha kwamba tunafikia katika uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma, jiandae Mheshimiwa Zainab Mndolwa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kupata muda wa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza sana Serikali, lakini pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyofanya pale bandarini. Kwa kipindi cha miezi ya nyuma pale, Waheshimiwa Wabunge wengi walilalamika humu ndani kwamba bandari yetu sasa watu wameikimbia wameenda Beira na Mombasa, lakini kwa jitihada za Serikali tumeweza kufanya vizuri, sasa hivi bandari yetu ipo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nataka kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri. Bandari yetu ya Dar es Salaam wateja wetu wakubwa ni watu wa Congo, Zambia, Malawi na nchi nyingine. Tayari watu wengi wameshaingia mikataba na wasafirishaji wa Tanzania, nasi Watanzania wengi tumechukua mikopo tukanunua magari na miundombinu mingine kwa ajili ya kupata hiyo mikataba ya kusafirisha hayo makontena kutoka bandarini na kwenda huko Congo na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu aliouweka Mheshimiwa Waziri, ni kwamba sasa tunaenda kuiua kabisa Bandari ya Dar es Salaam, *totally* inaenda kufa. Watu wengi wa Congo na Zambia watakimbia bandari yetu ya Dar es Salaam watahamia Beira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyabiashara anapoenda kununua bidhaa kule nje, kontena linabeba uzito wa tani 33 na tayari nao wameshafunga mikataba na viwanda kule nje. Sasa ukija ukibadilisha ghafla, maana yake ni lazima akukimbie kwa sababu hawezi. Pia walio na mikataba, tayari wameshasaini mikataba ya kubeba tani 33. Sasa naona Serikali imeenda kusaini mkataba na nchi za *East Africa* kama Kenya, Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hatuna biashara ya *transport* ya moja kwa moja na Kenya. Kenya ndiyo mshindani wetu mkubwa kwenye bandari. Kwa hiyo, kilichoingiwa hapa ni kutaka kututoa kwenye *mood* halafu watu watarudi Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wakenya wao wana sheria hiyo ya magari yenye tairi mbili toka zamani, lakini sisi tunakopeleka kama Zambia na Malawi, wao wanatumia *super single*. Sasa Serikali inapokuja leo kusema tu ghafla tubadilishe kutoka kwenye *super single* twende kwenye tairi mbili, haiwezekani, utaua watu na *pressure*.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, jitihada ambazo zimefanywa na Mheshimiwa Rais kuifufua bandari yetu ya Dar es Salaam, ni vizuri wataalam, tunaamini mmesoma vizuri, lakini hebu jaribuni kufikiri nje ya *box*, maana pengine hizi *degree* za makaratasi zinatusumbua, mtaua watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wajaribu kukaa na wadau ambao wameweza kumiliki hivi vyombo watusikilize. Naamini wasafirishaji wengi, ukitafuta Tanzania nzima wenye *degree* nyingi, wengi ni Darasa la Saba. Sasa

kwa *style* mnayoenda hii, hamjatusikiliza, wala hamjapata *experience*. Kwa hiyo, ni vizuri mkapata muda wa kuwasikiliza. Hizi sheria hamtungii magari, mnamaliza kutunga sheria, inaanza kutula sisi wenyewe na wengine wamo humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, ni vizuri tukaacha kubeza jitihada za Rais, hizi sheria ngumu ambazo zinaenda kuua bandari yetu, ni vizuri tukaziangalia upya na ikiwezekana tuziache, hazitusaidii katika Serikali inayotaka kukua kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest*, mimi nafanya biashara ya mabasi, nazungumza kwa ajili ya watu wenye mabasi. Biashara ya mabasi ni kubwa sana na unaweza ukaona mtu anamiliki mabasi 30, lakini hakuna mtu anayenunua basi kwa *cash*, wote wanakopa. Hata hizo *installments* tu za shilingi milioni tano kuzipata kwa mwezi ni shughuli kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizowekwa, mtu anafanya kosa moja, anapigwa faini ya shilingi milioni tano. Tafsiri yake sasa ninyi mnataka kumchonganisha Mheshimiwa Rais na wasafirishaji. Haiwezekani mtu kama alikuwa anapigwa faini ya shilingi 30,000/= na shilingi 250,000/=, ika-*shoot* kutoka hapo kwenda kwenye shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri apate muda, aache kupuuzwa mawazo ya wadau, aanze upya kuzungumza na wadau wamweleze kero zao na awasikilize. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la mabasi. Nampongeza Mheshimiwa Kangi alivyoanza alisema sasa mabasi yasafiri usiku wote. Unajua ni kitu cha kushangaza! Ukienda kwenye nchi tunazopakana nazo, watu wanasafiri usiku; na dunia hii imebadilika; na nchi hii inaenda kubadilika kuwa nchi ya viwanda. Sasa unataka watu walale. Najjuliza, ni kitu gani ambacho kinashinda Serikali kutengeneza utaratibu wa kuruhusu magari yasafiri usiku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli hiyo ndiyo sheria kwamba mabasi yataleta matatizo? Mbona treni inasafiri usiku? Ina maana hata tukianza kutumia treni ya *Stiegler's Gorge* hiyo, itasafiri mwisho saa saba? Si lazima ifanye kazi usiku na mchana? Watu wanataka kufanya kazi Dar es Salaam walale Morogoro au Dodoma halafu saa kumi waondoke kurudi Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba, kama tatizo ni usalama, afadhali kama Jeshi letu limepungukiwa Askari, tuchukue hata JKT wapewe semina wakae barabarani, gari zisafiri usiku na watu wawe na uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda nchi nyingine tunaona. Sisi tunasafirisha kwenye nchi za *East Africa*, wenzetu wamefanyaje? Mabasi hayaingii mizani. Mabasi kuyaingiza mzani ni ku-*create* tu rushwa, hakuna basi inayozidi zaidi ya shilingi 30,000/=, shilingi 15,000/= . Kwa nini, Serikali isione umuhimu wa kuondoa hii sheria ya mabasi kupita kwenye mizani? Kwanza mnaleta usumbufu kwa abiria, mnasababisha watu wanachelewa kwenye kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ikaangalia vitu ambavyo vimetukwamisha tuviondoe, twende kwenye Serikali ya kuvutia na watu wengine waje kufanya kazi hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naona huko kwenye usafirishaji, pia Idara yake katika Wizara ya Miundombinu, sasa hivi ukienda Dar es Salaam wameondoa *Hiace* kule mjini, hata ukija Dodoma leseni ya *Hiace* ikiisha hawataki, ukienda Mwanza hawataki. Mimi najjuliza; na nilifanya *research* ndogo tu. Ukienda kule Dar es Salaam, pamoja na kuziondoa zile gari (*Hiace*) kule ndani, lakini watu wanasimama kwenye daladala, wanatoka safari wanasimama, gari zinabeba watu mpaka 110, lakini watu wanapanda bodaboda na bajaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti iliyofanyika ya kuziondoa *Hiace* mimi sioni kama ni halali. Sana sana ni

kwamba tumewaonea wale wafanyabiashara. Ukiondoa *Hiace* ina matairi manne, mbona sisi gari zetu za Mawaziri zinaruhusiwa kupita kule? Kama ni hivyo na hizo gari ziondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye nchi nyingine zilioendelea, magari yana umbali wake ya kuwekwa; yape magari ya binafsi, wote tuning'inie kwenye daladala moja ndio mwone huo uchungu wa kuziondoa hizo gari huko ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali, pale ambapo tunakuwa hatuna umuhimu wa kushikiria sheria ambazo zimepitwa na wakati, leteni *amendment* humu tuziondoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kidogo kwenye ndege. Kwa bahati nzuri mimi ni *captain*. Unajua nikisema mimi ni Darasa la Saba watu hawaelewi! Mimi ni mtaalam wa kurusha *helicopter*. Kwa hiyo, lazima niwaambie kidogo hapa. Pamoja na huo ungo pia naweza kurusha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikiliza dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya hapa, alilalamika kwamba marubani wetu wa Tanzania wanabadilishwa tu kutoka *bombadier* kwenda *airbus* kwenda *dreamliner*, jamani hili sio basi, ndege ni kitu kikubwa sana. *Captain* wa ndege hawezi kuruhusiwa kutoka kwenye ndege moja kwenda kwenye ndege nyingine bila kupewa *training* na kupewa leseni ya kuendesha ile ndege. Hata kwanza wale *airbus* wasingewaruhusu kuwapa ndege rubani wa *bombadier* akaendeshe ndege ya *airbus* au *dreamliner*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mabadiliko ambayo pia na wenzetu wanatakiwa wayakubali, kwamba zamani tulizoea kuona marubani wazuri ni Wazungu, sasa hivi vijana wetu wamesoma vizuri, tunawapongeza. Kwa hiyo muwe na imani kwamba hawa watu wamepita kwenye *training* na wana leseni za kuweza kuendesha hiyo ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia limezungumzwa suala la faida; ndege huwezi ukaona faida leo. Sisi tunafanya usafirishaji, ukitaka kujua faida ya ndege, asimame Mchumi hapa aniambie, kama hutaona kuingiza kwenye hela uniambie wale ile ndege iliyowabeba, wale waliowahi Dar es Salaam wamepata faida gani na kule walikoenda kununua. Kwa hiyo ina *components* nyingi, lazima tuvumiliane tu, mtakuja kupata utaalam zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Mndolwa.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika taarifa hii.

MWENYEKITI: Dakika tano.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa taarifa yetu nzuri, pia naomba mapendekezo yaliyopo Serikali, iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ubinafsishwaji uliofanywa wa viwanda zaidi ya 156, lakini ni vichache tu ambavyo vinafanya kazi. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, tunaomba vile viwanda ambavyo havifanyi kazi, kwa sababu wamiliki wake wamevigeuza matumizi na wengine wamekwenda kukopa fedha kwenye mabenki na kufanya biashara ambazo hazihusiani na mikataba walioingia, tunaomba Serikali iunde Kamati Maalum ya kuvichunguza viwanda vile na kuvirudisha Serikalini ili kuweza kupatiwa wawekezaji wengine kuweza kuviendeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo katika viwanda ambavyo vinazalisha vinywaji baridi, tumetembelea viwanda vingi lakini changamoto kubwa ni uingizwaji wa

sukari ya viwandani, sukari ya viwandani haipatikani hapa nchini, huagizwa nchi za nje na Serikali ilipanga tozo kwa viwanda hivyo ambavyo vinatumia sukari ya viwandani asilimia 15. Wakati vinaingiza vinakatwa tozo ya asilimia 15 na Mamlaka ya Mapato (*TRA*), lakini sasa hivi ni takribani miaka mitatu Serikali hiyohiyo imechukua fedha za wenye viwanda haijarudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mabilioni ya shilingi wenye viwanda wanadai, na tulikwenda katika viwanda hivyo wakatuonesha barua mbalimbali walizosiandika ambazo wameomba Serikali iwarudishie kwa sababu fedha hizo walizikopa katika taasisi mbalimbali hapa nchini na zinatozwa riba, kwa hiyo Serikali imeshikilia fedha yao takribani miaka mitatu sasa hivi. Kwa hiyo Serikali kama Serikali tunahamasisha, wanahamasisha uchumi wa viwanda hapa Tanzania lakini yenyewe pia inakwamisha kwa upande mwingine kwenye viwanda vyetu kuweza kuendeleza viwanda kwa kushikilia fedha ambazo zinatumiwa kwenye viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali tunaomba wale wenye viwanda ambao fedha zao walizosiingiza katika sukari ya viwandani zirejeshwe kwa wakati ili ziweze kutumika katika mitaji yao kwa sababu walilalamika sana wakasema na mitambo mingine imesitishwa kwa sababu hawana mtaji wa kutosha. Pia kama inawezekana, waweze kusitisha utozaji ule, Serikali ianzishe viwanda vya ndani ambavyo vitazalisha sukari ya viwandani kuliko kuagiza halafu wanatozwa tozo hawazirejeshi kwa wafanyabiashara hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nazungumzia kuhusu utitiri wa kodi; utitiri wa kodi umesababisha baadhi ya wafanyabiashara kufunga biashara zao. Tunajua kabisa mtu akianza kufanya biashara anatakiwa alipe mapato kwa Serikali kwa kiasi anachopata, lakini sasa hivi Serikali inaanza kumtoa mtu mapato kabla hajaanza kufanya biashara. Naishauri Serikali iwapatie wafanyabiashara hao muda maalum (*grace period*) angalau ya miezi mitatu, wafanye biashara kisha ndiyo waweze kuwakadiria mapato yao, hiyo

itasababisha watu kuweza kujua mapato wanayopata kwa wakati na kuwa na *willingness* ya kulipia mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia pia katika Wizara ya Mazingira; tunaomba Wizara ya Mazingira kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kuwe na uvunaji endelevu wa miti. Wizara iandae maeneo maalum ya kupanda miti ambayo itatumika katika viwanda ambavyo vinatumia malighafi ya miti kwa sababu kuna viwanda vingine vinatumia miti, lakini sasa unakuta ukataji wa miti unakuwa hovy na kusababisha ukame katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wizara itenge maeneo maalum ya kupanda miti ambayo itasaidia pia katika viwanda vyetu kama malighafi. Pia itasaidia katika matumizi ya nyumbani kama mkaa na kuni kwa sababu gesi tunaona ni ghali mno na watu hawawezi kutumia gesi ambayo ni ghali kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kulikuwa na gesi asilia ambayo tunaomba Serikali iharakishe usindikaji wa gesi asilia ambayo itakuwa na unafuu zaidi kwa wananchi kuliko kuendelea kutumaini kwamba tutumie gesi tusitisha mikaa, mkaa kusitisha itakuwa ni ngumu, lakini Serikali ina mpango mkakati kupanga maeneo ambayo miti itapandwa, watu watakata miti na Serikali itapata mapato na watumiaji wa mkaa watumia na pia mazingira yataboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuzungumzia kuhusu matumizi ya mifuko ya plastiki; mifuko hii Serikali inataka isitishwa kutokana na uchafuzi wa mazingira. Hata hivyo, tunaishauri Serikali kabla ya kusitisha itupe njia mbadala au mifuko mbadala ya kuweza kutumia, ambayo badala ya kutumia *plastic* sisi tutatumia mifuko ambayo inaendana na mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Serikali katika ofisi ya mazingira wakati wa kampeni ya upandaji mti, naona sana miti inayopandwa ni ya vivuli, lakini naishauri Serikali tuwe na mkakati wa kupanda miti ambayo itakuwa ya matunda

pia kwenye sehemu ambazo zina rutuba sio kupanda miti ya vivuli tu. Kwa hiyo, nashauri Serikali wakati wa zile kampeni za upandaji miti tuangalie sehemu zenye rutuba tuweze kupanda miti ambayo pia tunaweza kupata matunda, vivuli na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri pia Serikali iweze kufuatilia haya yote katika Kamati yetu, kwa sababu mengi tulishayaeleza, ambayo tumependekeza Kamati yetu, tunaishauri Serikali iyatilie mkazo ili kuelekea Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nuru Bafadhili nimeshakutaja, halafu utafuata Mheshimiwa Ally Saleh (Alberto).

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuweza kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Kamati yangu ya miundombinu kwa taarifa nzuri iliyotolewa. Mimi ntazungumzia suala zima la Barabara yetu hii ya Dodoma – Dar es Salaam; kwa kweli Wizara imejitahidi sana kutengeneza barabara nzuri hii ya Dodoma – Dar es Salaam, lakini kuna tatizo linalojitokeza; Dodoma kama Jiji tukifika pale lhumwa karibu kilometa sijui 10 mpaka kufika hapa katikati ya jiji kunakuwa na giza mno, kwa hiyo naiomba Serikali ijitahidi angalau kutuwekea taa za barabarani ili unapoingia katika sehemu zile za kukaribia jiji ujihisi kweli naingia katika jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sio tu Barabara ya Dodoma – Dar es Salaam, ile barabara ya Iringa, ile barabara ya kwenda Kondo na barabara ya kwenda Singida, barabara zote hizi unapokaribia karibu na jiji ziwe zimewekwa taa kwa usalama wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna tatizo linalojitokeza katika hizo barabara. Katika barabara zile kuna zile *zebra crossing*, naiomba Serikali iwape wananchi elimu ya kuzitumia zile *zebra*, kwa sababu mwananchi anajua kuwa ukifika kwenye *zebra* pale gari inasimama anapishwa yeye, basi unakuta mtu anachezea simu, eti anavuka kwenye barabara anachezea simu. Sasa kuna madereva wengine wanakuwa na uvumilivu lakini dereva mwingine anapita tu. Hiyo inaweza ikasababisha vifo vya watu kutokana na uzembe wao ambao wameona kuwa Serikali imetengeneza sheria kuwa zile *zebra crossing* gari inasimama na wao wanavuka, sasa badala ya kuvuka *straight* yeye anachezea simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia sasa barabara yetu ya kutoka Dar es Salaam – Tanga, Dar es Salaam – Tanga tunaunganishwa na Daraja ambalo liko katika Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Tanga, Daraja la Wami. Kwa kweli daraja lile tunaambiwa na Serikali kuwa litatengenezwa na lipo katika mkakati wa kutengenezwa, lakini ninachoomba, Serikali ilipe kipaumbele lile daraja kwa sababu mwaka jana mwezi Desemba tu kwa siku mfululizo magari yalitumbukia mara mbili kwenye lile daraja. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itakapojenga lile daraja ihakikishe inajenga daraja pana ambalo litaruhusu magari kupishana kwa sababu pale magari wakati mwingine inabidi gari moja lisimame lipishe lingine na wakati mwingine gari inafeli breki, kwa hiyo yanaweza yakaingiliana na kuweza kusababisha ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu viwanja vyetu vya ndege; Uwanja wa Ndege wa Tanga una mgogoro na wakazi wa maeneo ya karibu ya ule uwanja. Kwa hiyo tunaiomba Serikali ihakikishe ule mgogoro unamalizika ili uwanja uweze kupanuliwa. Uwanja wetu ni mkubwa, hatuna sababu yoyote ya kuhamishwa uwanja mwingine, lakini tatizo linakuja kuna mgogoro uliopo kati ya wananchi pamoja na shirika la ndege, kwa hiyo tunaomba hilo Serikali ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuomba Serikali ihakikishe kama inavyosema kuwa itahakikisha kuwa inaunganisha barabara kati ya wilaya na wilaya. Katika barabara ya Tanga kuelekea Jimbo la Mkinga lakini kwenye Tarafa ya Maramba, kwa kweli mpaka leo barabara ile haina lami na wakati wa mvua kunakuwa na matatizo magari yanateleza na wakati mwingine wananchi pia wanashindwa kupitia. Kwa hiyo tunaiomba Serikali ihakikishe barabara ile ya Tanga – Maramba iwekwe lami ambayo itafika mpaka Daluni itaunganisha mpaka Korogwe, kwa sababu biashara nyingi zinafanyika kule lakini unakuta barabara haina lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, kuna mabango yale yanayowekwa ya alama mbalimbali za barabarani na watu wetu ambao sio waangalifu wala hawana uchungu na pesa za Serikali wanang'oa yale mabango kwa ajili ya kwenda kuuza vyuma chakavu. Naiomba Serikali ihakikishe katika zile alama za barabarani badala ya kuweka mabango yanayotumia mabati ihakikishe inaweka mabango yanayowekwa kwa kutumia zege kwa sababu mtu mpaka akaja akavunja zege itakuwa ni kazi kubwa, lakini yale mabati wanayang'oa na kwenda kuuza vyuma chakavu. Vilevile wito kwa wananchi, Watanzania wenzangu; tulinde miundombinu yetu ili tuweze kupata maendeleo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali kutuletea ndege; ni kweli watu wanabeza lakini vitu vingine jamani, Waswahili wana methali wanasema: “Mengine ehee, mengine mmh”. Kwa hiyo, tunasema kuletewa ndege pia kumetusaidia tumerahisisha kazi ya kusafiri kwa muda mrefu. Mwezi uliopita nilitoka hapa Dodoma asubuhi nikaenda Dar es Salaam, tulikwenda kwenye kikao cha Kamati na tukaweza kuwahi na tumefika Dar es Salaam kutokana na kurekebishwa miundombinu ya Daraja la Mfugale tuliweza kutoka *Airport* mpaka tukafika jengo la bandari kule mjini haikuzidi nusu saa, tumefika pale na tukaweza kuwahi kikao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vitu vingine sio tubeze, tunashukuru tumerahisishiwa kuliko tungepanda *Noah*,

ingebidi tuondoke siku moja kabla kuelekea Dar es Salaam na kwenda kuhudhuria hivyo vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alberto.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nataka kusema kwamba sisi wapinzani hatuna ugomvi na *ATCL*, hatuna ugomvi na ndege; ndege ni zetu na *ATCL* ni yetu, tunapokosoa, tunaposema ni kwa ajili ya kulifanya shirika liwe na nguvu zaidi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo yangu matatu nitakayozungumza, nianze kuondosha dhana ambayo inazidi kukua kwamba kukiwa na shirika la ndege ni huduma, hii sio sahihi na kwa bahati mbaya tunapandikiza fikra kwa Watanzania ambao baadaye shirika likifa itabidi tuwajibu kwa sababu kama ambavyo tulikuwa tunasema viwanda vingine ni huduma, viwanda kwa maelfu au kwa mamia vimekufa na faida yake hatukuiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kwamba, tunapandikiza fikra mbaya kwa watendaji wa shirika letu, kwamba wao hawalazimiki kuliendesha shirika kibiashara, hiyo ni *wrong concept*. Shirika ni *sustainability* na *profitability*, kama hamkufuata hivyo shirika linakufa, pesa ya umma inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Ethiopian Airlines* – moja ya mashirika ya mfano hapa mitaani kwetu; *Ethiopian Airlines* mwaka wa fedha 2016/2017, walitengeneza faida ya Dola bilioni 233, mwaka uliofuata yaani 2017/2018, wakatengeneza faida ya dola bilioni 229, wakajjuliza wameshuka kwa bilioni nne, wamefanya *inquiry* kwa nini wameshuka kwa bilioni nne, sio kwamba wamejiachia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tusijenge dhana ya kujiachia kwamba ni *service*, kwa sababu hatimaye shirika

likifa tutakuwa na tatizo, kwa hiyo tuiwekee *target management* ya ATCL kwamba lazima katika muda fulani mfikie lengo fulani. Hilo la kwanza. La pili ni kwamba, lazima wawe na *business program* ambayo inaonesha wanatoka hapa watafika hapa na *growth* iwe inaonekana mwaka hadi mwaka, tukiwaachia na kuwajengea dhana kwamba ni huduma tu, basi tutafika pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nimelisikia leo na nimefurahi, juu ya Uwanja wa Ndege wa Songwe. Siku zote nasema kwamba nchi nzuri haiwezi kuwa na *gateway* moja tu katika nchi yao, inabidi watengeneze *gateways* nyingi kwa suala la ndege. Uwanja wa Ndege wa Songwe ni *gateway* yetu ya kusini, tunaweza tukatawala na tukatengeneza biashara kusini ikiwa tutajipanga vizuri kwa uwanja ule, lakini leo nimesikia kwamba angalau sasa tenda imetangazwa ili kuweka taa katika Uwanja wa Songwe ili iwe *getaway* yetu ya kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mwanza ni *gateway* yetu ya Maziwa Makuu, Mwanza ikitumika vizuri ni mahali pazuri sana pa kuweza kutumia kuingia Maziwa Makuu, lakini sioni athari ya kiuchumi ya kujengwa uwanja mkubwa Chato. Nimekuwa najjuliza; hivi Chato ni *gateway* ya kwenda wapi kwetu sisi? Unaweka kiwanja pembeni ya nchi, hakuna utalii, hakuna biashara ya hivyo, halafu unatumia pesa nyingi badala ya kuimarisha viwanja ambavyo ni *gateway*...

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana kaka yangu mchangiaji, lakini naomba tu nimfahamisha kwamba Uwanja wa Ndege wa Chato umelenga kufungua utalii kwenye Mapori ya Akiba ya BBK ambayo ni Burigi, Biharamulo na Kimisi pamoja na Rubondo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante; Mheshimiwa Alberto.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake kwa sababu ni ndoto tu anayoyasema.

MWENYEKITI: Endelea na mchango wako.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri kwamba tungeweza kuwekeza zaidi katika maeneo ambayo yangeweza kuwa na maana kwetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuzungumza ni kujaribu kui-*turn*...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe mzungumzaji taarifa kwamba Mobutu Sese Seko wakati wa utawala wake alijenga uwanja kijijini kwake na sasa hivi imekuwa ni nyumba ya popo na watoto wanachezea mpira wa madasu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alberto.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali taarifa hiyo na Mji alioujengea unaitwa... (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mji alioujengea unaitwa Gbadolite...

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Milya, kaa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa umemaliza?

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: *No*, Mheshimiwa Alberto malizia, muda umekwisha.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji ambao alijenga unaitwa Gbadolite na ni kweli kwamba kumekuwa na makazi ya popo na njiwa...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linge linaloifanya Dar es Salaam *Airport*...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Chato ni sera ya Chama cha Mapinduzi, kwamba kila mkoa uwe na uwanja wake wa ndege. Mipango ya Mkoa wa Geita, sio sawa na mipango ya Arusha kwa sababu hata Arusha uwanja uko *KIA*, kwa hiyo nadhani wangeachana na suala la Uwanja wa Chato, huo ni mpango mkakati wa Mkoa wetu wa Geita.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alberto, malizia, dakika moja.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa imekataliwa kwa sababu udhahiri umejengwa kwa ajili ya upendeleo tu, hakuna kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kingine ni kuutengeza Uwanja wa Ndege Dar es Salaam uwe ni *hub*. Sasa hivi utakuta mtu akitaka kwenda Moroni...

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Akitaka kwenda *Seychelles*, akitaka kwenda Mauritius...

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Milya, kaa chini.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naishauri Serikali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Frank Mwakajoka, kwenye maendeleo ya nchi kuna vitu vingi vinazingatiwa kiuchumi na *strategic areas* za ulinzi...

Mheshimiwa Zitto kaa kimya. *Deployment ya rapid forces*, sio kila kitu tukiseme humu ndani.

Jioni tutaanza na Mheshimiwa Godbless Lema, atafuata Mheshimiwa Munde. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaanza kuchangia na nilishamtaja Mheshimiwa Godbless Lema ajiandae Mheshimiwa Munde.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nitaongea mambo *serious*, naomba wale watu wenu ambao mmewapanga kwa taarifa waniache nisikilizwe na Serikali ili muweze kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba mazingira ya kibiashara Tanzania yamekuwa magumu sana. Mfanyabiashara yeyote ili aweze kuwekeza anahitaji kitu kinachoitwa *confidence*. Katika Taifa hili na nimekuwa nikisema mara nyingi na nimemwambia hata *personal* Mheshimiwa Mpango, mitaji inayohama na watu ambao wana-*reallocate* biashara zao katika mataifa mengine ya jirani, ukiniambia nikutajie kwa namba makampuni ambayo yanaondoka ni mengi sana. Huwezi kujenga uchumi wa taifa bila kuimarisha *private sector*. Kiungo muhimu kabisa katika taifa ni *private sector*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Jimbo langu la Arusha Mjini kwenye kikao cha kodi ambacho tulikaa mwezi huu ulioisha, watu walio-*register* kufunga biashara walikuwa ni 650. Ukifanya utafiti wote hawa kitu kinachowasabishia wafunge biashara ni ujasiri katika kuwekeza katika taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa zinakuja takwimu za uongo juu ya ukuaji wa uchumi lakini wote ni mashuhuda na wewe ni shuhuda kwa sababu ni Mbunge wa Jimbo la Mjini kabisa Dar es Salaam ya kwamba *purchasing power* ya Watanzania ime-*decline* katika kiwango cha hali ya juu. Kwa bahati mbaya sana mnapokuja humu ndani kuongelea *inflation* kwamba imeshuka mnashindwa kutofautisha *inflation* na kuanguka kwa soko. Kinachoendelea mitaani ama kinachoendelea katika biashara za bidhaa ni kwamba nguvu ya manunuzi imeshuka na kwa sababu nguvu ya

manunuzi imeshuka maana yake ni kwamba watu wanashusha bei bidhaa ili angalau waweze kuuza vitu vyao waepuke hasara ya moja kwa moja sasa huku mkija mnasema ni *inflation* imeshuka. (*Makofi*)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa kaka yangu Mheshimiwa Lema ambaye hata anavyojieleza anaonesha ni mzalendo mzuri kwamba kinachofanyika na Serikali siyo inakatisha tamaa wanyabiashara lakini inatengeneza mifumo inayoweza kuaminika na kueleweka ambayo haijaingia makanjanja na ...

MWENYEKITI: Ahsante, umeeleweka, karibu Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye Sera ya Viwanda. Bunge lililopita nilisema hapa kwamba viwanda havijengwi kwa kauli mbiu vinajengwa kwa mazingira wezeshi na mazingira hayo wezeshi wanafanywa na Serikali kwa watu. Leo Sera yenu ya Viwanda 100 kila Mkoa nikiomba Bunge hili Mheshimiwa Waziri aoneshe viwanda viwili, hamuwezi kuonesha. Unajuliza Serikali hii ambayo inapigia kelele viwanda, inakwenda kupunguza bajeti ya kilimo na wakati kilimo ndiyo malighafi ya viwanda, unajuliza hawa watu wako *serious* na viwanda ama ni kelele tu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini viwanda vinasababishwa na *demand*, hakuna Mtanzania aliyepiga kelele *spirit* zitengenezwe, pombe aina za *spirit* zimetengenewa kwa sababu ya *demand*. Kwa hiyo, ili viwanda viweze kutengenezwa, ili *traders* waweze kufika

kwenye hatua ya kuona viwanda ni vitu muhimu kinachopaswa kufanyika ni watu wawe na mazingira mazuri, uchumi ukue, mishahara bora, kuwepo na *purchasing power* ili nguvu ya manunuzi ikawaambie wafanyabiashara kwamba kwa hali hii sasa mimi naona sihitaji kuagiza *tomato* kutoka India nahitaji kuwa na kiwanda cha *tomato* lringa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mazingira ya biashara yanatengenezwa na hali nzuri (*harmonization*) pamoja na *demand* na hiyo *demand* wa kwanza kuitengeza ni Serikali. Sasa Serikali yenu imeua *workshop*, Serikali yenu inawatanzama wafanyabiashara kama maadui, ma-DC na Wakuu wa Mikoa wanaumiza wafanyabiashara, wafanyabiashara wanawekwa ndani. Mheshimiwa Lukuvi kila anapokwenda ananyang'anya watu mashamba, Sheria na Sera ya Ardhi ni mbovu, leo nani anakuja kuwekeza Tanzania mahali ambapo Sheria ya Ardhi inasema ardhi ni mali ya Serikali. Hivi ni nani leo atakuja kufanya *investment* ya dola bilioni 50 ...

WABUNGE FULANI: Aaaaaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Mheshimiwa Lema taarifa kwamba watu ambao wananyang'anywa mashamba na Serikali wala hawaonewi ni kwa mujibu wa sheria. Wanaonyang'anywa ni wale ambao wamechukua mashamba kwa muda mrefu na wameshindwa kuyaendeleza kwa mujibu wa sheria, ndiyo kinachofanyika.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa taarifa na miongozo hatutaruhusu tena. (Makofi)

Mheshimiwa Lema endelea.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni tatizo kubwa sana kuwa na viongozi wanaokuja ndani ya Bunge wakiwa wamelewa, ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma, nimeshatoa maagizo sasa hamna taarifa wala mwongozo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona shati ya *Order Paper* humu ndani.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana unilindie muda wangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema endelea.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema ukiangalia namna Taifa linavyoenda sasa, anzia ma-DC na ma-RC na wote ninyi Waheshimiwa viongozi hapa ni mashuhuda wa *behavior* za ma-DC na ma-RC kwa wafanyabiashara, hiyo sasa imesababisha watu na viwanda kuondoka. Nilisema katika Bunge hili utajiri ni *prestige*, kama mimi nakuwa na fedha halafu fedha yangu inakuwa ni adhabu maana yake nitatafuta mahali ambako nina amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee *General Tyre* ambayo Kamati yetu imefanya *conclusion* vizuri sana. *General Tyre* toka imefungwa ni miaka mingi sana. Nimekuwa kwenye Kamati wakati wa Bunge la Mheshimiwa Makinda, tukaongelea kuhusu *General Tyre*, leo tunavyoongea *General Tyre* bado haijafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *demand* ya tairi nchi hii ni kubwa katika kiwango ambacho hatuhitaji kiwanda cha

matairi Arusha peke yake, tunahitaji viwanda vya matairi zaidi ya viwanda hata kumi. Leo tairi nchi hii zinatoka China, Taiwan, Japan, Marekani na Ujerumani. Hii *demand* yote ya matairi ndani ya nchi, nchi hii ingekuwa *serious*, kiwanda cha matairi kisingekuwa mpaka leo hakipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa ushauri kwenye Kamati pale kilipo kiwanda cha *General Tyre* ni katikati ya makazi, ni *elite area*, ni karibu heka 70, ukiweza kuuza heka moja pale ni karibu shilingi milioni 300 ama shilingi milioni 400 kwa mnada kwa sababu ni eneo *prime*. Maana yake ni nini? *General Tyre* ukiithamanisha kuwa pesa leo pale katikati Arusha ni zaidi ya shilingi bilioni 28 mpaka bilioni 30. Kiwanda cha matairi hakihitaji dola milioni 15 au 20 kuanza. Maana yake ni nini? Mtaji ni eneo lile kuligeuza kuwa pesa, nendeni kwenye maeneo ya *EPZ* yaliyoko katika Mkoa wa Arusha chukue zaidi ya heka 500 au 100 tafuteni mwekezaji atawakuta na ardhi na pesa, kiwanda tayari kitafunguliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bahati mbaya huku watu mme-*operate manual*, watu huku mna-*operate* kwa woga, mkiingia kwenye vikao mnashindwa kuongea mmekuwa waoga, mmepandikizwa hofu, mnashindwa kuwaza kisasa, mnashindwa kuwaza kibiashara. Ndiyo maana leo hata maana ya *broker* kuwa katika biashara mmeshindwa kujua. Mnashindwa kuwawezesha ma-*broker* kwa kuwapa leseni, mnashindwa kuwarasimisha ma-*broker* kuwapa mizani, leo mnakwenda kutafuta *broker* Kenya! Ni kijana mmoja kutoka Kenya ana kampuni yake ya thamani ya dola 1,000 za Kimarekani, amevaa suti, amekuja na *caravan* na wapambe Mawaziri wote mmekimbilia Arusha kwenda kusaini mkataba na *broker* Kangombo. Kangombo kutoka Kenya amekuwa wa maana kweli kwa sababu tu amekuja suti na *private jet*, Mawaziri wote mkaacha kazi mnapigwa na *style*, kwa sababu hamuwazi kimkakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Watanzania wanafikiria ninyi mnaweza mkawa solution ya nchi hii, waone

mawazo yenu na waone michango yenu. Hata angalia dressing style tu ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara utajua kabisa huyu hawezi kuleta transformation yoyote katika uchumi wa Taifa hili. (Makofi/Kicheko) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachosema ni nini? Nachosema ni kwamba biashara haihitaji nguvu, biashara haimhitaji Sirro, uchumi haumuhitaji Sirro, uchumi hauhitaji nguvu. Maduka ya *Forex* Arusha yamefungwa mpaka leo. Hivi kweli ninyi mna Usalama wa Taifa unawambia...

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara, hebu kaa chini.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Waitara sema.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara, nimeshakupa ruhusa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba tusikilizane...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hapana hapa hutuko sokoni.

MBUNGE FULANI: Ulishakataza lakini.

MWENYEKITI: Hapana huu ni utaratibu, siyo mwongozo wala taratibu, Mheshimiwa Msigwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE, MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 61(f)...

MHE. KABWE Z.R. ZITTO: Haipo hiyo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE, MWITA M.. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, *sorry*, Kanuni ya 64(1)(f) ambayo inasema Mheshimiwa Mbunge anayechangia hatatumia lugha ya matusi au lugha ya kuudhi au kudhalilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Lema anachangia amemu-*address* Waziri wa Viwanda kwamba hata nguo ambazo anavaa haziwezi kuleta *transformation* ya viwanda nchi hii.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE, MWITA M.. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni lugha ya kashfa na ya kudhalilisha. Kwa hiyo, kama anaweza akathibitisha kwamba namna ambavyo

Mheshimiwa Waziri anavaa haimfai athibitisha au afute hiyo kauli yake. Hii siyo sawasawa kabisa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huyu anayemaliza kuongea ukiangalia koti lake linaweza likatoa suti za...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, endelea na hoja yako.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Lema amevaa shati la *Order Paper*.

MWENYEKITI: Lugha ambazo siyo acha.

MBUNGE FULANI: Shati lako limefanana na *Order Paper*.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Lema amevaa *Order Paper*. *(Kicheko)*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la Benki Kuu na maduka ya kubalisha fedha Arusha. Leo navyoongea hapa hakuna duka la kubadilisha fedha za kigeni Arusha linalofanya kazi na Arusha ndiyo *centerya* utalii katika Taifa hili. Ukitaka kubalisha fedha ya kigeni Arusha Mjini ni lazima uende Kilimanjaro Moshi. Sasa hawa watalii wanaokuja Arusha wanataka kununua bidhaa ndani, wanataka ku-*spend* unampeleka benki ya *NMB, CRDB* akapange foleni, anasubiri kubadilisha fedha, mazingira magumu kama haya yanasababisha wale wanaotafuta watalii yaani *tourist operator wa-shift destination* kutoka Arusha na Tanzania kwenda Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuja kuniambia katika Bunge la bajeti *high season* ya kipindi hiki watalii watapungua wengi sana kwa sababu ya matatizo mengine lakini hata hili

la kubadilisha fedha. Unajiuliza, hivi inachukuaje miezi miwili kupata *solution* ya kurudisha maduka ya kubadilisha fedha yaanze kufanya kazi kama kawaida? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wamenyang'anywa fedha na wakienda kudai anaambiwa ukiendelea kudai tutakupa *money laundry*. Kwa sababu kuna ushuhuda wa watu wameteseka na kesi hizi watu wanaamua kuacha kudai fedha zao. Maduka haya kuna Sheria za *BoT*, sheria hizo zina faini pengine na vifungo, hatujasikia mtu mmoja anapelekwa Mahakamani leo ni mwezi wa pili maduka Arusha yamefungwa. Maduka mengine mmefunga mnasema eti Lema ana *Bureau de Change* kumi namwomba Mungu anisaidie niwe nazo yaani kama mna Usalama unawaambia mimi *Bureau de Change* kumi, mnakuja kufunga maduka ya kubalisha fedha eti mimi nina maduka, huo Usalama unawaingiza chaka sana maana yake haujui kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tanzanite hapa inakufa, mmem-*mislead* Mheshimiwa Rais tanzanite haichungwi na ukuta, rushwa ni *attitude*, mtaweka ukuta na kamera wale askari mnaowalipa 700,000 kwa mwezi tutawapa milioni 50 yatapita mawe bilioni moja, fikirieni vizuri. Leo mnasema mnaweka na kamera, tena mmesema kamera ziwekwe bila tenda. Kila mgodi Mererani una fensi, akili ilikuwa ni nini, kama mngokuwa hamuwazi *manual*, ni kila mgodi mnatoa *standard* ya kamera, mnaweka *internet* ninyi, mna *monitor* migodi yote kutoka Dar es Salam na kutoka Arusha bila ninyi kuweka kamera. (*Makofi*)

MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu tunasema pengine na hizi *dressing code* zinawaathiri uwezo wenu wa kufikiria, mko *so manual*. (*Makofi*)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko hapa naangalia nyumbani nikiwa Dodoma, usiku naamka naangalia nyumbani kwangu, namwambia mke wangu nje kuna watu ponyeza *alarm*, ita mlinzi, sasa ninyi mnashindwa kuwaza hivyo tu, leo mmepiga ukuta hakuna mawe, sasa hapa itakuwaje, Mheshimiwa watakuwa wanaiba, weka kamera bila tenda, mnaweka kamera bila tenda! Kila mgodi una ukuta, weka kamera, weka mtu pale, *TRA* wako pale, mgodi ukitoa mawe siyo siri kila mtu huwa anajua, Arusha nzima huwa inajua, maana yake ni kwamba *TRA* watakwenda pale sasa leo mmeweka ukuta hausaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi siyo duka la mkate, mawe hayatoki kila siku. Mwanzo mgodi ulitoa mawe mkakusanya shilingi milioni 800 mwezi unaokuja migodi haikutoa mawe mkamfukuza na Mheshimiwa Angellah, mkakusanya sijui 500,000. Mikataba tunaibiwa, lile siyo duka la mkate ama la *colgate* kwamba mawe yanatoka kila siku. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilivyokuwa mdogo kaka yangu alikuwa anahudumia mgodi. Nikawa mkubwa, nikawa Mbunge nikahudumia mgodi, nikawa Mbunge kipindi cha pili mgodi ukahujumiwa hatukuwahi kupata hata chembe moja ya mawe. Sasa ninyi mkikaa kule...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ni kengele ya pili, nilishakuongezea dakika mbili.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Lema akiendelea kuchangia, Mheshimiwa Waitara alimwomba sana Mheshimiwa Lema kutovunja Kanuni ya 61(g) kwa kutumia lugha za kuudhi na kudhalilisha watu wengine. Nasimama kama *Chief Whip* kumwomba tu Mheshimiwa Lema hiyo lugha kwa kweli siyo lugha ya Kibunge ni lugha ambayo si nzuri. Mtu hawezi kupimwa *credibility* yake kwa kutazama *dressing code* yake aliyonayo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Waheshimiwa Wabunge...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge upande huu si tusubiri basi tusikilize Mwongozo wa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA, NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge tutengeneze tabia ya kuheshimiana, tutengeneze tabia ya kuheshimiana utu wetu na ubinadamu wetu na namna vile ambavyo tulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Lema hebu afute hiyo kauli yake ikikuridhisha kama kwa mujibu wa kifungu hicho nilichokiomba muongozo ni kifungu stahili na ni kifungu kinachofaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumamosi wakati nakuja Bungeni nilikuwa nimekuja na *jeans*, Mheshimiwa Pareso akaniambia *jeans* hairuhusiwi japokuwa ni *weekend* nikaenda kubadilisha, nikarudi kwenye *sense* kumbe huwa kuna mavazi ya sehemu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema hoja ni ndogo tu yule ni binadamu mwenzio, ni Waziri, futa tu huo msemu yamekwisha.

MHE. GODBLESS J. LEMA: *No, nampenda sana Jenista na anajua nimekubali mpenzi. (Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Millya baadaye Mheshimiwa Munde. Mheshimiwa Millya.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kunukuu kitabu ambacho asubuhi tumeambiwa kinauzwa pale nje na Mheshimiwa Spika kwa sababu wengine wanapenda sana kunukuu vitabu vya nje, lakini hapa ndani wanaviacha wakijidai kama hawaoni, naomba nianze kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu chenyewe kinaitwa *Corruption in Agony, Contemporary Nyerere of our time, by Jacob Roman Lubuva*. Kinaanza hivi naomba niendeleo; *"many people in Africa in beyond consider the President's personal character, attitude and leadership style peculiar to his predecessors. Some equate his leadership qualities to leadership ethos of the founding father of Tanzanian Nation, his excellent, the late Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Some commentators have yet compared President Magufuli to some known architects of African Nations like Kwame Nkrumah and Nelson Mandela with reference to his hate of corruption, a sense of self-reliance and pro-poor attitude."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini anaendelea, *"The President remarkable achievement immediate and radical pro-citizen's socio-economic transformations and*

unprecedented fast truck of political campaigns. Consequently, the President has been and presence of pre-electric and social media global being committed. "Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Zitto...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto...

MHE. JAMES K. MILLYA: ...mimi najua Kimasai vizuri na unajua hilo, lakini Mheshimiwa Zitto wakati fulani nilipokuwa Rais wa Chuo Kikuu cha Tumaini ulikuwa mtu wa kawaida/ Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa hiyo, unajua kwamba najua kiingereza vizuri, najua kimasai na kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa kuanza hili, Mheshimiwa Rais amefanya mikutano miwili; mmoja, Ikulu kuhusu wafanyabiashara Tanzania nzima, lakini bado Mheshimiwa Rais juzi alifanya mkutano na wachimbaji wa nchi nzima wadogo wadogo kuhusu biashara ya madini. Lakini wenzetu hawa kwa sababu hawaoni na hawataki kutambua, bado wanaponda nguvu za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimetaja rushwa? Kampeni za wenzetu mwaka 2002, 2005, 2010 walisimamia ajenda ya rushwa, rushwa, rushwa! Ametokea mtu ambaye anapigana dhahiri kwa ajili ya rushwa kwa sababu hawa wafanyabiashara siyo wengi wazuri. Ukiona mtu anatoa mapovu kuwatetea ujue inawezekana amerambishwa kidogo, lakini ukweli ni kwamba wengine na naomba nieleweke vizuri, siyo wafanyabiashara wote wabaya, lakini kuna wafanyabiashara kweli imedhihirika pale mfano, madini pale *airport, Tanzanite* wameshakamata zaidi ya watu wengi wanaiba madini, na hao unawatetea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, naomba nitoe takwimu za *Tanzanite* tangu ukuta huu uwekwe mambo ambayo yalikubalika kuhusu Marekani miaka hata kabla ya mimi kuanza shule ya msingi. Ukuta huu

Mheshimiwa Dkt. Magufuli baada ya kuona kwamba madini yetu yanaibiwa sana akaamua kuweka ukuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye Kamati Teule ya Bunge leo hii watu wa Mererani na hii kauli ichukueni, watu wa Mererani wanapendelea ukuta, wanafurahia ukuta, madini yameongezeka bei. Mimi ni Mbunge, kauli hii inaweza ikanihukumu mwaka 2020 lakini uhakika watu wangu wanafurahia ukuta. Ukuta hauna shida na ukuta nauunga mkono sana, kwa hiyo, watu wengine wanaokuja kuongea kuhusu ukuta hiyo waache kabisa kwa sababu ukuta uko sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Kaa chini.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Taarifa.

MWENYEKITI: Kaa chini, kaa chini au nikwambie Kiyao? *Awile Mundu. (Kicheko)*

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitengo kinaitwa *TANTRADE* kwenye Wizara ya Biashara. Mheshimiwa Rais juzi juzi hapo aliwaambia watu hawa hawasaidii Serikali yetu vizuri kabisa. *TANTRADE* inaongozwa na mtu anaitwa Edwin, naomba nitoe ushuhuda, kuna *EXCO* itafanyika China mwaka huu. Kuna vijana wa Arusha wameomba kuhudhuria na wanasema Serikali hatutaki hata shilingi moja kwenu. Wameomba tangu mwezi wa Oktoba, 2018 mpaka leo isingekuwa Katibu Mkuu wa Mambo ya Nje juzi Arusha, isingekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara huyu kijana asingesaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, watu wetu hawa ambao wamepewa dhamana ya kuwasaidia Watanzania

kukuza biashara zao wawasaidie kweli kweli. Niombe kitengo hiki cha *TANTRADE* kiangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani vita ambayo saa nyingine Mheshimiwa Dkt. Magufuli anapigwa ni ya nini? Ni kwa sababau kama Mheshimiwa Dkt. Magufuli anaingilai *interest* ya Wamarekani, *interest* ya Wabelgiji, *interest* ya Wajerumani kwa sababu wafanyabiashara wao wamesimamishwa na Canada na wengine ndiyo maana wanasukuma. Ninaomba Serikali yangu tuwaangalie wafanyabiashara tuwasaidie haswa, tuwasaidie, tuweke mifumo rafiki ya kusaidia wafanyabiashara kwa sababu nchi hii kiuchumi tutafahamika tu kama ni wazuri kama tuki-*compete* mfano na Kenya na nchi nyingine kiuchumi. Ninaomba nia njema ya Mheshimiwa Rais kwa kuita ile mikutano miwili ipo, ninaomba watu ambao wanasaidia kwenye kitengo cha biashara wasaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikitika asubuhi sana, kama mtu anataka maamuzi ambayo yanafanywa kwenye nchi na yanufaishe na watu wa Msumbiji nilisikitika kidogo. Mheshimiwa Zitto nikikosea ni faida yako wewe mpinzani kwa hiyo wewe ninaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, ngoja ngoja, Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Naam!

MWENYEKITI: Rudi kwako na wewe Mheshimiwa Zitto kiti chako kitazame kiti kwangu usimtazame... (*Kicheko*)

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ni moja, kama Serikali imepitisha bei elekezi kwa ajili ya korosho kuwaokoa watu wetu wa kawaida, kwa nini mtu mmoja ambaye anajua...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Millya hebu subiri.

Mheshimiwa Mwambe heshima ni kitu cha bure sana, ulichangia hoja yako asubuhi ya maslahi yako na ukajibiwa vizuri tu. Sasa wengine wana hoja zao nimeshazua miongozo, miongozo nitaoa mwenyewe sasa na masuala yote nitafanya mimi, msishangae kama kiti kitaanza kubadilika. Mtu mzima, una familia, unaheshimika na siyo jambo zuri watoto wako wakaelewa kuwa Baba kule anasemwa kule kwenye Bunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Millya!

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa kangomba utawafahamu tu. Na ni kweli wangependa korosho ya Mozambique inunuliwe ili ya watu wetu isinunuliwe waanze kupiga kelele ndiyo nia yao. Lakini hujuma hiyo imeshafahamika na hakika hamtaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara husika, biashara ni muhimu sana na Mheshimiwa Rais ana nia njema sana. Niombe kama ikiwezekana Bunge hili liweze kuunda Kamati Maalum ya Wafanyabiashara ambayo inaweza ikasaidia kumuongoza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri kutanzia matatizo ya kwenye sekta hii ya biashara, ningeomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona, naomba niwasilishe, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Mchafu ajiandae Mheshimiwa Saul Henry Amon.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisimamisha mbele ya Bunge lako tukufu, lakini pia nipende kuipongeza Serikali katika mwaka wake wa fedha 2018/2019 imeweza kutenga

kiasi cha shilingi trilioni 4.2 kwa ajili ya sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu wa bajeti unakwenda vizuri kwani katika sekta hii ya uchukuzi na mawasiliano ina miradi mikubwa na mingi sana hivyo nipende kuipongeza Serikali...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Hawa Mchafu ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, msikilizeni atoe vipande sasa. *(Makofi)*

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nipende kuipongeza sana Serikali na niseme tu nipende kuishauri Serikali sambamba na ushauri tulioutoa kwenye Kamati kuhakikisha bajeti inatolewa kwa wakati ili miradi yote ya maendeleo iweze kutekelezeka kwa wakati ikiwa ni ishara ya kupunguza madeni lakini pia kuipeleka nchi yetu kwa kasi iliyokuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia mchango wangu wa kwanza katika Shirika la Ndege la ATCL, nipende sana kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, ndani ya kipindi kifupi ameweza kununua ndege sita na ndege zingine ziko njiani zinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme, hii imewezesha kurahisisha huduma ya usafiri wa anga lakini pia imeongeza idadi ya safari na miruko kitu ambacho kinakwenda kuchochea ongezeko la ajira, ongezeko la watalii nchini lakini pia mapato yanakwenda kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kutaarifu Bunge lako tukufu, mnamo mwaka jana mwezi wa nane, Shirika la ATCL lilizindua safari ya kwenda Entebbe - Uganda, lakini Bujumbura-Burundi. Niseme mwezi wa pili mwaka huu tunakwenda kuzindua safari ya kwenda Johannesburg -South Africa, Harare pamoja na Lusaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maendeleo makubwa, lakini nipende tu kuishauri Serikali, tumenunua Ndege zetu kwasababu ya safari za ndani, safari za kikanda na safari za kimataifa. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba mharakisha mchakato uliokuwepo kati ya TCAA ya Tanzania na CAA ya nchini China ikiwezekana hata mtumie Balozi zetu watupe majibu sasa ni lini mchakato unakamilika ili tuanze safari za kwenda Bombay. Sambamba na hilo pia nipende kuitaka Serikali kuharakisha mchakato uliopo baina ya nchi ya China na Tanzania ili kuhakikisha safari ya Guangzhou inaanza haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine upo katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Mwalimu Nyerere. Kumekuwa na changamoto kubwa ya ucheleweshaji kwa malipo ya *treasury voucher*, hii inapelekea mzigo kukaa muda mrefu bandarini. Hivyo itakumbukwa kwamba gharama za kuhifadhi mzigo bandarini wakati mwingine zinazidi hata ile gharama ya kilichonunuliwa zile bidhaa ama ile mizigo gharama yake inakuwa ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vyote ambavyo vina *exemption* kutoka kwake ni lazima taratibu wa GN zikamilike. Huwezi kutoa vitu vyenye *exemption* ya VAT kama GN haijakamilika na ukisema unatoa kwa utaratibu huo unakuwa umevunja sheria. Sasa ninataka niwaombe TRA maana hatuna sababu leo hii tuliuliza kwa nini viti vya uwanja wa ndege vya *terminal three* mpaka leo havijafungwa? Lakini kwa nini *lift* ya uwanja wa ndege wa *terminal three* mpaka leo haijafungwa? Ni kwa sababu tunaambiwa masuala haya ya GN hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mnafahamu TRA ule mzigo uko *exempted*, lakini ule mzigo pia unatakiwa ufike katika *terminal three*, vyombo vya usalama vipo. Ushauri wetu tunashauri TRA sambamba na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ikibidi hata muwa-escort mfike mpaka eneo husika wakati vinafungwa mpo, mnashuhudia kwamba kweli huu mzigo ama hizi bidhaa ni kwa sababu ya *terminal three*. Hatuna sababu ya kuchelewa kwa sababu ya masuala ya

GN, wakati sisi huku tunaendelea na hizo *process* za *GN* huku zinaendelea. Kwa kufanya hivi tutaharakisha ama tunahatarisha *process* ya mkandarasi kuongezeka anapata muda, muda wa mradi unakuwa ni muda mrefu zaidi muda ule wa kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine uko kwa Shirika la Posta Tanzania, Shirika la Posta lina changamoto kubwa ya kulipa *pension* ya wafanyakazi. Mpaka mwezi Juni, 2018 imelipa tayari shilingi bilioni 4.9 pasipo Serikali kuwarejeshea lakini wakati huo huo *TRA* inawadai Shirika la Posta deni la shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni hili limetokana na kipindi kile Posta inashindwa kujiendesha ama inashindwa kufanya biashara vizuri. Kilichopo hapa baba anamdai mtoto na mtoto anamdai baba. Kwa kuwa Shirika letu la Posta limeanza kuimarika na kwa kuwa Shirika letu la Posta liko kwa ajili ya kufanya biashara kushindana na akina *DHL*, kushindana na wakina *Forex*, ushauri hapa tunaoutoa Wizara ya Fedha na Mipango ikae chini na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Miundombinu waangalie namna bora aidha ya kuwaondoshea hili deni ama kama siyo kuwaondoshea hili kuwaponguzia hili deni kwa sababu Shirika la Posta linadai Serikali na Serikali inadai Shirika la Posta. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iliangalie hilo ili tuweze kusaidia Shirika la Posta lisimame vizuri na liweze ku-*compete* na Mashirika mengine ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine utakuwa kwa Shirika la Kampuni ya Meli (*MSCL*), nipende kuipongeza sana Serikali katika mwaka wake wa fedha 2017/2018 ilitenga takribani shilingi 24,496,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa meli mbili mpya. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoikimbiza nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 24 tayari zimeshatolewa na kilichokwenda kufanyika mpaka sasa tumeshalipia ama imeshalipiwa *advance payment* kwa sababu ya chelezo. Lakini pia nyingine niseme wamelipa

advance payment ya kuanza kujenga meli mpya na *advance payment* nyingine imetolewa kwa ajili ya ukarabati wa *MV Victoria* na *MV Butiama* kwa ajili ya Ziwa Victoria. Kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa sana tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kikubwa kile anachokifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Ulivyozungumzia viti vya *airport* na ushauri viongozi na watu wa usalama kama kuhakikisha Serikali haipotezi mapato, Waziri wa Fedha aligeuka akakutazama. Sasa nakuagiza utoke hapo uje kwa Waziri wa Fedha umueleze vizuri na yeye aelewe ili *airport* ifunguliwe ifanyekazi. (Makofi)

Mheshimiwa Nsanzugwanko ajiandae Mheshimiwa Amon, ajiandae Mheshimiwa Mbatia, *sorry* Mheshimiwa Komu halafu Mheshimiwa Mbatia.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, *I hope* nina dakika 10?

MWENYEKITI: Wewe sema ukichoka utaniambia. (Kicheko)

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Sawa, nilitaka kuwa na uhakika nisikukwaze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwanza niwape hongera sana wenzetu wa Serikali hususani Wizara hii ya Miundombinu ambayo ni Wizara kubwa, niwape hongera Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wake wote kwenye Wizara hiyo. Kazi ni nzuri mnayoifanya lakini bado naamini wana nafasi ya kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye mambo machache sana, la kwanza nianze na Wizara hii ya

Miundombinu. Hii Wizara ni Wizara kubwa sana, hii ni Wizara ambayo ina taasisi zaidi ya 120, ni taasisi ambayo inasimamia mambo muhimu sana, na kusema kweli ni taasisi ambayo ndiyo kama mishipa ya damu kwenye uchumi wetu. Ukizungumza barabara ipo miundombinu, ukizungumza reli ipo miundombinu, bandari, mawasiliano, viwanja vya ndege, posta na simu, majengo, vivuko nchini, hali ya hewa na kadhalika bado yote haya yako chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe wenzetu wa Serikali mko hapa, hii Wizara ni kubwa sana. Pamoja na uwezo mkubwa walio nao Waheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wa Wizara hii na Makatibu wao Wakuu bado ni jambo jema kama Mheshimiwa Rais ikimpendeza Mheshimiwa Rais Magufuli afanye kama tulivyoshauri kwenye Wizara ya Kilimo na Mifugo na kama alivyofanya kwenye Wizara ya Biashara na Viwanda. Aitenganishe Wizara hii ili kuwe na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano kwa sababu Wizara hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa maoni yangu ni kwamba inafika mahali hata watendaji wanakuwa hawawezi kufuatilia mambo yote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye jambo mahususi, hilo lilikuwa la jumla sana, nalo ni hili la ujenzi wa reli. Tunajenga reli ya *Standard Gauge*, jambo jema sana kwa uchumi wa nchi yetu; lakini niombe sana wenzetu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha huko hapa, pendekezo lililopo ukurasa wa 31 ni pendekezo la msingi sana, kwamba ujenzi wa reli huu tunaouzungumza utakuwa na maana kiuchumi kama njia hii itajielekeza katika hiyo njia ya Tabora, Kigoma na Msongati na sababu zake wala huitaji kwenda shule kuzijua. Ni kwa sababu wenzetu wa *DRC* Mashariki yake na Kusini Mashariki yake wana mzigo mkubwa wana mzigo mzito ambao unahitaji kupita kwenye reli, ndizo *economics* zake tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge reli msingi wake si kubeba bianadamu, reli msingi wake ni

kubeba mizigo tena mizigo mizito. Hii dhana ya kwamba utatoka Dodoma utakwenda Dar es Salaam na mchicha wako na mayai yako ni mambo ya kizamani haya. Reli ni ya kiuchumi, tunaomba wenzetu wasimamizi Serikalini wakubaliane na agizo la ukurasa wa 31, tujikite eneo ambalo reli hii inakwenda kubeba mizigo mzito na huko si kwingine, ni Mashariki ya Demokrasia ya Congo na Kusini Mashariki ya Congo. Kwa maana ya kwamba reli hiyo ikitoka Tabora ikaenda Kigoma ikapata *branch* kwenda Msongati, kwa maana ya Uvinza kwenda Msongati - Burundi na nyingine ikaenda Kigoma - *Lake Tanganyika* mpaka Congo. Maana yake ni kwamba mizigo huo ambao una kisiwa kuwa zaidi ya tani milioni nne kwa mwaka utafanya reli hiyo iwe ni ya kiuchumi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa niliseme ni reli ya TAZARA. Mimi ni mjumbe wa Kamati hii ya Miundombinu, hili jambo la reli tumelizungumza sana. Reli ya TAZARA au reli ya uhuru kuna mambo ambayo hayaeleweki vizuri, hii reli imefilisika. Ziko taarifa kwenye magazeti tumezisoma na nyingine zikimnukuu Mheshimiwa Waziri kuhusu namna wanavyoshughulikia jambo hili la TAZARA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba lazima mkataba huu wa TAZARA wautazame upya. Reli ya TAZARA inakufa na tunaambiwa sasa kuna wakodishaji eti wameanza kukodisha reli yetu ya TAZARA na ningependa pengine wakati wa kipindi cha bajeti kinachokuja Mheshimiwa Waziri wa Fedha mtueleze vizuri kwamba hii reli mnaikodisha kwa akina nani na kwa gharama gani, maana mahusiano yaliyokuwepo kati yetu na Zambia wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere na Mzee Kaunda yamebadilika sana. Kuna haja sasa kuanza kuitazama kiuchumi zaidi reli hii ya TAZARA na kuanza kuitazama kwa maslahi ya Tanzania zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni viwanja vya ndege na ndege za ATCL. Hivi viwanja vya ndege ni vya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nilikuwa napenda niseme tu labda, kwamba nimekuwa Mkurugenzi kwenye Kampuni ya *PUMA Energy* kwa miaka saba. Ile Kampuni ya *PUMA Energy* ni Kampuni ya Serikali, kwa maana ya asilimia 50 za kampuni ile ni za Serikali. Kwenye viwanja vya ndege na mauzo ya mafuta ya ndege katika soko la *SADC*, *PUMA Energy* ina asilimia 86.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Waziri namwambia *PUMA Energy* ina asilimia 50 za Serikali tena za kihistoria Mheshimiwa Waziri akawa haelewi vizuri. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili liko kwako, huyu ni ng'ombe wa maziwa, kama alivyokuwa anaita Mheshimiwa Mwijage, huyu ni ng'ombe wa maziwa tumpe majani, tumtunze ili tuendelee kukamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya ndege, si ndege zetu, hata ndege za majirani zetu na kampuni nyingine zinahitaji kuwa na uhakika wa mafuta yao na Kampuni ya *PUMA Energy* kwa miaka zaidi ya 13 sasa wameshikilia hilo soko vizuri na sisi kama Serikali tunapata asilimia 50 ya mauzo yao. Ni jambo jema na tunaomba sana wenzetu wa Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hilo jaribio la kuwatishia kampuni yenu wenyewe asilimia 50 eti kulinyima leseni ni jambo ambalo naona kama ni aibu kidogo. Ni vyema mjiridhishe na ukweli wa mambo haya ili muweze kujua ni kitu gani mnachokizungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni kuhusu kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la TEHAMA, jambo la mawasiliano ni jambo muhimu sana, ni jambo mtambuka. Ni maoni yangu kabisa kwamba kazi inayofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) hoja hii ya TEHAMA sasa ihame iende shuleni na kwenye vyuo; dunia imebadilika, dunia ni ya mawasiliano, dunia ni ya mitandao. Ushauri wangu kwa Serikali, ingekuwa ni jambo jema sana sasa Mamlaka hii ya Mawasiliano tuihishe tui-*link* na vyuo vyetu

na shule zetu ili sasa suala la kujifunza juu ya mitandao na TEHAMA katika shule zetu liwe jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nilizungumzie suala la barabara. Iko sera ya dhahiri ya barabara; kwamba sera yetu ya ujenzi wa barabara kama ilivyoainishwa kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM ni kuunganisha mikoa na mikoa. Hata hivyo bado kuna mikoa michache katika nchi yetu haijaunganishwa kwa mujibu wa sera hiyo ya barabara. Mikoa hiyo ni pamoja na Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katai. Tunawaomba wenzetu wa Wizara ya Ujenzi acheni kuanzisha miradi mipya, kamilisheni miradi ambayo mmeshaianza ili barabara hizi zikamilike. Haingiii akilini wanaanza miradi mipya wakati miradi ya zamani bado haijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii barabara toka Nyakanazi mpaka Kabingo huko Kakonko ina mwaka wa kumi haijakamilika, leo hii barabara kutoka Kidahwe kuja Kasulu ina mwaka wa 11 haijakamilika, acheni kuanzisha miradi mipya tukamilishe miradi iliyopo. Tunaishukuru Serikali na wewe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa jitihada mlizozifanya kupitia wenzetu wa *African Development Bank* kwa mradi mkubwa wa barabara kutoka Kabingo – Kibondo – Kasulu mpaka Maruku kwenda Burundi. Ni juhudi kubwa nzuri lakini tunaomba zisimamiwe ili kazi hiyo iishe. Ni kilometa 261 na kwa kawaida tunadhani ndani ya miaka mitatu/minne au mitano inaweza ikawa imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika ujenzi wa miundombinu ni suala la umeme. Ningependa kujua, maana umeme nao ni miundombinu vilevile, ningependa kujua ujenzi wa *Hydro* ya Malagarasi umefikia wapi ambao hatimaye umetuingiza kwenye mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, najua muda wangu unakimbia, ni kuhusu jambo ambalo limezungumza na Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara na kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja amelizungumza na mimi pia

napenda kuliunga mkono. Tumeambiwa, kwa mujibu wa *report* ya Kamati, kwamba kuna viwanda 156 vilibinafsishwa, viwanda kama 50/56 vinafanya kazi na viwanda vingine 100 havifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashawishika kukubaliana kwamba kuna haja sasa Bunge hili liunde Kamati Maalum, si lazima iwe Kamati Teule, iundwe Kamati Maalum isaidiane na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara ili tuweze kujua hivi viwanda 100 *plus* vilivyobinafsishwa hatima yake ni nini? *Otherwise* itabaki ni wimbo tu kila siku viwanda, viwanda ambavyo havifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Tume ikiundwa inakuwa ya Kibunge tu wala si lazima iwe teule. Iwe Tume Maalum ambayo itakuwa na Waheshimiwa Wabunge wenzetu wachache pamoja na wenzetu wa Kamati ya Biashara na Viwanda, wapitie viwanda hivyo 100 *plus* ambavyo vimebinafsishwa lakini havifanyi kazi. Vinginevyo huu ni mwaka wa tatu, ni hadithi kila siku, kwamba viwanda, viwanda, lakini viwanda vyenyewe havifanyi kazi kama ambavyo tungetarajia vifanye kazi viweze kuingiza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ningependa kuzungumzia huu mradi wa chuma wa Liganga na Mchuchuma. Sisi wachache ambao tumebahatika kufika pale, ukifika Liganga, Mchuchuma na pale Mbamba Bay utaona Mwenyezi alikuwa na makusudi yake. Liganga ni mlima, mlima wote wa Liganga umejaa chuma, chini ya mlima ule kuna mto mkubwa. Ukienda kilometa 32 ukitoka Ludewa unakutana na eneo linaitwa Mchuchuma. Mchuchuma ni mto mkubwa sana na eneo lote la Mto limejaa makaa ya mawe, ni kama Mwenyezi Mungu alisema ninawapa makaa ya mawe mpate moto wa kuyayeyusha na maji ya Mto Mchuchuma uweze kupoza chuma chenu hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ukienda Kusini Mashariki kuna Bandari ya Mbamba Bay, ni kama

triangle una chuma, una makaa ya mawe na una bandari ya Mbamba Bay. Sasa kwa nini Serikali hamchukui hatua za makusudi (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, nakushukuru muda wako umekwisha, hoja yako nzuri na Mawaziri wamesikia, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda yupo. Sasa tunampa Mheshimiwa Amon wajiandae Mheshimiwa Komu, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Mwigulu.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitangulize kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa hatua za makusudi za kuanzisha na kulifufua Shirika la Ndege Tanzania ambalo limefanya tuwe na usafiri wa uhakika na kupunguza ajali nyingi ambazo tungepata hasa viongozi kwa kutembea kwa barabara. Vilevile kwa hatua zake za makusudi kujenga reli ya *Standard Gauge* pamoja na Mradi kubwa kabisa wa Umeme wa *Stiegler's Gorge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo vilevile nataka kuongea mimi machache kwa Mheshimiwa Waziri Mpango - Waziri wetu wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ina usumbufu hasa katika uingizaji wa mizigo na hili ninalizungumza na nitakuwa nalizungumza ili uweze kuliangalia. Mimi maombi yangu ni kumwomba Mheshimiwa Waziri Mpango na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara wajaribu kuwaita wafanyabiashara wanaoingiza mizigo ndani ya nchi hii, kwa sababu hatuwezi kuzungumza kwamba sisi tunajitosheleza kwa viwanda na kuwekewa vikwazo vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama wanasikiliza sana mimi mara nyingi Mheshimiwa Rais huwa namsikiliza sana, lakini wangesikiliza na kufuatalia kwa nini anasema punguzeni vikwazo? Amewaambia kuhusu majengo, amewaambia kwamba kodi hizi za juu mnazong' ang' ani watu hawana na ndiyo maana mnashindwa kuzikusanya. Muangalie vile alivyoondoa riba kwenye malimbikizo ya kodi watu wamelipa kiasi gani. Kwa hiyo, zile riba kubwa zikiondoka watu watalipa bila matatizo. Vilevile kuna vikwazo vingi na vikubwa sana kwenye taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali kwenye uingizaji wa mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uingizaji wa mizigo kutoka nje ya nchi; na ndiyo maana nimeomba viwanda na biashara pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukiwaita wafanyabiashara nikiwemo na mimi mwenyewe kwa sababu na-*declare interest* kwa sababu nafanya hizo biashara tuzungumze kwa nini watu wanakwenda porini kwa nini watu mipaka ni mingi, mikubwa na mirefu sana. Mfanyabiashara anahangaika na muda, hakuna mfanyabiashara anayehangaika na kingine, anahangaika na faida yake na muda. Sasa unapomkalisha mfanyabiashara kwanza Serikali haipati faida na mfanyabiashara hapati faida. Matokeo yake ni kwamba tunarudisha na kufifisha uchumi wa nchi nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa nini nazungumza kuhusu vikwazo vya biashara ambavyo vipo wakati wa uingizaji mizigo. Unakuta idara ni nyingi za Serikali zinazotoa vikwazo, *TRA* anakwambia mimi nimeimalizana na wewe ingiza, *TBS* anakwambia mimi na wewe tumemalizana ingiza, anakuja mtu wa vipimo anakwambia hapana mimi kwangu hujamaliza vipimo, nianze kutumia vipimo. Hujamaliza anakuja mtu wa mionzi anakwambiwa tunataka tuangalie hizo peremende ulizoleta kuhusu mionzi. Kwa hiyo, unakuta tunarudisha nyuma sana uingizaji wa mizigo na kusababisha watu kuona kwamba ni kero kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo naomba mngekaa kama Serikali. Vilevile kama hiyo sheria ilitungwa hapa na imetengeneza vikwazo, kwa nini msiirudishe hiyo sheria hapa ili iondolewe vikwazo? Hilo nalizungumzia la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili hawa wafanyabiashara mnawatengenezea *monopoly*, kwa sababu haiwezekani kwamba kila mfanyabiashara atakayekwenda kununua mizigo nje ya nchi atakwenda kwenye viwanda moja kwa moja, si rahisi hata kidogo. Nitajitolea mfano mimi mwenyewe, mimi nauza vipodozi, nijitolee mwenyewe, nisimpe mtu mwingine. Vipodozi ni aina 40; nikatafute makampuni 40 waje wafanye *inspection* mahali niliponunulia mizigo imetoka Uingereza, Canada, Marekani, Italy na kote huko wakague? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali Tukufu, na ninaamini hata Mheshimiwa Rais angeambiwa angesema tuje tukaguliwe hapa hapa Tanzania. Mtu anende akanunue alete mizigo yake akaguliwe hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani mnataka kuniambia kwamba kule ndiko wanajua kuangalia bora kuliko Tanzania ambayo nyie ndio mnaiona *physically*? Hilo ningelifanyia kazi na hilo watu wanakimbia na kunung'unika sana; hawawezi kuwaambia kwa sababu hawawezi kuwafikia, lakini mimi niliowafikia nataka mlielewe hilo mlizungumze mkae viwanda na biashara pamoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili kuwarahisishia wananchi na kurahisisha ukusanyaji wa kodi. Kwa sababu mfanyabiashara hawezi kukubali, ametoka *South Africa* umemzua mpakani, mpaka ni mrefu ukiliangalia Ziwa Nyasa lote lile ni mpaka. Ukienda moja kwa moja Mto Songwe – Tunduma - Zambia mpaka wapi kote ni mpaka, mtu ataamua kupita mahali pengine popote ili aweze kungiza kwa sababu yeye biashara yake anataka ifanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesimama kuchangia nakuomba kwa hilo tu kwamba naomba

Mheshimiwa Waziri Mpango na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara muwaite wafanyabiasha kama alivyofanya Mheshimiwa Rais kuangalia kero za wafanyabiashara ya madini juzi ilipendeza sana mbele ya watu. watu waliongea wakaongea mpaka sasa hivi nina imani mnalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini vilevile hili mkilizungumza, mkalipeleka kwa Mheshimiwa Rais kwamba kikwazo cha watu kuingiza mizigo ndani ya nchi hii ni hiki hapa; wanavyozungumza watu wote kwamba Serikali sikivu ni kwamba Mheshimiwa Rais wetu ni msikivu kwa mambo yetu yanayotusumbua ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, nami nimesimama kwa ajili ya hilo. *Otherwise* napongeza sana na ninaunga mkono Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuongea. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Mbatia ajiandae.

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni kitu cha muhimu sana na ni kitu ambacho ni cha kufa na kupona, kwa sababu bila mazingira binadamu anaweza kuwa hatarini kutoweka kama viumbe vingine ambavyo vinatishika sasa hivi kutoweka. Uwekezaji unaofanywa katika mazingira hauakisi hali hiyo. Kwa hiyo, niungane na Kamati kwamba iko haja ya Bunge kuisukuma zaidi Serikali kuona umuhimu wa mazingira na kuwekeza inavyotakiwa katika mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii kauli ya Mheshimiwa Rais ya juzi kwamba watu sasa wanaruhusiwa kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo yale ambayo ni tengefu na maeneo ya vyanzo vya maji. Sisi hatuna ugomvi na hilo, lakini tunasema kama kweli tunataka kufanya kazi kwa misingi ya kisheria na ili isiwe hii ni kugawa peremende

kwa sababu za kiuchaguzi, halafu baada ya uchaguzi wananchi waje wapate taabu kama wanavyopata kwenye maeneo mengine, Serikali ilete sheria, ilete mapendekezo ya marekebisho ya sheria, tuijadili hapa Bungeni, tuiptishe, ili watakaokwenda kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo ambayo Mheshimiwa Rais ameyasema, yaweze kuwa salama hata baada ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, niende sasa kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara. Kumekuwepo na kutokutekeleza mikakati mbalimbali ambayo tunaiweka. Hii mimi nasema kinachofanyika kwa kweli ni matamko tu, siyo mkakati. Ukiangalia, kuna mambo mengi ambayo yametajwa katika mpango wetu wa miaka mitano wa maendeleo. Leo ukiangalia ni kwa kiasi gani tunatekeleza yale ambayo tumeyaazimia, utashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwepo na miradi ya kimkakati, mfano ujenzi wa viwanda ambavyo vinaweza vikachochea mageuzi ya viwanda katika nchi hii. Hivyo viwanda viko vingi. Kuna Kiwanda cha *General Tyre*, Mheshimiwa Lema amesema sana hapa, hakuna chochote pamoja na uwekezaji mkubwa ambao unazidi zaidi ya shilingi bilioni 20 ambao umekwenda kule. Pesa zile zimetupwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa Mchuchuma na Liganga, kuna zaidi ya shilingi bilioni 20 nazo zimetupwa tu. Kuna Mradi wa Magadi Soda Engaruka, kuna zaidi ya shilingi bilioni sita zimekwenda kule, hakuna chochote kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali kama hiyo, nafikiri ipo haja ya kuangalia upya; na ili Bunge liweze kufika mahali pa kutoa maelekezo kwa Serikali, ili tuwe na vipaumbele ambavyo tunavifanyia kazi na tusiwe na haya matamko ambayo kwa namna moja ama nyingine yanaendelea kutumika kama vichocho kwa ajili ya kutengea fedha na kupiga fedha. Kwa sababu ukiangalia

Kamati inavyosema, Kiwanda cha *General Tyre* ni kama hakipo tena na hakitawezekana, lakini utashangaa mapendekezo ya bajeti yatakapokuja hapa, wanasema tunahitaji shilingi fulani kwa ajili ya kwenda kufanya utafiti, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo Kiwanda cha Urafiki ambapo sisi Tanzania ni wabia kwa asilimia 49, lakini kwenye Hotuba ya Kamati hapa wamesema kuna fedha zilikopwa na wabia wenzao wale wa China, wameandika pale *Yu 217,000* lakini Kamati inasema haifahamu hizo fedha zilikwenda wapi na zilifanyia nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati inasema hivyo, mwakilishi wetu pale ambaye ni Serikali, hajui kwamba hizo fedha zilizokopwa zilikweda kufanya nini na ziko wapi? Sasa katika hali ya namna hiyo ni kitu ambacho kwa kweli, kinaleta kichefuchefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo miradi, kuna mtu alizungumza hapa akasema tunawasifia Serikali ya Awamu ya Tano kwa kufanya *radical change*. Sasa *radical change* kwenye kitu gani? Ingekuwa *radical change* mngetuambia leo mnajenga Mchuchuma na Liganga. Ingekuwa ni *radical change* mngesema mnajenga Engaruka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *nim-quote* Mheshimiwa Waziri Stephen Wassira. Wakati fulani akiwa anawasilisha Mpango wa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2014/2015 alisema hivi: "Kwa upande wa Mradi wa Magadi Soda Bonde la Engaruka, Arusha, kazi ya kuchonga mashimo 12 kwa ajili ya uhakiki wingi na ubora na magadi umekamilika, ambapo imebainika kuwa eneo la Engaruka lina magadi yenye mita za ujazo bilioni 4.68 kiasi ambacho ni kikubwa kutosheleza uchimbaji wa magadi soda kwa zaidi ya miaka 400. Upatikanaji wa magadi soda utasaidia katika viwanda vya madawa, sabuni, nguo, rangi na viwanda vya kuchakata chuma."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyosoma hii, nikajua kumbe ndiyo maana Mheshimiwa Stephen Wassira anataka kurudi tena agombe Urais. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko Bwawa la Kidunda ambapo tungelijenga, linahitaji uwekezaji wa shilingi bilioni 251, leo tusingekuwa tunaenda kwenye *Stiegler's Gorge* kwa sababu tungepata umeme, tungepeta maji ya kumwagilia, tungepata uchumi mkubwa wa miwa, utalii na uvuvi. Sijui tumelogwa na nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uchumi wa gesi ambao ulihibiriwa sana, lakini leo tumeshafika 7% tu ya *utilization*, mbali na uwekezaji mkubwa tuliouweka pale kujenga bomba kutoka kule Mtwara mpaka Dar es Salaam kwa pesa ya mkopo ambayo tunapaswa tulipe miaka na miaka na hakuna chochote ambacho mnasema. Leo mnasema mnafanya *radical change*, mnafanya *radical change* kwenye kitu gani? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya biashara; na hapa nataka nimrejee ndugu yangu Mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Mpango. Katika hali ya biashara, wakati wanawasilisha mapendekezo ya hali ya uchumi alisema watahakikisha kunakuwepo na kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu. Wakasema watajenga mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji, na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa Waheshimiwa walivyoingia madarakani, kwa mujibu wa Benki yetu Kuu ya Tanzania, ile *economic monthly review*, deni la ndani, ambapo walisema vilevile watalipunguza, Novemba, 2015, lilikuwa shilingi trilion 7.9. Leo, yaani mwaka 2018 kwa takwimu za Benki Kuu ya Tanzania, deni la ndani ni shilingi trilion 14. (*Makofi*)

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo *radical change* iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *Tanzania World Bank Economic Update, Report Number 11*, utakuta umasikini katika nchi hii kwa kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano, wamezalisha watu masikini kwa miaka hii mitatu, milioni mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye urahisi wa kufanya biashara, hali imeendelea kuwa mbaya. Kuanzisha biashara tulikuwa wa 129 mwaka 2015, leo ni wa 162. (*Makofi*)

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ujenzi tulikuwa wa 126, leo ni 156. Kusajili mali (*property*) tulikuwa wa 133, leo ni 142. Kupata umeme tulikuwa wa 83, hapo tumepiga hatua kidogo kwa moja, tuko 82 sasa hivi. Biashara mpakani tulikuwa wa 180, leo wa 182.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni kwa sababu ya sera mbaya, ni kwa sababu ya misururu ya kodi, ni kwa sababu ya taasisi nyingi za udhibiti, ni kwa sababu ya kukosekana *one stop window*; ni kwa sababu ya Sheria za Kodi zisizokuwa rafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali imeamua kufanya biashara na kuacha jukumu lake la msingi la kisera la kuwa *facilitator*, kuwa mwezeshaji; imeamua kuwa mshindani. Mifano ipo. Leo tunafanya biashara ya kwenye ATCL kwa asilimia 100, *that is very wrong*.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu*)

MHE. ANTHONY C. KOMU: Sasa leo tunaenda kununua korosho.

MBUNGE FULANI: Wamelipa mikopo ya benki.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)

MHE. ANTHONY C. KOMU: Leo tunaenda kuingia kwenye biashara ya korosho kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akili ya kawaida, sisi tulipaswa tufanye *subsidy*, tulipaswa tu *subsidize*. Kama walikuwepo wafanyabiashara waliotaka kununua ile korosho kwa shilingi 2,700/=, sisi tungewaongezea hiyo shilingi 600/= tukawakopesha. Leo tungekuwa tunahitaji shilingi bilioni 200 tumalize biashara ya korosho. Leo tunataka shilingi bilioni 900, tumechukua Jeshi letu la Wananchi wako kule wanapigana vikumbo na wananchi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeua kabisa mfumo wa korosho. Baada ya mwaka huu kwisha, nani atanunua tena korosho? Mwaka kesho tena Serikali wataenda kununua korosho? Mmeua Bodi ya Korosho, mmeshindwa kui-*replace*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili tatizo la korosho, kwa mujibu wa hii *economic review*, maana sijui *Economic Review* ya Benki yetu ya Tanzania, kwenye *balance payment* tume-*experience deficit* ya dola milioni 500. Halafu mnasema mnafanya *radical change*. Ipi? (Makofi)

MBUNGE FULANI: Wapi?

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawaomba sana; wafanyabiashara waliokuwa wanafanya biashara za ku-*supply stationaries* sijui kwenye Jeshi la Polisi, waliokuwa wanafanya biashara ya kuchapa vitu mbalimbali, leo wanaofanya ni *TISS*, Usalama wa Taifa. Wanaenda kufanya... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. (Makofi)

Mheshimiwa Mbatia, ajiandae Mheshimiwa Mwigulu.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami nichangie Taarifa ya Kamati mbili zilizoko mbele ya Bunge letu. Nitaanza tu kwa kukumbusha wajibu wetu sisi Wabunge. Wakati wa Taarifa za Kamati Bunge wajibu wake namba moja ni yale majukumu kwa Taifa; tunaacha tofauti zetu nyingine zote; na ndiyo wajibu wa kuisimamia Serikali vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya Kamati ya Miundombinu, mimi ni Mjumbe. Taarifa yetu tunazungumzia kuhusu suala la bandari. Ukiangalia bandari zetu hasa Dar es Salaam na wale wengine wote wanaosimamia, kwenye maoni yetu ya Kamati tumeeleza namna gani ilivyo bora watu wetu kupata elimu au weledi katika Mataifa mbalimbali. Sasa nilikuwa najaribu kuangalia kwetu sisi Tanzania ambao kati ya nchi 38 za Afrika ambazo wana bandari, Tanzania tupo kwenye hali gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari zetu; nasisitiza, bandari zetu tukijilinganisha na bandari nyingine Afrika, Bandari za *Egypt* katika mambo ya *Container Terminal* ina uwezo wa *container* 2,900,000, Durban 2,600,000, Tangier Morocco 2,500,000 na Dar es Salaam 501,000. Kwenye mizigo, Bandari ya *South Africa* ni tani milioni 72, Mombasa tani milioni 31, Dar es Salaam tani 13,800,000 kwa mwaka. Ukiangalia kwenye *region* yetu hii, *East Africa* yote na *Central Africa*, Mombasa ndiyo wanaongoza. Sasa hapa ni kwa nini tunafikia kwenye hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema kwa nini tumefikia kwenye hali hii, hebu tuangalie hapa Tanzania uwezo wetu wa *forex*. Utalii kwa takwimu za Benki Kuu za mwezi Novemba ni bilioni 2.4, asilimia 28; dhahabu, *US Dollars* bilioni 1.5, asilimia 17.6; bandari, *transit goods*, bilioni 1.23, asilimia 14.5; mazao yote ya kilimo ni dola milioni 883 ambayo ni asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia bandari yetu ambalo ndilo lango kuu la uchumi, ambapo tunategemewa na Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, *DRC Congo*, Malawi, hata mpaka na Sudan; uwezo wa bandari yetu huwezi ukasema unawekeza, lazima ziende sambamba. Bandari na reli lazima ziendane sambamba, upende usipende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wa bandari na iko kwenye Taarifa ya Kamati yetu, huwezi ukaweka vinginevyo kabla hujaangalia mzigo mkubwa wa bandari unapatikana wapi? Kwa hiyo, kipaumbele cha kiuchumi lazima kabisa bila kumung'unya maneno lazima tungewekeza kwenye tawi la Tabora, Kigoma, Uvinza na Msogati. Ambapo sasa ukiunganisha na bandari yetu ya Dar es Salaam ndiyo unaweza ukasema sasa hapa uchumi wako unaenda barabara, badala ya kuanza mambo mengine labda ya kisiasa na mambo ya namna ambayo hayawezekani kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumzia bandari? Sisi ukanda wetu una urefu wa kilometa za bahari 1,424 na *strategically* tungetumia bandari yetu tu, *forex* ambayo mwaka jana, kwa takwimu za *BoT*, dola bilioni 8.5 tungezipata zote kutoka Bandari ya Dar es Salaam. Leo hii Bandari ya Dar es Salaam kama tulivyosema hapa ni asilimia 14 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui tunafikiriaje? Lazima tuangalie hata washindani wetu wa Afrika, wakati sisi tunazungumzia mambo ya *20 equivalent units* za mambo ya *container*, ukizungumzia Shanghai peke yake ni zaidi ya milioni 40 wakati sisi ni 501,000. Sasa *radical change* katika uchumi itakuwaje kama hatuwezi tuka-*think globally* na tukauza dhahabu *in local solution*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia bandari za Afrika. Kuanzia *South Africa* mpaka Na. 13, unaenda *South Africa*, unaenda *Egypt*, Nigeria, Morocco, Algeria, Congo, Kenya, *Ivory Coast*, mpaka Na. 13 wala huoni

Tanzania tuko wapi? Sisi tuko hoi bin taaban. Kwenye mizigo kwa mwaka ni tani milioni 13.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwekeza vizuri katika Bandari ya Dar es Salaam kwenye *wharfage* badala ya Serikali au Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa maana ya Hazina kuchukua zaidi ya bilioni 400 wangewaachia bandari wawekeze *serious* kwenye bandari ili bandari zetu ziweze kuwa na nguvu za kutosha katika kutekeleza wajibu wake. Vile vile tumezungumzia bandari za nchi kavu miaka nenda rudi, miaka nenda rudi, songa, panda hivi *and so forth*, waende wakajifunze duniani wanafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia bandari nizungumzie kidogo barabara za Jiji la Dar es Salaam, barabara za Jiji la Dar es Salaam ni zaidi ya miaka kumi sasa na iko ukurasa wa 38, tumezungumzia suala la muda unaopotea barabarani, suala la mafuta, suala la msongo wa mawazo (*stress*) na suala la uchafuzi wa mazingira. Tulipozungumzia Dar es Salaam mpaka nakumbuka taarifa ya Chenge *one* na mkakati tufanye nini? Tukaja na mawazo na Serikali ikaja na *MV* Dar es Salaam kwa ajili ya kusafirisha watu kwa njia ya maji, naomba niulize Serikali leo *MV* Dar es Salaam ipo wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ingesaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam na ingesaidia kuzuia uchafuzi wa mazingira na muda wa kufanya kazi ambapo kila siku msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam unagharimu Taifa hili zaidi ya shilingi za Kitanzania bilioni nne kwa utafiti uliofanyika takribani miaka kumi iliyopita tangu mwaka 2009. Sasa Mheshimiwa Januari Makamba na mkakati wake wa mazingira na nini ile *MV* Dar es Salaam ipo wapi? Ili iweze kufanya kazi kwa mujibu na taratibu zinazosaidia, ni Serikali hiyo hiyo moja. (*Makofi*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ipo Dar es Salaam sawa kama ipo wapi basi tuhakikishe

kwa sababu gani? Usafiri ulio rahisi kuliko mwingine wowote na unarahisisha ni usafiri wa majini na utasaidia katika mikakati ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizingumzie kuhusu barabara zetu ambazo nimezungumzia za Dar es salaam lazima kuwepo na mkakati madhubuti zile *by pass, flyovers* kuahakikisha tunaondoa na kuwekeza kwelikweli kwa sababu pale ndiyo lango kuu la uchumi ndiyo uchumi wetu zaidi mapato yetu ndani asilimia karibu takribani 80 tunapata katika Jiji la Dar es Salaam sasa *either you like or not* lazima tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la hizi barabara ambazo zinasaidia katika maendeo mbalimbali huwezi katika karne hii tukaanza kuzungumzia kabla hatujaunganisha barabara za Mikoa ya Katavi - Kigoma, Katavi - Tabora, Kigoma - Kagera, Njombe - Makete na Mbeya kwa pamoja ili kuhakikisha nchi nzima miji yote mikuu imeunganishwa kwa barabara za lami na ni sera ya Serikali kuhakikisha kipaumbele kinawekwa kwenye barabara zote kwenye miji yote mikuu kuhakikisha imeunganishwa kwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nizingumzie kidogo kuhusu Kamati ya Viwanda na Biashara, ule ukurasa wa 80 ambao unazungumzia mazingira ya kufanya biashara yaliyo rafiki, tukiri kwamba *private sector* ni *engine* ya uchumi wetu, lakini leo hii mazingira ya wafanyabiashara na Kamati imeandika hapa katika ukurasa wa 80 yamekuwa ni magumu kwelikweli na yamekuwa ya hofu. Sasa tutapata wapi fedha kama tunafanya wafanyabiashara ni washindani wa Serikali, badala ya Serikali kuwawezesha wafanyabiashara kujenga mazingira rafiki ya kikodi, kujenga mazingira rafiki ya uwekezaji, kujenga mazingira rafiki na wakitoa kauli watoe kauli, kwa mfano, niulize lile suala la *refundable*, zile fedha billion 32 kwenye viwanda vya sukari hasa viwanda vya soda, mbona hawajarudishiwa kodi yao? Naomba warudishiwe fedha hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduka ya fedha za kigeni Mkoa wa Arusha amesema Mheshimiwa Lema hapa yapo kwenye hali mbaya na zile fedha zao mlizochukua Benki Kuu muda umetoshwa, warudishiwe fedha zao *immediately* ili wafanyabiashara hawa waweze kuendelea kufanya shughuli zao, kama wana makosa waelezwe hayo makosa na kama wameshafanya ukaguzi wao wazirudishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Arusha katika uchumi, utalii, tumekubaliana hapa *forex* kwenye utalii ni zaidi *dollar billion* 2.4 ambayo ni sawa na asilimia 28 ya fedha zote za *forex* ni za utalii na Jiji la Arusha ni la utalii. Sasa *forex* mnafunga, sasa tumlilie nani na watu wafanye nini? Sasa kama tukifanya maamuzi ya namna hii ya kupararazi *forex* katika Jiji la Arusha ambayo ndiyo *radical change, this is very unfortunately. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe kwamba wakati wa Kamati za Bajeti kama zinarudia kwa sababu wa muda, sisi Wabunge jukumu letu namba moja ni kuhisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi, kwa sababu sisi tumekuja hapa ili kuweza kusimamia kodi za wananchi, sisi tumekuja hapa kwa ajili ya wananchi ambao ni walipakodi, wajibu wetu namba moja ni kuisimamia Serikali, kuishauri Serikali, kuweka kando tofauti ya vyama vyetu vya siasa ili kuona Taifa letu linapewa kipaumbele na wajibu wa Mbunge namba moja ni kwa Taifa lake, Taifa lake, Taifa lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi leo hii huu ukurasa wa 80, unasema mazingira ya kufanya biashara yamekuwa magumu na ugumu huo kwa kiasi kikubwa unasababishwa na uwekezaji wa Sheria mbaya za kodi na kwa kuwa hali hiyo imepelekea baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kufunga biashara zao ambao hali hii haitoi tafsira nzuri kwa ustawi wa Tanzania, lakini pia wawekezaji nchini. Sasa niombe Serikali na niishauri kwa nia ya dhati kabisa, mkinena maneno myasimamie maneno yenu, mkisema ni mazingira rafiki, kweli yaonekane rafiki, kama ni kodi kwenye biashara kwa mfano kwenye utalii kuna kodi zaidi 50, yatakuwaje mazingira rafiki na mazingira wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa kusema na kuomba tena chonde chonde, tujaribu kuangalia tusiangalie humu ndani tukapongezana humu Tanzania, tujiangalie Afrika tupo kwenye *position* gani? Kidunia tuko kwenye *position* gani, elimu ya teknolojia dunia hii na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani sisi tuko kwenye *position* gani? Tukiweza ku-*think global and have a local solution*, naamini tutafanya *radical change* kuondoa hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwigulu, jiandae Mheshimiwa Genzabuke.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja zetu hizi ambazo ni muhimu sana zilizo mezani. Jambo la kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya yeye pamoja na wasaidizi wake, lakini pia niwapongeze Mawaziri walioko katika Wizara hizi ambazo leo ajenda hizo ziko mezani hapa Bungeni kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia nimesikiliza pia hata hoja za wachangiaji wengine. Tunapoongea masuala makubwa hasa ya kitaifa ni vizuri sana tukawa tunapata tafsiri zilizo sahihi, kwa sababu usipopata tafsiri zilizo sahihi zinaweza zikasababisha taharuki kwenye mambo ambayo hayapo. Nilikuwa namsikiliza shemeji yangu Mheshimiwa Komu pale ameongelea kipengele kimoja *cha balance of payment (BoP)*.

Waheshimiwa Wabunge jambo alilokuwa analisemea Mheshimiwa Komu ni jambo la kiuchumi na unapoangalia *performance* ya uchumi katika Taifa huangalii kigezo kimoja na ambacho mabadiliko yake yanabadilika majira kwa majira, unaangalia vigezo ambavyo vinatokana na utekelezaji wa kiseru *per se*. Kwa mfano, huwezi ukasema uchumi wetu umeyumba kwa kuangalia kigezo cha *BoP* kwamba imerekodi *deficit* katika majira ambayo katika Taifa letu si majira ya uvunaji, si majira ya mavuno, ni majira ambayo

kwa vyovyote vile hata ukiangalia katika miaka mingine katika Taifa lolote katika majira ambayo si ya mavuno utakuta *BoPina-deteriorate* kutokana na kwamba si majira ya kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia vigezo kama mfumuko wa bei ambacho ni kitu cha kisera, ukaangalia vigezo kama akiba ya fedha katika Taifa ambacho ni kigezo cha kisera Tanzania imevunja rekodi na tumepata taarifa kwamba zile *minimum requirement...*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Nimeshasema taarifa hamna tena kaa chini na Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Zitto, rudi kwenye kiti chako

MBUNGE FULANI: Zitto ndiyo Mwalimu wenu.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Imezidi miezi mitatu, iko zaidi kwa mbali kabisa miezi mitatu ambayo huwa inapimika katika *importation* lakini na mfumuko uko chini kwa muda mrefu, yaani siyo mfumuko ambao unayumbayumba ambao mwekezaji yeyote angetakiwa kuangalia katika Taifa aone jinsi suala lilivyo. Hivi vigezo vingine ambavo amevisemea vinavyohusiana na *indicators* za ufanyaji wa biashara, labda nimwombe kwenye hili Mheshimiwa Waziri na Wizara yake watafute *copy* ya vitabu vile vya *blue print* ambayo ilishapitishwa na Serikali na ilishakuwa tayari kwa ajili ya utekelezaji na baadhi ya mambo tayari yameshaanza kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yale hata siku ambapo Mheshimiwa Rais alikutana na wafanyabiashara ni mambo yaliyotolewa ufafanuzi na wafanyabiashara waliondoka wakiwa wameridhika. Siku ile wao wenyewe ni mashahidi kwa sababu jambo hilo halikuwa kifichoni, lilikuwa *live*. Wafanyabiashara walipopewa mambo ambayo Serikali ya CCM imeshafanya, waliona kazi iliyofanyika. Hii *blue printing* ambayo tayari ilishapitishwa inatoa majibu mengi ya vitu hivi vilikuwa vinasema *ranking* yake ambavyo

anavisemea vinashusha *ranking* ya nchi yetu katika ufanyaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utamaduni hasa hasa wa kiafrika kupenda kusema mabaya ya kwako na kudhania kwingine kuko vizuri. Ukienda nchi nyingi za Afrika wao wanatolea mfano mambo mazuri ya Tanzania, ukienda kwenye *SADC* watatolea mfano Tanzania, ukienda *EAC* watatolea mfano Tanzania, ila ukirudi Tanzania watasema tume-*stack*. Sasa ni utaratibu wa kutokujisomea labda kujua wengine wanafanyaje? Haya ambayo tunaweza tukayasema ambayo Mheshimiwa Lema alisema *purchasing power* ni utaratibu wa kujua unaanzia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa ni lazima ufanye utaratibu wa kuondoka kwenye *vicious circle* lazima uvunje ile *circle*, ukiamua kutokuvunja *vicious circle* kutokutoka kwenye mduara ule wa umaskini utaendelea kuwa kwenye umaskini. Natoa huo mchango na kwa sababu tunaongelea mambo ya viwanda nasema lazima utoke kwenye *vicious circle* ili hili somo waweze kulielewa. *Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unatokaje kwenye *vicious circle* ili uweze kwenda kwenye viwanda, lazima kwanza uweke miundombinu ambayo ni *very solid* na niipongeze Serikali kwenye hili, haisemei tu kwenye matamko ama kauli mbiu kama mchangiaji mmoja alivyosema, hatua tunazona ambazo zinaenda kwenye miundombinu ambayo ni *very solid* kwenda kwenye viwanda. Moja ya kitu kinafanyika ni kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *requirement* ya msingi sana katika nchi yoyote inayotaka kwenda kwenye viwanda. Ukiamua kuwa na vile walivyokuwa wanafanya babu zetu kusaga kwa mawe au unaweza ushitaji umeme lakini kama unataka kwenda kwenye *solid foundation* ya viwanda lazima uwe na umeme wa uhakika. Jambo hili Serikali imefanya tena kwa makusudi na halijafanyika mafichoni, mnaona maeneo ambayo uwekezaji kwenye umeme unaenda na mambo haya yataenda mpaka vijijini. Kwa hiyo, kwenye hili

la *solid foundation* kwenye miundombinu moja ni umeme; la pili ni maji; lakini la tatu hata hii miundombinu mikubwa ya usafirishaji, tumeona kwenye reli, lakini tumeona kwenye barabara na kwa sababu ili uchumi uwe *inclusive* inaenda mpaka kwenye barabara za vijijini na huko kuna *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo machache ambayo napenda kushauri; jambo la kwanza kwenye ushauri; kwa sababu tunatengeneza miundombinu ya miaka mingi itakayohimili uchumi wa viwanda, ni vizuri sana kwa sasa hivi kila mkoa jambo ambalo Mheshimiwa Raisi ameshalisitiza mara nyingi likafanyiwa kazi la kuwa na *industry tax*, watu wanaotaka kuwekeza kwenye viwanda wasije wakawa wanaenda kuuziana maeneo na wenyeji, mwisho tunakuja kujikuta kuna kiwanda kipo kwenye makazi na hiyo inatokea utiririshaji maji machafu pamoja na vitu vingine katika makazi, jambo hili limesemwa sana kwa hiyo wenzetu waliopo kwenye kule mikoani lakini pia na Idara zinazohusika ni vyema sana wakalizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni vizuri sana kufanya ile *zoning* nchi yetu ili kuondoa migogoro kwa sababu population inaongezeka na ardhi ni ile ile ni vizuri sana kama tunataka kulifanikisha jambo hili ambalo limeshaanza kufanyiwa kazi vizuri tukawa na *zoning*, lazima kuwa na maeneo ambayo yameshajitambulisha yenyewe ili yaweze kupewa kipaumbele katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kanda ya Kati kuna mambo ya alizeti, lilikuwepo hili jambo la *cluster* ambalo lilishaanzishwa, ni vema likatiliwa nguvu, kuwe na *corridors* ambazo ni mahususi kwa ajili ya mchele, hapo tutakapoweza kuwa wauzaji wakubwa wa mchele kidunia, maeneo mengine ya ng'ombe wa nyama, maeneo mengine ng'ombe wa maziwa ili kuondoa mwingiliano kwamba wale wengine wamepanda mchele wale wengine wamepitisha mifugo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa sababu nilishaona kingele imegonga na Watanzania kwa

ujumla, ni vyema tukaendelea kutambua nguvu tuliyonayo kwenye upande wa soko la bidhaa zetu, matumizi ya bidhaa kwa maana ya kupenda bidhaa zetu. Hili ni jambo ambalo litatusaidia lakini kama tutategemea vya wenzetu na wenzetu wakategemea vya kwao ni dhahiri kwamba sisi vya kwetu vitakosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata Bungeni kanuni zetu hizi tulizoweka kama sisi wanaume zinatutambua tu kwamba tunatakiwa tuje tumevaa hizi *western suit*, mngetafuta siku nyingine msembe Wabunge wa kiume tungeruhusiwa mashati ya vitenge yanayotokana na bidhaa za kwetu hapa, unakuwa nadhifu na shati la Kitanzania, lakini siyo hii ambayo ipo kikanuni kabisa kwamba, lazima uje na suti ya kimagharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa Mheshimiwa Genzabuke, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Bhagwanji na Mheshimiwa Dkt. Mollel dakika tano, tano.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia. Kwanza naomba niwapongeze Wenyeviti wote wawili kwa taarifa zao nzuri, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyojitabisha kwa ajili ya Watanzania, anafanya kazi usiku na mchana ili kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu reli ya *SGR*, reli hii inakwenda sambamba na viwanda pamoja na kilimo, vitu vyote vinashabihiana. Naomba kushauri wakati tunaendelea na ujenzi wa reli, tuweze kulima mazao ya

biashara lakini niishukuru Serikali kwa jinsi ilivyokuja na mpango wa kilimo wa mchikichi. Katika Mkoa wa Kigoma tukiwekeza katika kilimo cha mchikichi na huku reli ikiwa inajengwa, wakati reli ya *SGR* inakamilika, mazao yale ya mchikichi yatakuwa tayari yanaanza kustawi na kuvunwa na kupelekwa sokoni. Kwa hiyo, kupitia reli hiyo tutaweza kusafirisha mawese kupeleka katika viwanda. Hivyo, naipongeza Serikali kwa kwenda sambamba na mambo ya ujenzi wa miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niishukuru Serikali kwa kutoa pesa kwa ajili ya kujenga barabara kutoka Kankoko – Kibondo – Kasulu - Buhigwe naipongeza sana Serikali kwa kuweza kuliona hilo. Naomba wakati barabara hiyo imejengwa iweze kujengwa *border post* kwa ajili ya kusafirisha mizigo inayotoka Burundi kuja Tanzania ili waweze kufanya biashara kwa kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma umepakana na nchi jirani ya Kongo pamoja na Burundi na sisi Kigoma tunalima mahindi, maharage, mpunga pamoja na mihogo. Kwa hiyo *border* katika Mkoa wa Kigoma kwa maana ya Wilaya zote nne zimepakana na nchi jirani; ukienda Kakonko imepakana na Burundi, ukija Buhigwe imepakana na Burundi, lakini ukija Kigoma Vijijini nayo imepakana na nchi ya *DRC*. Kwa hiyo tunaomba *boader* iweze kujengwa ili wananchi wa pande zote mbili, wananchi wa Tanzania pamoja na wananchi wa kutoka Burundi na Kongo waweze kufanya biashara kwa kushirikiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri, reli ya *SGR* iweze kuanzia Kigoma kabla ya kwenda Kigali kwa sababu mizigo mingi inatokea Burundi na Kongo na inapitia Kigoma. Kwa hiyo, naomba kabla ya kwenda kujenga Kigali, ianzie Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo linawasumbua sana wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Mara nyingi watu wa Uhamiaji wamekuwa wakiwasumbua wafanyabiashara kwa kuweka vikwazo mbalimbali kwamba

siyo Watanzania kitu ambacho kinawakatisha tamaa wananchi wakati mwingine wanashindwa kufanya biashara kwa uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watu wa Uhamiaji waliangalie suala hili wasiwazuie wananchi kufanya biashara ila wawaelimise waweze kujua ni jinsi gani wale watu ambao wapo mipakani wanaweza kufanya biashara kwa kushirikiana na nchi jirani. Tukiendelea kuwasumbua wananchi ambao wanatokea mipakani tutaendelea kupoteza mapato. Serikali haitaingiza mapato kwa sababu wananchi hawatatumia *border* watatumia vichocho kwa ajili ya kuingiza biashara zao sokoni. Kwa hiyo, tutakuwa tumepoteza mapato kwa sababu ya kusumbuliwa na watu wa Uhamiaji.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Mollel jandae Mheshimiwa Bhagwanji na Mheshimiwa Dkt. Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niende moja kwa moja katika kuchangia kwenye Kamati ya Miundombinu, nianze nayo kwanza. Naipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa ambazo imefanya na hasa Mheshimiwa Rais katika kulifufua na kuiendeleza *TTCL*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa *TTCL* ilikwishakufa lakini kwa jitihada na weledi mkubwa wa Rais wetu tumeona sasa shirika hili tayari limekwishafufuka. Ni matarajio yangu kwamba sasa litakwenda kujiendesha kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili shirika hili liweze kujijendesha kwa faida naishauri Serikali kuona ni namna gani Wizara na Taasisi zinaweza kulipa yale madeni ili pia liweze kuendelea kutoa gawio kama walivyoweza kufanya kwa mwaka jana. Pasipo kulipa haya madeni bado itakuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika viwanja vya ndege. Naipongeza pia Serikali na Kamati kwa jinsi ambavyo wametuletea ripoti inayoonyesha jitihada za Serikali katika ujenzi huu wa uwanja wa ndege na hasa *Terminal III*. Uwanja huu utakapokamilika utapokea kwa siku watu zaidi ya 2,000, hili pia litasaidia kuleta watalii na wageni wengi kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina ushauri kwa Serikali kwa sababu pamoja na jitihada hizi nzuri lakini suala la miundombinu hasa kwa watu wenye ulemavu bado ni tatizo. Katika viwanja vyetu vya ndege hakuna *lift* ambazo zinaweza kuwasaidia watu wenye ulemavu. Mara nyingi ukienda katika uwanja wa ndege hata ile *lift* iliyopo wakati mwingine unakuta haifanyi kazi. Kwa hiyo, watu wenye ulemavu, wagonjwa inakuwa shida kufika katika viwanja vya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tumeona kwamba wengine wanalazimika kuwabeba, siyo kila mtu atapenda kushikwashikwa kubebwa kupandishwa kwenye ndege kutokana na ule umbali. Kwa hiyo, niwaombe sana Serikali na hasa Wizara husika kuona ni jinsi gani tunaweza hii miundombinu ili angalau basi na watu wenye ulemavu waweze kufurahia mazingira hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi sana ukifika maeneo mengine kama Dubai unapotua tu kwenye uwanja tayari unakuta kwa mtu mwenye ulemavu miundombinu imeandaliwa na mtu huyu inakuwa ni rahisi kufika eneo ambalo anataka. Kwa hiyo, naishauri Serikali kuona ni kwa jinsi gani wataboresha miundombinu na kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu. Naipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa miundombinu ambayo tumeona sasa Tanzania yetu ni kwa jinsi gani tunaunganishwa na barabara ambazo zimejengwa. Barabara hizi zitaweza kukuza uchumi, kipato kwa mtu mmoja mmoja lakini kwa maeneo mengi wananchi wataweza kusafirisha bidhaa zao kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itawasaidia wao badala ya kuuza bidhaa zao katika maeneo yale ambayo kwa namna moja au nyingine hawezi kupata fedha ambazo wanatarajia wao lakini wakitoka pale na kwa sababu kwa hivi sasa miundombinu tayari ipo itasaidia sasa kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja lakini pia kuongeza pato kwa kwa Serikali yetu kwa sababu itapata kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye barabara, naomba tu Serikali kwa sababu nimechunguza na kuona wamejitahidi kuweka alama za barabarani na alama hizi zipo kuhakikisha kwamba hapa kuna watu wenye mahitaji maalum wanataka kuvuka, tumeona sasa hivi zebra zinaheshimika sana. Hata hivyo, maeneo mengi ambapo kuna alama zinazowawezesha watu wenye ulemavu waweze kuvuka bado ni tatizo Watanzania hawaheshimu alama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Bhagwanji atafuata Mheshimiwa Agness Marwa halafu Mheshimiwa Dkt. Mollel.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimepata nafasi hii ili kuzungumzia mambo yetu ya bajeti. Nampongeza Rais wangu Dkt.

Magufuli kwa Ilani yake ya CCM anaboresha Tanzania yetu na kutuondoa katika umaskini wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Mawaziri na Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Miundombinu na wajumbe wote. Sisi tunafanya kazi kuendana na wito wa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo machache mazito. La kwanza ni bandari. Bandari yetu Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri wanasimamia vizuri kuanzia Dar es Salaam, Mtwara, Tanga na Zanzibar. Kwa upande wa Tanga tumepata mambo ya mafuta basi tutapata mapato zaidi na vilevile kwa Zanzibar tuboresha bandari yetu, Muungano wetu inahusu kuboresha bandari yetu tuweze kuongeza makontena zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu Reli ya *Standard Gauge*. Nampongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri, sisi Kamati tumetembelea kuanzia Dar es Salaam, Morogoro kushuhudia ujenzi wa *Standard Gauge*. Reli hii italeta mapato kwa sababu tutaenda mpaka Mwanza na nchi za jirani kupakia mizigo na kupata fedha za kutatua matatizo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais na Kamati yaani Mheshimiwa Magufuli amesimamia kuleta ndege sita (6). Nia na madhumuni yake ni kuondoa umaskini katika Tanzania yetu, tunasimamia nchi yetu na wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameleta ndege sita (6) na zinafanya kazi moja kwa moja. Hata hivyo, naomba kuboresha iende ndege China na India kuleta watalii Tanzania mpaka Zanzibar. Mungu amsaidie Mheshimiwa Rais Magufuli, *Inshallah*, Mungu amzidishie alete meli pia na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naenda kuzungumzia barabara. Barabara yetu inafanya kazi nzuri kuanzia Dar es

Salaam, Morogoro, Arusha, Mwanza. Barabara hii tukiiboresha basi italeta mapato zaidi na tutafikia uchumi wa kati. Kwa sababu unapotoka Zanzibar au nchi nyingine ile mzigo inafika mpaka nchi nyingine hivyo tutaongeza mapato na kuondoa umaskini wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie kuhusu kuboresha Shirika la Posta na *TTCL*. Watu wa Posta najua wanafanya kazi kwa juhudi sana, amezungumza mwenzangu hapa, kwa hiyo tuongeze mishahara yao. Vilevile *TTL* kuhusu mambo ya mtandao, wananchi wanapenda mitandao ya kuzungumza baina yao, basi tuwaongeze nguvu *TTCL* waweze kuongeza huduma hii kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naipongeza Serikali yangu, nampongeza Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Magufuli, nampongeza Rais wa Zanzibar, tuwe pamoja na tuongeze mambo mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na Tanzania. Kwa hayo machache, naipongeza nchi yetu na Tanzania yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marwa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuchagua siku ya leo ukizingatia na mimi ni mjumbe wa Kamati wa Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa moyo wake wa dhati wa kujali Watanzania lakini pia wanyonge kwa kukubali kwa kutoa shilingi trilioni 15 kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Kipekee niishukuru sana Kamati yangu ya Miundombinu ikiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Kakoso na Naibu wake ambaye sasa hivi ni Meneja, kwa kufanya kazi nzuri sana ya kutuongoza na kutupitisha katika mambo mbalimbali kwa kushirikiana na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli narudia tena kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Magufuli na kumpongeza sana sana. Kwa mtu kama mimi ambaye nimekuwa Mbunge kipindi cha kwanza kwa kutokea moja kwa moja kule Nyachalakenye tena nilikuwa muuza dagaa lakini sasa na mimi naweza kutunga sheria, kwa kweli ni jambo la kumshukuru Mungu na kumpongeza Rais wetu anaonyesha ni jinsi gani anavyofanya kazi na kuwakwamua Watanzania. Nami sasa ni msomi kati ya wasomi na nipo vizuri kwa sababu tulipoanza tu Kamati alitutumia wanasheria wakatufundisha, wakatupika tukaiva tukawa vizuri na sasa tunaweza kutunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kupitia Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa mafaniko makubwa, tukianza na mafanikio upande wa barabara na madaraja. Kwa upande wa barabara sasa Tanzania nzima barabara zinatengenezwa tena kwa kiwango cha lami; ni barabara ambazo zinapitika vizuri na zinasaidia kuunganisha sehemu moja na nyingine hata kufikia vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha nyuma kwetu kule Mara ilikuwa ukitoka Musoma kufika Dodoma ni lazima utumie zaidi ya siku tatu lakini ukifika pale Singida kulikuwa kuna watu wanawaimbisha watu mtaji wa maskini sasa hivi naamini kuna barabara ya lami na hawawezi tena kufanya matukio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa madaraja kwa kweli Serikali imefanya kazi nzuri sana hata kama wale jirani zetu hawaoni wanasema mwenye macho haambiwi tazama basi Watanzania wapiga kura wanaona kwamba ni kazi kubwa sana imefanyika. Mfano ni kule kwetu Mkoa wa Mara kuna lile daraja na Mto Mara ambalo linaunganisha Tarime na Serengeti. Kwa kweli ilikuwa siyo sehemu nzuri na imeua sana watu lakini pia ilikuwa ni sehemu ambayo ulikuwa huwezi kupita mpaka uzunguke, hata uchumi ulikuwa huwezi kukua kutokana na kutumia muda mrefu barabarani kwa ajili ya kuzunguka kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Sasa hivi barabara ile imeunganishwa kutokana na lile daraja na limetengenezwa na wazawa tena wazawa wazalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba sana ndugu zangu Watanzania na haswa wale mnaofanya shughuli kama hizo muwe wazalendo kama wale waliotengeneza Daraja na Mto Mara tutafika mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niishukuru sana na kuipongeza tena Kamati yangu ya Miundombinu kwa kazi nzuri tuliyoifanya. Tumeweza kuzunguka karibu mikoa yote ya Tanzania, tulizunguka mwezi mzima tukiwa tunafanya kazi za kuangalia minara simu, madaraja, barabara na ubora wake na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiwa tunazunguka

...

(Hapa kengele lililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha?

MWENYEKITI: Ndiyo maana yake, unga mkono hoja.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mollel ajiandae Kanali Masoud.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema ili Taifa lolote liweze kuendelea linahitaji viti viwili vya msingi. Taifa linahitaji uchumi shirikishi na siasa shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na uchumi shirikishi. Ili uweze kuwa na uchumi shirikishi katika nchi ni lazima kuwepo na motisha ya kufanya watu wako waweze kuwa wanatafakari kwa kina na kuwa wabunifu wazuri na kutengeza mifumo ambayo itakujenga uchumi wa nchi yao. Nitolee mfano wa *Bill Gates* wa Marekani ameweza kukaa chini na kugundua na kutengeneza fursa za kiuchumi kwenye eneo la *computer* na huko akawa tajiri na akatengeza uchumi wake na akatengeza ajira. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi ambao siyo shirikishi ni ule uchumi ambapo anatokea fisadi mmoja mwenye fedha zake, anakamata nchi, anaenda kwenye eneo moja tuseme la mawasiliano, anakamata zile fursa, anazuia watu wengine kuingia kwenye hizo fursa anakuwa tajiri peke yake na anakamata mpaka lkulu. Mojawapo ya uchumi usio shirikishi ni uchumi ambao mtu anaweza akaja akachukua ardhi ya Tanzania, akachukua hati, akaenda akakopa fedha na asiendeleze, akawazuia Watanzania kutumia ile ardhi na hakuna kitu chochote ambacho Watanzania wanakipata. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana utasikia wenzangu wa upande wa pili wanalalamika sana ambao wameshindwa hata kutumia milioni 400, sielewi kwa nini tunahangaika na watu kama hao kusikiliza ushauri wao. Ndiyo maana Mheshimiwa Lema leo kwa mara ya kwanza pamoja na kujua migogoro ya ardhi iliyopo kwenye Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha amesimama hapa anapinga watu kunyang'anywa ardhi na Wizara ya Ardhi. Anakataa kwa sababu anajua kwamba wanaotaka kumpeleka Hai kwenda kugombea Ubunge ni hao mafisadi ambao tayari Kilimanjaro wamepandishwa kama wahujumu uchumi. Hicho ndicho kinamfanya Mheshimiwa Lema leo aweweseke...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema nimeshazuia taarifa, nitakupa baadaye.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Ajenge hoja, zuia matusi Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Sasa unabishana na Kiti Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Zuia matusi Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Dkt. Mollel wewe ni Daktari tunategemea utatoa mchango kwa kutumia lugha ya Kibunge.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Lema aliwatukana hapa Mawaziri.

MWENYEKITI: Wewe Jacqueline Msongozi kaa kimya. Endelea Mheshimwa Mollel. *(Makofi)*

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusheshimu sana lakini tunajua kuna watu wanafadhiliwa kuingia kwenye siasa na watu wachafu na ndiyo tunawadhibiti. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kama ulivyonunuliwa wewe.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la siasa shirikishi ni kama kazi ambayo nchi yetu leo imefanya kuwa na Muswada ambao utafanya leo mwanamke wa Tanzania hii ijulikane ni mfumo gani utamfanya afike hapa Bungeni na siyo aletwe kutoka mfukoni mwa watu wachache. Leo tumepitisha Muswada ambao utafanya rasilimali za vyama vyetu, tuna vyama ambavyo akigombana Mwenyekiti na watu wengine hatujui mwisho wa siku mali ziko wapi. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Oooooooooo.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ndiyo siasa shirikishi tunazosema. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda
wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa
Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Ahsante muda wako umekwisha.
Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kanali Masoud.

MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS: Mheshimiwa
Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa dakika
hizi chache niweze kuchangia machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa na safari ya
maendeleo au yako binafsi na ukajiwekea malengo,
ukichelewa kufika kwenye malengo uliyokusudia hutakiwi kwa
mtu mwenye busara kutoa lawama, kutoa ukali au kukaripia
watu. Mtu mwenye busara atakaa kitako kufikiria kitu gani
kilimkwamisha asifikie yale malengo aliyojipangia na
baadaye kutatua ili safari yake atakapoianza tena aweze
kufika alikokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano,
imejikita kabisa katika kuleta maendeleo ya viwanda ili
kwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa, lakini
safari hii kila taasisi imekabidhiwa jukumu lake. Kidogo
nitaizungumzia *SIDO* ambayo kwa hakika nimeiona kwa
macho yangu na kuwasikia watendaji wa sehemu hii
wakizungumza mashaka na matatizo yanayowakumba. *SIDO*
imepewa majukumu ya kukuza wajasiriamali, kutoa elimu,
kutoa ushauri na mambo mengine kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yote
waliyopewa, jukumu kubwa ni elimu inayotakiwa iwafikie
wajasiriamali ili waweze kuzalisha kwa tija. Uwezo walionao
SIDO hivi sasa hauwezi kabisa ukafanikisha malengo haya
waliyopewa, hivyo niombe sana Serikali katika jambo hili
wawaangalie wenzetu wa *SIDO* kuwawezesha kwanza

wapate nyenzo zitakazowasaidia lakini pia fedha ya kutosha itakayowafikisha walipokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la viwanda vilivyobinafsishwa, limezungumzwa sana hapa na sisi katika kamati tumelizungumza sana hili. Nafikiri bado hatujawa *serious* katika hili, wapo watu wamepewa viwanda na hiki ni kipindi kirefu karibu miaka ishirini na, wamepewa mikataba hawajaitekeleza bado tunawaangalia tu, niombe Serikali muda umefika sasa waliopeva viwanda wakavichukulia mikopo, waliopeva viwanda wakauza mashine sasa ni wakati wao wa kuanza kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tumelijadili kidogo katika Kamati ni mkakati wa Serikali wa kuhakikisha sasa mafuta ya kula yanazalishwa nchini. Mikakati hi tumeiona kwa maandishi na ina lengo zuri, lakini mote nilimosoma, labda sikusoma vizuri, lakini mote nilimosoma sikuuona mkakati wowote ule ambao unazungumzia wazalishaji wa alizeti hapa nchini. Mkakati unazungumzia viwanda lakini haujalenga malengo gani yatafanywa, kipi kitafanywa, watasaidiwa nini wazalishaji ili zao hili lilimwe kwa wingi na viwanda vyetu vipate malighafi ya kutosha itakayowawezesha sasa kufikia lengo tullilolikusudia la Taifa la kuchakata mafuta hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nimekusudia kulizungumza kidogo, ni wafanyabiashara wa viwanda wanaosafirisha bidhaa zao hapa nchini kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru wenzetu wa *TFDA* kwa mashirikiano mazuri wanayoyafanya kati yao na wenzao wa *ZFDA*. Bado nataka kuzungumzia tatizo linalojitokeza hasa kwa kiwanda chetu kimoja kule Zanzibar ambacho kinafungasha kahawa, chai, sukari kwa ajili ya Mashirika ya Ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaposafirisha mizigo kuja nayo Tanzania Bara wanapofika bandarini, *custom* wanasema hiyo *ZFDA* hawaifahamu, lakini mashirikiano kati ya *ZFDA* na *TFDA*, ni mazuri. Wanachofanyiwa hawa sasa

wanatakiwa baada ya kufika na bidhaa bandarini waende *TFDA* wakachukue barua ya kuwatambua, wakishachukua barua wapeleke bandarini, baada ya kutoka bandarini ndio wanakwenda kufanya shughuli nyingine za kuhakikisha mzigo ule unafikishwa unakokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la kushangaza zaidi watu hao hao kiwanda hicho hicho bidhaa hiyo hiyo, watakapopeleka tena mara ya pili wanatakiwa tena waende *TFDA* wakachukue barua ya uhakiki wa kuhakikisha kwamba hii *ZFDA* inatambuliwa. Niiombe sana Serikali katika jambo hili tuondoshe vikwazo hivi ili wenzetu wanaosafirisha bidhaa kutoka Tanzania Visiwani wanapozileta Tanzania Bara kusiwe na vikwazo vya kuwasumbua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango mzuri. Sasa Waheshimiwa tunaingia upande wa Mawaziri, tunaanza na Mheshimiwa Mgumba, dakika tano; Mheshimiwa Kamwelwe; dakika 10; Mheshimiwa Makamba; dakika 10; Mheshimiwa Kakunda; dakika 10; Mheshimiwa Kairuki; dakika 10; na Mheshimiwa Dkt. Mpango, dakika 10. Mheshimiwa Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili kutoa mchango kwenye hoja iliyokuwepo mbele yetu. Kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote waliopata nafasi ambao wametoa mchango wao na sisi kwa niaba ya Wizara ya Kilimo kuna hoja chache zimetugusa, mawazo yote waliyoyotoa tunayachukua na tunaendelea kuyafanyia kazi ili kuboresha biashara hii, sekta ya kilimo iende vizuri. Kuna hoja ziko kama tatu au nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ni hoja ya kurasimisha mfumo wa kangomba kwenye korosho. Kuna wengine Waheshimiwa Wabunge wamefananisha kilimo cha

mkataba na biashara ya kangomba. Biashara ya kangomba imekataliwa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi Ghalani, Sheria Na. 10 ya mwaka 2005; Sheria Tasnia ya Korosho Na.18 ya Mwaka 2009 na kanuni zake za Mwaka 2010, mwongozo Na. 13 wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani wa mwaka 2018, lakini pia na Sheria ya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013, zote hizo zimevipa mamlaka Vyama vya Msingi vya Ushirika na vyama vya Vikuu ndio wenye jukumu la kukusanya korosho kutoka kwa wakulima na kuzifikisha kwenye maghala ya masoko yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sheria hizo nilizotitaja, hayupo yeyote mwingine anayeruhusiwa kununua au kukusanya korosho kutoka kwa wakulima isipokuwa wakulima wenyewe kupitia vyama vyao vya msingi na ushirika, hivi ni kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge au Wabunge wanaona sasa sheria hizi zimepitwa na wakati hazina manufaa labda kwa Taifa au kwa wakulima, basi kwa mujibu wa kanuni zetu, Kanuni ya 81 ya Toleo la Januari, 2016, inaruhusu Mbunge kuleta hapa hoja binafsi, ailete hapa, basi itachakatwa, ikionekana inafaa itapitishwa, lakini sisi kama Serikali kazi yetu kubwa ni kusimamia utekelezaji wa sheria kwa sababu sheria hii ilipitishwa na Bunge lako Tukufu hapa, tutaendelea kuisimamia ili sheria hii iendelee kutekelezwa. Mpaka sasa mfumo unaotambulika kisheria na kikanuni na kimwongozo ni mfumo wa stakabadhi ghalani na korosho zote zitaendelea kukusanywa na vyama vyetu vya ushirika na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja nyingine imetolewa kuhusu kuna kesi ngapi ambazo zipo mahakamani au polisi. Labda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kesi zipo za kutosha na ushahidi upo na zipo ngazi mbalimbali, kuna kesi zipo ngazi ya polisi zingine ziko mahakamani. Kwa mfano, wiki moja iliyopita nimetoka Newala na nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Newala, walikuwa na kesi zaidi ya 47 na mojawapo ni korosho, mtu walipomkamata na tani 10 anasema korosho zile

zimetoka Malinyi Morogoro, unaona namna gani kwamba udanganyifu upo na maana yake ametoka Morogoro amepita Pwani, amepita Lindi mpaka Mtwara na kufika Newala na Newala kwenyewe sio mjini kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizo kesi zipo na kama Mheshimiwa Mbunge bado ana nia ya kutaka takwimu sahihi kwa sababu ni suala la kitakwimu, tutampatia baada ya Bunge hili atuone afike pale Wizara tutampatia takwimu kesi ngapi na ziko mahali gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja imetolewa hapa kusema turuhusu uagizaji wa korosho kutoka Mozambique. Hilo haliwezekani kwa mujibu wa sheria kwa sababu korosho za Mozambique *grade* yao iko chini...

MWENYEKITI: Malizia.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):... zikija hapa zitatuharibia ubora wa korosho zetu na soko bei yake itapungua, hatuwezi kufanya hilo lazima tuwalinde wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kamwelwe, jiandae Mheshimiwa Makamba.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni yangu katika mawasilisho ya Kamati za Kudumu za Bunge zote mbili. Nianze kwa kuwashukuru Wenyeviti na Kamati zao kwa kufanya kazi nzuri na hasa Kamati yangu ya Bunge ya Kudumu ya Miundombinu kwa jinsi ambavyo imeonesha weledi mkubwa sana kwenye Wizara yangu. Maeneo mengi sasa wanayafahamu vizuri na imekuwa ni bahati tu kwa sababu ajira yangu yote ilikuwa kule ndio maana naweza nikaenda nao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru sana kwa michango yao ambayo ni michango ya kujenga. Wamezungumza vizuri sana na kila wakati wananipa maoni na hayo maoni Serikali inayafanyia kazi. Kwa hiyo, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge, imeshauri katika maeneo mbalimbali, wameelekeza kwamba fedha za miradi ya maendeleo zitolewe kwa haraka. Nitoe taarifa kwamba nimshukuru sana Waziri wa Fedha hata mwezi wa 12 alitoa shilingi bilioni 200 na tumelipa tayari kwa ajili ya miradi ya barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusiana na bandari, kwa sababu bandari ndio lango kuu la uchumi katika nchi yetu. Waheshimiwa Wabunge wamependekeza kwamba asilimia 40 ya makusanyo ya bandari, basi yabakie kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bandari. Baada ya tamko hilo niliwasiliana na Waziri wa Fedha lakini kwa mujibu wa sheria kwa sasa, hela zote za *retention*, hiyo Sheria ya *Retention* imeshafutwa ili ziweze kubakizwa kwenye taasisi za Serikali. Kwa hiyo hela yote inakusanywa na kupelekwa Hazina, lakini sisi tutaomba na kwa sababu bandari, inakarabatiwa sasa hivi kwa kuongeza kina, tunajenga magati nane kutoka sifuri mpaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule tayari tumeshakamilisha gati namba moja na ndio lenye kina kirefu lina mita 15 kwenye *low tide*, kwa hiyo meli kubwa inaweza ikakaa pale na sasa hivi tunaendelea na *study* kwa ajili ya kuongeza pia kina cha ule mlango wa kuingilia meli kubwa. Kazi inaendelea vizuri na kwa kusimamiwa pia pamoja na hii Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ununuzi wa *flow meter* ili tuwe na *flow meter* zenye uhakika na mpango wetu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na maeneo matatu ya *flow meter*. Kwa sababu wakati mwingine tunakuwa na meli zaidi ya sita za mafuta, sasa zikichelewa sana zinasababisha gharama kwa watumiaji.

Kwa hiyo, tayari Serikali mwaka ujao wa fedha *study* zimeshafanyika, tutaomba fedha ili tuweze kuongeza *flow meter*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge imezungumzia kuongeza gati namba 13 na namba 14, tayari tumeshafanya mazungumzo na Benki ya Dunia baada ya kukamilisha huu mradi unaoendelea unaojenga magati nane, tutakwenda tena tukaongeze hayo magati namba 13 na namba 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango ya wabunge wamechangia kuhusiana na hii sheria mpya, Sheria mpya ya Kudhibiti Uzito wa Magari ambayo ni ya *East Africa*. Chanzo cha sheria hii ni usikivu wa Serikali, lakini pia ni usikivu wa Serikali kutoka kwenye Bunge na Wabunge walikuwa na haki kwa sababu miradi mingi tulikuwa tunatekeleza, lakini baada ya muda mfupi, barabara zinaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maoni ya bunge lako Tukufu, Serikali ilii-*engage consultant*, ilitoa fedha, wakafanya *study*, ile *study* ndio iliyotuelekeza kwamba haya magari ya *super single* ndio yanayoongoza kuharibu barabara, kwa nini? Kwa sababu wanatumia *size* ya matairi ambayo ni 385/85 lakini kama *size* ya matairi itakwenda kwenye 465/67, basi hiyo *effect* haiwezi kuwepo. Sasa kwa sababu tayari tunayo sharia, niwaombe tu wasafirishaji waendeleo kutumia sheria hiyo, lakini kama itabidi, itabidi tena tuite *consultant* ili tuweze kufanya *study* nyingine kwa ajili ya kuboresha. Serikali ni wasikivu na bandari haiwezi kufanya kazi bila reli, lakini bandari haiwezi kufanya kazi bila barabara pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wametoa mfano mzigo wa Zambia, ni kweli kabisa Zambia wana mzigo wa tani zaidi ya milioni 10 wanasafirisha kwa mwaka. Hata hivyo, mzigo unaopitia bandari ya Dar es Salaam ni tani milioni 2.2, ni malengo yetu sisi kwamba tuweze kuchukua mzigo mkubwa zaidi. Ndio maana nishukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia pia reli ya

TAZARA, reli ile inatakiwa kubeba tani milioni tano kwa mwaka, lakini sasa hivi inabeba chini ya tani laki tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali ilitoa shilingi bilioni 10 tunakarabati vichwa saba ambavyo vitakamilika kabla ya mwezi wa Saba ili tuendeleo kuongeza sasa uwezo wa ile reli kubeba mzigo zaidi. Malengo yetu kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge kwenye Kamati ya Miundombinu, tutakaa pamoja na wenzetu wa Zambia, kwa sababu reli ile tunaichangia mali kwa asilimia 50 kwa 50. Tutakaa nao ili tuweze kuboresha zile sheria za zamani, tuboresha ili sasa tuweze kuona ni namna gani kwamba tuta-improve matumizi ya ile reli ili iweze kutumika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulikaa tumekodisha kampuni moja ya wa *South Africa* ambayo inaitwa *Calabash*. *Calabash* ni kampuni ya wastaafu waliokuwa wanafanya kazi kwenye reli ya *South Africa* kule. Baada ya kustaafu wamenunua vichwa na mabehewa kwa hiyo tumewakodisha ndio wanaobeba mzigo kupitia ile reli, tunawalipa kwa kila *trip*, kila trip moja wanalipa milioni 20 na bado nafasi hiyo ipo hata Watanzania wengine wanaweza wakafanya hivyo na *Calabash* wameongeza uwezo wa kubeba mzigo, wanabeba tani 150,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi ya kuzungumza, lakini nikushukuru kwa kunipa hii nafasi na niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makamba, jiandae Mheshimiwa Kakunda.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, taarifa ya Kamati. Nianze kwa kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri ambayo imeifanya na kwa taarifa nzuri ambayo imeitoa. Pia nishukuru Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe kwa ushirikiano

mzuri ambao wamekuwa wanatuonesha, kwa msaada ushauri na maelekezo mbalimbali, ambayo wamekuwa wanatupatia, kwa hiyo nampongeza sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Sadiq Murad pamoja na Kamati yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunayapokea Maazimio yote ya Kamati yanayohusu mazingira kama yalivyoandikwa kwenye ripoti ya Kamati, ambayo yapo ukurasa wa 81 na 82 ambayo yanahusu mazingira. Ni maazimio mazuri na hatuna mabadiliko yoyote katika hayo maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie mambo mawili matatu tu yaliyojitokeza kwenye taarifa ya Kamati ambayo labda yanahitaji maelezo kidogo. La kwanza lipo kwenye ukurasa wa 57 ambapo Kamati imesema, kuwa kutegemea gesi ya *LPG* kama nishati mbadala ni kuwaumiza Watanzania kwa kuwa bei ya nishati hii ni kubwa na inaendelea kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka hili jambo likae sahihi kwenye kumbukumbu za Bunge na Wabunge kwa ujumla, kwamba ukiangalia takwimu za matumizi ya nishati hapa nchini, nishati ya *LPG* ni moja ya nishati ambazo bei yake inashuka kila mwaka. Mtungi wa kilo tano, kilo sita mwaka uliopita ulikuwa Sh.21,000, sasa hivi ni Sh.17,000. Mtungi wa lita 15 ulikuwa Sh.55,000, sasa hivi Sh.45,000 na tunaona *trend* kwamba uwekezaji na usambazaji kwenye *LPG* unaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sekta ambazo hazithaminiwi kwa ukuaji mkubwa lakini zinakuwa kwa kasi ni hii ya nishati ya *LPG*. Kwa hiyo, nataka tu ieleweke wazi kama sisi kama Serikali tunaunga mkono wawekezaji katika tasnia hii na tunaamini kwamba sisi na wenzetu wa

Wizara ya Nishati ambao wanahusika na udhibiti tutachukua hatua za kiseru kuhakikisha kwamba tunailea tasnia hii ili ikue na Watanzania wapate nishati hii ya *LPG* ya

gesi ya mitungi kwa bei nafuu na mahali popote walipo.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani jambo la msingi kujua kwamba, nchi yetu bado kwa sehemu kubwa inategemea rasilimali asili kwa maendeleo yake, kwa shughuli za kilimo, shughuli za ufugaji na nyinginezo. Kwa hiyo, uhifadhi wa mazingira katika haya maeneo una nafasi kubwa zaidi ya kuisaidia nchi yetu. Napenda Bunge lichukue uongozi kama ambavyo Kamati imechukua uongozi katika kuhakikisha kwamba masuala ya mazingira yanatiliwa maanani sana katika mipango yetu ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaongea hapa na Naibu Waziri wangu, tunahesabu Wabunge waliochangia hii Kamati ni wangapi wamegusa masuala ya mazingira, ni Wabunge watatu tu. Tunajua kwa sababu ya umuhimu wa masuala ya viwanda na biashara, lakini nataka niseme bila hifadhi ya mazingira hakuna viwanda na biashara. Tunataka tuseme kwamba Tanzania, Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane tafadhali! Tanzania ni moja ya nchi tano zinazoongoza duniani kwa kukata misitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku inayoenda kwa Mungu kila dakika, kila siku, tunakata misitu kwa kiwango cha kiwanja cha mpira, kila dakika, kila siku; kila dakika inayopita hapa Tanzania, misitu inayofyekwa ni *size* ya kiwanja cha mpira wa miguu. Hizi takwimu zimeanza kuchukuliwa mwaka 2010. Kwa hiyo, fikiria kwa miaka tisa mfululizo kila dakika unakata *size* ya kiwanja cha mpira wa miguu, asilimia 61 ya nchi yetu inakaribia kuwa jangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kwa uchumi ya *land degradation, forest degradation* ni takriban shilingi bilioni 2.2 *dollar* kwa mwaka kwenye uchumi au asilimia ya *GDP*. Kwa hiyo, hatua hizi zote tunazochukua za kuisukuma mbele nchi yetu kimaendeleo, kama hatutahifadhi mazingira zitakuwa ni za bure, kabisa. Kama hatutachukua hatua madhubuti za kuhifadhi mazingira, kilimo, uvuvi, ufugaji itakuwa ni bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi kuna mbinu mpya ya kupima utajiri wa nchi na utajiri wa watu, inaitwa *natural per capita natural resource capital*, yaani maliasili hizi za nchi nzima zinathaminiwa na kila Mtanzania anapewa kwa *per capita*, thamani yake. Kwa miaka 20 iliyopita utajiri wa maliasili wa kila Mtanzania umeshuka kwa asilimia 35. Kwa hiyo hizi *physical asset* zinaongezeka, lakini *natural capital*, utajiri wa maliasili wa kila Mtanzania unapungua kwa asilimia 35 katika kipindi cha miaka 20 iliyopita. Kwa hiyo, kwa sababu idadi yetu inazidi kuongezeka kwa kasi, hili jambo ni la muhimu na la kulitazama. Kwa hiyo, ningependa Bunge lako lichukue uongozi kwenye eneo hili la hifadhi ya mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo limezungumzwa hapa ni lile suala la mita 60 na athari zake kwa shughuli za watu na maelekezo ya Mheshimiwa Rais yaliyotoka ya kutazama sheria hizo ili kuweza kuruhusu watu wafanye kazi. Ni dhahiri kabisa kwamba Watanzania wengi wanategemea maeneo chepechepe, mbogamboga nyingi tunazokula mijini michicha, *cabbage* na nini vinazalishwa kwenye maeneo haya na maeneo haya pia yanatoa; ukienda kule kwa ndugu zangu, kule kwetu kwa Bwana Shangazi tunaita vitivo, ukienda kule kwa ndugu zangu kwa akina Mwamakamba kule unyalukolo wanaita vinyungu na kadhalika. Kwa hiyo tunaelewa kwamba kuna baadhi ya Watanzania wanategemea haya maeneo ya chepechepe kwa ajili ya maisha yao na Serikali za Mitaa zinapata kodi humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tayari Wizara sita tutakaa na kuangalia namna gani tunaweza kuhakikisha kwamba ruhusa inatolewa huku hifadhi ya mazingira ikizingatiwa. Moja ya nyenzo tulizonazo ni Kifungu cha 57 cha Sheria ya Mazingira, kinasema kwamba:

“Kwa kuzingatia Kifungu cha (2) ndani ya mita sitini hakutafanyika shughuli yoyote ya binadamu ya kudumu au ambayo kwa asili yake inaweza kuharibu mazingira...”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sheria imepiga marufuku shughuli ndani ya mita sitini. Kifungu hicho hicho cha 57(2) kinasema: Waziri, kwa maana ya Waziri mwenye dhamana ya mazingira, anaweza kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo hayo yaliyoelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo nililolisema awali, sheria yenyewe imeweka uwezekano wa Serikali kuruhusu shughuli kufanyika kwa masharti maalum. Kwa hiyo, sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais na kwa mamlaka niliyopewa kama Waziri mwenye dhamana ya Mazingira, tutaweka miongozo ya kuendesha shughuli za kibinadamu katika haya maeneo; miongozi ambayo itazingatia hifadhi ya mazingira, lakini pia upatikanaji wa riziki za watu. Kwa hiyo tutaweka namna ambayo kwa mfano aina ya mazao unayoweza kulima, ukaribu na kwenye kingo, matumizi ya mbolea za kemikali, ruhusa ya kutoingiza udongo kwenye mto na kadhalika. Miongozo hii itakuwa *technical* na itatumika kuzuia jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili jambo linawezekana kufanyika, hakuna *contradiction* hapo kwa sababu sheria yenyewe imetoa ruhusa hiyo na tutaitumia sheria hii kuhakikisha kwamba azma ya Kiongozi wetu inatimia, lakini azma vilevile ya hifadhi ya mazingira inatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kakunda, jiandae Mheshimiwa Kairuki, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mpango.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makuzi yangu nimefundishwa lugha ya staha, uvumilivu na heshima kwa wakubwa na wadogo. Namwomba Mungu azidi kunidumisha katika hulka njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hii nazipongeza sana Kamati zote, ikiwemo Kamati yetu ya Biashara na Mazingira, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Wametoa

maoni na ushauri mzuri na sasa sisi Serikali kazi yetu kubwa ni kuyachukua maoni na ushauri na kuufanyia kazi kwa manufaa ya Watanzania ambao wametutuma wote tuje kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojadili hoja humu Bungeni ni muhimu sana tukazingatia mambo muhimu ya msingi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Julai, 2017 Bunge hili lilipitisha sheria mbili kubwa, Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umilikiwa Maliasili ya Mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio ya Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Kwenye Mikataba Inayohusu Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kipindi hicho hicho Bunge lilifanyia marekebisho makubwa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Lengo la hatua hizo lilikuwa ni kurejesha umiliki na udhibiti wa rasilimali zetu za Taifa kwa faida ya Watanzania walio wengi. Huo ndio msingi tulioutumia kufanya maamuzi ya kuifanyia mapitio ya kina baadhi ya mikataba, ikiwemo Mkataba wa Mradi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka na Mkataba wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga na miradi mingine ya aina hiyo. Tutakapokamilisha mapitio hayo tutatoa taarifa kwa Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ufafanuzi kuhusu eneo la biashara. Tunao mfumo uliopitishwa na Serikali wa kujenga mazingira rafiki ya kufanya biashara na katika maeneo kadhaa tumeanza kufanya utekelezaji hususani kwa mfano kwenye eneo la ushirikiano kati *TFDA* na *TBS*, hii ni mifano michache. Tunakamilisha mpango kazi utakaoanza rasmi utekelezaji wake 2019/2020 na kwa kufanya hivyo, tutapunguza sana gharama za ufanyaji wa biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Mheshimiwa S. H. Amon wa kukutana na wafanyabiashara au waagizaji wa bidhaa kutoka nje, tumeuchukua na tutaufanyia kazi mimi na Mheshimiwa Mpango, Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipozungumzwa kuhusu uhasi wa *balance of payments*, nilisikitika kwa sababu ilihitajika sana uchambuzi wa kina. Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwezi Julai, 2018 imeonesha Tanzania imeuza zaidi katika soko la *SADC* na mauzo yameongezeka kutoka *dollar* milioni 397 mwaka 2017 hadi *dollar* 413 milioni ambayo ni ongezeko la asilimia 12; na wakati huohuo tumepunguza uagizaji kutoka *SADC* kwa asilimia 12. Maana yake ni kwamba tumepata mafanikio chanya kwenye soko la *SADC*. Sasa hizi hatua bado tunazingeza kwenye masoko mengine. Dalili hiyo inaonesha kwamba Viwanda vya Tanzania vimeanza kufanya vizuri zaidi ukilinganisha na viwanda vya nchi nyingine hasa katika bidhaa kama unga wa ngano, sabuni, saruji, mabati na bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Menyekiti, aidha, hatua ambazo Serikali inaendelea kuzichukua hususani katika ujenzi wa reli, barabara za lami za kitaifa na mikoa, viwanja vya ndege, bandari, umeme, mawasiliano ya simu, maji, huduma za afya, elimu hususani wahitimu wenye ujuzi mbalimbali (*skills*) ambao watakuwa na michango mikubwa kwenye viwanda, ni hatua ambazo zitaboresha sana mwelekeo wetu kuelekea kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kuhusu kuimarisha utendaji wa mashirika yetu kama *SIDO*, *NDC*, *TEMDO*, *CAMARTEC*, *TIRDO*, *EPZA*, *TAN-TRADE*, *TBS* na hata Wizara yetu ya Viwanda na Biashara, tutaufanyia kazi ushauri mzuri ambao Bunge limeutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, tunahamasisha viwanda na hata Waheshimiwa Wabunge tunawahamasisha wamiliki viwanda. Tumeweke vipaumbele vitatu muhimu; kipaumbele cha kwanza, ni viwanda vya kusindika au kuchakata mazao ya kilimo na mifugo; sekta ambazo zinategemewa na asilimia zaidi ya 75 ya Watanzania. Kipaumbele cha pili, ni viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika zaidi majumbani na kwenye sekta ya

ujenzi ili kulihudumia vizuri zaidi soko la ndani; na kipaumbele cha tatu, ni viwanda vinavyoajiri watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana tushirikiane kwa pamoja, sisi wote ni Watanzania, tukianza kutoleana maneno machafu hatutasonga mbele. Tushirikiane kama Watanzania kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania ili Taifa letu liweze kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa. Kati ya viwanda 156 vilivyobinafsishwa, viwanda 88 vinafanya kazi, sawa na asilimia 56, viwanda 68 havifanyi kazi. Kati ya viwanda 88 vinavyofanya kazi viwanda 64 vinafanya kazi vizuri, tena kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuonesha kwamba vinafanya kazi kwa faida kuanzia mwaka 2013 mpaka 2018 viwanda hivi hadi Oktoba, 2018 vimelipa kodi zaidi ya shilingi trilioni 4.6 *TRA* wanayo takwimu. Kati ya viwanda 64 visivyofanya kazi viwanda 20 vimefutwa kwenye orodha baada ya kubainika kwamba vililuzwa kwa rejareja; yaani vililuzwa mali mojamoja na vingine vimekosa sifa ya kuendelea kuitwa viwanda. Viwanda 14 tumeshavirejesha Serikalini baada ya wenye viwanda kutoonesha *business plan* ya kuvifufua na kviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumevichukua Serikalini ili tuvitafutie wawekezaji wengine ambao watakuwa na nia ya kuwekeza mtaji ambao utavifufua viwanda hivyo na kuendelea na uzalishaji. Viwanda 34 vinafuatiliwa kwa karibu utendaji wake kwa mujibu wa ahadi zao za kufufua uzalishaji ambazo wametuahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *General Tyre*; Serikali ilikamilisha tathmini ya kiwanda iliyoshauri kiwanda hicho cha *General Tyre* kifufuliwe kwa ubia na sekta binafsi kwa uwekezaji wa mitambo ya kisasa. *Government Notice* ya tarehe 11 Mei, 2018 ilikabidhiwa *NDC* na kiwanda rasmi kilikabidhiwa *NDC* tarehe 20 Disemba, 2018. Baada ya

tathmini ya kina ya mali zote na madeni ambayo inaendelea NDC sasa itachukua hatua ya mwisho ambayo ni kualika makampuni yatahayokuwa tayari kwa ubia ili yalete maombi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Bunge lako Tukufu tuwe na subira wakati hatua muafaka hizi zinachukuliwa na hakuna haja ya kutoleana maneno ambayo yatafukuza hata wale ambao pengine wangeweza kuwa *prospective* kwenye uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mwelekeo mzuri kwa sekta zote. Sekta ya viwanda haiwezi kuendelea bila kuwa na uwekezaji kwenye sekta nyingine, huwezi kujenga viwanda bila kuwekeza kwenye sekta ya miundombinu. Hakuna eneo lolote la uwekezaji ambalo linaweza likavutia wawekezaji kama hakuna barabara inayofika kule, hakuna reli inayofika kule, hakuna umeme, hakuna maji, kwa hiyo hivi vitu vinategemeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuwa na viwanda vya *Agro processing* kama kilimo hakifanyi kazi vizuri; na ndiyo maana katika mkakati maalum wa maendeleo ya viwanda katika nchi hii tumesema lazima uwe na mkakati wa pamba hadi nguo; yaani *C to C (Cotton to Cloth)*. Ili uweze kufikia malengo mahususi ya kutumia malighafi ya pamba vizuri zaidi ndani ya nchi lazima uwe na viwanda ambavyo vitatengeneza nguo kutokana na pamba inayozalishwa ndani ya nchi. Lazima kama unataka kuwa na viwanda vya mafuta;

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Namalizia Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima uwe na uzalishaji mzuri wa alizeti ili uweze kukamua mafuta ya alizeti vizuri. Kwa hayo ndiyo mambo ambayo tunayafanya na mwelekeo ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kairuki, tunamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mpango.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipende tu kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na nipende kipekee kuwapongeza sana Kamati yetu hii ya Bunge kwa ripoti hii nzuri na niwahakikishie tu kwamba nitafanya nao kazi kwa karibu. Niwashukuru kwa mchango wao na ushauri mzuri walioutoa na yote walioyatoa tutayazingatia. Zaidi pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameweza kuchangia hoja hii hususan katika masuala yanayohusu sekta ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipende tu kuanza kwa kuwapa *comfort* Waheshimiwa Wabunge, kwamba katika sekta ya uwekezaji Tanzania tumekuwa tukiendelea kufanya vizuri, hususan katika suala zima la kuvutia wawekezaji. Hata ukiangalia katika ripoti ya *World Investment Report* ya mwaka 2018 ambayo ilitolewa na *UNCTAD* imeonesha pia kwamba Tanzania katika nchi za Afrika Mashariki tumeongeza katika kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka jana tu peke yake takribani *dollar* za Kimarekani bilioni 1.18 zimetufanya tumekuwa wa kwanza tukifuatiwa na Uganda na Kenya imekuwa ni nchi ya tatu. Kwa hiyo nipende tu kusema kwamba ni vyema tusibeze jitihada mbalimbali zinazofanyika, muhimu tu kwamba tuendeleo kushirikiana na kuhakikisha kwamba tunaimarisha uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende sasa kipekee kujibu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Kamati lakini pia na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ilikuwa ni kuhusiana na changamoto mbalimbali katika mazingira ya ufanyaji wa biashara. Ukiangalia kwa kiasi kikubwa katika ripoti ya Kamati yetu ya Bunge, lakini pia Waheshimwa Wabunge wengi wamejikita sana katika masuala mazima ya changamoto zinazojitokeza, utitiri wa kodi, mifumo ya udhibiti, kuwa na *regulatory authorities* nyingi ambapo nyingine unakuta zimekuwa zikikwamisha jitihada mbalimbali.

Nipende tu kusema kwamba tayari kupitia Serikali mwaka 2016, ilifanya utafiti na ikafanya uchambuzi wa kuangalia changamoto mbalimbali na kero ambazo zinajitokeza katika mazingira ya kufanya biashara nchini, lakini pia katika masuala mazima ya uwekezaji. Ndiyo maana ukiangalia mwaka 2018, mwezi Mei Baraza letu la Mawaziri kupitia Serikali liliweza kupitisha *Blue Print* (Mpango) wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara. Vile vile tunayo *Programme* ya Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji na tayari tumeshaanza kuandaa *road map* pamoja na Mpango Kazi Jumuishi (*Comprehensive Action Plan*) ya miaka mitatu ambayo tayari tunashirikiana na *ESRF* katika kuhakikisha kwamba hili linaenda kutekelezwa. Tunaamini wiki ijayo tutaweza kukaa na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mpango kazi huu jumuishi unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kuwatoa hofu tena Kamati kama ambavyo wamekuwa wakitushauri, lakini pia katika maelekezo yao ambavyo wametoa katika taarifa hii, kwamba ni vyema sasa wapate taarifa ya utekelezaji, lakini pia waweze kupata namna ambavyo changamoto hizi zimeweza kutatuliwa. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati yetu kwamba suala hili litakapoendelea kufanyiwa kazi tutawaletea taarifa ya utekelezaji ya mpango wetu huu jumuishi wa kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja nyingine ya sheria za kodi. Kimsingi Kamati imekuwa ikifanya ulinganisho na kodi mbalimbali zinazotowazwa hususan katika kodi za forodha katika nchi zingine za Afrika Mashariki na nyinginezo na kwamba vyema sasa katika utozaji wa kodi tukaangalia mazingira yetu tuliyonayo, lakini pia kuangalia wakati tulionao kwa sasa. Nipende tu kusema kwamba Serikali imekuwa sikivu na ndiyo maana kupitia Wizara ya Fedha tumemsikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameunda Kamati ya Mapitio ya Kodi au *task force* kwenye *reforms* za kodi lakini pia ametoa mpaka tarehe 10 Februari, yeyote ambaye ana mapendekezo kuhusiana na mapitio ya kodi na maboresho basi wanaweza kuwasilisha huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ilikuwa ni kuboresha au kufanya mapitio ya Sera yetu ya Uwekezaji, pamoja na Sheria ya Uwekezaji. Nipende tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hili ni eneo ambalo nitahakikisha katika mwaka huu ujao wa fedha suala hili linakuwa limetekelezwa. Niombe tu ushirikiano tutakapoleta Muswada huu Bungeni, basi tuweze kuupitisha kwa kutambua kwamba utakuwa umeondoa changamoto nyingi. Maana ukiangalia hivi sasa katika Sheria yetu ya Uwekezaji kwa mujibu wa kifungu cha 20, unakuta tunao wawekezaji wa miradi maalum (*strategic investors*), wanavyo pia vivutio mbalimbali vya kodi na vingine visivyo vya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo unakuta upande mmoja vivutio vyao vimetajwa katika Sheria ya Uwekezaji; lakini upande mwingine bado tunazo Sheria zingine za Fedha na Kodi ambazo unakuta zinakwamisha kuweza kuwapatia vivutio kama ambavyo wamepewa mikataba kwa mujibu wa *performance contracts*. Suala hili nalo pia ni eneo ambalo tutalizingatia tutakapofanya mapitio yetu ya Sera ya Uwekezaji pamoja na Sheria yetu ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia ya kuboresha vituo vyetu vya *One Stop Center* au vituo vya kutolea huduma za pamoja. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeendelea kuboresha huduma za *One*

Stop Center na hivi sasa tumeongeza Taasisi nyingine takribani tano na kuongeza *TFDA*, tumeongeza *NIDA*, *NBS*, *NEMC* pamoja na *OSHA* na wenyewe pia sasa hivi wako *under one stop shop* ya *TIC*. Vile vile tunaendelea kuongeza idadi ya Watumishi walioko katika Idara yetu ya Kazi, katika *One Stop Center* ya *TIC*, lakini pia tumeshaunda mfumo wa kielektoniki wa *Tanzania Investment Window* ambao unawasaidia wawekezaji wetu wanaotaka kuchakata au kuwasilisha maombi yao kwa ajili ya kupata cheti cha uwekezaji na maombi ya vibali mbalimbali vya kazi. Kwa hiyo, tunawakaribisha wakati wowote, mifumo hiyo ya kielektoniki ipo lakini pia kwa wale watakaotaka kufanya kwa mifumo (*manual*) huduma hizo pia zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia ni suala zima la upatikanaji wa ardhi. Kumekuwa na changamoto hususan katika kubadilisha ardhi kutoka katika ardhi ya kijiji kwenda kwenye ardhi ya jumla, lakini pia imekuwa ikichukua muda mrefu na wakati mwingine wamesema miaka miwili, mpaka miaka mitatu. Napenda tu kusema kwamba ni maeneo ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi na Wizara ya Ardhi; na kwa kweli wamekuwa wakitupa ushirikiano mkubwa kuhakikisha kwamba kila mara wawekezaji wetu wanapokuja, basi wanaweza kupata ardhi zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la zaidi tu, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia alishatoa maelekezo kwa Halmashauri zetu, kuhakikisha kwamba wanatenga maeneo maalum ya uwekezaji, lakini siyo kutenga tu maeneo. Katika eneo hili naomba sana Halmashauri zetu, tuweze kusikilizana vizuri. Wako ambao wamekuwa wakitenga maeneo ya uwekezaji, lakini uhakiki unapoenda kufanyika, idadi ya ekari zinazotajwa unakuta ni tofauti na idadi ya ekari hizo ambazo wao wamesema wamezitenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi tunataka maeneo maalum ya uwekezaji ambayo tayari yameshalipiwa fidia, hakuna mgogoro wa ardhi, lakini yameshapimwa na yameshaandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia TIC pamoja na EPZA wameendelea kutoa ushirikiano kwa Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba maeneo haya yanatengwa na yanakuwa ni maeneo ambayo yametengwa kwa kufuata Sheria zetu za Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni matamko ya viongozi mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ni eneo ambalo pia Kamati nashukuru na wenyewe wameweza kulizungumzia. Napenda tu kusema kwamba kazi kubwa inafanyika katika kuvutia wawekezaji. Hatuwezi kufikia katika kiwango hicho cha kupata FDI's za zaidi ya bilioni 1.18 ya Dola za Kimarekani kama hatupeani ushikiano; kama Taasisi mbalimbali za uhibititi na mamlaka nyingine zinazohusika katika kuwezesha uwekezaji, hazitoi ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mamlaka za Serikali za Mitaa, tunajua kwamba wao ndio kioo kwetu kule katika Mikoa, Wilaya na Halmashauri zao, basi tujitahidi kuzingatia Sheria na tujitahidi zaidi kuweka mazingira wezeshi ili kuweza kuwavutia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda ilishaandaa mwongozo wa namna ya kujenga uchumi wa viwanda, nasi pia kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, tutakaa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia ...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, malizia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI WA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:
...kuhakikisha kwamba tunatoa mwongozo wa kuona namna gani Mamlaka za Serikali za Mitaa kweli zitaweza kuchukua nafasi yao kule waliko katika kuwezesha uchumi lakini zaidi kuhakikisha kwamba tunavutia uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi, lakini kwa sasa napenda tu kusema kwamba tutakuja kueleza mengi kadiri siku zinavyozidi kuendelea. Zaidi, naomba sana ushirikiano na Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kupata *brief profile* za maeneo yenu ya uwekezaji ili tuweze kuvutia uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mpango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami nichangie hoja hizi zilizoko mbele yetu na hasa kwa kuzingatia kwamba mimi ni mdau wa kila Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na ninawapongeza Wajumbe na Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa uchambuzi wao mzuri sana, naamini kabisa utatusaidia Serikalini. Labda nianze na moja, lile linalohusu Shirika letu la Posta na hususan fedha zile ambazo walizitumia kulipa pensheni kwa wafanyakazi ambao walikuwa wameajiriwa *East African Post and Telecommunications*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Septemba tarehe 30, 2016, tulikuwa tumepokea maombi ya kurejesha takribani shilingi bilioni 5.1 ambazo zilitumika kuwalipa pensheni wastaafu. Kati ya fedha hizo, ilipofika Februari 28, 2017 tulikuwa tumerejesha shilingi bilioni 2.7. Kwa hiyo, napenda tu kusema kama Serikali, tutaendelea kupunguza hilo deni kadiri mapato yanavyoruhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni lile la shilingi bilioni 26 ambalo linadaiwa na *TRA*, naomba niifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kupitia ule utaratibu wa *Tax Amnesty*, kiasi cha shilingi bilioni 12 ambacho kilitokana na riba kimesamehewa kupitia Mamlaka ya Mapato. Hivi

karibuni Shirika letu la Posta limeleta maombi ya kufutiwa kiasi cha shilingi bilioni 14.8. Naomba niseme tu hili tunaendelea kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho upande wa Shirika la Posta, ni ushauri kwamba sasa tuliondoe kwenye orodha ya mashirika ambayo yanasubiri kurekebisha. Hili suala tunaendelea kulifanyia kazi; na kama ambavyo tumefanya hivi karibuni kwa Shirika la Bima la Taifa *NIC*, tunakamilisha utaratibu pia wa kuliondoa Shirika la Posta kwenye orodha ya mashirika ambayo yanatakiwa kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba tayari nimetekeleza agizo lako na natumaini utaendelea kuruhusu tuendeleo na mawasiliano na Mheshimiwa Hawa. Tayari tumezungumza na nimemwonyesha hapa, *Government Notice* ambayo tulishaitoa kwa ajili ya kutoa hati ya msamaha kwa bidhaa ambazo zinatumiwa kwa ajili ya kujenga *Terminal Three* ambapo *items* takribani 277 zimepata msamaha kuanzia Januari tarehe 3. Kwa hiyo, nafikiri hilo limekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda lingine liseme kidogo alilisema Mheshimiwa Kishimba, kodi kwenye madini na hasa dhahabu, nimwombe tu, nakumbuka alichangia vizuri sana kwenye Mkutano wa Mheshimiwa Rais na Wachimbaji Wadogo wa Madini, kile kikao tulichofanya kwa siku mbili, tarehe 22 mpaka 23 Januari, 2019. Kama Serikali, tulipata mapendekezo mengi na namwomba tu avute subira kidogo tu, atapata majibu muda siyo mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo limesemwa sana ni marejesho ya ile asilimia 15 ya *import duty* kwa *importation* ya sukari ya viwandani. Niseme tu kwamba Serikali imeanza kulipa; na mpaka kufikia Desemba, Serikali imerejesha shilingi bilioni 11.84 kwa Makampuni, *SBC* tumepeleka shilingi bilioni 3.5, *BONITE* shilingi bilioni 1.7, *Nyanza Bottling* shilingi bilioni 1.5, Coca Cola Kwanza shilingi bilioni

1.9, Bakhresa shilingi bilioni 2.3 na *Jambo Food Products* nusu bilioni. Kwa hiyo tumeanza kulipa na tunaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme pia kuhusu *GN* ambayo nimeshahielea lakini niliseme tu kwa ujumla. *GN*, Sheria zile za Kodi pale ambapo sheria zinaniruhusu kusamehe kodi, zinanitaka kama Waziri wa Fedha, nijiridhishe kwanza na bidhaa ambazo zinahusika, kama zinakidhi, lazima nijiridhishe kwamba bidhaa hizo, au msamaha huo unazingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ni kwamba, tunajitahidi ili misamaha hiyo, isitumike vibaya. Kwa hiyo, kwa miradi mingi, kwa siku za karibuni tunatoa tunaita *Global GN* ambayo inarahisisha, lakini tumewabana Mawaziri wasimamizi wa Sekta husika, waji-*committ* kwa maandishi na kuhakikisha kwamba bidhaa zile zinazoombewa msamaha basi zinakidhi matakwa ya Sheria ya Kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maduka ya fedha za kigeni, niseme kwamba zoezi tullilofanya hivi karibuni kupitia Benki Kuu, lilituonyesha mambo mengi ambayo siyo mazuri; kwanza maduka haya yalikuwa ni mengi mno bila sababu, mengine yalikuwa hayakidhi vigezo na mengine yalijihusisha katika utakatishaji wa fedha haramu na mbaya zaidi, ni kwamba Benki Kuu iliona kuna hatari ya kuhatarisha *Financial Stability* katika Taifa letu. Hili hatutalikubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea kufuatilia kwa karibu, nasi tunaamini kabisa kwamba mabanki yaliyopo yanatosha kabisa kutoa huduma ya kuuza fedha za kigeni. Kwa hiyo, tunaendelea kufuata kwa karibu lakini la msingi sana ni kuhakikisha *Financial Sector Stability* katika Taifa letu inalindwa. Lngine lilisemwa hapa kwamba, hawaoni *reforms* kubwa ambazo tumefanya katika Taifa letu na hili linanishangaza kidogo. Kwa kipindi kifupi katika miaka mitatu, tumeongeza makusanyo ya mapato katika nchi yetu kutoka shilingi bilioni 850 kwa mwezi kwenda karibu trilioni 1.4. Jitihada za Mheshimiwa Rais, za kupiga vita Rushwa ni *reforms* za wazi kabisa ambazo ni *transformative*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya uwezaji mkubwa sana kwenye miundombinu na kwenye umeme. Zote hizo kama hazionekani ni *transformative*, basi kweli nashangaa. Tumeshughulikia sana suala la *efficiency* kwenye *public service*. Jamani vitu vingine tuwe *honesty* kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la ndani, *in bottom line* ni kwamba linaliopika, tumefanya uchambuzi, lakini ni muhimu kwamba tunahakikisha deni hili linakwenda kugharamia miradi ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *as long as* tunaendelea kuhakikisha kwamba ni himilivu kwa vigezo vya ndani, halina tatizo, kaa na amani kabisa. Ukitumia *BoT Monthly Economic Review* ni muda mfupi sana. Nadhani na Mheshimiwa huyu alikuwa mmoja wa watu waliokuwa darasani kwangu miaka ile, ni vizuri akakumbuka kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa nakuongezea dakika tano. (Makofi)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda tu kulihakikishia Bunge lako Tukufu, vipo vigezo sasa; tumemaliza *Household Budget Survey* mwaka 2017, tumehakiki kwa kushirikiana na baadhi ya wadau wetu na tutaleta taarifa rasmi katika Bunge ili kulieleza Taifa *Household Budget Survey* imeonyesha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu, kwa mfano, *basic need poverty* imepungua kutoka asilimia 28.2 sasa imefikia asilimia 26.4. Vile vile umiliki wa rasilimali walizonazo wananchi wetu imeongezeka, lakini vilevile ajira katika sekta ambazo zinakua haraka, nayo imeongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa vigezo tu hivi vichache, ujue kwamba hii ni uhalisi, siyo namba tu. Nilisema suala juu ya vikwazo na usumbufu wakati wa kuingiza mizigo. Serikali inapokea ushauri, tutakaa na Wizara ya Viwanda na

Biashara kama ilivyoshauriwa, tutazungumza na waagizaji wa bidhaa nchini; na ipo fursa na hasa baada ya Bunge hili, tutakutana nao ili tuweze kuona shida iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunafanya hivi kama Serikali, lakini kwa sababu ya wingi wa makundi na mgawanyiko ndani ya sekta binafsi, tumekuwa tunakutana na *Apex organizations*. Kwa kikao kile cha Sekta ya Madini tuligundua kwamba unapata zaidi kwa kuzungumza na makundi maalum badala ya kuzungumza na haya makundi Wakilishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakutana nao ili tuweze kuona namna nzuri zaidi ya kushughulikia upungufu. Kwa hiyo, ni jambo jema halina tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali mnafanya kazi nzuri sana. Kamati ya Viwanda na Biashara, ukurasa wa 16 wamesema pesa za sukari hazilipwi; Mheshimiwa Mbatia amesema pesa za sukari hazilipwi; ninyi toka Desemba mmelipa. Huyu Afisa Habari kwenu anafanya kazi gani? Kwa sababu pesa hizi zikilipwa, zinatoa *comfort* kwa wawekezaji. (*Makofi*)

Nakushukuru. Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. (*Makofi*)

MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwasilisha na kupokea maoni ambayo wameyatoa Waheshimiwa Wabunge juu ya Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya

hasa kwenye Sekta hii ya Miundombinu. Ametekeleza miradi mikubwa sana ambayo Serikali imeanza kuitekeleza na imeonekana kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ya usimamizi wa Serikali, nawapongeza Mawaziri, na Waziri mwenye dhamana ambaye anasimamia hii sekta, kwa kazi kubwa sana aliyofanya kwa Kamati. Ushirikiano ambao ameuonyesha umetekeleza miradi ambayo ni mingi na ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa aliyofanya ya kusukuma fedha kupeleka kwenye Sekta ya Miundombinu ambako kumeonekana miradi mingi ambayo imeanza kutekelezwa na zaidi kulipa fedha nyingi za Makandarasi waliokuwa wanadai, karibu ya zaidi shilingi trilioni tatu zimelipwa kwa kipindi cha miaka hii mitatu iliyokuwa na malimbikizo ya madeni huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni 12. Kati ya hao, 11 wamechangia kwa kuzungumza na Mbunge mmoja amechangia kwa maandishi. Nawapongeza sana na kuwashukuru kwa kazi kubwa ambayo wameitoa na ushauri wao karibu asilimia kubwa umepitia mapendekezo ya Kamati. Mjumbe wa kwanza alikuwa ndugu yetu Mheshimiwa Musukuma, ametoa mapendekezo yake na kuishauri Kamati juu ya magari ambayo yanatumia *super single*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ambayo ametoa Mheshimiwa Mbunge, Kamati ilishatoa mapendekezo na yalishaanza kufanyiwa kazi na Serikali. Kwa bahati nzuri, Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Isaack Kamwelwe, amezungumza nia ya Serikali kuangalia upya sheria ambayo ipo, nasi kama Kamati tunasisitiza kwamba, ni vyema Serikali ikaliangalia hilo, kwani nchi yetu siyo kisiwa, tumekaa katika maeneo ambayo ni ya mzunguko, ambapo tunahitaji kuwa na mawasiliano na nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ambayo ameyatoa Mbunge Kamati ilishatoa mapendekezo na yalishaanza kufanyiwa kazi na Serikali kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Isack Kamwelwe amezungumza nia ya Serikali kuangalia upya sheria ambayo ipo na sisi kama Kamati tunasisitiza ni vyema Serikali ikaliangalia hilo kwani nchi yetu sisi sio kisiwa, tumekaa katika maeneo ambayo ni ya mzunguko ambayo tunahitaji kuwa na mawasiliano na nchi za jirani, kwani maeneo mengine ambapo tulitunga sheria hii hii, wapo wanaoitekeleza na wapo ambao hawaitেকেlezi. Kwa hiyo, ni vyema Serikali ikaliangalia upya na waweze kuliangalia kwa manufaa mapana ili liweze kufanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjumbe mwingine aliyechangia Mheshimiwa Ally Saleh alizungumzia sana juu ya Shirika la Ndege ambalo mawazo yake makubwa alikuwa anashauri kwamba Shirika la Ndege lisiwe la kutoa huduma tu bali liwe la kibiashara na watendaji wajue shughuli ya kuliendesha hili shirika linahitaji ufanisi mkubwa. Kamati ilishatoa mapendekezo katika ukurasa wa 33 hadi 34, tumetoa mapendekezo juu ya kuliboresha shirika hili, lakini bado yapo mambo ya msingi ambayo ni vyema akayafahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika lina mpango wa kuweka *business plan* ambayo shirika linalo. *Plan* yao ni ya kuanzia mwaka 2016 hadi 2017 na sasa wanayo *plan* ya 2017 hadi 2022 ambapo wamejipanga kuwa na *Bombardier* nne, *Airbus* tatu, *Boeing* mbili na pia wamepanga safari za nje na walishaanzisha Entebbe na sasa wanajipanga kwenda Harare, Lusaka, Guangzhou na baadaye wana mpango wa kwenda Kigali, Nairobi, Lubumbashi na London ili kuweza kushiriki kwa karibu sana kwenye biashara ya nje ambayo itatusaidia sana kukuza sekta ya utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hawa Mchafu ameipongeza Serikali kwa jitihada ambazo zimefanywa. Naamini kwa ambaye anaona, anaona juhudi kubwa sana za Serikali ambazo zimefanywa, miradi mingi imetekelezwa,

lakini ushauri alioutoa ni juu ya kuzingatia umuhimu wa kutoa fedha kwa wakati. Kwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Waziri amelitolea ufafanuzi na bado Waziri mwenye dhamana, Waziri wa Fedha kaeleza jinsi ya mikakati ambayo anaendelea kulipa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amepongeza Serikali kwa ununuzi wa ndege na kuanzisha safari za nje. Vile vile amezungumzia masuala ya GN inayosababisha kuchelewa kwa miradi, kwa nini vifaa visipelekwe *site* mapema. Hili tumelishauri kama Kamati na tunaomba Serikali ilizingatie kwani linachelewesha sana miradi ya maendeleo hasa pale ambapo panahitajika kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa vinavyohitaji kwenda kufanya kazi. Tunaomba Serikali ilifanyie kazi kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, amezungumzia sana juu ya umuhimu wa ujenzi wa reli. Kama mnavyofahamu Serikali imeanza kutekeleza miradi ya reli kwa ujenzi wa kiwango cha *standard gauge*. Reli hiyo imeanza kujengwa Dar es Salaam mpaka Morogoro lakini kipo kipande cha kutoka Morogoro kuja Dodoma. Mipango ya baadaye ya Serikali ni kuhakikisha reli inajengwa kufika Tabora, Tawi la Mwanza na Tawi la Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali kwamba mapendekezo yaliyopendekezwa na Kamati ni vyema yakaangaliwa upya kwani sisi tunaamini kwamba eneo la ukanda wa maziwa ndilo ambalo litakuwa na mzigo mkubwa sana. Kwa hiyo tunaamini Serikali wataangalia na karibu mapendekezo waliyoyatoa yapo kwenye ukurasa wa 31 na Kamati ilishatoa mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kazungumzia juu ya ujenzi wa kuimarisha TAZARA. Reli ya TAZARA ni muhimu na kielelezo pekee cha cha urafiki kati ya nchi ya Tanzania na China na ndugu zetu wa Zambia. Tunaomba Serikali ilifanyie kazi kwa haraka sana ili kulinusuru shirika hili kwani bado lina nafasi ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Amon Saul amepongeza Serikali kwa ununuzi wa ndege na imesaidia sana kupunguza ajali za viongozi; tunashukuru na tunapokea pongezi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa James Mbatia amezungumzia suala la bandari, umuhimu wa watu wetu kupata elimu, weledi katika mataifa mengine; bandari na reli lazima viende sambamba; suala la mizigo mikubwa reli ielekezwe huko ndiko msingi wa kiuchumi. Nami nimepitia na nimeeleza mapendekezo yaliyokuwa yameelezwa na Kamati. Karibu asilimia kubwa ya mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge mengi ni yaleyale ambayo tumeyatoa kwenye Kamati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nuru Bafadhil amezungumzia juu ya kuimarisha barabara ya Chalinze kwenda Tanga hadi Kilimanjaro, hasa lile daraja la Mto Wami. Naamini Serikali ilishaanza kulifanyia kazi na tayari sio muda mrefu mkandarasi ataanza kulifanyia kazi eneo lile husika. Pia kashauri juu ya umuhimu wa kuweka taa kwenye Jiji la Dodoma; mapendekezo hayo tunayapokea na tutawaambia Serikali waweze kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Genzabuke amezungumzia reli ya *standard gauge*, pia amezungumzia juu ya ujenzi wa barabara ya Kibondo mpaka Kakonko. Barabara hizi zipo kwenye mpango na tayari Serikali ilishaanza kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Mollel ametoa pongezi kwa Serikali kufufua *TTCL*, shirika lijiendeshe kwa faida na wizara na taasisi zilipe madeni; viwanja vya ndege hasa *Terminal III* itasaidia kuleta wageni wengi toka nje, miundombinu kwa watu wenye ulemavu ni muhimu kuzingatia. Naamini Serikali kila inapojenga viwanja huwa inazingatia yale ambayo Mheshimiwa Amina Mollel ameyapendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya ujumla; nitoe pongezi za dhati kwa Serikali kwa kuweza kukubali ushauri wa Wabunge kwa kiwango kikubwa sana. Ndio maana asilimia kubwa, Kamati yangu imepokea pongezi nyingi kwa sababu miradi mingi imetekelezwa. Tunaomba sana Serikali iweze kuzingatia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni eneo la bandari. Ili bandari iweze kufanya kazi vizuri na ili bandari iweze kutoa msaada kwenye bandari zingine hasa za maziwa makubwa; Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa ni vyema tukaijengea uwezo. Tunapendekeza Serikali izingatie na kiasi cha asilimia 40 ya mapato yake kiweze kupelekwa bandarini ili iweze kusimamia miradi ambayo ina nafasi kubwa ya kusukuma shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iangalie upya sheria hasa hii inayokataza magari ya *single custom/ super single*. Eneo hili ni vyema Serikali ikalitazama upya kwani tusipoliangalia tutawafanya wafanyabiashara wa nchi za nje wakashindwa kutumia barabara zetu na kukwepa kwenda kufanya shughuli sehemu zingine. Tunaomba hili Serikali tunajua ni sikivu, wataliangalia kwa makini ili waweze kulichunguza na kuufanyia kazi ushauri ambao Wabunge wameutoa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kwa jitihada ambazo wamezifanya na kupokea ushauri wa Wabunge. Mheshimiwa Waziri Mpango amezungumzia mambo ambayo kimsingi yalikuwa yanaleta tabu kidogo hasa kwenye utekelezaji wa miradi. Tunawahimiza ile misamaha ya kodi ambayo kimsingi inaweza ikachelewesha miradi, tunaomba sana waiangalie kwa kina wasipende kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lijualikali amechangia kukwama kwa ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara. Kubwa zaidi ni kuchelewa kwa msamaha wa kodi;

tunaomba wahusika wakae pamoja waweze kutekeleza kwa haraka kwani miradi inapochelewa inalifanya Taifa liingie gharama kubwa zisizokuwa stahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishukuru tena Serikali na tunaahidi sisi kama Kamati kuendelea kuipa *support* na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa Kamati tutayafanyia kazi na tutaendelea kuishauri Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mwenyekiti kwa kazi nzuri na majibu sahihi kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati imefanya kazi nzuri na majibu mengi ya Serikali yamekuwa mazuri, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2018.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Sasa taarifa hii ni rasmi kwenye kumbukumbu za Bunge kuhusu shughuli za Kamati za mwaka 2018.

Mwenyekiti Kamati ya Viwanda na Biashara.

MHE. SULEIMAN A. SADIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi tena kuja kumalizia shughuli ambayo tumeianza asubuhi ya leo. Pia naomba nikushukuru kwa mara ya pili kwa jinsi ulivyoweka mstari katika suala lililozungumzwa na Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha ameleta habari njema, amezungumzia kwamba ile *refund* ya *industrial sugar* ya 15% Serikali imeanza kulipa na wameanza kulipa tokea Desemba na wewe ukaweka mkazo hivi hakuna watu wenu wakalieleza hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tulilizungumza hili muda mrefu, tulipata vilio vya wenye viwanda, wakasema mitaji yao imeganda, imekwama, wanashindwa kuendelea na uzalishaji na wengine wakatishia hata kufunga viwanda. Leo Serikali imefanya kazi kubwa, wameanza kulipa; Kamati ilikuwa ipaswe kuambiwa mapema. Mheshimiwa Dkt. Mpango tunakushuru sana kwa hili na niishukuru sana Wizara kwa kuanza kulipa na tuwaombe kama Kamati waendeleo kulipa, bado kuna wengine wamebaki endeeleni kuyafanyia kazi. Hii ni Serikali sikivu na sasa ni kweli Tanzania ya viwanda imeanza kusikilizwa, hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango na hongereni sana Wizara zote zinazosimamia jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuwashukuru wachangiaji wote waliochangia katika hotuba ya Kamati ya Viwanda na Biashara, niwashukuru Wabunge wote lakini naomba kwa sababu ni wachache mno niwatambue. Waliochangia kwa kuzungumza ni Waheshimiwa Wabunge 15; Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Kishimba, Mheshimiwa Kiteto, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Mndolwa, Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Millya, Mheshimiwa Nsanzugwanko, Mheshimiwa Amon, Mheshimiwa Komu, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Genzabuke na Mheshimiwa Mollel pamoja na Makamu Mwenyekiti Kanali Masoud. Nawashukuru sana wote hao waliochangia kwa kuzungumza

na kuna mmoja amechangia kwa maandishi Mheshimiwa Peter Lijualikali. Nawashukuruni sana wote ambao mmeunga mkono na kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambao yamezungumzwa sana katika michango ya Wabunge ni maeneo ambayo tumeyasema sisi kama Kamati, maeneo ambayo Kamati imeiomba Serikali iyafanyie kazi haraka, maeneo ambayo Kamati ilishaomba Serikali au ilishawashauri Serikali kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza lilikuwa ni suala la *VATrefund* ya 15%; wapo Wabunge wamelizungumza sana hili na Serikali imeanza kulishughulikia. Naipongeza sana Serikali katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni viwanda vilivyobinafsishwa; hapa katika eneo la viwanda vilivyobinafsishwa kuna shida kidogo. Kuna shida kwa sababu zile *data* ambazo tumeletewa sisi kama Kamati na hizi data ambazo zinaendelea kutolewa haziendi sawa. Sisi Kamati na Wizara tunatakiwa wote tunyooshe mstari. Waziri anaposema viwanda vinavyofanya kazi vizuri sana 68 sisi tunasema sio 68, kwa hivyo hatuendi vizuri. Nitaomba Mheshimiwa Waziri tukae tuyaweke sawa haya mambo na Kamati ilikuwa inaomba sana tupate *data* za uhakika kwa sababu nia na madhumuni wote twende kwenye mstari ulionyooka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la viwanda vilivyobinafsishwa limebeba eneo kubwa la uchumi wa nchi yetu. Viwanda hivi vingine vinakosesha ajira, Serikali inakosa mapato, lakini kubwa zaidi Watanzania wanakosa bidhaa. Viwanda hivi vingine vilikuwa vina mitaji, wengine walikuwa wana *business plan* nzuri, wengine wamekopa mabenki, leo viwanda vingine havipo na mashine hazipo. Kwa hiyo, tunaomba eneo hili Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia Serikali muwe sikivu sana katika eneo hili. Tunaomba maazimio yetu yafanyiwe kazi kwa ubora wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa sana ni suala la Liganga na Mchuchuma. Kamati ilishauri kwamba suala hili linahitaji uwekezaji mkubwa na Kamati imeshauri kwamba kama inawezekana tungeanza kuuza *raw material*, ile *raw material* tukianza kuuza gharama zitakuwa ni ndogo lakini tukisema tujenge kiwanda gharama bado ni kubwa, kutahitajika gharama za kila aina. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba suala hili Serikali imeliona na nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Mawaziri wameanza kuyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo Wabunge wamelizungumza zaidi ni mazingira ya kufanyia biashara. Ni kweli kulikuwa na tatizo ambalo ni kubwa, Serikali imekuwa sikivu, Mheshimiwa Rais ameshafanya vikao mbalimbali na *private sector*, Wizara wameshafanya mikutano mbalimbali na wadau na sisi kama Kamati tumeshashiriki kwenye baadhi ya mikutano yao. Ombi letu kama Kamati ile mikutano ya wadau iendeleo, iwe ni mikutano ya mara kwa mara. Tutakuwa tunapata changamoto na kuzitatua haraka iwezekanavyo. Vikao kama vile inaonekana vimesitishwa, tunaiomba sasa Serikali ianze kuvifufua vikao vile na mazungumzo ya mara kwa mara yaendeleo kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kuipongeza Serikali, zipo tozo ambazo zimeanza kuondolewa. Zipo tozo ambazo zilikuwepo kwenye *blue print* wameanza kuzianya kazi kwa upande wa *OSHA* zipo tozo tano zimeondolewa. Kwa hiyo, Kamati yale ambayo imependekeza yameanza kushughulikiwa lakini bado tunahitaji iende kwa kasi zaidi kwa sababu malalamiko ni mengi kuliko vile yanavyoshughulikiwa. Inaonekana kuna mwanga kwamba kazi imeanza kufanyika na naipongeza sana Serikali. Naipongeza sana Serikali kwa sababu sasa hivi Mheshimiwa Rais ametuwekea Wizara ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hii Wizara ya Uwekezaji tuna matumaini makubwa kama Kamati kwamba, tutafanya kazi kubwa, tutapata wawekezaji wengi na wawekezaji wengi watakuja kwa sababu Serikali ni sikivu. Katika hili

nimpongeze Mheshimiwa Waziri Angella leo amezungumza maneno ya maana sana na ameunga mkono juhudi zote za Kamati, kwa pamoja tutafika Mheshimiwa Waziri karibu sana kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mengine limezungumzwa suala la wafanyabiashara kukaa pamoja, hili lilianza kufanyika; Serikali ilianza kukaa pamoja na wafanyabiashara. Tunaomba utaratibu ule uendelee na Mheshimiwa Rais tunampongeza na yeye mwenyewe kwa juhudi zake, alishakaa na taasisi mbalimbali, alishazungumza suala la kodi na tozo na matumaini yangu kwamba mambo haya sasa yanaanza kushughulikiwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kiwanda cha Urafiki, kiwanda hiki kinasuasua muda mrefu na kiwanda hiki kimepata mwekezaji ambaye toka ameingia ni hasara, hakuna faida yoyote kwenye Kiwanda cha Urafiki. Ajira zilikuwa 2,000, sasa hivi kuna ajira chini ya 400; kiwanda kilikuwa kinapata faida, sasa hivi ni hasara kwa miaka na miaka. Kamati inaomba juhudi za haraka zichukuliwe, Urafiki ilikuwa inazalisha mazao mazuri, vitenge vizuri, Watanzania wengi walikuwa wanakimbilia pale. Tunaomba juhudi za haraka zichukuliwe ili Kiwanda cha Urafiki kirudi kwenye enzi za Mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la bajeti ya usimamizi wa mazingira kwa kweli haiendani na kasi ya uharibifu wa mazingira. Katika hili naomba nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri January, amezungumzia hapa kwamba Wabunge waliochangia ni watatu; jamani mazingira ndio uhai wa viwanda Tanzania, mazingira ndio kila kitu katika nchi yetu. Leo tunapoonyesha kwamba hatutambui mazingira tunawakatisha tamaa wataalam na tunaikatisha tamaa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sasa Wabunge wajue kwamba bila ya mazingira hakuna viwanda, bila ya mazingira tunaharibu nchi yetu, mazingira tukiyahifadhi vibaya hata kilimo kitaharibika. Wabunge

wapewe elimu zaidi Mheshimiwa Makamba waweze kutambua nini maana ya uhifadhi wa mazingira. Mheshimiwa January nakuunga mkono sana katika hili, sisi kama Kamati tumeridhika na kauli yako elimu bado ni ndogo hasa kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba bajeti itengwe ya kutosha katika eneo la uhifadhi wa mazingira ili tuweze kudhibiti uharibifu unaoendelea. Uharibifu ni mkubwa sana kwenye migodi, viwanda, mito na vyanzo vya maji. Suala la tabianchi linatumaliza kwelikweli, kwa hiyo tunaomba sana haya mambo yote yaende pamoja lakini bajeti ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia haya, lakini Mheshimiwa Lema amezungumzia sana suala la Kiwanda cha *General Tyre*, *General Tyre* sisi kama Kamati tumelizungumza sana na zipo ahadi mbalimbali za Serikali. Sisi kama Kamati tunatilia mkazo zile ahadi za Serikali zifanyiwe kazi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *General Tyre* kinapoteza mapato, Watanzania wanakosa matairi bora, ajali barabarani ni nyingi na mara nyingi sana Kamati imejifunza mali zinazozalishwa Tanzania zina ubora wa hali ya juu. Bidhaa za ndani ya nchi yetu zina ubora wa hali ya juu ukilinganisha na bidhaa kutoka China, India na mataifa mengine. Kwa hiyo, Watanzania wanapenda sana bidhaa za ndani na tuendelee kuzisimamia ili Watanzania wapate kilicho bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengine yamezungumzwa katika eneo hili, sisi tunaomba tuyatilie mkazo kwa maana ya haya yote sasa yafanyiwe kazi kwa hatua zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo pia tunaomba lifanyiwe kazi ni suala la gharama za uzalishaji. Suala la gharama za uzalishaji wataalam watusaidie,

viwanda vya Tanzania vinaonekana gharama za uzalishaji zipo juu na kuna mifano hai kuanzia kwenye sukari, chuma, mabati na ndio maana leo mabati kutoka China yamezagaa Tanzania, wanasema ni mabati feki kwa sababu ni mabati ya bei nafuu. Gharama za uzalishaji ndani ya nchi yetu zimekuwa juu, tunaomba kikosi kazi cha wataalam wakishirikiana na Wizara ya Fedha walifanyie kazi hili ili tujue kuna tatizo gani, kuna shida gani katika eneo hili ili wale ambao wana viwanda waweze kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo ambalo tunatakiwa sote kwa pamoja tulione na tulifanyie kazi. Vipo viwanda vilivyobinafsishwa leo vimekuwa ni viwanda vya mfano vinatoa gawio kubwa kwa Serikali. Kamati inashauri viwanda hivi vilindwe, mfano, viwanda vya sementi, viwanda vya sigara, viwanda vya mabati kama *ALAF* na viwanda hivi vyote vya bia kama Serengeti, *TBL* na hawa ambao wanatoa gawio ni viwanda ambavyo vimebinafsishwa pamoja na viwanda vya sukari vinavyofanya vizuri Serikali ikae na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea wadau wana dukuduku, wadau wale wana mambo yao, tusipokaa nao tutawakatisha tamaa na gawio litashuka, uzalishaji utashuka na mapato ya nchi yatapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali yule ng'ombe anayetoa maziwa mengi tuendelee kumlea, tumpe majani mengi ili aendelee kutoa maziwa mengi, huo ndio wito wa Kamati. Pia wale ng'ombe ambao hawatoi maziwa, tuendelee kutafuta namna yoyote ya kuhakikisha na wale ng'ombe wanaendelea kutoa maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu viwanda vilivyobinafsishwa 156 asilimia 70 ya viwanda hivi vikifanya kazi, Taifa litapata ajira mapato ya nchi yataongezeka. Hapa Wabunge wengi wameshauri Mheshimiwa Spika aunde Kamati maalum ya kwenda kulisimamia hili na sisi kama Kamati tulisema hatuna tatizo na hilo, uamuzi ni uamuzi wa Spika. Kama inaundwa iundwe, tujue ukweli kwamba kuna nini katika jambo eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba zipo juhudi zinaendelea kufanyika na Kamati inaipongeza Serikali, zipo juhudi mbalimbali ambazo tayari tumeziona, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais anatekeleza kwa vitendo suala la Tanzania ya Viwanda. Kamati iko bega kwa bega na yeye na Kamati tutashirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba tunasonga mbele kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipitishie mapendekezo yetu ya Kamati kuwa azimio la Bunge kama yalivyoletwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante Mwenyekiti kwa majibu mazuri, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali taarifa ya shughuli za Kamati za mwaka 2018 maoni na mapendekezo ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda,
Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa
Mwaka 2018 ilipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda na sasa hii taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara kwa Shughuli za Kamati za mwaka 2018, ni taarifa rasmi ya Bunge.

Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri mliyofanya pamoja na Wenyeviti, majibu ya Mawaziri,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

majibu ya Waziri wa Fedha ambaye naye ametoa majibu murua kabisa kuonesha kuwa sasa madeni ya watu yanalipwa.

Baada ya maneno haya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.25 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Februari, 2019, Saa Tatu Asubuhi)